Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 10 Februari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge jana katika kikao cha jioni saa kumi na moja ilitokezea kwamba upande wa Serikali hakuwapo Waziri hata Naibu Waziri hata mmoja yaani wote hawakuwepo si kitu cha kawaida hata kidogo imetutia wasiwasi wengine kwa sababu huwezi kujua dunia sasa kumetokea hini.

Kwa hiyo, nadhani hatuwezi kupuuza tukajidai hakuna lililotokea. Kwa hiyo, jana alilazimika Mheshimiwa Naibu Spika ambaye alikuwa kitini kuahirisha shughuli kabla hata ni pale pale katika dakika tano tu. Jambo hili linahitaji ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliarifu Bunge vipi ilikuwa hivyo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maelezo mafupi tu juu ya kilichotokea jana.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 9 Februari, 2009 kikao cha Kumi cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu kilipoanza saa kumi na moja jioni, Mheshimiwa Anna Makinda Mbunge, Naibu Spika wa Bunge aliamua kusitisha shughuli za Bunge na kuahirisha hadi leo saa tatu asubuhi.

Uamuzi wa Mheshimiwa Naibu Spika, ulitokana na kutokuwepo kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri ndani ya ukumbi wakati shughuli za Bunge zilipoanza.

Mheshimiwa Spika, kuanzia saa saba na nusu mchana Baraza la Mawaziri lilikuwa linakutana chini Uenyekiti wa Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Sheni katika Ukumbi wa mikutano ya Baraza la Mawaziri ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Kikao hicho kilihitimisha shughuli zake saa nne usiku jana.

Moja ya agenda za kikao hicho ni waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kuanzisha ghala la forodha kwa ajili ya bidhaa za mafuta. Waraka huo uliwasilishwa na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mbunge kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge ambaye alihitajika Dar es Salaam kwa kazi maalum. Muda wa kuanzia kwa shughuli za Bunge saa kumi na moja ulipofika sehemu kubwa ya Mawaziri na Naibu Mawaziri wachache walikuwa kwenye kikao cha Baraza.

Kwa hiyo, ilipofika saa kumi na moja na robo ilibidi kuamba ridhaa ya Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mwenyekiti wa kikao ili baadhi ya Mawaziri waruhusiwe kuondoka katika kikao cha Baraza kwenda kuhudhuria kikao hicho Bunge ambacho kilikuwa kimeshaanza. Baada ya muda mfupi Mawaziri hao walirejea na kutoa taarifa kuwa kikao cha Bunge kimeahirishwa hadi leo saa tatu asubuhi. Walieleza kuwa sababu ya kuahirishwa kwa kikao hicho ni kutokana na kutokuwepo kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uelewa niliokuwa nao wakati niko kwenye kikao hicho cha Baraza la Mawaziri ilikuwa ni kwamba Mheshimiwa Marmo, ambaye hatukuwa naye kwenye kikao angekuwa Bungeni. Lakini vilevile Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Uchumi ambaye naye hakuwa kwenye kikao tuliamini angekuwepo angalau kuweza kuchukua nafasi ya Serikali na baadhi ya Naibu Mawaziri ambao kwa kawaida hawaingii kwenye Baraza. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Marmo alikuwa anaumwa na Naibu Waziri alichelewa na yeye.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kutumia fursa hii kukuomba wewe radhi na Bunge lako Tukufu kwa tukio hilo wakati wote Serikali imekuwa ikijitahidi sana kupanga shughuli zake kwa namna ambayo haitaathiri utendaji wa shughuli za Bunge. Tukio la jana ni bahati mbaya na halikukusudiwa. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itajitahidi kutekeleza wajibu wake kwa namna ambayo haitakwamisha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa makofi hayo naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wameelewa nini kilitokea na mmetutoa wasiwasi basi sasa tunaendelea na kipindi cha maswali ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 136

**Juhudi za Kupambana na Tatizo la Mihadarati**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafanya juhudi kubwa ya kupambana na tatizo la Mihadarati nchini na kwamba tatizo hilo linaendelea kupamba moto na Tanzania ni kati ya nchi vinara inayolima Bangi:-

(a) Je, ni sababu zipi zinaendelea hali hiyo?

(b) Je, ni watuhumiwa wangapi wa Mihadarati waliotajwa na Hayati Amina Chifupa wameshachukuliwa hatua na ni hatua zipi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni, Tanzania imekuwa moja ya nchi za mstari wa mbele katika ukamataji na utekelezaji wa Bangi. Dhana ya kwamba Tanzania ni kati ya nchi vinara zinazolima bangi siyo za kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sababu zinazopelekea kuongezeka kwa kilimo cha bangi hapa nchini ni pamoja na:-

§ Hali ya Mazingira ya Nchi kijiografia. Kilimo cha bangi kinafanya sehemu za milimani na misitu minene ya asili kusikofikia kirahisi.

§ Ushirikiano mdogo kutoka kwa wananchi kabla ya uhamasishaji na mapambano dhidi ya ulimaji wa bangi.

§ Hulka ya tamaa ya utajiri wa haraka haraka kwa baadhi ya wananchi wetu huwa inachochea kuongezeka kwa kilimo cha bangi hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006 mpaka 2008 zaidi ya watuhumiwa 35,000 walitajwa na kukamatwa kwa makosa mbalimbali ya dawa za kulevya kutokana na taarifa za Raia wema akiwepo Hayati Amina Chifupa. Kwa kuwa hizi ni tuhuma ambazo ziko katika ngazi mbalimbali za upelelezi na mahakama si vema kuwataja hapa Bungeni.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa bangi ni aina ya magugu na tumeona polisi mara nyingi wamekuwa wakiangamiza bangi kwa kuchoma moto, na polisi wanavuta moshi ule wa bangi ambao unaweza kuwadhuru. Je, Serikali haiwezi kutafuta aina ingine ya kibiolojia au dawa ili kuangamiza magugu yale kabisa na tutokomeza bangi moja kwa moja?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bangi ni aina ya magugu na wakati wa kuteketeza bangi askari wanaofanya hivyo huwa wanavuta ule moshi. Hakuna

uthibitisho wa kitaaluma unaotuonyesha kwamba moshi ule una madhara makubwa, utafiti utafanywa ikifahamika hivyo basi kutakuwa na tahadhari ambazo zitachukuliwa kwa wale wanaoteketeza bangi sio tu polisi bali hata wananchi wanaojihusisha na mazoezi hayo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ya nyongeza, mbali na bangi kuna mihadarati mengine inayoingia ikiwemo kokeini ambazo kwa kiwango kikubwa zinatumiwa na vijana na vijana wamekuwa wakiathiriwa sana na madawa ya kulevya ambayo ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Je, Serikali ina mikakati gani kuzuia uingizwaji wa madawa hayo ili vijana waokoke kutokana na matatizo waliyonayo sasa hivi?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli athari ya bangi baina ya vijana nchi yetu ni kubwa jitihada zinazofanywa ni nyingi ikiwa ni pamoja na kuanzisha kitengo maalum cha kuratibu mapambano dhidi ya madawa ya kulevya ikiwa ni pamoja na kokeini. Tumeona mapungufu katika kitengo hiki ikiwa ni pamoja na kukosa fedha za kuendesha oparesheni za kupambana na dawa za kulevya.

Hatua kambambe ambazo kwa sasa zinachukuliwa na Serikali ni kuunda mamlaka yenye Bajeti yake maalum kwa ajili ya kutatua tatizo hili tofauti na sasa ambapo operesheni ufanyika kwa kutumia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani upande wa polisi, upande wa *immigration* lakini pia Bajeti ya usalama wa taifa na idara zingine kama vile posta.

Hatua ya kuanzisha mamlaka haya imefikia ngazi ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kujadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu yaani *IMTC* wakati wowote kutoka sasa Muswada wa kuanzisha mamlaka hayo utaletwa Bungeni.

Na. 137

**Matatizo ya Mipaka ya Vijiji**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ipo kwenye mchakato wa kupima vijiji na kuweka mipaka ili kuepusha migogoro ya Ardhi:-

(a) Je, Serikali inafahamu tatizo la mpaka baina ya vijiji vya Ahsante Nyerere Kasulu na Kijiji cha Basanza?

(b) Kama inafahamu. Je, ni hatua gani zilizochukuliwa katika kutatua mgogoro huo?

**NAIBU WAZIRI NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ipo kwenye mchakato wa kupima Vijiji na kuweka mipaka ili kuepusha migogoro ya Ardhi. Hadi kufikia Desemba, 2008 Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilikwishapima jumla ya Vijiji 211 katika Mkoa wa Kigoma. Vijiji ambavyo havijapimwa ni 21.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitambua tatizo la mipaka baina ya vijiji vya Ahsante Nyerere Wilayani Kasulu na Kijiji cha Basanza Wilayani Kigoma. Mipaka ya Vijiji vya Basanza na ile ya Ahsante Nyerere ndio mpaka kati ya Wilaya ya Kigoma na Kasulu. Tatizo hili lilisababishwa na kutokuwepo na usahihi wa mipaka kati ya Wilaya hizi kutokana na vifaa duni vya upimaji (*standard sheet na prismatic compass)* vilivyokuwa vikitumika kwa wakati huo. Tatizo la kutokuwepo usashihi wa mipaka ndilo lililokuwa chanzo cha kijiji cha Ahsante Nyerere kulalamika na hatimaye kung'oa jiwe (*beacon*) moja la mpaka uliowekwa.

(b) Mheshimiwa Spika, hapo awali mipaka ya eneo moja na jingine iliwekwa kwa kuzingatia alama za Asili *(Natural Features)* kama vile Milima, mabonde na mito. Kwa kuzingatia mabadiliko ya hali ya Hewa, alama za Asili zimekuwa zikibadilika na hivyo kutotoa tafsiri sahihi ya mipaka.

Katika kutatua mgogoro wa mipaka, katika vijiji vilivyotajwa Serikali kupitia Wizara Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwaka 2007 iliwatuma wataalam wapimaji Ardhi *(Land Surveyors)* kupima upya mipaka ya vijiji hivyo kwa kutumia kifaa cha upima upya mipaka ya vijiji hivyo kwa kutumia kifaa cha upimaji cha kisasa (*Global Positioning System (GPS*) chenye usahihi wa kiwango kikubwa.

Kifaa cha kisasa cha upimaji (*Global Positioning System)* kinaonyesha eneo lilipo katika uso wa Dunia *(Geographical location)* kwa kuzingatia *Latitude* na *Longitude*. Kwa mantiki hiyo mpaka wa sehemu moja na nyingine utaendelea kujulikana hata baada ya miaka 20 kupita.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sasa hakuna utata katika suala la mpaka kati ya vijiji vilivyotajwa hata hivyo katika kujiridhisha zaidi Serikali imeanza kufanya uchunguzi kuhusu mpaka wa vijiji vya Ahsante Nyerere na Masanza.

Endapo itabainika kwamba bado lipo tatizo la vibaka hata baada ya upimaji wa mipaka hiyo kurudiwa upya tatizo hilo litashughulikiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mjibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri

ya Wilaya Kigoma Diwani wa Kata Matendo Mzee Karago, alileta hoja ambayo ilikubaliwa na Madiwani wote kwamba wakati wa ugawaji wa Wilaya za Kigoma, kwa bahati mbaya vijiji vya Zeze, Kwaga, na Kalela viliondolewa wilaya ya Kigoma na kupelekwa wilaya ya Kasulu.

Je, Serikali hivi sasa inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba vijiji hivyo vinarudishwa katika wilaya Kigoma? Hasa ukizingatia kwamba kuna mchakato wa ugawaji wa Kigoma kati ya wilaya Kigoma, kati ya wilaya Kigoma na wilaya ya Uvinza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa taarifa tu mimi nimewahi kufanya kazi katika mkoa wa Kigoma kwa miaka mitano kwa hiyo ndugu yangu Zitto Kabwa ajue hilo na nina hakika kwamba anajua kwa hiyo haya maeneo anayotaja ya Zeze na haya mengine yote aliyoeleza hapa nayafahamu, mimi nilikuwa kada wa Chama cha Mapinduzi katika Chuo cha CCM Kihinga. *(Makofi/Kicheko)*

Nilikuwa naomba hivi haya matatizo aliyoyaeleza hapa, kama yapo utaratibu wetu sisi kama mipaka ilikwenda ikabadilika na vijiji hivi vikahamia Kasulu sasa vinatakiwa virudi katika wilaya ya Kigoma Vijijini utaratibu wetu sasa hivi tumeanzisha kitu kimeanzishwa *DDC* tunatakiwa tuende pale tukazungumze halafu tuende kwenye regional consultative committee twende tukayazungumze mle ndani na yakiletwa kwetu sisi TAMISEMI nina hakika kwamba tutamshauri Mheshimiwa Waziri ili aweze kufanya kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema.

Na. 138

**Heshima na Tuzo za Taifa**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya shughuli za Rais (*Presidential Affairs* Cap. 502(1962 na Cap.9 (2202) kifungu cha 4 inampa Rais mamlaka ya kutunuku heshima, nishani na tuzo mbalimbali kwa Watanzania wanaotimiza vigezo vilivyowekwa:-

(a) Je, zipo aina ngapi za heshima na tuzo na vigezo vyake ukiachia heshima na nishani ambazo hutunukiwa wanajeshi wa majeshi ya ulinzi?

(b) Je, ni Watanzia wangapi wametunukiwa nishani hizo kuanzia Serikali ya Awamu ya Pili (1985) hadi Awamu ya Nne?

(c) Je, kuna watunukiwa ambao wamewahi kuondolewa heshima hizo kwa kwenda kinyume na masharti yake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Zipo aina 14 za Nishani za Taifa ambazo hutunikiwa kwa watu wa makundi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wenye sifa zilizoainishwa kwenye Nishani hizo.

Watanzania 300 wamekwishatunukiwa Nishani mbalimbali kati ya mwaka 1985 hadi sasa, akiwemo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ambaye alitunukiwa Nishani ya *The Order of the United Republic* mwaka 1980. (*Makofi*)

Kwa sasa hakuna mtunukiwa yeyote ambaye amewahi kuondolewa heshima hiyo. Kwa kuwa ofisi yangu ndiyo inayoratibu shughuli ya Nishani heshima hiyo. Kwa kuwa ofisi yangu ndiyo inayoratibu shughuli ya Nishati za Tifa, haijawahi kupokea taarifa yoyote kuhusu Mtunukiwa yeyote kwenda kinyume na masharti ya nishani yoyote.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Utawala Bora kwa majibu yake mazuri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya nishani zimetengenezwa siku nyingi na zimekaa muda mrefu na madini yale uenda ikawa mepesi pesi na zimechakaa. Je, kuna uwezekano wa kuzirejesha ili zikawa *will re-cycode* na kupatiwa nyingine?

La pili kwa kuwa masharti yale hayatajotolewa bayana inakuwa vigumu kuangalia kama kuna mtu anakiuka masharti, kwa mfano nishani hizi zinatakiwa zivaliwe nyakati gani?

Je, Waziri haoni kwamba ni vizuri nishani hizi masharti yakatolewa ili tusaidie kuweza kutoa maelekezo na katika hilo hilo ningependa kusema kwamba kwa rekodi aongeze nishani ya Azimio la Arusha Daraja la Tatu ambalo nilitukiwa 1995 mwezi Oktoba?(Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuziangalia nishani hizo na kuziboresha tunachukua ushauri wake na namshukuru kwa kutukumbusha hilo.

Swali lake la pili anazungumzia kuhusu masharti ambayo hayapo katika nishani hizo na kubaliana naye kwamba sheria hiyo iko *silent* na pengine ni vizuri tukitizamana hilo pia. Niseme tu kwamba tunashukuru ushauri wake kwa kutokana na uzoefu wake ameweza kutushauri hayo pengine ilikuwa ni *oversight*.

La mwisho hii la ushauri wa nishani ya Azimio la Arusha tunalichukua yote inatokea kutokana na *discretion* na yule anayetoa hizo nishani kwa hiyo nadhani pia ni ushauri mzuri.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilitoa nishani kwa wapiganaji wetu waliokuwa Comoro walipofanikiwa kwenda kurejesha amani kupitia *operation democrasia* kule Comoro na katika baadhi ya viongozi waliopewa nishani ni Waziri wa Mambo ya Nje na ushirikiano wa Kimatifa, lakini walioenda kupigana kule ni wanajeshi. Je, Serikali ikasema ni kwanini Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hakupewa nishani hiyo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwanini amepewa Mheshimiwa Benard Membe nishani hiyo ni kwa sababu yeye ni mmoja wa waliofanya maamuzi na alisimamia utekelezaji wote wa masuala yale yaliyotokea kule Comoro. Kwa hiyo, alistahili ikumbukwe tu kwamba ni discretion na busara ya Rais ndiyo inayotumika katika kutoa nishani hizo, kwa hiyo hakuna sababu yak um-*question* Rais kwanini alitoa nishani hiyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi ukumbuke tupo wazee ambao na sisi tunarajia kupata nishani sijui kwanini hazipo. (*Kicheko*)

Na.139

**Uimarishaji wa Taasisi za kutoa Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba**

**MHE. RIZIKI O. JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wananchi wa Dar es Salaam kuwa Serikali itaimarisha Taasisi za kutoa Mikopo kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba bora.

Je, ni hatua gani iliyofikiwa katika kutekeleza azma hiyo njema?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi, wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2005, aliahidi kuhusu wananchi kuwezesha kujenga nyumba bora kupitia mikopo ya nyumba. Aidha, ilani ya uchaguzi ya CCM kifungu 68 (f) inaelekeza Serikali kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa wananchi kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa kipindi cha mika mitatu iliyopita Serikali imefanikiwa kuweka mifumo ya kiutendaji na kisheria inayojenga mazingira ya kuwawezesha wananchi wengi kuwa na nyumba bora kupitia mikopo ya nyumba. Mifumo hiyo ni pamoja na ifuatayo:-

Kwanza, Serikali imeanzisha idara ya Nyumba katika Wizara yangu ambayo pamoja na mambo mengine inaratibu masuala ya nyumba ikiwa ni pamoja na kusimamia, kuanzishwa na kuimarisha taasisi na taratibu za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

Pili, katika Mkutano wa Bunge uliopita Oktoba 2008, Bunge hili lilipitisha Miswada miwili ya sheria yenye kuweka mazingira ya mikopo ya nyumba kuanza kutolewa.

Miswada hiyo tayari imepata ridhaa ya Mheshimiwa Rais, yaani Sheria No. 17 ya mikopo ya nyumba *(The Mortgage Finance Special Provision Act No. 17*) na sheria Na. 16 ya Hatimiliki za sehemu ya Majengo (*The Unit Title No. 17*).

Sheria hizi zikitumika kwa pamoja zitaleta manufaa yafuatayo:-

(a)Wananchi watapata fursa ya kukopa kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba bora kwa masharti ya muda mrefu miaka 10 hadi 20 na riba nafuu.

(b)Wawekezaji katika sekta ya ujenzi wa nyumba na kuuza (*Real Estate Developers)* watajitokeza kwa wingi na kujenga majengo hasa ya ghorofa na kuwauzia wananchi sehemu za majengo hayo (*Flats*) kwa kuwa wanunuzi sasa watakuwepo.

(c) Sekta ya ujenzi wa nyumba itapanuka sana na itasisimua sekta zingine kama viwanda vya ujenzi wa nyumba, viwanda vya samani na kadhalika. Vile vile itapanua sana ajira nchini kuongeza pato la Serikali na kuinua uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ili sheria hizi zianze kufanya kazi zinatakiwa zitungwe Kanuni zitakazosimamia utekelezaji wake. Mheshimiwa Rais, wakati akilihutubia taifa tarehe 31 Januari, 2009, aliagiza Wizara yangu iharakishe kukamilisha Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba utungaji wa Kanuni hizi upo katika hatua za mwisho kabisa. Lengo ni kuzikamilisha haraka ili utaratibu wa upatikanaji wa mikopo ya nyumba uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliagiza kuwe na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria hizi mbili ili wananchi wazitumie kupata mikopo ya nyumba. Utaratibu huo unaandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama Benki Kuu, chama cha wenye Mabenki na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, aidha elmu imeanza kutolewa pia kwa wenye mabenki ili nao wazielewe Sheria hizi na wazitumie kukopesha wateja wao. Mabenki yaliyopo nchini

kwa kutumia sheria hizi wameahidi kuanza kutoa mikopo ya nyumba kama moja ya biashara yao kwa wateja wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi utekelezaji wa suala hili unakwenda vizuri na nalishukuru Bunge lako kwa kutoa ushirikiano mkubwa katika mchakato huu wa kuanzisha utaratibu wa mikopo ya nyumba ili kuwawezesha wananchi kujenga ama kununua nyumba.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato unakuwa ni mrefu sana katika utekelezaji wa mambo katika Serikali yetu.

(a)Je, hatuoni kwamba suala hili la mchakato huu ambao ameuelezea Mheshimiwa Waziri tutafika mwaka 2010 bado utekelezaji huu haujafanyika na pia kudhoofisha shughuli hizi ambazo zitawafaidisha wananchi?

(b)Kwa sababu mkopo huu ambao amesema Mheshimiwa Waziri, utatolewa kwa muda wa miaka kumi ama ishirini, ukiangalia kipato cha wananchi wa Tanzania ni kidogo sana, Watanzania walio wengi kipato chao ni cha chini.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba muda huu ni mfupi sana na kuna haja ya kuongeza muda angalau miaka 30 ili wananchi waweze kufaidika na suala hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato kuwa mrefu ni kweli kwamba suala la utungaji wa Sheria hizi umechukua muda ni kwa sababu tu ilitakiwa kushirikisha wadau mbalimbali ili jambo hili liweze kufanikiwa, ilibidi tushirikishe benki mbalimbali, tushirikishe hawa wakopaji wenyewe, vyama vya wapangaji nyumba na wananchi kwa ujumla ndiyo maana imehcukua muda mrefu.

Lakini sasa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi sasa utaratibu umekamilika, kanuni kusema kweli wataalam wameshazimaliza, wameshaniwasilishia ofisini kwangu ila tu nimesema kabla sijazisaini nimesema kwamba tuwaite tena wadau wazitazame ili tutakapoanza utekelezaji kusije kukatokea vikwazo vikwazo.

Juzi wamekutana na wadau wametoa maoni yao. Kwa hiyo, wakati wowote nitatia saini na utaratibu uu utaanza mapema. Kwa hiyo, haitafika 2010 kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Ila mwaka huu huu 2009 utaratibu utaanza pengine hata kabla ya mwezi Juni, kwa sababu tulichokukwa tunangoja ni Kanuni ambazo zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, la pili, mikopo kutolewa kwa muda mfupi. Mikopo hii ya nyumba duniani kote ni mikopo ya muda mrefu ni tofauti na ile mikopo ya kibiashara ambayo inakwenda mwaka mmoja mpaka miaka mitano. Hii unaanza kulipa miaka 10, 15 mpaka miaka 20 na imezingatia hicho kipato kidogo, unalipa kidogokidogo mpaka baada ya miaka 20 basi mkopo umemaliza na nyumba ni yako.

**MHE. DR. SAMSON FERDINAND MPANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwamba je, mpango huu unahusiana na nyumba za *National Housing Cooperation* au nyumba nyingine ambazo zitajengwa hivi karibuni?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango huu ambao ni mpya utahusu wale wote ambao watakuwa wanajenga nyumba kwa ajili ya kuuza. Duaniani kuna watu biashara yao ni kujenga nyumba na kuuza. Hapa nchini hawapo kwa sababu tu soko halikuwapo na wanunuzi hawakuwapo lakini sasa baada ya mikopo kuanza wanunuzi watakuwepo. Kwa hiyo, wajenzi wa nyumba na kuuza vile vile wanunuzi wa nyumba na wenyewe watajitokeza. Kwa hiyo, utahusu wajenzi wote ambao watakuwa wanajenga nyumba na kuuza ikiwemo pamoja na *National Housing.*

Ameuliza habari za nyumba za sasa za *National Housing.* Nataka niseme kwamba tukianza utaratibu huu *National Housing* tumeshawapa maelekezo kwamba wabadilishe utaratibu wao.

Sasa hivi *National Housing* wanapangisha nyumba tu na kukusanya kodi kila mwezi baada ya kuanzisha utaratibu huu wa mikopo *National Housing* sasa na wenyewe watakopa, watajenga nyumba na kuuza. Sasa watakuwa ni wajenzi wa nyumba na kuuza wataondokana na jukumu lile la kupangisha.

Hizi nyumba wanazozipangisha karibu nyingi wataziuza. Hawatauza zote, lakini nyingi watauza watabakiza chache ili wazitumie hizo kama dhamana kule benki maana yake wakiuza zote watakosa kitu cha kuweka dhamana benki.

Kwa hiyo, *Nationa Housing* nyumba nyingi watawauzia Watanzania ili wao waingie katika biashara ya kujenga na kuuza.

Na 140

**Miradi ya Umwagiliaji – Manyoni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Manyoni ina miradi saba mikubwa ya umwagiliaji ambayo ni Uwakala Kijiji cha Lusilile, Udimaa Kata ya Kitinku, Nyamagogo Kata ya Chikuyu, Mtiwe Kata ya Chikuyu, Msemembo Kata ya Makulu, Saranda Kata ya makulu na Ngaiti Kata ya Mvumi; na kwa k uwa, miradi hiyo hufanya kazi wakati wa masika tu kwa sababu ya ukosefu wa mabwawa na kusababisha uzalishaji kuwa duni.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kuwa ni fedha kiasi gani kilitumika katika miradi hiyo?

(b) Je, Serikali itapeleka lini fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ili kutokukwamisha miradi hiyo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Skimu za Umwagiliaji za Lusilile, Udimaa, Nyamagogo, Mtiwe, Msemembo, Saranda na Ngaiti katika Wilaya ya Manyoni zilijengwa na Serikali kupitia *Program* Shirikishi ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji *(PIDP)* iliyoanza mwaka 2000 hadi 2006.

*Program* ililenga maeneo kame ya Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Tabora, Mwanza na Manyara ikitumia teknolojia ya uvunaji maji ya mvua hasa kwa ajili ya zao la Mpunga.

Miradi hii ilijengwa kwa kuzingatia dhana ya kufanya kazi wakati wa mvua kwa kukinga maji katika mito ya masika (*seasonal rivers*) na kuyachepusha katika majaluba hata kama mvua haikunyesha katika eneo husika la mradi. Kwa mfano, mara nyingi skimu zilizo katika Wilaya ya Manyoni zinapata maji yanayoletwa na Mto Bubu wenye chanzo katika mlima wa Hanang. Hii ni aina ya umwagiliaji katika mazingira ya maeneo yasiyo na mito inayotiririka wakati wote (*perennial rivers*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali ilitumia jumla ya Shilingi 1,411,333,675/= kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo yenye jumla ya hekta 1,125 ili kulima zao la Mpunga na kunufaisha jumla ya wakulima 1,716.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga mabwawa katika Mikoa kame ili kvuna maji ya kuongeza uwezekano wa kuendelea na kilimo hata wakati mvua zinapokatika. Katika mwaka wa 2002, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa kushirikiana na Wahandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ilifanya usanifu wa mabwawa

katika skimu za Umwagiliaji wa Lusilile, Saranda na Msemembo. Lakini kwa wakati huo fedha za utekelezaji hazikuweza kupatikana kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Kinachotakiwa ni kufanyika sasa ni kufuata utaratibu wa kuomba fedha za ujenzi wa mabwawa hayo kwa kuyaingiza katika *Program* ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Manyoni na kuyaombea fedha za utekelezaji kutoka katika *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambayo inaendelea. Wilaya ya Bahi ni mfano mzuri wa kuigwa kwa sababu wamefuata utaratibu kwa kushauriwa na Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kati. Wamepata jumla ya shilingi bilioni 1.9 katika mwaka wa 2007/2008.

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inashauriwa kufuata utaratibu huo kuomba wa fedha za ujenzi wa mabwawa kwa kuwa, usanifu wa mabwawa hayo umekamilika na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo bado inaendelea hadi mwaka 2013.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa, wakulima hawa wa Skimu hizo zote tano wanamsumbua sana Mbunge wa Jimbo hilo ingawa yeye kafungwa mdomo hapa hata na mimi pia kwenye ziara zangu. Kwa kuwa Serikali imetambua kabisa kwamba Skimu hizi zingeweza kufanya kazi nzuri hata wakati wa kiangazi.

Je, kwa kuwa utaratibu aliouleza hapa unasuasua Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna kila sababu ya kutafuta uwezekano mwingine ili mabwaya yajengwe yaweze kutunza maji haya ya masika ambayo ni mengi yanapotea bure ili wakulima hawa waweze kufanya kazi ya umwagiliaji wakati wa kiangazi ili kuzalisha vipato vyao kwa njia ya kilimo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ni mzuri na unatekelezeka ninachoweza kusaidia au kusema si kusaidia ni wajibu wangu ni kwamba nitawatuma wataalam wa umwagiliaji wa Kanda ya Kati waende Wilaya ya Manyoni wajaribu kushauriana na Halmashauri ili kuharakisha utekelezaji wa miradi inayokusudiwa. (*Makofi*)

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo la maji Manyoni na sehemu nyingine za Tanzania limeendelea kuwa kubwa sana na linahitaji mkakati wa lazima na wa makusudi wa kitaifa. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie hapa kama Serikali ina mkakati gani katika Bajeti inayokuja kuhusu fedha zaidi kwa ajili ya kukwamua matatizo ya maji kwa sababu mfuko wa Benki ya Dunia kwa kadri ninavyofahamu mimi umekwama?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, kama ifuatavyo:-

Naomba kuthibitisha kwamba Serikali ina mkakati na ni mkakati wa kitaifa wa maendeleo ya Sekta ya Maji. Jana nilipata nafasi ya kutoa kauli kwa niaba ya Serikali na nilielezea kwa kirefu nini tunafanya hasa kuhusu suala la maji vijijini.

Napenda vilevile kusema kwamba fedha tunazopata za kutekeleza mpango wa mpango wa maji kitaifa ni mfuko wa pamoja yaani *Basket Fund* ambao Serikali yetu inachangia lakini vile vile washirika wetu wa Maendeleo wanachangia.

Napenda tu kusema kwamba fedha za Benki ya Dunia hazijakwama isipokuwa zina urasimu na jana niliahidi kwamba tutafanya kazi kama Serikali kujaribu kuondoa huo urasimu ili miradi itekelezwe kwa haraka.

Lakini niseme vilevile kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amelihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maji kama Sekta itapewa kipaumbele katika Bajeti ya mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tuna Mzee wetu *Senior MP* hawa wanaitwa Ma- *Senetor* katika Mabunge mengine. Swali la nyongeza Mheshimiwa John Samwel Malecela!

**MHE. JOHN SAMWEL MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikushukuru sana kwa kuniona ingawaje nimesimama mwisho mwisho.

Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri baada ya majibu yake safi ambayo amejibu kwenye Bunge hili. Tunazo Wilaya katika nchi yetu ambazo zinajulikana wazi kabisa kwamba zina matatizo ya maji mwaka hadi mwaka. Kwa mfano wilaya ya Newala, Wilaya ya Dodoma, Wilaya ya Singida, Wilaya ya Arusha na kadhalika.

Sasa kama kweli Serikali inasema kwamba suala hili la maji litatiliwa mkazo. Je, Waziri haoni umuhimu wa kwamba angalau tuanze na hizi Wilaya ambazo zimekuwa na matatizo tangu kale mpaka sasa tumalize halafu ndiyo tuende mahali pengone? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mh! Hili swali gumu yaani mathalani kama Urambo tusubiri tu! Mheshimiwa Waziri Majibu tafadhali! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Samweli Malecela Mzee wetu Malecela, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo;

Moja ya vigezo vya kutuma fedha katika maeneo mbalimbali nchini kwetu ni ukubwa wa tatizo la maji. Kwa hiyo, hili tunalizingatia katika kupeleka raslimali katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni pamoja nakupeleka raslimali za fedha Newala, Dodoma, Singida hata Mwanga.

Mheshimiwa John Samwel Malecela anaweza kushangaa kwamba pamoja na mito mingi iliyoko katika Wilaya ya Rungwe na maji yanayotiririka kutoka kila mahali lakini ni 46% tu ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe wanaopata maji safi na salama. Kwa hiyo, nao wamo katika hicho kipaumbele pamoja na wananchi wa Urambo. *(Makofi)*

Tukisema tuwaache wananchi wote tumalize kwanza haya matatizo ya maeneo kame basi kwa sababu maji ni uhai tunaweza kukuta sehemu nyingine watu hawapo wakati tunaendelea kutekeleza miradi ya maji katika maeneo ambayo yana matatizo.

Kwa hiyo, tutajaribu kuangalia uwezekano wa kukitumia hasa kigezo hiki cha kuangalia tatizo lenyewe ili tupeleke raslimali zaidi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Bado Wizara hiyo hiyo swali sasa linaulizwa na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido.

Na. 141

**Mradi wa Bwawa la Umwagiliaji la Kiseria**

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2005 Serikali ilichimba Bwawa la umwagiliaji katika kijiji cha Kiseria ambalo lilitumia fedha nyingi sana na kwamba mradi huo haujakamilika hadi sasa.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi huo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ya Kilimo na Chakula kupitia Kituo cha Umwagiliaji na Huduma za Ufundi cha Kanda ya Kilimanjaro, ilifanya uchunguzi wa Kitaalam ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Kiserian kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji wa matumizi ya watu, kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

Uchunguzi huo ulifuatiwa na ujenzi wa Bwawa ambalo ulianza mwezi Julai, 2005 na kukamilika Mei, 2006 ukitekelezwa na wataalam kutoka katika Kituo cha Umwagiliaji na Huduma za Ufundi, Kanda ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi huo wa Bwawa, kazi zifuatazo zilitekelezwa na kukamilishwa.

1. Ujenzi wa tuta la Bwawa;

2. Ujenzi wa kitorosha maji (*spillway*);

3. Ujenzi wa maumbo ya kutolea maji (*draw – off structure or intake and outlet structure*);

4. Ujenzi wa Birika kwa ajili ya kunyweshea mifugo (*cattle trough*); na

5. Ujenzi wa kituo cha bomba la maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Bwawa hilo sasa limekamilika na linahifadhi maji kwa kiasi mvua zinaponyesha. Hata hivyo, kazi ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo lote la Bwawa iliyokuwa inafanywa na Halmashauri ya Wilaya haikuweza kufanyika. Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji ulikuwa utekelezwe katika awamu ya pili baada ya Bwawa kukamilika.

Bwawa la Kiserian limejengwa kufuatia ombi la wananchi wa Kijiji cha Kiserian kupitia kwa Mbunge wao Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* kuanza, utaratibu uliopo sasa wa kuomba fedha za miradi ya umwagiliaji ulianzia katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPS).* Miradi ambayo haipitishwi na Halmashauri ya Wilaya haiwezi kujadiliwa na kuombewa fedha za nyongeza kutoka katika mifuko ya *ASDP* ya Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani (*District Irrigation Development Fund*) *(DIDF)* au Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Developement Fund*) *(NIDF).* Wataalam wa Wizara yangu kutoka Kituo cha Umwagiliaji cha Kanda ya Kilimanjaro wameishauri Halmashauri ya Wilaya kutoka Kituo cha Umwagiliaji cha Kanda ya Kilimanjaro wameishauri Halmashauri ya Wilaya ya Longido iweke mradi huu katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DASPs)* na hatimaye kuuombea fedha toka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani *(DIDF)* ili utengewe fedha na kutelezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mradi huu wa Kiserian Wizara yangu imeanza kutekeleza mradi wa Bwawa la Ingodini tayari Wizara imesaini kandarasi ya ujenzi na kampuni ya *MS Alan Ltd* ya Dar es Salaam tarehe 28 Januari, 2009. Ujenzi wa Bwawa utachukua wiki 18 kuanzia tarehe ya mkataba na utagharimu shilingi milioni 606,791,040,000/=.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kukamilisha kazi zilizobaki hususan ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, halmashauri ya Wilaya ya Longido inashauriwa tena

kufuata utaratibu uliopo wa kuomba fedha za kutekeleza miradi ya umwagilaji kwa pamoja na wananchi wa kijiji cha Kiserian kuibua mradi huu na kuingiza katika Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo *(DADPs).*

Hatua hii itawezesha kuomba fedha za nyongeza kutoka katika mifuko ya kitaifa niliyoitaja. Katika kufanya hivyo, Halmashauri inaweza kuwatumia Watalaam wa Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kilimanjaro katika kuandaa miradi itakayoombewa fedha za utekelezaji.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri yenye matumaini na faida kwa wananchi wa Longido napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Bwawa hilo lilipochimbwa wameacha udongo mwingi sana yaani kifusi ndani ya Bwawa ambalo linazuia Bwawa kuwa na maji mengi. Je, Waziri atakubaliana nami hicho kifusi kiondolewe ili kuweza kuruhusu maji mengi katika Bwawa hilo?

Pili, kwa kuwa mradi ule ni mkubwa sana na bado Wizara haijakabidhi Halmashauri si ingependeza sasa baada ya kumalizika Wizara ikabidhi Halmashauri ili uendeshaji uwe mikononi mwa Halmashauri kwa sasa?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kiserian lina matatizo ya kidogo ya ufundi mojawapo ni kwamba maji hupotea yaani Bwawa halitunzi maji kwa muda mrefu. Tunajaribu kuangalia tatizo ni nini, inawezekana tatizo ni udongo maji yanapotea chini ya ardhi lakini tatizo lingine ni kwamba liko katika eneo la jua kali. Kwa hiyo, maji hupotea kama mvuke. Lakini tutaangalia pamoja na hayo matatizo ya kiufundi nini kinaweza kufanyika pamoja na hilo alilolisema la kuondoa kifusi. Naomba hayo tuyazungumzie katika ushauri tulioutoa wa sehemu ya pili ya mradi.

Kuhusu Wizara kukabidhi mradi naomba kuthibitisha hapa kwamba itakuwa furaha kubwa kwetu kukabidhi mradi wakati wowote ule kwa sababu kwa kweli huu ni mradi wa wananchi wa Longido na tutafanya mipango tukabidhi lakini hatutaondoka moja kwa moja tutashirikiana na Halmashauri ya Longido katika hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita R. Kawawa, samahani sana nimekuona, si rahisi sana kukuona lakini leo ni vizuri sana nimekuona . (*Kicheko*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ufupi wangu kwa kweli mara kwa mara unakuwa hunioni lakini nakushuru leo umeniona vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii naomba nami niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imetekeleza kwa kiasi kikubwa ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 katika ujenzi wa vibanio na mifereji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwenye miradi ya Mgumbasi, Nambecha, Mchomoro, Msindo, Kitanda, Msanjesi, Liuni, Namaoka, Amani na mingine inayoendelea.

Je, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wanaweza kuja kuitembelea baadhi ya miradi hiyo na kupata mawazo ya wananchi wanaolima maeneo hayo na kuona jinsi gani Serikali itakavyoweza kuendelea kutusaidia?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Miradi aliyoitaja ni mingi na inaonyesha juhudi za Serikali katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini.

Nathibitisha kwamba majaaliwa tukipata afya njema ni nia yangu kutembelea Namtumbo kukagua miradi aliyoitaja Mheshimiwa Vita Kawawa. (*Makofi*)

Na. 142

**Ugawaji wa Dawa kwa Kutumia Indent System**

**MHE. HASNAIN GULAMABAS DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugawaji wa dawa unaofanywa na *MSD* kwa kutumia *Indent System* unachelewesha sana ufikishaji wa dawa hizo katika hospitali, vituo vya afya na zahanati katika Wilaya ya Kilwa.

Je, kwa nini Serikali isirekebishe mfumo huo ili dawa hizo zisichelewe kufikishwa sehemu husika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI NA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mbunge Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mfumo wa uagizaji dawa katika Wilaya ya Kilwa kwa sasa ule ujulikanao kama *Integrated Logistics System (ILS)* na siyo *Indent System*. Huu ni mfumo wa uagizaji dawa na vifaa kulingana na mahitaji na mgao wa fedha. Zahanati na Vituo vya Afya katika Wilaya hiyo huandaa mahitaji yake ya dawa na vifaa tiba na kuagiza kutoka Bohari ya Dawa, Kanda ya Mtwara.

Mfumo huo umechukua nafasi ya mfumo wa zamani uliojulikana kama *Kit System* ambapo zahanati na Vituo vya Afya vilikuwa vinapelekewa dawa kila mwezi bila kujali mahitaji yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Wilaya ya Kilwa ilikuwa na Zahanati 40, vituo vya afya 5 na Hospitali ya Wilaya moja. Katika kipindi hicho, *MSD* ilipokea maombi ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba kutoka katika zahanati na vituo vya afya 36 mara tatu; yaani Januari, Aprili na Oktoba. Aidha, vituo vitatu vilipeleka *MSD* maombi ya mahitaji yake mara moja tu na vituo sita havikuwasilisha kabisa maombi ya mahitaji ya dawa na vifaa.

Kwa utaratibu, Mganga Mkuu wa Wilaya anatakiwa kuhakikisha kwamba vituo vyote vilivyopo chini yake vinaagiza mahitaji yake ya dawa na vifaa tiba kwa wakati. Aidha kwa kuwa ndiye anayezipokea kutoka *MSD* anatakiwa kuhakikisha kuwa dawa hizo zinawasilishwa kwenye vituo husika kwa wakati na muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ucheleweshwaji wa usambazaji wa dawa katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati katika Wilaya ya Kilwa hausababishwi na mfumo wa *Integrated Logistics System* bali kasoro za kiutendaji za watendaji wanaosimamia utoaji wa huduma katika Wilaya hiyo. Hivyo basi, kwa sasa Serikali bado haijaona ulazima wa kufanya marekebisho ya mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Kilwa kuweka utaratibu wa kufutilia kwa karibu utoaji wa huduma za afya katika Wilaya hiyo ili kupunguza kero ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba hususan katika zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN GULAMABAS DEWJI:**Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hali ni mbaya sana katika vituo vya afya Pande, Mandawa na Nanjilinji wakati nilipokuwa natembelea kwenye vituo hivyo hali ilikuwa ni mbaya sana na hakuna dawa hata kidogo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataniambia nini kuhusu uzembe wa *MSD* unaofanywa na *MSD* kuzikalia pesa za Halmashauri bila kuwataarifu mapema, uzembe huo unasababisha vituo vyetu kukosa dawa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI NA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba utaratibu ni Wilaya husika iweze kupeleka maombi yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini si kweli kwamba *MSD* huwa inakalia pesa zile na haiwapatii katika sehemu zile ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge. Ninachotaka kusema ni kwamba hata kama *MSD* itaonekana kwamba dawa hakuna lakini bado kuna maelekezo ambayo Halmashauri imepewa kutumia pesa ambao wanazo katika Halmashauri kuweza kununua dawa katika vyanzo vingine na katika maduka binafsi.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba bado nasisitiza kwamba wakati Wilaya ya Kilwa inatakiwa kupeleka mahitaji yake kwa wakati ili iweze kupata dawa kutoka *MSD* lakini inapotokea kwamba zile dawa hazijapatikana bado wana uwezo ambao wamepewa kisheria kuweza kununua dawa katika maduka binafsi. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, sasa hivi Serikali ina utaratibu mzuri sana wa kabisa wa kwamba vifaa vilivyokuwa havina *standard* wanaviharibu yaani wanavi- *destroy*. Sasa hivi *Central Medical Store* unanunua *BP Machine* haifiki hata mwezi imeshakufa unajikuta baadhi ya hospitali wanakuwa na *BP Machine* moja kwa ku-*share* kwa sababu nyingine zimeharibika. Kwa mfano Hospitali ya Tumbi, Kibaha, Mkoa wa Pwani.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kwa hivi vifaa ambavyo havina *standard* na vinaharibika hara kaharaka vinavyoagizwa na *Central Medical Store (MSD)?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI NA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumetokea malalamiko kwamba baadhi ya vifaa vinavyonunuliwa na *MSD* vinakuwa havina ubora.

Kazi ya *MSD* ni kuhakikisha kwamba inanunua, kusambaza na kusimamimia ununuzi wa vifaa vyenye ubora. Sasa inapotokea kwamba vifaa vinapopelekwa kutoka *MSD* ni vibovu ushauri kwamba inatakiwa mara moja maeneo husika ambayo yamepokea vifaa hivyo wavirudishe kule *MSD* ili waweze kutoa hiyo ripoti na kuvirudisha hivyo vifaa ili iweze kuonekana ni kwa sababu gani vifaa hivyo vimeonekana ni vibovu na sisi wakati huo tutachukua hatua kupitia kule *MSD.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Mbunge katika sehemu ya Tumbi na sehemu nyingine zozote ambazo zimepokea vifaa vibovu kutoka *MSD* basi mara moja watoe taarifa ili Serikali iweze kuchukua hatua inavyostahiki.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, *MSD* inahusika na ununuzi wa vifaa tiba, ningependa kujua Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze.

Je, vitanda vya wazazi ambavyo hivi sasa havipatikani katika baadhi ya zahanati na vituo vya Afya. Je, ni lina vitanda hivyo vitapatikana ili kuondoa tatizo kubwa la wazazi kujifungua katika vitanda vya mbao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli *MSD* inashughulika na ununuzi wa vifaa tiba vikiwemo vitanda vya akinamama vya kujifungulia. Kawaida vitanda vinapatikana *MSD* na ndiyo maana tunasema eneo husika linatakiwa liainishe mahitaji yake na kupeleka *order* zao *MSD,* na kama wakati huo itakapokuwa *MSD* havipatikani, basi ndiyo pale wanaweza wakaenda katika maduka yale ambayo ni ya *private*.

Kwa hiyo, katika maeneo yale ambapo vitanda vya kujifungulia havipo si busara kumzalisha mama mjamzito katika kitanda cha mbao kwa sababu kwa vyovyote vile hata yule muuguzi anayemfanyia huduma ya kujifungua itakuwa ni tabu kumzalisha katika kitanda ambacho hakistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa wote na kwa wale wote ambao wanatoa huduma wahakikishe kwamba zahanati na vituo vya afya na hospitali zinanunua vitanda vya kuzalishia akinamana katika Bajeti walizonazo, na wale ma-*DMO* waliopo katika hospitali zao na maeneo yao wafanye ukaguzi kuhakikisha kwamba vitanda vinapatikana na mahali popote watakapoona wanawazalishia akinamama katika vitanda vya mbao kwa kweli si sahihi. Kwa hiyo, wale tutawachukulia hatua, na sisi kama Wizara tutafuatilia.

Na. 143

**Ukarabati na Uanzishwaji wa Chuo cha Ufundi cha Walemavu**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mwaka 2008/2009 Serikali imetenga shilingi 132,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Wasioona Mtapika ili kianzishwe Chuo cha Ufundi cha Walemavu:

(a) Je, ukarabati huo unatarajiwa kuanza na kukamilika lini?

(b) Je, ni fani zipi zinatarajiwa kutolewa na Chuo hicho na kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wangapi kwa mwaka?

(c) Je, mafunzo yatakuwa yanatolewa kwa muda gani na ni gharama kiasi gani zinatumika katika kuandaa vifaa vya kufundishia na malazi kwa jumla?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara iko katika mchakato wa kumtafuta mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Chuo cha Ufundi cha watu wenye ulemavu Mtapika Masasi. Ni matarajio yetu kuwa mradi huu unaweza kukamilika mwaka 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya kufungwa, Chuo cha Mtapika kilikuwa kinatoa mafunzo ya useremala kwa watu wasioona. Baada ya kukamilika kwa mradi wa ukarabati Chuo kitaongeza idadi ya wanafunzo kwa kuchukua watu wasioona pamoja na watu wenye ulemavu wa aina nyingine. Chuo kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 kwa mwaka. Aidha, fani zinazotarajiwa kufundishwa kwa watu wenye ulemavu katika chuo hicho ni Useketaji, Useremala, Umeme, Ushonaji Nguo, Kilimo cha Bustani na Brela.

(c) Mheshimiwa Spika, baadhi ya fani zitafundishwa kwa muda wa mwaka mmoja na nyingine kwa miaka miwili kwa kutegema mtaala wa fani husika. Vifaa vya kufundishia fani ya useremala vipo na bado vitaendelea kutumika. Aidha, tathmini ya gharama za vifaa vya nyongeza kwa ajili ya fani mpya zitkazoongezeka itafanyika mara baada ya kukamilika kwa mradi wa ukarabati.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amesema kwamba Wizara ipo katika mchakato wa kutafuta mkandarasi.

Je, Wizara haioni kwamba hii kazi ya kumtafuta Mkandarasi wangeiachia Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili kuweza kuharakisha kumpata mkandarasi na pale zitakapopatikana fedha wakaingiza katika Halmashauri hii ya Wilaya ya Masasi ili waweze kusimamia na kuharakisha ukarabati wa majengo hayo ili Chuo kiweze kufunguliwa?

La pili, kwa kuwa walemavu walio wengi wamekuwa wakiikosa elimu ya sekondari.

Je, Wizara hii ya Afya haiwezi ikafanya mazungumzo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili majengo hayo yatakapokuwa tayari wakafungua sekondari ya ufundi ambayo itachukua walemavu ili waweze kupata elimu ya sekondari na ufundi ili watakapotoka hapo na wao waweze kupata ajira na kujiajiri wao wenyewe wakiwa na elimu ya kutosha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuhusu kutafuta mkandarasi kwamba kazi iachwe Halmashauri ya Wilaya Masasi. Sasa hivi Ustawi wa Jamii upo Wizara ya Afya ni kwamba sisi kama Wizara tunacho kitengo cha majengo ambacho kipo kule Makao Makuu. Lakini vile vile Ustawi wa Jamii bahati mbaya haina kitengo cha Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya. Wazo lake ni nzuri, nafikiri na sisi kama Wizara huwa tunafikiria kwamba sasa hivi ni wakati umefika ili tuweze kupeleka Afisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri ili kuweza kuhakikisha kwamba haya masuala ya ustawi yanashughulikiwa katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa maana hiyo, bado lakini hii haizuii kama Wizara kushirikiana na Halmashauri ili kuhakikisha kwamba mkandarasi anayepatikana ni yule anayetoka pale Masasi ili aweze kutoa huduma hizo. Kwa hiyo, huu ushauri tunauchukua.

La pili, Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa walemavu wengi wanakosa elimu ya sekondari na kwamba kile chuo cha Mtapika kama tutakifanya kiwe shule ya sekondari ya ufundi ili wale walemavu waweze kupata elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi katika eneo lile. Hili ni wazo nzuri, hata hivyo sasa hivi hiki chuo cha Mtapika kwanza watu wenyewe wa kule Masasi wanatumia majengo ya kile chuo kwa madarasa ya sekondari. Kwa hiyo, tumewaazimia. Kwa hiyo, bado mimi naona siyo vibaya ili kama itawezekana tutakapomaliza yale majengo tuifanya iwe shule ya sekondari kwa sababu naamini ni kweli kwamba elimu ya sekondari hasa kwa walemavu inakosekana.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningependa tu niseme kwamba siyo lazima kwamba kile Chuo cha Mtapika basi tukifanye iwe shule ya sekondari kwa sababu ya walemavu, tunataka elimu hii ya sekondari itolewe shirikishi kwamba watu wote wenye ulemavu siyo lazima tu wapelekwe Masasi.

Kwa maana wanaweza wakapata elimu hii ya sekondari katika maeneo yanayohusika katika Mikoa mingine yenyewe shule za sekondari. Kwa hiyo, elimu ya sekondari siyo lazima itengewe eneo lake husika wote wanaweza wakapata elimu ya

sekondari katika shule zetu za sekondari ambazo zipo katika Kata na kwenye maeneo mengine. Ahsante sana.

**SPIKA:** Swali fupi la nyongeza na majibu pia naomba yawe mafupi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Chuo cha Wasioona kilichopo Singida Mjini kinafanana kabisa na Chuo hiki cha kwenye swali la msingi; na kwa kuwa Serikali ilikwishatenga fedha kupitia Bajeti ya mwaka 2008/2009 kukarabati chuo hicho ambacho kina hali mbaya sana, majengo yake yamechakaa na yamepasuka mpaka sasa hivi kuna bweni wanachuo hao hawakai tena kwa sababu ni vipofu tunaogopa linaweza likaanguka wakapondwa na wao hawaoni.

Je, Serikali ina tatizo gani sasa kuzitoa zile fedha ili ziweze kukarabati hicho chuo ili kuwanusuru hao wanachuo wasioona?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kule Singida kuna Chuo cha Wasioona na kwamba tulikuwa tumekitengea fedha katika Bajeti yetu na tulikuwa tumeahidi kwamba tungekifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Spika, tunachosubiri sasa hivi ni kupatikana kwa zile fedha tumezitenga katika Bajeti, lakini hela itakapokuwa tayari tutaendelea na ule ukarabati.

Na. 144

**Tanzania Education Authority (TEA)**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, madhumuni ya Kuanzishwa kwa Mfuko wa Elimu *(TEA)* ni kufanya mabadiliko katika Sekta ya Elimu kwa uchangisha fedha kwa ajili ya Mfuko huo ambao utatoa fedha hizo kwa vyuo na shule mbalimbali nchini:-

(a) Je, ni nini uwiano wa mgao wa fedha hizo kati ya Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ufundi *(VETA)*, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Msingi na Vyuo vya Ualimu?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha za mfuko huo kilipatikana katika vipindi vya mwaka 2007/2008 na 2008/2009?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha katika fedha hizo zilizopatikana kwenye sehemu ya (b) ya swali ziligawanywa kwenye Vyuo vya Ufundi yaani Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT)*, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia *(MIST)* na Chuo cha Ufundi Arusha *(TCA)?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Vyuo vya Elimu ya Ufundi vilivyo chini ya *VETA* si sehemu ya wanufaika wa fedha za Mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania kwani mafunzo hayo hugharimiwa na "*Skill Development Levy*" chini ya Sheria ya Bunge Na. 1 ya mwaka 1994. Tangu mwaka 2001 Taasisi za Elimu zilikuwa zinapewa mgao wa fedha kulingana na maombi ya Taasisi husika na kwa kufuata vigezo vilivyowekwa na Mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania. Hadi Juni 2008 jumla ya miradi ya elimu 861 ilifadhiliwa na Mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa thamani ya shilingi bilioni 27,986,442,993/=. Hata hivyo kuanzia mwaka 2008/2009 Mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania umeweka mwongozo wa mgao wa fedha za ufadhili kutoka kwenye Mfuko wa Elimu kwa kufuata uwiano ufuatao:-

Vyuo Vikuu vinatengewa mgao wa asilimia 40, Vyuo vya Ufundi asilimia 30; Vyuo vya Ualimu asilimia 5; shule za sekondari asilimia 20 na shule za msingi na awali asilimia 5.

(b) Mheshimiwa Spika, katika vipindi vya mwaka wa fedha 2007/08 na 2008/2009 kiasi cha fedha za Mfuko wa Elimu kilichopatikana ni shilingi bilioni 5,691,806,493/= na kwa kipindi cha nusu mwaka hadi kufika tarehe 31 Desema, 2008 (mwaka wa fedha 2008/09 ni shilingi bilioni3,269,695,677.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 fedha kiasi cha shilingi milioni 18,610,000/= zilipelekwa Chuo cha Ufundi Arusha na shilingi milioni 380,560,764 zilipelekwa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Chuo cha Ufundi Mbeya hakikupata mgao wa fedha katika kipindi hicho.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kina na mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa, sera ya Sayansi na Teknolojia pamoja na ile Sera ya Elimu ya Ufundi za mwaka 1996 zinaelekeza kuongeza idadi ya Wahandisi, *technicians* na *Craftsman* kutoka uwiano uliopo wa sasa wa Mhandisi mmoja kuwa na *technicians* wawili na *craftsman* 14 kwenda Mhandisi mmoja kuwa na *technicians* watatu na *craftsman* 18; na kwa kuwa uwezekaji katika sekta hii unahitaji fedha nyingi na kubwa.

Je, Serikali itakuwa tayari kupitia upya uwiano huo ili kuongeza fedha katika sekta hii ya ufundi ambapo wahitimu wa Vyuo hivi wanapomaliza wanakuwa na uwezo wa kutengeneza vitu na hivyo kurahisisha kujiajiri?

(b)Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaeleza ni sababu zipi zilizopelekea Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kutopata mgao wa fedha mwaka 2007/2008?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana mafunzo ya ufundi ya Sayansi na Teknolojia naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi tunaandaa mtaala mpya ambao utawezesha kumfanya mwanafunzi anayeanza kusoma katika *Certificate level one* na *level two* awe darasa la saba au *form four* kuweza ku-*upgrade* hadi kufikia kupata digrii.

Huu ni mtaala mzuri sana ambao utatuwezesha kupata uwiano aliouzungumza Mahenge, kuna taasisi pamoja na zile ambazo zinamilikiwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambazo zinaanzishwa zote hizo zitakuwa katika mchakato mzima wa kuhakikisha kwamba tuna technicians wa kutosha na pia tuna Wahandisi wa kutosha. Kwa hiyo, Serikali hili inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hili la kuhusu Taasisi ya Mbeya ni kwamba hatutoi fedha bila kuombwa na bila kuletewa maombi na kuonyesha kwamba wana *project* ambayo inataka kufanyika.

Kwa hiyo, Taasisi ya Mbeya haijaomba fedha kule Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Na. 145

**Somo la Usafi wa Mazingira Mashuleni**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la usafi wa mazingira linaendelea kuwa tatizo kubwa katika Taasisi mbalimbali:-

Je, ni kwa nini somo la usafi wa mazingira lisifundishwe kuanzia shule za msingi ili Watanzania wengi wazoee tabia ya usafi tangu utotoni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum Mbeya, kama ifuatavyo:-

Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 inasisitiza upokeaji wa mada za elimu ya mazingira katika mitaala yote ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Kwa kuzingatia umuhimu huu, mabadiliko ya mitaala ya mwaka 1996 na 2005 yamezingatia uchopekaji wa mada za elimu ya mazingira katika mihtasari ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Vilevile baadhi ya kozi za Elimu ya Watu Wazima zinahusisha elimu ya mazingira.

Somo la usafi wa mazingira hufundishwa katika masomo ya Sayansi, Haiba na Michezo Elimu ya viumbe, jiografia na Stadi za Kazi. Hivyo, vipengele vya elimu ya usafi wa mazingira vinafundishwa katika masomo mengi kama suala la mtambuka, na si somo linalojitegemea. Aidha, vyuo vikuu pia vinatoa Shahada za Elimu ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya mazingira kwa jamii, imefanikiwa kuchopeka mada husika katika ngazi zote za elimu kuanzia elimu ya awali hadi ya chuo Kikuu.

Aidha, napenda kutoa wito kwa viongozi wa ngazi mbalimbali, mkiwemo Waheshimiwa Wabunge, kila mtu kwa nafasi yake, kuhimiza elimu ya usafi wa mazingira ili kutatua tatizo la uchafuzi wa mazingira lililopo nchini. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa shule ikiwa ni pamoja na wanafunzi, walimu pamoja na mazingira yake ni lazima viwe mfano wa usafi katika jamii. Je, Naibu Waziri anachukua hatua gani kwa zile shule za msingi na sekondari ambazo hazina vyoo vya kudumu au hazina vyoo kabisa?

La pili, wakati wa miaka ya nyuma na tabia nzuri sana ambapo shule zilikuwa zinafuatiliwa kwa kufanya ukaguzi wa mwili wa mwanafunzi kila siku ikiwa ni pamoja na kucha, nywele, meno na kadhalika pamoja na mandhari yake hivi sasa tabia hiyo haipo kabisa. Je, Naibu Waziri yupo tayari sasa kuzielekeze shule zote nchini zirudishe tena tabia ile ambayo ilikuwa nzuri inajenga tabia ya usafi kwa mtoto hadi anapokuwa mtu mzima? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, shule za msingi na za sekondari katika moja ya vigezo ambavyo zinasababisha zipate usajili ni kuwa na vyoo, tena vyoo kwa idadi ya wanafunzi inayostahili. Endapo Mwenyekiti wa *NEMC* anakiri kwamba zipo shule hazina vyoo, nitaagiza wakaguzi wangu wakazifunge mara moja, maana wamekiuka kanuni na masharti ya ufunguaji shule.

Naomba nimweleze Mheshimiwa Hilda Ngoye ukaguzi wa afya za wanafunzi na mavazi yao unafanyika, ndiyo maana tumepiga marufuku kule shuleni wanafunzi wasifunge kucha ndefu wakifunga wanaambiwa wakate, wakikataa wanarudishwa maana hiyo ni stahili ya mtu ambaye anajitegemea na mambo mengine mengi. Kwa ufupi

niseme ukaguzi ule unaendelea pale ambapo unalegalega naomba wote wanaonisikia katika uongozi wa shule za msingi na sekondari, basi waone umuhimu wa kurudia kukagua wanafunzi maana vinginevyo tutakuwa hatuwalei katika maadili na usafi unaostahili kimazingira.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea tuzingatie muda. *(Makofi)*

Na. 146

**Ufutaji wa *Prospecting/Mining License* Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mgodi wa Geita *Gold Mine Limited* una leseni ya *Special Mining Licence (SML)* ambayo imechukua eneo kubwa, lakini kwa sasa eneo linalozunguka leseni hiyo ambalo nalo kampuni hiyo imejilimbikizia kwa kukata *Prospecting Mining Licence (PML)* na kuwazuia wachimbaji wadogo wadogo kuchimba kwenye maeneo hayo:-

Je, Serikali iko tayari kufuata *'PML'* hizo ili wachimbaji wadogo wadogo wapewe?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa dhahabu wa Geita una leseni ya uchimbaji madini *SML 45/1999* iliyotowa mwaka 1999. Leseni hiyo ina ukubwa wa kilometa za mraba 196.25. Aidha, leseni imezungukwa na leseni za utafutaji madini yaani *Prospecting Licence* na siyo *Prospecting Mining Licence* kama ambaya Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza kwenye swali. Vile vile kuna maombi kadhaa ya leseni za utafutaji madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998, Serikali haiwezi kutafuta leseni iliyotolewa kihalali kwa lengo la kuwapatia wachimbaji wadogo wa madini eneo la kuchimba madini. Leseni ya mtafutaji au mchimbaji yeyote wa madini, mkubwa au mdogo, inaweza kufutwa endapo tu kuna ukiukwaji wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama Sera ya Madini na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inavyoainisha kuhusu suala la kuwasaidia wachimbaji wadogo, Wizara yangu imeandaa mikakati mbalimbali ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo

wa madini hapa nchini. Mojawapo ya mikakati hiyo ni utengaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni kama vile ambavyo niliainisha jana wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru Mbunge wa Tarime kuwa ni maeneo ni Kilindi, Morogoro na Kilosa yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 2,698.42 ambapo yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali *GN no.359* ya tarehe 26/7/2002, Maganzo lenye jumla ya kilomita za mraba 148.7 lililotangazwa kwenye Gazeti la Serikali *GN No.528* la tarehe 3 Desemba, 2004 na Mererani lenye jumla ya kilomita za mraba 104.9 lililotangaza kwenye Gazeti la Serikalil *GN No. 120* ya tarehe 8 Septemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini kuwa maeneo mengi yako chini ya leseni kubwa, hali ambayo inasababisha wachimbaji wadogo kukosa maeneo ya kuchimba madini, Serikali ilianzisha utaratibu wa kuzungumza na kampuni zenye leseni za utafutaji mkubwa wa madini ili ziachie kisheria maeneo ambayo kampuni zimeshayafanyia utafutaji wa madini wa kina na kubaini kuwa haziwezi kuendesha uchimbaji wa madini kwa faida lakini wachimbaji wadogo wanaweza kuchimba madini hayo na kujiongezea kipato. Hivyo, kila inapobainika kuwa kuna maeneo ambayo kampuni zenye leseni kubwa haziwezi kuchimba madini kwa faida, Serikali imekuwa ikifanya mazungumzo na kampuni husika kuwaomba waachie maeneo hayo ili yaweze kuchimbwa na wachimbaji wadogo bila ya kuathiri shughuli za utafutaji mkubwa wa madini. Utaratibu huu wa mazungumzo umewezesha kupatikana kwa maeneo yafuatayo ambayo kwa sasa yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Rwamgaza (Geita) hekta 710 kutoka *PL 215/1994* ya Kampuni ya *IAMGOLD (T) Ltd.,* Nyarugusu (Geita) Hekta 540 kutoka *PL 4634/2007* ya Kampuni ya *IAMGOLD (T) Ltd,* Sekafi na Mumbwi (Handeni) hekta 25.84 kutoka *PL 4287/2007* ya Kampuni ya *Shadhilu Group (T) Ltd,* Malolo-Winza (Mpwapwa) hekta 3,900 kutoka maombi HQ-P15511 ya kampuni ya *Luguruni Mining Co. Ltd* na Makoro (Mbinga) ambapo *PML 53* zimetolewa kutoka ombi la leseni namba 513 na 517 ya kampuni ya *World Gem Supplies Ltd.*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yako kwenye mchakato wa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni Ngasamo Wilayani Magu (hekta 229), Matabe Wilayani Chato (hekta 880) pamoja na Nyasemero (hekta 172) na Rwabasi (hekta 449) Wilayani Musoma Vijijini.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Kwa kuwa imedhihirika kwamba wachimbaji wakubwa wanapokuja kawaida wachimbaji wadogo wadogo huwa wanaondolewa na imet hibika katika Wilaya ya Geita kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao mpaka sasa hivi wanakaa katika jengo la Mahakama bila maelezo yoyote ambayo Serikali imeshayatoa. Mara nyingi huwa wanasema kwamba bado kesi iko mahakamani kiubinadamu:-

(a) Serikali inasemaje kuweza kuwasaidia hawa wananchi ambao wako katika eneo lile na hawana sehemu ya kwenda? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kampuni ya *Geita Gold Mine* imechukua maeneo yote ya dhahabu ambayo yamezunguka katika maeneo yale na imechukua kama leseni za utafiti. Katika maeneo yale kuna vijiji kama Isamilo, Lwenge, Isabilo, Nyarugusu, Nyakabale na maeneo mengine ambayo yamezunguka katika vijiji vile na wananchi wale mpaka sasa hivi hawajui watakwenda wapi katika leseni zile.

Je, Serikali inasema nini kuhusu vijiji hivi watakuwa na ubia katika kampuni ile au Serikali inasemaje kama suala hili la vijiji hivi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la nyongeza ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza ni suala ambalo liko mahakamani na kama unavyofahamu Bunge hili Tukufu masuala yakiwa mahakamani kanuni na taratibu haziruhusu tuliongelee.

Lakini kwa taarifa tu ni kwamba maoni ya Serikali ni kwamba kilichokuwa kinaendelea kilikuwa kimefuata utaratibu wa kawaida. Lakini kwa sababu suala lenyewe liko mahakamani naomba kwa sasa tusubiri mahali ambapo hitimisho la mahakama litakapokuwa limetolewa halafu tuone kitakachofuatia ni nini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba Kampuni ya Geita *Gold Mine* imechukua maeneo yote na wananchi wa vijiji alivyovitaja, Mheshimiwa Mbunge hawajui watakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli anajua kaka yangu huyu kwamba maeneo haya yote yaliyotolewa leseni kwa Kampuni hizi na sio Kampuni ya Geita *Gold Mine* peke yake. Ziko Kampuni nyingi lakini pia wako hata wananchi wengine wa Geita wenye leseni ambao wamepewa maeneo hayo.

Kwa maeneo ambayo yamechukuliwa kihalali tunafahamu kwamba taratibu za sheria zinafuatwa, inapofikia mahali kwamba wawekezaji wanataka kuanza uendelezaji wa haya maeneo ambayo wameyachukulia leseni taratibu zinafuatwa na mahali pa wananchi kwenda kama uendelezaji ya kwa mfano uchimbaji unaanza kama inavyofahamika si jambo ambalo tunasema tunawa-*displace* wananchi bila ya kujua waelekee wapi, kwa sababu kuna masuala ya fidia lakini pia kujua kwamba fidia hiyo inayotolewa inaweza kuzingatia maslahi yao ya wakati huo lakini pia maslahi yao ya siku zinazofuatia kuanzia wakati huu ambapo mahali hapo walipo wamekuwa wamehamishiwa.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla sheria zipo kulinda maslahi ya pande zote mbili wananchi lakini pia kwa upande wa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Leo Mheshimiwa Esther Nyawazwa kweli nakuhurumia ebu sasa uliza swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize suala dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba suala liko Mahakamani lakini Serikali ni ya wananchi. Wananchi wale wako kwenye mahema tangu mwaka 2007. Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake la nyongeza anaomba Serikali mnaonaje wananchi kuliangalia suala hili kuhakikisha kwamba wananchi wanasimamiwa na Serikali yao pamoja na kwamba suala liko Mahakamani, Serikali nayo ina nia gani kuwasaidia watu wako kwenye mahema toka mwaka 2007? (*Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nafahamu mimi mwenyewe kama sehemu ya Watanzania kama ambavyo sisi wote tuliokuwa hapa ni sehemu ya Watanzania tunafahamu suala la ubinadamu.

Lakini Mheshimiwa Nyawazwa na Waheshimiwa wengine wa maeneo haya ya Geita wanafahamu kwamba Serikali kwa muda wote imekuwa ikishirikiana na hawa wananchi ambao bado kesi yao iko Mahakamani. Tunafahamu Wilaya au uongozi wa Wilaya ya Geita umekuwa ukishirikiana na wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema suala hili ni zito si jepesi kama ambavyo labda miongoni mwetu wangependa tulielezee. Tunafahamu mambo mengi ambayo pengine si sahihi, sio muafaka kuyasema hapa kuhusu kwa nini wananchi wale wakati mwingine wamekuwa wakijitokeza kwenye vyombo vya habari kuonekana wanaishi kwenye mahema.

Ziko habari nyingi lakini kama nilivyosema suala lenyewe liko bado Mahakamani, kesi ikiisha yako mengi ambayo sisi kwa upande wa Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka zingine zote tunaweza kulitolea ufafanuzi kwa sababu niseme kuna hekaheka nyingi zinaendelea kuhusu jambo hili. Lakini kwa sasa inatosha kusema kwamba tuiachie Mahakama kwanza ifikie suluhisho la kutoa maamuzi halafu sisi tutaendelea kutoa ufafanuzi na kulinda maslahi ya pande zote mbili.

Na. 147

**Uhitaji wa Umeme - Katoro Nyarugusu**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA(K.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa maeneo ya Katoro na Nyarugusu wanahitaji Benki kwa ajili ya kutunza na kusafirisha fedha zao; na kwa kuwa watu wa Benki wamesema wako tayari kupeleka huduma ya Benki kwenye maeneo hayo, lakini kutokana na kukosekana kwa umeme wanashindwa kufanya hivyo:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu kupeleka umeme kwenye maeneo hayo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwishaeleza hapa Bungeni wakati tukijibu swali la Mheshimiwa Mbunge katika Mkutano wa Nane tarehe 15 Agosti, 2007 na Mkutano wa Kumi na mbili tarehe 29 Agosti, 2008, kuwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya upelekaji umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge umekamilika kwa msaada wa Serikali ya Sweden. Gharama ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo pamoja na vile vya Bukoli na Bukondo ni shilingi 3,771,376,147. Fedha hizi zitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilomita 109 kutoka Geita Mjini hadi Bukondo kupitia vijiji vya Nyarugusu, Bukoli na Katoro, na uwekaji wa *transformer* 10 za ukubwa na *KVA 200.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kupeleka umeme kwenye maeneo ya Nyarugusu na Katoro kupitia utekelezaji wa mradi unaofadhili na Serikali ya Marekani chini ya programu ya "*Millennium Challenge Cooperation (MCC).*

Mkataba wa makubaliano kuhusu ufadhili wa mradi huu kati ya Serikali za Tanzania na Marekani uliwekwa saini tarehe 17 Februari, 2008. Mchakato wa utekelezaji wake ulianza mwezi Novemba, 2008 kwa kuajiri Mhandisi Mwelekezaji *ESBI International* ya Ireland kwa kushirikiana na *Norconsult A.A* ya Norway na *Africare* ya Marekani, ambaye kwa sasa anafanya upembuzi yakinifu ili kuandaa makadirio hitajika kwa ajili ya kuandaa zabuni kama Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 inavyoelekeza. Baada ya tathmini ya gharama kukamilika, fedha za mradi zitatolewa kulingana na tathmini hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengi wote ambao wa mikoa 6 inayohusika na mradi huu wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* kwa maana ya Mikoa ya Mwanza, Iringa, Dodoma, Morogoro, Mbeya na Tanga pia Mkoa wa Kigoma kwa ule mradi wa kuzalisha umeme kupitia maporomoko ya maji kule Mto Malagarasi huu utekelezaji wake umeshaanza na tunapenda kutumia nafasi hii kueleza kwamba tutaendelea kuwapa taarifa kadri ambavyo siku zinakwenda.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nataka kuuliza kama ifuatavyo.

La kwanza, kwa kuwa mradi huu wa kupeleka umeme katika maeneo katika Jimbo la Busanda ni sawasawa kabisa na mradi wa kupeleka umeme katika Jimbo la

Nyang'wale kutokea kijiji cha Kasamwa, Busolwa, Nyijundu, Nyalubele, Kakora hadi Karumwa. Na kwa kuwa miradi hii ya Serikali mingi huwa inachelewa sasa nyingine kwa visingizio mbalimbali ikiwemo maneno mchakato, upembuzi yakinifu, *design* au usanifu wa kina, *go ahead,* sijui wanasema *no objection* na visingizio vingi sana. Na kwa kuwa mradi huu umeme wananchi wanausubiri kwa siku nyingi sana naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri atamke hapa Bungeni watu hawa wataona umeme lini?

La pili, kwa kuwa kuna baadhi ya miradi inafanyika na sehemu inapopita mradi kama huu wananchi huwa hawapewi fidia kabla ya mradi kufanyika na hivyo baadae unapata matatizo ya madai. Je, katika mradi huu wa umeme wa kupeleka katika Jimbo la Nyang'wale na Busanda na miradi yote nchini Serikali itakumbuka kutoa fidia kwanza ya mazao, nyumba na mali zingine ambako mradi huu unapita badala ya kuweka mradi kwanza halafu fidia baadae ili kuondoa usumbufu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali haitoi visingizio inapokuwa inatoa taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali. Sisi sote hapa ni viongozi ambao tunafahamu kwa niaba ya wananchi masuala haya yana utaratibu wake kama ambavyo tunasema kuna hatua za kuanzia. Kwa mfano sasa hivi tuko kwenye hatua ya Mkandarasi Mwelekezi ambaye tayari ameshapatikana, huyu Mkandarasi Mwelekezi itabidi apate Wakandarasi ambao watatekeleza miradi hii inayofadhiliwa na *MCC* kwa mikoa 6 kwa ule utaratibu wa kawaida ambao unafanyika chini ya Sheria ya Manunuzi.

Sasa hili si suala la kusema visingizio ndio utaratibu wenyewe utakaopatikana wataalamu wataingia *site* na kuanza kazi. Kwa hivi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba atapata taarifa nafahamu na miradi yake kama alivyoitaja iko kwenye *MCC.* Nyang'wale pale tunafahamu na tutahakikisha kwamba mradi umetekelezwa na taarifa tutakuwa tunakupa kwa kadri ambavyo taratibu zinaruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kwamba mara nyingi wamekuwa hawapati fidia kabla ya miradi. Tunafahamu, sheria imeelekeza kwamba mwananchi yoyote asiathirike kabla ya kutimiziwa haki zake ama kupata stahili yake. Kama imeshajitokeza kwa uzoefu mbalimbali kwamba wakati fulani jambo hilo lilitokea kwa namna hiyo ilikuwa ni bahati mbaya ama ni kasoro za kiutendaji. Lakini msingi ni kwamba wananchi wapate fidia zao na stahili kabla ya mradi huu kuanza. Kwa hivi Mheshimiwa Mbunge tunamhakikishia kwamba sheria na kanuni zinazingatiwa katika utekelezaji wa miradi hii.

Na. 148

**Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Dar es Salaam**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina maelezo gani juu ya mchakato wa ujenzi wa Machinjio ya Kisasa katika Jiji la Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam kwa sasa lina wakazi takriban milioni 4 wanaoongezeka kwa asilimia 4.3 kwa mwaka. Kwa kuzingatia idadi hiyo na shughuli nyingi za kiuchumi zilizopo, ni dhahiri kuwa Jiji hilo lina mahitaji makubwa ya nyama kuliko miji mingine hapa nchini. Hata hivyo, machinjio yaliyopo hayana ubora wa kuzalisha nyama safi na salama kwa wakazi hao.

Kwa sasa, machinjio zinazotumika ni za Ukonga na Vingunguti zilizopo katika Manispaa ya Ilala, makaro ya Suka na Tegeta yaliyoko katika Manispaa ya Kinondoni na makaro ya Hassan Shebe, Jabir na Kiatwa yaliyopo katika Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, upembuzi uliofanyika tarehe Machi, 2004 kuhusu ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Jiji la Dar es Salaam ulibaini kuwa:-

(i) Jiji la Dar es Salaam linahitaji ng'ombe takriban 800 na mbuzi/kondoo 1,500 kwa siku.

(ii) Ulaji wa nyama kwa wakazi wa Dar es Salaam unazidi wastani wa kilo 10 kwa mtu kwa mwaka.

(iii) Machinjio itakayojengwa inatakiwa iwe na uwezo wa kuchinja ng'ombe 500 na mbuzi/kondoo 1,400 kwa siku na itoe fursa kwa machinjio nyingine kufuata viwango vya ubora wa machinjio zinazotakiwa kujengwa.

(iv) Gharama ya ujenzi iliyotayarishwa na Jiji pamoja na Manispaa zake ilikuwa ni shilingi bilioni 31.2.

Ili kutekeleza mradi huu makubaliano kati ya Jiji na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam yalikuwa kama ifuatayo:-

(i) Machinjio ijengwe katika Manispaa ya Ilala kwenye eneo la Gongo la Mboto kilipokuwa Kiwanda cha Nguo *(KILTEX).*

(ii) Jiji lichangia *USD 1,000,000* sawa na T.Shs. 1,267,200,000 na kila Manispaa ichangie *USD* 500,000 sawa na Tshs. 633,600,000

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kiasi cha *USD 2.246.5* milioni sawa na *T.Shs. 2,846,764,800* zimeshachangwa kati ya hizo, Jiji la Dar es Salaam limetoa *USD* 1,100,000 sawa na T,Shs. 1,393,920,000 Manispaa ya Ilala *USD* 435,000 sawa na Tshs.

551,145,000, Manispaa ya Temeke *USD* 152,900 sawa na T.Shs. 110,246,400 na Manispaa ya Kinondoni *USD* 147,500 sawa na T.Shs. 186,912,400 na michango bado inaendelea. Fedha kutoka Manispaa tajwa na Halmashauri ya Jiji zote zilihamishiwa kwenye akaunti ya *East African Meat Co. Ltd*. Kampuni ya Ubia iliyoundwa na Manispaa na Jiji mnamo mwezi Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhamasisha uharakishaji wa utekelezaji wa mradi huo muhimu kwa kutoa ushauri wa kitaalamu unaohitajika katika mchakato mzima wa kukamilisha ujenzi wa machinjio hii kwa manufaa ya afya hususan kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na kwa uchumi wa nchi kwa ujumla.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kumwuliza. Kwa kuwa miaka kadhaa sasa imeshapita toka *process* ilipoanza mpaka sasa karibu miaka 5 bado mradi huu *infact* haujaanza. Na kwa kuwa ninavyoelewa mimi ni kwamba ameajiriwa mtaalamu maalum pale kutoka Zimbabwe anaitwa *Somebody* Chipanze, lakini mpaka sasa hivi mradi huu bado unasuasua. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba, Jiji limeshachangia, lakini zile Halmashauri nyingine za Dar es Salaam bado hazijamaliza kuchangia. Je, Serikali haioni kwamba hiyo ni hasara na kama ni hasara inashauri nini.

Swali langu la pili, kwa kuwa machinjio mengi hapa nchini hayana miundombinu bora hasa mifereji ile ya maji. Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye machinjio utatapika na hutamani hata kununua nyama. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka machinjio yake katika nchi yetu hii ya Tanzania kuwa bora hasa za vijijini?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri, lakini Mheshimiwa Faida unasema Spika akienda atatapika, wewe ulitapika au? (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Sijaenda huko Mheshimiwa Spika. Ningekwenda nisingenunua nyama.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, tatizo kwa nini ule mradi haujaanza ni kwamba fedha zinazotakiwa ni shilingi bilioni 31 lakini zilizokwisha kupatikana ni shilingi bilioni 2.8. Kwa hiyo, mradi hauwezi kuanza mpaka hizo fedha zimepatikana. Kwa hiyo, kusema kwamba mradi unaingiza hasara tatizo ni kwamba fedha hazijapatikana mara zitakapopatikana mradi utaanza mara moja na hasara hiyo tunayoisema itakuwa haipo.

Kuhusu hali ya machinjio nimekagua machinjio ya Morogoro, Vingunguti sikuamini kwa kile nilichokiona pale Vingunguti hali ni mbaya. Kwa hiyo wito tunaoweza kuutoa ni kwamba kwa kweli wananchi wa Tanzania hawawezi kuendelea kuwa na hali mbaya ya machinjio. Kwa hiyo, wale wote wanaohusika wanatakiwa

kuhakikisha kwamba machinjio ni safi na pale ambapo itaonekana kwamba ni pachafu hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuongeza muda bado tumesalia na maswali mawili ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo nitamwomba Katibu aweze kuyaweka kwa kesho.

Ila kabla hatujaacha kipindi cha maswali baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mmeniandika hapa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii katika swali la nyongeza linalotokana na Swali Na. 142 lilisikika kama vile ni marufuku sasa kina mama Tanzania kujifungulia watoto kwenye vitanda vya mbao. Sasa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameniandikia kwamba hii inaweza kutia hofu wakunga wakawaacha hao ili kwa hofu kuchukuliwa hatua. Sasa hilo nalo ni baya tena. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri namwomba afafanue hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi. Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wakati nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kutokea Dar es Salaam aliulizia kuhusu suala la kuwazalisha akinamama katika vitanda vya mbao.

Mheshimiwa Spika, wakati nilipokuwa nikimjibu nilisema kwa kweli si busara kumzalisha mwanamama katika kitanda cha mbao kwa sababu hata yule mkunga ambaye anampa huduma atakuwa anafanya kazi chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, niliendelea kusema kwamba napenda kutoa wito kwa Waganga Wakuu wa Wilaya wahakikishe kwamba wananunua vitanda na kupeleka katika vituo vya kutolea huduma hizi nikimaanisha zahanati na vituo vya afya. Nikasema kwamba endapo labda sikueleweka vizuri naomba sasa nitoe ufafanuzi na kama sisi tutafanya ufuatiliaji na kama ikionekana kwamba Madaktari au Waganga Wakuu wa Wilaya hawakuweza kupeleka vitanda hivi kama wanazo fedha basi hatua zitachukuliwa dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba nafahamu kuna hali ambayo sasa hivi vituo vya kutolea huduma hususan za kuzalisha akinamama katika zahanati na vituo vya afya bado ziko duni na kwamba vifaa vya kutolea huduma hizi bado havipo ndio maana nikasema kwamba Waganga Wakuu wenye fedha katika akaunti zao wanunue vifaa hivi na kupeleka mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama sikueleweka vizuri basi naomba hiki ninachozungumza sasa hivi kichukuliwe kwamba ndio tamko ambalo nalisema. Naendelea kusisitiza kwamba Waganga Wakuu wa Wilaya husika waangalie katika Bajeti zao fedha kama wanazo wapeleke vitanda vya kuzalishia ili kuwarahishia Manesi wanaotoa huduma waweze kutoa huduma hizi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ufafanuzi huo ambao umeliweka sawa jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge sasa ni matangazo tunaanza na wageni. Orodha ni ndefu. Kwa hiyo, nitawaita kwa makundi tu siwezi kuwataja kila mmoja. Wageni wa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, ni familia yake wakiongozwa na Mzee Khalifa Said Mnonji, naomba wote wanne wasimame. Wale pale ahsante sana.

Wageni wa Mheshimiwa Omar Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini ni Kamati ya Utekelezaji ya UWT ikiongozwa na Mwenyekiti Amina Saidi. Kamati ya Utekelezaji Morogoro Mjini wale pale karibuni sana. (*Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Suleiman Saddiq ni Ndugu Salim Ali msanii na msoma mashahiri mashuhuri. Yule pale, ahsante sana, karibu sana. Mgeni wa Mheshimiwa Shally Raymond ni Ndugu Leah Ngoti Moshi, mjasiriamali. Yule pale ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni kutoka *USAID* ambaye kwa cheo ni *Programme Officer* kwa masuala ya UKIMWI anaitwa Bwana Aaron Canel, yule pale. *You are welcome Mr. Canel. It is a pleasure to have with us here and we very much appreaciate your government's contribution to the fight against HIV AIDS.*

*Thank's very much. (Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia na Chama cha Wabunge Maskauti ambao ni viongozi wa Chama cha Maalbino nchini wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Chama hicho Ndugu Ziada Nsembo na naomba basi wote wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha Maalbino wasimame, tafadhalini, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Sisi Wabunge tunatambua sana matatizo mnayoyapata ndiyo maana hivi punde nitarejea ofisini niweze kusalimiana nanyi. Ahsante sana. Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Missanga kutoka jimbo lake wanaongozwa na Mwenyekiti, wote Wenyeviti hawa wawili Ndugu Juma Nkindwa na Ndugu Chima kutoka Kata za Ilisya na Kata ya Minyuge. Wasimame, wale pale pamoja na Makatibu Ndugu Sulemani na Dagau. Karibuni sana karibuni sana. Nawashukuru sana kwa zawadi ambazo mlizonipatia nilipokuwa Singida juzi. Nyinyi ni watu wakarimu sana sana. Ahsante sana. (*Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Ndugu Fidelis Mwaipopo. Yule pale karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini ni Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya Ndugu Athanas Kapunga. Yule pale amefuatana na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Jiji la Mbeya wale pale. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini na pia Mheshimwa Joseph Mungai, Mbunge wa Mufindi Kaskazini ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mufindi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya hiyo Ndugu Joannes Kaguo. Ahsante sana.

Wewe mtu unabeba kura nyingi kweli. Mwenyekiti wa CCM na Mwenyekiti wa Halmashauri, hongera sana. Pia Mwenyekiti wa CCM Kata ya Makungu Mgololo Ndugu Benedict Mdeta. Yule pale karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 23 wa Chama cha Waheshimiwa Wabunge kutoka maeneo ya wafugaji. Wale wafugaji nadhani ni wale kushoto kwangu pale maana yake naona. Ahsante sana. Poleni kwa matatizo wanayowasibu hivi sasa lakini nina hakika Serikali itayapatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ameomba Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane leo saa 5.00 ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Hassan Khatib, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anahitaji saa 5.00 asubuhi hii Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, muwe na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Dr. Raphaed Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA* Tawi la Tanzania, anaomba wakutane leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Spika na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa *CPA* Tawi la Tanzania.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania anaomba saa 7.15 Wajumbe wote wa *APNAC Tanzania* wakutane katika ukumbi wa *African Dream's Conference Centre,* itifaki mbalimbali za Mkutano huo zimezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Maskauti anaomba Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Maskauti pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Huduma za Jamii, Nje, Ulinzi na Usalama, Katiba, Sheria na Utawala wakutane leo saa 7.00 mchana Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, naona sijui inagongana na kitu kingine sina hakika. Lakini nadhani ufumbuzi utapatikana kwa sababu pia tunayo *Speaker's Lounge* ya zamani inaweza kutumika kwa madhumuni hayo. Kwa hiyo, Wabunge wote wa Chama cha Maskauti.

Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ameniomba nitangaze kwamba saa 7.30 mchana Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tutakutana kwenye ukumbi wa kawaida.

Wabunge hao watakutana saa 2.00 usiku mara baada ya kuahirisha Bunge, Kamati ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) itafanya Mkutano katika Ukumbi wa Pius Msekwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge jana chini ya Kanuni ya Tatu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alitakiwa athibitishe kwamba kuna uwezekano vijana wanaofeli kidato cha sita wanakubaliwa na kupewa leseni ya kufundisha. Amefanya kazi na leo asubuhi amenionyesha *SMS* za kutoka sehemu mbalimbali wakituhumu kwamba majina waliyoyaleta ni ya vijana ambao inaelekea walifeli na sasa wana vyeti. Sina uhakika sana na hilo kwa sababu ni ujumbe wa *SMS*, kwa hiyo, kulimaliza nadhani nitamwomba Mheshimiwa Dr. Slaa alifikishe kwa Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi ili uchunguzi ufanywe na hatimaye haki itendeke. Huwezi kumwita mwongo bila uchunguzi, ndiyo maana yakipelekwa Wizarani Serikali itatafuta kwa majina na majina yapo. Sasa Kiti hakiwezi kukataa, unasema sikubali, hapana. Lazima ichunguzwe.

Waheshimiwa Wajumbe, niliahidi kutoa ufafanuzi, naomba utulivu. Kutuoa ufafanuzi wa kauli ya Mheshimiwa Jaji Mkuu wiki iliyopita kwamba Bunge linaingilia Uhuru wa Mahakama, maelezo ni marefu kwa hiyo, sitaki kuyasoma. Ninachotaka kuwaambieni, hili tutaligawa, lina kila kitu *authority*, maelezo. Kwa hiyo, kila Mheshimiwa Mbunge atapata nakala. Kwa kifupi tu, hilo lililosemwa ni kwamba Mheshimiwa Jaji Mkuu alighafirika na sivyo ilivyo.

Bunge la Jamhuri ya Muungano linayo madaraka na mamlaka ya kushughulikia malalamiko yoyote dhidi ya mtu ambaye ni Mbunge kwa upande mmoja na mtu ambaye sio Mbunge wa upande wa pili. Madaraka na mamlaka hayo yanatokana na masharti ya Ibara ya 100(1) ya Katiba na ukisoma pamoja na fungu la tatu la Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge sura ya 296, kwa kifupi Ibara ya 100 inasema hivi; *"Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano* (msisitizo) *au katika Mahakama."* Uhuru huu wa Mbunge kuongea hapa hauwezi kuhojiwa hata katika Mahakama, ndivyo katiba inavyosema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kuona hili, ili kuwezesha malalamiko ya raia wa kawaida dhidi ya Mbunge yasikilizwe, ndiyo tulitungwa Kanuni ya 71 inayoruhusu Spika kuletewa malalamiko na akifanya hivyo havunji Sheria wala Katiba. Lakini maelezo kamili yapo hapa. Mabunge ya Uingereza yanafanya hivi hivi, Mabunge ya Canada yanafanya hivi hivi, kwa hiyo, hatua ambayo tulichukua ni sahihi tu na mtaona katika maelezo haya.

Niseme tu kwamba, Mahakama nazo hutunga Sheria. Kwa mfano, katika hukumu iliyohusu Mgombea Binafsi, Mahakama imediriki kufuta Sheria ya Bunge. Kwa hiyo, mambo haya ukiyatazama, hata Serikali nayo hutunga Sheria ndogo. Kwa hiyo, vitu hivi twende navyo tu bila kusema kuna tatizo. Ni mambo ambayo yaliwekwa na kuhifadhiwa ndani ya Katiba na ni sahihi kwa sisi sote kuangaliana. Amesema Mbunge mmoja, *Checks and Balances* inapopita kipimo ndiyo inakuwa tatizo. Lakini kwa mambo yetu humu ndani ya Bunge ndiyo maana tuna Kamati ya Maadili, inafanya kazi kama

Mahakama. Inaapisha viapo na kusikiliza malalamiko sio tu ya Wabunge, hata watu wengine. Ninao Waraka wa Chama cha Mawakili Tanzania unaeleza vizuri sana dhana hii. Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Slaa alinitumia hii iwe sehemu ya maelezo. Kwa hiyo, nao huo nitaugawa ili tuweze kujielimisha kwenye dhana hii.

Naambiwa kwamba nilisahau kutangaza Mkutano wa Wanachama wa *TAPAC*, kwa hiyo, Mkutano wa *TAPAC* utafanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa hapa mikutano mingi itafanyika kwenye Ukumbi wa Msekwa saa 7.00 sijui tutafanyaje? Basi tutaelewana huko huko baada ya kugongana huko huko.

Mwisho, shughuli za Bunge. Sasa baada ya jana nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu hapa ni Waheshimiwa Wabunge 39. Nataka niwaombe hivi, mawazo mengi yanayoingia kwenye mpango ni mazuri sana, sasa tujitahidi basi kwa sababu wengi wataachwa. Kwa hiyo, tujitahidi tumalize leo jioni na orodha itakapoishia, basi wengine watoe kwa maandishi hata kama watamkabidhi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kesho, yote ni msaada, kwa sababu hayo pia nimeagiza kwamba mawazo yote yatakayotolewa kwa maandishi nakala tupewe ili yaingie katika *Hansard* ili kuwe na ukamilifu wa ushauri ambao tunatoa kwa Serikali kuhusu jambo hili. Ninakusudia kwamba Bunge tumalize kesho jioni saa mbili kasarobo. Sasa ili hilo lifanyike, itabidi Mtoa hoja afunge mjadala leo jioni ili kesho tuweze kuwa na muda wa kutosha wa kuzingatia taarifa zile mbalimbali za Serikali kuhusu masuala ambayo sote tunayafanya ambayo yabasubiri kutolewa taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, nina udhuru na nimemwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kuja kuendeleza shughuli zilizopo.

*(Hapa Mhe. Anne S. Makinda Alikalia Kiti)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, habari ya asubuhi.

**WABUNGE:** Nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya DNA ya Binadamu wa Mwaka
### *(The Human DNA Bill, 2009)*

### Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008
### *(The Fertilizer Bill, 2008)*

*(Miswada Iliyotajwa Hapo Juu Ilisomwa kwa Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA KAMATI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge Kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kazi Nzuri na Ufanisi Alioufanya katika Kipindi Chake cha Uenyekiti wa Umoja wa Afrika

**MHE. WILSON M. MASILINGI- MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha hoja ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kabla sijaendelea na uwasilishaji napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kubwa na ndogo ndogo kwa kutuwezesha kuwepo ndani ya ukumbi huu na kuendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwatakie kheri ya mwaka mpya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu Waziri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na Watanzania wote kwa ujumla. Nimkaribishe na kumuahidi ushirikiano wangu Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale - Mbunge mpya wa Mbeya Vijijini nikimpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Pia napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Richard Nyaulawa na wananchi wa Mbeya Vijijini kufuatia msiba mkubwa uliowafika. Aidha, natoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Muleba Kusini kufuatia mauaji ya watoto wetu wenye ulemavu wa ngozi (Maalbino) katika kijiji cha Itongo, Kata ya Nshamba na kijiji cha Nyamilanda kitongoji cha Kishoju, Kata ya Kebtembe, mauaji ambayo yalifanyika kwa njia za ukatili. Nawapa pole sana. Nikienda kule mara baada ya Bunge nitaenda kuwafariji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maazimio mawili kutaka Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na nitayawasilisha kufuatia mpangilio wa orodha ya shughuli za leo kama ulivyowekwa kwenye *Order Paper* katika Mkutano huu wa Kumi na Nne, Kikao cha Kumi na Moja. Sipendi kupoteza muda mwingi kwa sababu ni maazimio ya Bunge na kwa maelezo mafupi tu ni kwamba tumepata ushirikiano mkubwa sana kutoka Serikalini kupitia Wizara ambazo tunazisimamia. Mawaziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki na watumishi wao. Kazi zetu zilikuwa zinakwenda vizuri, tunashukuru kwa ushirikiano wao na kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanazozifanya na ushirikiano tulionao katika Kamati yetu na kwa kauli moja tuliafiki kulete maazimio hayo mawili kama yanavyoonekana kwenye shughuli za leo na nitayasoma moja baada ya lingine niyawasilishe kwa pamoja chini ya maekezo yako Mheshimiwa Naibu Spika,

Kabla sijaanza kuyasoma, naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Col. Salehe A. Farah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Col. Feteh Saadi Mgeni, Mheshimiwa Ali Amer Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Mohamed Sanya, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Lazaro Nyarandu na Katibu wetu Athuman Hussein, namshukuru sana kwa kazi nzuri na ushirikiano tunaoupata katika Kamati yetu kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa chini ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niyasome maazimio ambayo tunayaleta mbele ya Bunge hili ili yawe ni maazimio ya Bunge kwa kufuata mpangilio wa shughuli za leo Bungeni. Azimio la kwanza linahusu Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Tanzania kwa kazi nzuri na ufanisi aliouonyesha katika kipindi chake cha Uenyekiti wa Umoja wa Afrika.

**KWA KUWA,** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapenda kutambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mafanikio yaliyopatikana Barani Afrika wakati wa kipindi cha Uenyekiti wake wa Umoja wa Afrika;

**NA KWA KUWA,** chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Umoja wa Afrika umejivunia mafanikio katika maeneo ya uimarishaji wa Umoja huo na Taasisi zake, Ulinzi na Usalama na fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

**NA KWA KUWA,** pamoja na majukumu mengine, katika kipindi cha Uenyekiti wake, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alisimamia kwa makini uendeshaji wa vikao vya Umoja wa Afrika, hususan kuhusu mjadala mgumu na nyeti wa kuanzisha Serikali moja ya Afrika;

**NA KWA KUWA,** kutokana na tofauti kubwa zilizokuwapo kati ya nchi zilizotaka Serikali ya Afrika ianzishwe mara moja na zile zilizotaka Serikali hiyo ijengwe hatua kwa hatua, mjadala huo ulitishia kusambaratisha Umoja wa Afrika;

**NA KWA KUWA,** katika kuendesha mjadala huo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa msikivu, mstahimilivu, mwenye subira na alionyesha na kudhihirisha uwezo mkubwa wa kujenga maridhiano na kipaji chake hicho kilimwezesha kutoa mwongozo uliokubalika na pande zote;

**NA KWA KUWA,** Uenyekiti wake uliepusha kutokea kwa zahama yoyote ambayo ingesambaratisha Umoja wa Afrika na matokeo ya juhudi zake ni kufikia uamuzi wa kuigeuza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuwa Mamlaka ya Afrika itakayoratibu shughuli zinazohusu maeneo yenye maslahi ya pamoja na yaliyokubalika na nchi wanachama;

**NA KWA KUWA,** Mamlaka hiyo itakuwa na madaraka zaidi katika kuratibu shughuli za Bara la Afrika na kujenga utangamano zaidi kuliko uliopo chini ya Kamisheni ya sasa;

**NA KWA KUWA,** Rais Jakaya Mrisho Kikwete alisimamia uzinduzi wa Baraza la Uchumi na Utamaduni la Umoja wa Afrika ambalo linalenga kuwapa wananchi wa kawaida sauti katika uendeshaji wa shughuli za Umoja wa Afrika kupitia uwakilishi wa Asasi zisizo za Kiserikali *(ECOSOCC);*

**NA KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameboresha mafao ya wafanyakazi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika wakati wa kipindi cha Uenyekiti wake, kwa lengo la kuwaongezea wafanyakazi hao ari ya kufanya kazi kwa bidii;

**NA KWA KUWA,** katika eneo la Ulinzi na Usalama, Bara la Afrika lilikabiliwa na changamoto kubwa wakati wa kipindi cha Uenyekiti wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete;

**NA KWA KUWA,** katika kukabiliana na changamoto hizo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alisaidia kurejesha amani na utulivu nchini Kenya na kukomesha uasi kwenye Kisiwa cha Anjouan;

**NA KWA KUWA,** katika tukio la kwanza la aina yake, Umoja wa Afrika ulitumia nguvu za kijeshi kumwondoa Col. Mohamed Bacar aliyeasi huko Kisiwani Anjouan na kurejesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini Comoro;

**NA KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alisimamia kwa mafanikio, utatuzi wa mgogoro sugu wa Burundi na jitihada hizo za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete zilihitimishwa kwa Serikali ya Burundi na kikundi cha *PALIPEHUTU – FNL* kukubaliana kuendelea na zoezi la kutekeleza Mkataba wa kusitisha mapigano kati yao tarehe 4 Desemba, 2008;

**NA KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika amechangia katika kutafuta suluhu nchini Zimbabwe, Mashariki mwa Kongo *DRC* na katika mgogoro wa Darfur nchini Sudan;

**NA KWA KUWA,** juhudi zake zimeliletea Bara la Afrika sifa kubwa na imani kuwa panakuwepo na mshikamano na uongozi madhubuti, Umoja wa Afrika unaweza kutatua matatizo yanayolikabili Bara letu;

**NA KWA KUWA,** kutokana na mchango wake mkubwa, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameliacha Bara la Afrika katika hali iliyo tulivu zaidi kuliko lilivyokuwa kabla ya Uenyekiti wake;

**NA KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia na kulinda misingi na Katiba ya Umoja wa Afrika, Mkataba wa Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika pamoja na Tamko la Lome la Mwaka 2000 linalokataza ubadilishaji wa Serikali za nchi za Kiafrika bila kufuata na kuzingatia utaratibu wa kidemokrasia;

**NA KWA KUWA,** kwa kuzingatia msingi huo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikemea mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika nchini Mauritania na Guinea;

**NA KWA KUWA,** kwa kuzingatia msingi huo huo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alizisimamisha nchi hizo kushiriki kwenye shughuli za Umoja wa Afrika hadi hapo zitakaporejesha utawala wa kidemokrasia;

**NA KWA KUWA,** juhudi za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete zilidhihirika pia katika kutetea maslahi ya kiuchumi ya Bara la Afrika na katika kutekeleza azma hiyo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alishiriki kikamilifu katika kuhimiza ushirikiano wa kiuchumi na nchi tajiri, ikiwemo Japan, China na nchi za Kundi la G.8 linalojumuisha nchi tajiri duniani;

**NA KWA KUWA,** juhudi hizo zilifungua milango katika nyanja mbalimbali za kiuchumi kwa nchi za Bara la Afrika na kutokana na juhudi hizo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ametoa mchango mkubwa katika kulitetea na kuliletea heshima na maendeleo Bara la Afrika;

**NA KWA KUWA,** juhudi zake zimeijengea Tanzania heshima kubwa kwa kuliongoza Bara la Afrika katika kipindi kigumu;

**NA KWA KUWA,** kutokana na busara hizo, Rais Jakaya Mrisho Kikwete amekabidhi Uongozi wa Umoja wa Afrika kwa Mheshimiwa Kanali Muamar Gaddaffi salama salimini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nne linaazimia kwamba, kwa kauli moja linampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ufanisi aliouonyesha katika kipindi chake cha Uenyekiti wa Umoja wa Afrika, 2008 hadi 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa naomba niwapongeze Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kutuletea hoja hii muhimu. Mara nyingi Watanzania wamefanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuleta heshima kwa nchi yetu ya Tanzania na hii pia ni mara nyingine ambapo mwana wa Tanzania ameonyesha uwezo wake mkubwa katika kuongoza Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, nami najumuika na Kamati hii na kuunga mkono kauli hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa Addis Ababa, katika kikao kilichopita cha Wakuu wa Nchi Wanachama, kuna mtu mmoja aliniliuza swali, huyu anatoka Chama cha CCM? Nikasema ndiyo. Huyu amelelewa na Julius Nyerere? Nikasema ndiyo umepatia. Kwa hiyo, heshima hii ambayo ametupa Rais pia ni kielelezo kikubwa cha malezi bora ndani ya itikadi ambayo imemwezesha Rais kufika hapo akaweza kuwahudumia Watanzania, lakini pia akalihudumia Bara la Afrika. Ni jambo la kujivunia na sifa kubwa kwa nchi yetu na hasa kwa Chama cha Mapinduzi ambacho kimemlea Rais Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Ndugu zangu, kipindi hiki cha mwaka mmoja kama ilivyoelezwa katika kauli hii, Mheshimiwa Rais wetu amefanya kazi kubwa sana. Napenda kusema tu kwamba yote haya ameyafanya, lakini bado amepata nafasi ya kuwa mgeni katika Bunge la Afrika katika Kikao chetu cha Kumi cha Bunge la Afrika na alitoa hotuba ambayo ilimsisimua kila mtu ndani ya Bunge lile na kufanya majadiliano kutokana na hotuba hiyo yaweze kuliongoza lile Bunge kuwa na nguvu zaidi ya kuangalia ni jinsi gani tutakavyoelekea katika Umoja huu wa Afrika na pia kuhakikisha kwamba masuala muhimu ya maendeleo ya watu wa Afrika na mshikamano kama alivyouweka Rais wetu ilikuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba huu mwaka ulikuwa ni wa mafarakano makubwa. Kubwa katika Afrika kulikuwa na mafarakano ambayo yametokana na uchaguzi. Matatizo ya Kenya na matatizo ya Zimbabwe yametokana na watu kutokukubali demokrasia ichukue mkondo wake. Lakini Rais Kikwete bila kupendelea katika haya yote mawili alisimama kidete na kutoa miongozo ambayo imesaidia kutatua matatizo ya Zimbabwe na matatizo ya Kenya katika uchaguzi. Hili ni fundisho hata kwa sisi Watanzania ya kwamba tutakapokuwa kwenye uchaguzi wa mwaka 2010 ni vyema tuzingatie misingi ya demokrasia ambayo itatuepusha na matatizo haya yaliyowakumba wenzetu wa Kenya na Zimbabwe katika kutokukubali mkondo wa demokrasia na kauli za wananchi. Hili ni tamko ambalo sisi katika Bunge la Afrika tumelitoa kwa nguvu zetu zote kwamba Afrika itanusurika tu iwapo tutakubali misingi ya demokrasia ambayo tumejiwekea.

Lakini haitoshi, ni lazima sisi kama nchi tuige mfano wa Rais wa kuelekeza misingi iliyo bora tusifike katika mifarakano hiyo. Kwa sababu wakati mwingine chaguzi zinakuwa zimeandaliwa vibaya, watu wanakashifiana na watu wana tamaa ya madaraka, ndiyo maana tunafika hapo mahali ambapo watu wanapoteza maisha ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgogoro wa Mauritania, Rais Kikwete amesema wazi kwamba kwa sababu kuna watu walikuwa wanasita, wengine wanasema mapinduzi haya ni salama, lakini ametoa kauli wazi kwamba mapinduzi ni mapinduzi, hakuna mapinduzi ya kirafiki wala mapinduzi ambayo ni ya amani ambapo ameweka pia msingi bayana.

Lakini kwa sababu muda wetu ni mfupi, nifupishe haya mazungumzo kwa kusema jambo moja pia ambalo amelifanya. Kulikuwa kumetokea matatizo ambayo nchi wanachama wa *Court* ya Ulimwengu ambayo imejipa madaraka ya kuchukua Viongozi mbalimbali duniani na kuwafikisha Mahakamani, katika kipindi chake imewezekana kabisa, amefikisha katika Umoja wa Mataifa kwamba inaelekea kwamba Viongozi wa Afrika ndiyo wanaoburuzwa kwenda *The Hague*, bila utaratibu na bila kuheshimu haki za binadamu na hili pia ameliwekea misingi bila kulionea haya.

Ndugu zangu, kazi alizozifanya katika kipindi hiki ni kubwa. Ningependa Watanzania tutambue, wakati mwingine kwa sababu hatukuwa tumejua haya yote, hatukujua kwamba amejitolea kiasi gani kufanya kazi hizo zilizokuwa zinamhitaji kama Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na wakati huo huo kuwahudumia Watanzania. Inahitaji mtu mwenye kujitolea sana na kujinyima sana muda wake binafsi ili aweze kuyatimiza haya yote kwa pamoja na aliyaweza kwa kiwango ambacho wengi ambao hatukuwa tunamwona katika harakati hizi za Afrika tulifikiria ya kwamba ni kazi nyepesi, lakini ni kazi ngumu na nzito na hapa ndipo nadhani anahitaji pongezi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia basi, ni vyema pia nikawataja wale waliohusika katika kumsaidia kwa sababu mimi nilikuwa niko karibu sana na kazi hizi za Umoja wa Afrika. Mmoja wapo ni Waziri wetu Mheshimiwa Bernard Membe ambaye naye kwa nafasi hii, nchi inaposhika uwenyekiti maana yake ni kwamba vikao vile vya Mawaziri wa Nchi za Nje, Mwenyekiti wake anakuwa ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Tanzania. Vikao vya Mabalozi ambao nao wanakuwa na nafasi yao katika kuchanganua mambo kabla ya vikao vya Wakuu wa Nchi walioko Addis Ababa, Mwenyekiti wao anakuwa ni Balozi wa Tanzania, Addis Ababa. Kwa hiyo, Waziri Bernard Membe, naye kwa kuwa mwenyekiti wa vikao hivi mbalimbali vinavyoandaa vikao vya Wakuu wa Nchi, ameonyesha umahiri wake, ameonyesha uwezo wake wa kusimamia hivi vikao, naye naomba nimpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi aliyeko Addis, Ndugu Mahundi na Maofisa waliokuwa wakimsaidia na wenyewe katika kipindi hiki wamefanya kazi yao kwa uaminifu kabisa. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa kwa kumalizia ni kwamba, mimi kwa kumwona jinsi Rais wetu alivyofanya kazi na wasaidizi wake, nilijisikia Mtanzania mara kumi, mara mia moja kwa kuona kazi nzuri aliyoifanya. Kila mara nilijisikia hivyo na ni matumaini yangu kwamba tusisite hata siku moja kuwapa moyo Watanzania wengine walioko nje ambao wanafanya kazi katika maeneo mbalimbali ili na wao wapate nguvu ya kuifanya kazi yao vizuri na kuleta sifa alizozileta Rais wetu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa kuzingatia muda ulivyo mfupi, ninaomba nami niunge mkono Azimio hili na kusema ya kwamba kwa kweli Rais wetu anastahili sifa na pongezi hizi ambazo zimetolewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, ahsante sana. Umetuongezea yale ambayo umeyaona wewe mwenyewe na umeshiriki na sisi wenzio umetusaidia kuyaelewa. Sasa namwita Mheshimiwa Juma Killimbah, atafuatiwa na msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kabla ya kumwita mtu toka Serikalini.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, labda na mimi nianze kwa kujieleza kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati - Mheshimiwa Masilingi kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa tukishirikiana na Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii niwapongeze Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi ambayo wamekuwa wakiifanya muda wote na kwa kushirikiana na Serikali ili kuhakikisha mambo yetu yaliyo muhimu hasa Diplomasia ya uchumi jinsi kama inavyokusudiwa katika sera ya Mambo ya Nje inatekelezeka kwa jinsi ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii niipongeze Serikali, nikianzia na Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe pamoja na Naibu wake Balozi Seif Idd na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi ambayo wamekuwa wakiionyesha na wamekuwa wakishirikiana na Kamati yetu kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianzie kwa kuunga mkono Azimio hili lililoletwa mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba ni Azimio ambalo ni sahihi kabisa ambalo sisi kama Watanzania ambao tupo ndani ya Bunge hili Tukufu, ni wajibu wetu sasa tutumie nafasi hii tuliyopewa kwa kuhakikisha kwamba tunaonyesha zile shukrani na kuonyesha kwamba kwa kazi ambayo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliifanya katika kipindi cha kutuwakilisha sisi kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, ukweli ni kazi ambayo inastahili ipongezwe na ni kazi ambayo inastahili iungwe mkono kwa sababu Mheshimiwa Rais alituwakilisha vyema sana katika kipindi chake cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoweza kusema, kama tulivyo Tanzania ni nchi ya amani na utulivu na bahati nzuri maeneo haya ya amani na utulivu ni misingi bora ambayo imeasisiwa na Waasisi wetu, Marehemu Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na Marehemu Abeid Aman Karume. Ninaamini kabisa ndio maana hata wakati Rais anatuwakilisha kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika ameweza kuhakikisha suala la amani linakuwa ajenda kubwa kabisa katika kipindi chake na ndio maana aliweza kuhakikisha pale palipotokea mifarakano katika baadhi ya nchi, yeye alisimama na kuhakikisha mifarakano hiyo inaondoka mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya hapa kwa majirani zetu wa Burundi ambao walikuwa na mgogoro wa muda mrefu hasa kikundi kile cha *PALIPEHUTU-FNL* ambacho kilikuwa kinaongozwa na Agaton Luasa pale alipofikia na kuweza kuhakikisha kwamba wameondoa tofauti zao na sasa wale watu waliokuwa nje ya Burundi kwa muda mrefu wakarejea Burundi na sasa Burundi inaendelea kuwa ni nchi ya amani. Kwa hiyo, hizi ni juhudi ambazo zimefanywa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni juhudi ambazo tunatakiwa tumpongeze sana Rais wetu kwa umakini na kuhakikisha kwamba amani nchini Burundi inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mzungumzaji aliyepita, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella amezungumzia juu ya utatuzi wa masuala yaliyojitokeza kuhusiana na chaguzi za nchi za Serikali ya Zimbabwe na Kenya, ni dhahiri watu hata tunapofikia tunabeza juu ya juhudi zinazofanywa na Serikali yetu chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tunakuwa hatutazami au hatuoni ukweli halisi kwamba ni juhudi zipi ambazo zinafanyika.

Tumeshuhudia Kenya walikuja watu tofauti na watu wa aina mbalimbali kutaka kusuluhisha ule mgogoro, lakini Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipokwenda akaingia kama Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, masuala ya Kenya yalitatuliwa na amani nchini Kenya ikarejea kama kawaida. Hii ndio maana nasema kwamba inatokana na misingi bora iliyowekwa na Waasisi wetu na amani na utulivu tulionao nadhani ya nchi yetu. Kama tusingekuwa na amani na utulivu, naamini kwamba pasingeweza kuwa na amani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi Mongella amezungumzia vizuri sana. Mimi bahati nzuri nilihudhuria Mkutano wa *PAP* nikiwa na Rais wakati anazindua Bunge hilo. Wakati ametoa hotuba ile baada ya kumaliza, wakati tunatoka, nilibahatika kukutana na Wabunge wale wa *PAP* na baadhi ya Wabunge niliokutana nao wakaniambia, nyie mmetoka Tanzania? Ndio mko pamoja na Rais! Nikawaambia, ndio. Wakaniambia tungekuwa na Marais 20 wa namna hii Afrika, basi tungepiga hatua kubwa sana. Haya ni maneno yanayozungumzwa na Wabunge wa Kenya, maneno yanayozungumzwa na Wabunge kutoka Zimbabwe, ni maneno yanayozungumzwa na Wabunge wa kutoka Zambia na ni maneno ambayo yanazungumzwa na Wabunge wa *PAP*. Kwa hiyo, ni hakika kuonyesha kwamba Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni mahiri sana ameweza kutuwakilisha sawasawa katika uenyekiti wa Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia nielezee tu namna Rais wetu kwa kipindi alichokuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na hasa alipokazia masuala ya uchumi, kuhakikisha kwamba Afrika inakuwa moja na hasa katika masuala ya muhimu kabisa ya kiuchumi. Ninaamini kabisa busara ya Rais wetu ilielekeza kutaka kuijenga Afrika kuwa moja na kuondoa zile tofauti ambazo tumekuwa na *block* ndogo ndogo za kiuchumi. Akasisitiza juu ya kuwa na mahusiano ya *block* moja hasa katika hizi Kanda. Kwa mfano, Kanda ya Afrika Mashariki, tuna mchanganyo wa Jumuiya mbalimbali, wengine wako *SADC*, wengine wako *COMESA* na tuna Wengine wako *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii yote mimi naamini kwamba Mtukufu Rais alipokuwa katika Mkutano wa *CHONGAN* pale Uganda, alisema kwamba kuna umuhimu na ipo haja ya makusudi tuwe na *block* moja ambayo itakuwa ni yenye nguvu ambayo itatufanya tuendelee kiuchumi katika hizi Kanda kuweza kupiga hatua kwenda mbele. Naamini kwamba hatua hizo ni hatua za busara sana na ni hatua ambazo zinahitaji kupongezwa kabisa ili kuondokana na umaskini miongoni mwa wananchi ambao tunawaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, nasema kwamba mimi naunga mkono Azimio hili na ni dhahiri sisi tulio ndani ya Bunge hili Tukufu na Watanzania kwa ujumla tunashukuru na kupongeza hatua nzuri za uwakilishi ambazo zimefanywa na Rais wetu. Tunapongeza hizi hatua tukielewa kwamba, Afrika bado ina uchanga hasa kwenye masuala mbalimbali. Ziko kauli ambazo zilikuwa zinaonekana kupitia nafasi hii ya Uenyekiti wake kwamba sasa kuwe kuna suala la uharakishaji wa uundwaji wa Serikali ya Afrika. Lakini Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika Uenyekiti wake aliweza kusimamia masuala ya msingi kabisa kuhakikisha hatua kwa hatua zifuatwe ili kufikia Serikali ya Afrika. Kwa hiyo, hizi ni hatua za kupongezwa na Rais ambaye yuko makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili kwa aslimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba mwongozo wako. Mbele yetu kuna Maazimio Mawili. Azimio Na.5 linalohusu Amiri Jeshi kupeleka Majeshi ya Ulinzi Darfur ambalo ndio nimejiandaa na ningependa kulizungumzia kwa kuliunga mkono na hili Azimio Na.6 ambalo wenzangu wameshaliwakilisha vizuri. Naomba mwongozo wako, kama nahitaji kusubiri hadi lisomwe au naweza nikaendelea na mchango wangu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Endelea, kwa sababu ukisoma hapa ni Azimio la Bunge Kuunga Mkono Umuzi wa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kupeleka Kikosi cha Kulinda amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudan. Kwa hiyo, linahusika. Nasikia hawajasoma, kwa hiyo, mpaka siku nyingine labda.

Haya Tunaendelea! Naomba Mheshimiwa Nyalandu ukae, naambiwa watalisoma baadaye. Kwa hiyo, namwita Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, napenda nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati kwa Azimio ambalo limeliwasilishwa mbele yetu la kumpongeza na kuunga mkono utendaji wa Mheshimiwa Rais alipokuwa Mwenyekiti wa Taaisisi yetu muhimu ya Umoja wetu wa Afrika. Kusema kweli kazi

aliyoifanya imesaidia sio tu kuonyesha jinsi Tanzania ilivyo na uwezo wa kutoa viongozi wa Kimataifa, lakini vile vile imelitangaza jina la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vile vile kuwashukuru viongozi wote wa Afrika ambao sio tu walimchagua, bali walimchagua awe Mwenyekiti wao, lakini vile vile walimuunga mkono katika utendaji wa kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tulipokuwa kwenye mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC, COMESA* pamoja na Afrika Mashariki, toka mwanzo ilikuwa uanzishwe ukanda huru wa kibiashara wa *SADC*, *COMESA* na *EAC*. Lakini Mheshimiwa Rais alipotoa hotuba yake, alisema tusiishie tu kwenye ukanda huru wa kibiashara, twende hatua zaidi ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa *SADC, COMESA* na *EAC*. Wakuu wote wa nchi waliokuwepo walisema wanaungana naye na ushauri wake usiwe ushauri tu, bali uwe uamuzi wa kikao kile. Huo ni ushahidi wa kuonyesha jinsi ambavyo viongozi wenzanke walimuunga mkono katika utendaji wake wa kazi za kila siku na waliheshimu uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia uzoefu wake, lakini vile vile na busara zake, Mheshimiwa Rais vile vile aliwezesha kupatikana kwa amani kule nchini Kenya, majirani zetu tunajua matatizo yaliyotokea. Lakini vile vile kule Zimbabwe hatimaye wameweza kupata maafikiano. Lakini vile vile na Afrika nzima katika kipindi chake imeweza kuwa imara na kubaki kwenye misingi ya kuvumiliana, kubaki kwenye misingi ya kudumisha amani na na hata hivi karibuni katika Mkutano ambao ulifanyika hivi karibuni ambapo alikabidhi uenyekiti wake kwa Mheshimiwa Rais wa Libya.

Vile vile katika kikao aliweza kutoa mchango mzuri ulioweza kutoa taswira ya Afrika, ifanye nini katika kuendelea na katika kuzidi kujenga ushirikiano. Yote haya ni heshima kwa nchi yetu, ni heshima kwa Bunge letu na vile vile ni heshima kwa Watanzania. Kwa hiyo, naunga mkono Azimio kama lilivyowasilishwa na Kamati, lakini vile vile naungana na Bunge na tunasema kwamba tunaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, fahari yangu ya kuwa Mtanzania imeongezwa mara dufu na rekodi ya uongozi uliotukuka wa Rais Jakaya Kikwete akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Mheshimiwa Rais Kikwete alikabidhiwa uongozi wa *AU* katika kipindi kigumu kupita vyote tangu umoja huu uasisiwe miaka 46 iliyopita: migogoro mikubwa ya kisiasa iliyosababisha umwagaji damu Kenya na

Zimbabwe; hali ya vita na wasiwasi nchini *DRC*, Somalia, Sudan na Madagascar; mgogoro wa kifedha Duniani (*global financial crisis*); vifo vya viongozi maarufu Afrika Rais Levy Mwanawasa wa Zambia na Rais Lansana Coute wa Guinea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa ujasiri mkubwa pamoja na udhaifu mwingi wa *AU* alikabiliana na changamoto zote hizo na kurejesha hali ya kawaida sehemu nyingi Barani Afrika. Ameondoka kwenye kiti hicho huku nchi nyingi zilizokuwa kwenye majaribu makubwa zikiwa shwari: Burundi, Comoro, Liberia, Afrika ya Kati na Ivory Coast. Hongera sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mwenyekiti Spika, naunga mkono Azimio la Kamati yako kwani kweli Mheshimiwa Rais alifanya kazi nzuri sana alipokuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Vifuatavyo ni vielelezo vya mafanikio yake.

(a) Alifuatilia migogoro ya bara hili ikiwemo ya *DRC*, Somalia, Darfur, Zimbabwe, Saharawi, Comoro, Mauritius na kadhalika.

(b) Alikwamua mgogoro wa baada ya uchaguzi wa Kenya baada ya tume ya *AU* ikiongozwa na DK. Kofi Anan Waheshimiwa Mkapa na Gracia Maschel kuelekea kushindwa.

(c) Ameliwakilisha vizuri Bara la Afrika katika mikutano ya Kimataifa nje ya Bara hili – Umoja wa Ulaya, Marekani, Japan na kadhalika.

(d) Amesifiwa sana na Wabunge wote wa Bunge la Afrika alipolihutubia Bunge hilo katika mkutano wa 10 mwezi Novemba 2008 kiasi wakamfahamisha na Rais Baraka Obama wakati ule akiwa Rais mteule. Amesaidia sana uimarishaji wa *PAP*, uamuzi Na. 98.

(i) Hali ya usalama na jitihada za kutatua migogoro katika maeneo mbalimbali yakiwemo; eneo la maziwa makuu – Rwanda, Burundi, *DRC*, Kenya, Uganda na Sudan, *DRC*, Zimbabwe, Somalia, Saharawi, Comoro na kadhalika.

(ii) Uchumi; umuhimu wa kutatua tatizo la njaa na jinsi ya kuzalisha chakula cha kutosha ndani ya Bara hili na kuuza nje, matumizi bora ya nishati na umwagiliaji, kuboresha miundombinu na mawasiliano, kuzuia/kutatua migogoro.

(iii) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuliunga mkono Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti Mstaafu wa Umoja wa Afrika na vyombo

vya habari vilitangaze Azimio hili ili Afrika na Dunia zifahamu kuwa Watanzania wanamuenzi Rais Kikwete, kwani wahenga walisema mcheza kwao hutunzwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono.

**MHE. WILSON M. MASILINGI – KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa tena niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Kama ilivyo utaratibu ndani ya Bunge hili, niwatambue haraka haraka waliochangia katika mjdala wa hoja yetu. Wa kwanza aliyechangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Getrude Mongella – Mbunge na Rais wa Bunge la Afrika; Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala - Mbunge na Waziri wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Waliochangia kwa maandishi ni wawili tu. Wa kwanza, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na wa pili Mheshimiwa Athuman Janguo. Wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi wameunga mkono hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nasisitiza maneno kwamba ni lazima**.**

Tutambue mchango wa viongozi wetu wanapofanya kazi vizuri , tumefanya hivyo na nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza na mnaoshiriki kwenye ukumbi huu bila kuzungumza lakini mnaonyesha kwa kupiga makofi mnaunga mkono hoja ya Azimio hili la Bunge kwamba tuepuke mifarakano ambayo chimbuko lake ni tamaa ya madaraka na tuweze kujitolea mhanga pale inapokuwa tunaangalia maslahi ya Taifa na maslahi ya Bara la Afrika.

Ninashukuru mchango ulioongezwa wa Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwamba siyo tu alikuwa anashughulikia masuala ya Bara la Afrika, lakini hata kwenye eneo letu hili la Afrika Mashariki na Kati ameweza kutoa ushauri wa busara ambao ulikubalika mara moja wa kuunda Umoja wa Forodha utakaounganisha nchi za *SADC*, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi za *COMESA* ili tuweze kuharakisha maendeleo ya wananchi wetu. Ana mambo mengi aliyoyafanya.

Katika hoja yetu tulijibana kwa sababu ya muda. Tungeorodhesha, tusingemaliza. Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete ana busara nyingi, amefanya kazi nyingi sana na kwa kuleta hoja hii na ninyi mkaunga mkono, tunawashukuruni sana. Kwa hiyo, nisiendelee kuchukua muda wa Bunge kwa sababu tuna Azimio lingine fupi ili tuweze kukamilisha kazi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge Kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kazi Nzuri na Ufanisi Alioufanya katika Kipindi Chake cha Uenyekiti wa Umoja wa Afrika liliridhiwa na Bunge)*

## AZIMIO NA. 2

### Azimio la Bunge la Kuunga Mkono Uamuzi wa Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Kupeleka Kikosi cha Kulinda Amani Katika Jimbo la Darfur, Nchini Sudan

**MHE. WILSON M. MASILINGI – KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Azimio linalofuata na bila kuchukua muda mwingi zaidi, ninaomba niendelee kulisoma ili kuruhusu mjadala kuanza. Azimio la Bunge la Kuunga Mkono Uamuzi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete akiwa Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Kupeleka Kikosi cha Kulinda Amani Katika Jimbo la Darfur, Nchini Sudan.

**KWA KUWA,** Umoja wa Mataifa uliiomba rasmi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika shughuli za kulinda amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudan, kwa kutoa askari watakaojumuika na askari wa nchi nyingine kwenye majeshi ya pamoja ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika katika Jimbo la Darfur, Sudan *(UNAMID);*

**NA KWA KUWA,** nchi yetu kwa sasa haina sheria inayomruhusu Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kupeleka Vikosi vya Askari wa kulinda amani kwenye nchi nyingine; na pia kwa kuzingatia uharaka uliotakiwa wa kutekeleza ombi hilo la Umoja wa Mataifa ifikapo mwezi Machi, 2009;

**NA KWA KUWA,** Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe aliwasilisha ombi hilo kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili lijadiliwe;

**NA KWA KUWA,** baada ya kulijadili, Kamati hiyo ililiona ombi hilo kuwa ni heshima kubwa kwa Taifa letu kwa kuzingatia sifa ya Tanzania kuwa ni kielelezo cha amani na utulivu Duniani;

**NA KWA KUWA,** Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliamua kuliunga mkono ombi hilo;

**NA KWA KUWA,** Mchango wa Tanzania wa kupeleka kikosi cha askari wa kulinda amani kwenye nchi nyingine kitakuwa ni kitendo cha kipekee na cha kihistoria kutokana na ukweli kwamba Tanzania haijawahi kupeleka kikosi cha askari wa kulinda amani nje ya nchi chenye ukubwa wa kikosi kinachokusudiwa kupelekwa huko Darfur, nchini Sudan ambacho kitajitegemea kwa silaha, mpangilio na uongozi;

**NA KWA KUWA,** kikosi cha askari wa kulinda amani cha Tanzania kitaungana na vikosi vya nchi nyingine kadhaa ambavyo tayari vipo katika Jimbo la Darfur, nchini Sudan na kufanya idadi ya askari wa majeshi ya *UNAMID* kufikia 17,000 chini ya dhamana ya Umoja wa Mataifa;

**NA KWA KUWA,** jukumu la kikosi cha askari wa kulinda amani cha Tanzania, kama ilivyo kwa vikosi vya nchi nyingine, litakuwa ni kulinda amani na siyo kupigana vita;

**KWA HIYO BASI,** Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nne, linaazimia kwamba, kwa kauli moja, linaunga mkono uamuzi wa Mkuu wa Nchi, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kupeleka kikosi cha askari wa kulinda amani katika Jimbo la Darfur, nchini Sudan kuanzia mwezi Machi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Azimio la Bunge kumuunga mkono Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kupeleka Kikosi cha Kulinda amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1989 Rais wa sasa hivi wa Sudan aliongoza mapinduzi ya kijeshi na baada ya hapo Sudan ni nchi ya wapagani (watu wasio na dini), ni nchi ya Wakristo wale wa Kusini, ni nchi ya Waislam wale wa Kaskazini. Lakini hapo hapo ikaanzishwa *Sharia Law*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo makubwa sana nchini Sudan hasa baada ya kile kipindi. Wote tufahamu kwamba haki popote inapofanyika, huinua Taifa. Mwaka 1993, *The Revolution Council* ya Sudan walijiondoa na kuanzisha Utawala wa Kiraia na mchakato huu wa Civilian *Rules* ukaanza wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Sudan imekumbwa na matatizo mengi sana ya mapigano ya ndani kwa ndani kuanzia mwaka 2003. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa wale Wapiganaji wa Darfur walipoanza kupambana na Serikali yao. Hadi kufikia sasa hivi tunaambiwa zaidi ya watu 200,000 wamefariki dunia. Lakini, katika Darfur watu wengi wamefariki dunia siyo kwa sababu ya kupigwa risasi, lakini ni kwa sababu ya njaa, magonjwa na kwa sababu wengi hawa wako maeneo ambayo siyo makwao. Zaidi ya watu milioni 2.5 wamekuwa hawana makazi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Darfur lina moja ya tano ya *population* ya nchi ya Sudan na niliangalia dunia sasa hivi inatumia karibu bilioni moja kila mwaka kwa ajili ya kuwalisha chakula na misaada mingine ya kibinadamu kila mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ni nini, *US$, Tshs?*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** *US$.* Vile vile wanatumia zaidi ya dola za Kimarekani milioni 2.5 kwa ajili ya misaada inayokwenda katika shughuli za ulinzi wa amani. Hizi ni fedha nyingi, lakini watu hao wameteseka sana kwa sababu ya uongozi mbaya. Kama nilivyosema, pamoja na kwamba nchi yetu inachukua jukumu madhubuti la kupeleka Kikosi cha Kulinda amani cha kuungana na nchi nyingine, ninaomba itambulike kwamba Sudan kama Serikali, wamekuwa na matatizo makubwa sana ya kutoweza kuhimili hali ya amani katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanaoitwa *Janjaweed Militias*, ukienda Sudan unaambiwa hawa ni Waarabu, Wabantu au Waafrika, lakini wote ni weusi na wote wanafanana. Ukiangalia, huwezi ukatofautisha Mwarabu ni yupi na Mwaafrika ni yupi kwa sababu wana ngozi hiyo hiyo. Ukienda Khatoum, kila mtu anajiita ni Mwarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo hili limeua watu wengi sana katika Darfur. Kwa kipindi kirefu sana kabla ya Mheshimiwa Rais kuchukua uenyekiti, nchi nyingi za Afrika zilikuwa zimenyamaza, zilikuwa hazilizungumzii suala la Darfur kwamba ni tatizo kama vile ilivyokuwa kwa Mugabe, watu wake wanakufa, hali ni mbaya, lakini watu walikuwa wanalindana. Mheshimiwa Rais Kikwete alisimama kidete kama ilivyokuwa kwa upande wa Zimbabwe na kwa upande wa Sudan. Kwanza katika kuhimiza amani na mazungumzo yaliyofanyika chini ya Umoja wa Afrika na kupata mafanikio makubwa sana kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kwa mara ya kwanza Umoja wa Afrika unapeleka Jeshi kubwa sana Sudan, na ni matumaini yetu kwamba Jeshi hili litafanikiwa na kwamba Serikali ya Sudan haitaendelea kuwabugudhi. Tunafahamu baadhi ya majeshi yaliyokuwepo Sudan katika Darfur yamekuwa yakichokozwa ama na ***Malicious*** ama na wanajeshi wa Sudan kwa sababu wao wa *air power*, wana ndege za kivita na kadhalika. Sasa hivi katika azimio hili, Jeshi la Afrika linategemewa kuwa na watu 17,000 ni watu wachache sana, Umoja wa Mataifa miaka mitatu iliyopita walikisia wakasema Jeshi la watu 20,000 na Polisi wanaweza wakahimili kulinda amani ya Darfur pamoja na kutoa huduma za kipolisi ambazo zinahitajika kwa sababu kuna watu wengi sana. Watu milioni 2.5 ni zaidi ya wananchi wote wa Burundi. Kwa hiyo, ni eneo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Umoja wa Mataifa *Resolution* ya 1706 walitoa azimio hilo kwamba ni lazima kuwe na askari sio chini ya 20,000. Ningeomba na kusisitiza kwamba nchi nyingine za Afrika ziongeze idadi ya wanajeshi wafikie 20,000 kwa sababu tunataka wanajeshi wetu wakienda kule wawe salama na wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu Utawala wa Sudan. Hatuwezi kabisa sisi kama wananchi wa Afrika tukaendelea kuwafumbia macho watu ambao wanavunja haki za binadamu na kutokusaidia hali ya usalama wakati tunajua wana mafuta mengi, wana vifaa vingi vya kisasa na watu wao wanakufa njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sehemu kubwa sana ya kugharamia majeshi yanayokwenda itolewe na nchi ya Sudan kutokana na mali zao za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika kuunga kwangu mkono ninaliomba Jeshi la Tanzania wakati vijana hawa wanakwenda wapewe zana za kisasa, wawezeshwe vizuri waweze kupambana na hali yoyote itakayoweza kutokea katika eneo la vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa nitamke kwamba naiunga mkono hoja hii asilimia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nitoe pongezi kwa Mwenyekiti na Kamati yake ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kamati ya kudumu ya Bunge, kwa kubuni na kuleta hoja hii mbele yetu kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa hoja hii ni kwamba Nchi yetu mpaka sasa kama ilivyosemwa kwenye hoja yenyewe hatuna sheria ambayo inamruhusu au inayoweza kumwezesha Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu kupeleka majeshi kwenye *Peace Keeping Operations,* kwa hiyo, hatua hii ya kuileta hapa Bungeni na kupata ridhaa ya Bunge ni hatua muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina historia ya amani. Sisi ni wapenda amani sana na tumepigana vita moja tu katika kipindi cha uhai wa nchi yetu, lakini tumeshiriki katika kutatua migogoro mingi sana, tumewasaidia wenzetu wa kusini mwa Afrika ikiwemo Afrika Kusini, Angola, Msumbiji kujipatia uhuru kutoka katika makucha na mikono ya watu waliokuwa wanawatawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesaidia katika migogoro ya *Great Lakes Region* na Rais wetu ameshiriki toka alivyokuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na sasa ni Rais, katika kipindi chake cha urais tumeona amesaidia tena katika mgogoro wa Comoro ambapo tulikwenda na kumwondoa Ndugu Bakar ambaye aliingia kwa nguvu na sasa tunaombwa kutokana na sifa yetu nzuri na kutokana na umahiri wa majeshi yetu tumeombwa na Umoja wa Mataifa ili nasi tuchangie katika vikosi hivyo.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Kwenye maazimio kunakuwa na mwongozo wa Spika? Haya Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Kwa sababu wa sasa Mheshimiwa Waziri alipokuwa anachangia katika kuunga mkono hoja alisema kwa asilimia moja, sasa nataka kujua kuna utaratibu wa kuunga mkono asilimia moja au arekebishe kwa sababu ya taratibu za *Hansard*.

**WAZIRI WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilikosea kusema naomba *Hansard* irekodi kwamba naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema kwamba tumeshiriki katika *Peace Keeping operations* na kujaribu kuleta amani katika nchi nyingi sana ikiwemo *DRC*-Burundi, Rwanda na sasa tumeitwa twende Darfur kutoka na imani ambayo umoja wa mataifa inayo juu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wenzetu wa Kenya na Uganda wanashiriki kikamilifu katika kufanya biashara na *Southern* Sudan na wanafanya biashara kubwa sana. Sasa sisi tunapeleka majeshi, tumeombwa tupeleke Majeshi na tutapeleka majeshi yetu Darful na tukishakamilisha hiyo au hata kabla hatujakamilisha wananchi wetu waanze na wao kuzitumia fursa hizi za kufanya biashara nzuri na *Southern* Sudan tusipeleke Majeshi peke yake halafu huku hatupati faida nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wananchi wetu na hasa wafanyabiashara wetu waanze kuchangamkia fursa hizi za kufanya biashara na *Southern* Sudan kwa sababu hii kwanza itatupa nguvu zaidi na sababu kubwa zaidi ya kuendelea kupeleka majeshi yetu kule na kutafuta amani katika Durfur.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nchi nyingi zimeomba kwamba huyu Bwana Bashir apelekwe kwenye *International Criminal Court*(*ICC*), Tanzania pamoja na nchi nyingine za Afrika zimesema hapana asipelekwe kwa sasa, akipelekwa sasa haitasaidia kupatikana amani kwa Sudan, kwa sababu tunaamini pia tuanze kuleta amani halafu mambo ya *Justice* yafuate baadaye, kwa sababu wakimpeleka kule Mahakamani anaweza akakutwa kweli ana makosa lakini vurugu itakayokuwako huko Sudani haitawasaidia wananchi wa Sudan. Kwa hiyo, tuanze kutafuta amani halafu *Justice* itafuata na *Justice* tunayoitaka sisi iwe ni ile *restorative Justice* ambayo haina mtu wa kusema huyu kashindwa, huyu kashinda ila ni ile ya kuwa watu mnakaa pamoja mnaunda labda *reconciliation Commission* ambayo mtu anakwenda na kukubali makosa yake mnasameheana ili nchi iweze kwenda mbele, mtakapofikia hatua ya kumfunga au kumnyonga huyu bwana ana makundi yake na yale makundi yataendeleza uhasama katika Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili hatuliungi mkono. Kwa hiyo, tunaunga mkono kwa nchi yetu kusema kwamba wasimshitaki Bashir kwa sasa lakini kwanza tutafute amani kisha tutatafuta *Justice*.

Mhehsimiwa Naibu Spika, nilitaka tu niseme kwamba Rais wetu amekuwa makini sana na ametoa mchango mkubwa sana katika masuala ya *peace Keeping* katika Afrika na katika dunia kwa ujumla na ombi hili lililetwa na Umoja wa Mataifa. Sisi tulikubali na Bunge naomba nalo likubali kwamba tutoe tamko hapa la kuunga mkono azimio hili ili Rais wetu aweze kupata nguvu ya kupeleka Majeshi yetu huko Sudan ili yakasaidie katika *Peace Keeping Operations*. Naomba kusema, naunga mkono hoja ya azimio hili na tulipitishe. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MCHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii inayokidhi matakwa ya kikatiba, Ibara ya 44 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni sehemu muhimu ya jumuiya ya Kimataifa iliyojijengea heshima kubwa tangu uhuru miaka 48 iliyopita kama nchi iliyo mstari wa mbele katika kupigania haki, uhuru, usalama na umoja Duniani. Hivyo basi, hatuna budui kushiriki kwenye kampeni hii ya Kimataifa ya kulinda amani Darfur kufuatia uamuzi wa Baraza la Usalama la Umoja la Mataifa kuridhia mpango wa kupeleka askari 26,000 wa kulinda amani huko Sudan.

Mheshimiwa Spika, tunaenda Darfur kama sehemu ya majeshi ya kulinda amani ya *AU*. Tusingeweza kubaki nyuma kutokana na historia yetu na nafasi tuliyokuwa nayo ya uongozi wa *AU*.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya watu 200,000 wamepoteza maisha na watu zaidi ya milioni 2.5 hawana mahali pa kuishi kutokana na mgogoro huo ulioanza 2003. Sitakuwa na sababu za msingi kutokuunga mkono Azimio hili.

**MHE. WILSON M. MASILINGI-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa tena niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu azimio ambalo linatamka bayana;

Azimio la Bunge la kuunga uamuzi wa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wa kupeleka kikosi cha kulinda amani katika Jimbo la Darful, nchini Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha kabisa, kama ilivyo utaratibu katika Bunge letu, niwatambue waliochangia kwa kuzungumza. Kwanza ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, ninawashukuru sana hawa waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi na

Wabunge wote mliojaa kwenye ukumbi huu kwa kushiriki kuunga mkono azimio hili la Bunge liweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kuongeza idadi ya wanajeshi ili kuimarisha ulinzi au utunzaji wa amani ndani ya Darful kutoka nchi nyingine tutalifikisha kwa wahusika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa waweze kushauriana namna ya kulifikisha kunakohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sudan kugharamia *Operation* kutokana na mafuta yao ni ushauri mzuri na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itashauriwa na izingatie na kufikiria na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, mambo aliyotueleza ni ya msingi latika kuunga mkono hoja mia kwa mia tunayatambua mawazo yake na kuyaheshimu kwa sababu ndiyo anatoka upande wa Serikali lakini kwa sababu yeye ni sehemu ya Bunge na ni Azimio la Bunge ameongeza nguvu sana katika msingi mzima wa Azimio lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi wameunga mkono mia kwa mia Azimio lenyewe na ushauri uliotolewa ni huo huo kama ulivyo kwenye Azimio lenyewe. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima ninaomba tulipitishe Azimio hili kwa kauli moja kama mlivyoanza mhitimishe kwa kauli moja ili tuweze kushiriki katika ulinzi wa amani nchini Sudani katika eneo la Darful.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Waunge mtaona kwamba Kambi ya Upinzani hawajasema taarifa walizotoa kwa Kiti ni kwamba wao ni Wajumbe wa Kamati hii kwa hiyo walishiriki kikamilifu kwenye eneo walipokuwa kwenye Kamati.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge Kuunga Mkono Uamuzi wa Mkuu wa nchi,*
*Kiongozi wa Serikali, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi*
*na Usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*wa Kupeleka Kikosi cha Kulinda Amani katika*
*Jimbo la Darfur, Nchini Sudan*
*liliridhiwa na Bunge)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka

**wa Fedha 2009/2010**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Kufuatana na muda mpaka saa saba tunaweza kupata wachangiaji watatu. Tutaanza na Mheshimiwa Omar Kwaang'w, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Habibu Mnyaa atafuatia.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru na kutokana na muda nitajitahidi kusema machache na pengine kupanga yale ambayo yanawezekana kwa muda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu umepangwa kwa kuzingatia dira ya Taifa ya maendeleo kufikia mwaka 2025. Vilevile imepangwa kwa kuangalia Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, lakini vile vile na malengo ya milenia pamoja na MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwanzo huu ningependa nitumie nafasi hii tuone nguvu za wananchi, kuna haja ya kupongeza nguvu za wananchi katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kwanza kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa kushiriki vizuri kwa nguvu zao katika kuchangia maendeleo ya Taifa hili na hususani katika sekta ya elimu, wananchi wa Jimbo la Babati Mjini pamoja na viongozi wao Waheshimiwa Madiwani watendaji na wengine wote wamejitahidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga shule za sekondari kwa Kata zote kwa Jimbo hilo. Nawapongeza sana na mimi nipo pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niingie katika mpango wenyewe, nianze na sekta ya barabara, sekta ya barabara ndiyo sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kwa sababu sekta nyingine zote iwe ya elimu, ukitaka kusambaza elimu utatumia barabara, ukitaka kusambaza maji utatumia barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna haja ya kufungua nchi kwa sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba barabara kuu zinakamilika na kuunganisha nchi hii ili kwa kweli tuinue uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba mpango huu umegusa Ilani ya CCM kwanza nianze kusema kwamba kama mpango huu umezingatia ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ruhusa yako kifungu cha 125(b) kinasema kwamba; kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa-Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara ya Miundombinu ilitoa taarifa yake ya utekelezaji wa ilani lakini katika ile taarifa sikuona hii barabara kutoka Mijingu, Dodoma mpaka Iringa. Sikuiona kabisa! Katika mpango huu wa sasa iko wapi?

Ningependa kujua kama kweli tunaangalia ilani na kwa namna ambavyo imeelekezwa hapa, ningependa nione kwamba tunachukua hatua gani kuona kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami kwa ahadi ya miaka mitano hii mpaka 2010 ambayo ni mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika mtandao wa barabara, lengo ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na uzalishaji mzuri na kuhakikisha kwamba barabara inatumika vizuri. Barabara ya kutoka Minjingu-Babati kwenda Singida nina hakika malengo yake vilevile ni kuunganisha barabara kutoka Bandari ya Tanga kuja mpaka Arusha Babati, Singida, Shinyanga na Mwanza ili bidhaa zinazotoka kwenye bandari ya Tanga ziweze kufika na kwenda kwenye nchi jirani, ndiyo namna ya kuunganisha ili kuhakikisha kwamba tunavuna mapato yanayotokana na uunganishaji wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii katika taarifa niliyosoma ya Wizara ya Miundombinu, maandalizi yote yamekamilika, lakini wameeleza kwamba mkataba haujasainiwa, sasa tunataka kujua mkataba unasainiwa lini ili barabara ya kutoka Minjingu, Babati, kwenda Singida inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona juzi kwamba tayari wakandarasi wameteuliwa na pale Magugu Mkandarasi ameanza kujenga kambi yake, lakini taarifa iliyopo ni kwamba mkataba haujasainiwa. Kama umesainiwa sasa, tungependa tufahamu ili tuone barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa kwenye sekta hii, barabara ambayo inatumia fedha nyingi sana kwa kweli ni ubadhirifu, ni changamoto kubwa sana na hasa hii inayotokana na wakandarasi kushindwa kumaliza kazi na baadaye kuleta hasara kubwa sana kwa nchi. Sina haja ya kuiendeleza sana kwa sababu katika maswali ya hivi karibuni tumesikia jinsi ambavyo Wakandarasi wanavyoshindwa kumaliza kazi na kuweka hasara kubwa sana kwa nchi. Fedha ambazo zingeweza kuokolewa zingeweza kujenga shule zetu zote na zingeweza kuimarisha hata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba Serikali iweke udhibiti wa kutosha katika eneo hili la Wakandarasi, hapo tunaweza tukasogea badala ya fedha nyingi sasa kuanza kutumika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni sekta ya elimu. Nilikuwa naangalia ugawaji wa fedha katika sekta hii ya elimu. Mwaka jana tulikubaliana kwamba asilimia 19.8 ambayo ndiyo kipaumbele kwa nchi hii iende kwenye sekta ya elimu, fedha zimekwenda, lakini ukiangalia ugawaji wa fedha hizo kwa sekta yenyewe, elimu ya msingi na awali inapata asilimia 67.4, halafu elimu ya sekondari inapewa asilimia 9.2 kwa mgao huo huo, elimu ya vyuo vya ualimu inapata asilimia 1.7 na ukaguzi wanapata asilimia 0.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya juu pamoja na Vyuo Vikuu na Taasisi zake zote za elimu ya juu wanapata asilimia 23.3 tu. Ugawaji wa namna hii wa rasilimali unaathiri sana maendeleo ya nchi na hasa ukiangalia elimu ya juu ambayo ina mambo

mengi sana. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia ugawaji wa namna hii. Tunasema kipaumbele kwenye elimu, lakini ukienda kwenye elimu ule ugawaji unakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine Serikali ina haja ya kuangalia vizuri zaidi matatizo yanayoikabili sekta ya elimu ya juu na sekta ya elimu ya kawaida ya sekondari na elimu ya chini ili kuona kwamba ni namna gani tunaweza kuwekeza kwenye sekta ya elimu.

Meshimiwa Naibu Spika, sina uhakika lakini muundo wa Wizara sasa nadhani ndiyo unaleta matatizo, pengine kuna haja ya Serikali kuangalia muundo mpya wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, vinginevyo ugawaji wa rasilimali katika eno hili uzingatie sana mahitaji muhimu kwenye sehemu zake zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye sekta ya afya. Katika Sekta ya Afya, kwanza niseme kwamba sasa hivi tupo kwenye robo ya tatu ya bajeti ya Serikali kama sikosei. Lakini fedha za maendeleo hazijakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Tumebakiza kota moja, sasa sijui miradi hii ambayo mwaka jana tumeipigia kelele sana hapa inatekelezwa namna gani? Mfano Mkoa wa Manyara tulikubaliana kwamba hapa Serikali itatoa shilingi bilioni mbili kuanza ujenzi wa hospitali ya Mkoa, mimi sijaona lolote! Mpaka sasa sijui ni matayarisho gani yanafanyika; sina hakika kama Wizara ya Fedha imetoa hizo bilioni mbili ili sasa itakapofikia mwezi wa sita nyingine ziombwe na tujue kwamba ujenzi wa hospitali umekwishaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ni mingi, nimetoa mfano wa hospitali ya Mkoa wa Manyara pale Babati na nina hakika pengine katika maeneo mengine fedha za maendeleo hazijatoka, hata tulipokuwa tunatembelea kwenye vyuo vikuu Serikali haijatoa fedha za maendeleo na sasa ni kota ya tatu, tumebakiza kota moja tu sasa sijui katika mpango huu tunatekelezaje malengo haya tunayoyasema ya MKUKUTA, Millenia, kuzingatia ilani na mambo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme hilo katika eneo hilo, lakini kwenye sekta ya afya nataka niseme kidogo juu ya eneo hili la dawa. Serikali inatumia fedha nyingi sana kununua dawa na tumekuwa tukiilaumu *MSD* kwamba hatupati dawa. Lakini je, tunaangalia wadau wengine wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi bei ya dawa inapanda kama mafuta yanavyopanda na kushuka, sasa tunahitaji nini? *EWURA* nyingine ya kuangalia kwamba bei za dawa hazipandi bila utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani Serikali iangalie kwamba dawa zake nyingi zinakwenda kwenye maeneo ambako mimi nadhani kuna tatizo kubwa. Kwa hiyo, eneo hili la dawa ni muhimu sana kwa sababu ya mambo ambayo tumejiwekea kwenye huduma ya Mama na Mtoto, Wajawazito pamoja na Wazee hawapati hizi huduma sawasawa. Ni lazima Serikali ijue udhibiti wa dawa unakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kilimo. Naona kengele ya kwanza imelia. Naomba Waziri wa Kilimo anisikilize vizuri. Kuhusu vocha za pembejeo, hapa tumepitisha fedha zile za *EPA* karibu milioni 40 kwenda kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula, hizi vocha za pembejeo zina matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hazijakwenda kwa walengwa na ninataka niseme kwamba katika utaratibu huu mmeweka urasimu mkubwa sana. Urasimu wa kwanza katika kugawa zile vocha kunakuwa na Afisa Kilimo, Mtendaji wa Kijiji pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji, halafu kuna Wakala na Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, *systems* zote hizo zimeleta matatizo makubwa sana. Kwanza, katika utaratibu wa vocha, wapo watu ambao wamekwenda kuchukua hizo vocha, hawana mashamba. Pili wapo ambao wamechukua mbegu tu wameacha mbolea na vile vile wapo ambao wamechukua fedha na wakazitumia katika kununulia vitu vingine, iwe *cement*, baiskeli na vitu vingine. Sina matatizo na hayo lakini kwa kweli kama tunataka kumlenga mkulima ili tupate mapinduzi ya kilimo, utaratibu huu kwa kweli wa kuwa na urasimu wa watu wengi namna hii haufai.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu hivi haviendi kwa mkulima kwa sababu vingine vinabaki kwa wakala. Wakala atapeleka benki vocha zake, atalipwa fedha zake na bado atakuwa amebakiwa na mbolea pamoja na mbegu; zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani utaratibu mzuri ni wakulima hawa tuwakopeshe. Wana dhamana ambayo ndiyo shamba lile, siyo kuwaambia walete fedha nusu halafu na sisi tunaweka ruzuku, hapana! Tuwakopeshe na iundwe Kamati pale Kijijini, itajua huyu mtu ana shamba ekari moja na anakopeshwa mbolea pamoja na mbegu halafu anasimamiwa na kuonyesha kwamba kweli amepanda na pale tutajua kwamba kwa ekari moja uzalishaji unapanda kiasi gani kama tunataka kulenga pengine watu elfu kumi ndiyo tutaweza kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawakopesha watu wengine kwa kuangalia *salary slip*, kwa nini tusiwakopeshe hawa wakulima kwa kuangalia shamba lake hilo la ekari moja? Ili kuhakikisha kwamba baada ya mavuno basi dhamana yake ipo pale, hiyo laki karibu na elfu sitini ambayo ingepita kwenye pembejeo angeweza sasa kulipa. Lakini utaratibu wa warasimu wote hawa kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Tunahitaji kudhibiti na mimi napendekeza namna nzuri ni kumkopesha mkulima kwa ekari moja ili tuone mapinduzi ya kilimo katika ekari moja tunapata nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hizi vocha, ambao wamechukua hizi mbegu, kwa kweli wanachofanya ni kuuza mbegu na wengine wengi waliochukua hawana mashamba, kwa hiyo, wanauza hizo mbegu. Sasa fedha hizo tumezipitisha hapa hazitakwenda kufanya chochote, hakuna mbolea iliyoingizwa shambani wala mbegu, zitabaki kwa mawakala na kwa watu wengine wenye uwezo na sisi tunaka kulenga watu wa kipato cha chini ili wafanye mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia mpango huu wa mwongozo wa bajeti mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watalaamu wote wanaoshughulika na mipango Wizara ya Fedha kuhusu mpangilio mzima wa kuhakikisha kwamba Tanzania mwakani tunapunguza tegemeo la nje, lakini pia kuhakikisha kwamba wananchi wetu nao wanafaidika na matunda yanayozalishwa na jasho lao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niende moja kwa moja ukurasa wa 13 wa kitabu hiki cha mwongozo kama walivyoandika watalaamu wetu na Mawaziri wetu, naanzia upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi imegawanyika katika sehemu nyingi na kila mmoja kama tunavyosema ina mambo ambayo inabidi yapate kipaumbele. Ukurasa wa 14 katika upande wa miundombinu kwamba Tanzania kuwa kituo na sehemu muhimu ya biashara ya usafirishaji, mawasiliano ya kikanda na kimataifa kwa kuendeleza na kuendeleza Bandari za Dar es Salaam Mtwara na Kigoma, reli ya kati, barabara na viwanja vya ndege, mimi nasema hili ndilo jambo pekee ambalo litaweza kuikomboa kama wachangiaji wengine walivyosema kwamba bila ya miundombinu bora nchi hii hatuwezi kuendelea. Kwa hiyo, barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, ni lazima ziboreshwe na zipewe kipaumbele katika bajeti ijayo na wananchi waweze kufaidika na kuweza kupata matunda kupitia njia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba kwamba katika mpango huu wa bajeti jamani angalieni bandari ya Mafia, tumechoka kuchonyotwa na chumvi. Chumvi inachonyota maji ya bahari yanapoingia kwenye kidonga au sehemu inayokuwa wazi inaumiza. Ndugu zangu msiopita baharini hali ni mbaya sana, kuna vijidudu vinavyoathiri miili yetu, kuna mapanga yanakata, kuna urumba na kuna takataka nyingi. Tumechoka, tunaomba tutengenezeeni bandari na mchakato uanze hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaosema, hata kule Jimboni tunaonekana kama sisi kazi yetu ni kusubiri uchaguzi ndiyo tunalisema jambo hili, tunaomba bajeti ya safari hii mamlaka ya bandari pesa ilizokuwa nazo tujenge wenyewe bandari kwa pesa zetu, toeni pesa hata kama ingelikuwa bilioni ngapi, hakikisheni mwaka 2009 bandari inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ninalotaka kulizungumza ni kwamba moja ya mambo ambayo tunaathirika, pia katika kuboresha taaluma zetu, elimu hata biashara, kilimo ni watalaamu, kwa hiyo, Serikali muweke mafungu maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata kusomesha vijana wetu na tunapata wataalamu hasa wa kada ya afya kwa maana ya madaktari na wauguzi, Walimu na maafisa ugani wa kilimo na mifugo bila ya hivyo haya yote tunayofanya bila ya kuwa na wataalamu hakuna tutakachokuwa tunakifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kazi yetu sisi kutangaza, leo kutakuwa na semina kuhusu kongomano la kilimo cha aina fulani cha madarasa, mtaalam hakuna, anakwenda anababaisha pale wakiondoa pale wanaacha vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba hili Serikali iangalie, wataalam ni jambo la muhimu sana na vituo vya utafiti wavipe kipaumbele ama vyuo vya misitu ama vyuo vya kilimo na ufugaji, bila utafiti hakuna kitu kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine mimi nafikiri hakuna hata Mbunge mmoja ama mwananchi au kiongozi yeyote ambaye katika nchi hii atasema maji yasipewe kipaumbele. Kwa hiyo, naomba sana bajeti ijayo wahakikishe kwamba maji hasa ya kunywa kwa binadamu na mifugo yao lazima tuyape kipaumbele kwamba fedha zitengwe. Lakini nashukuru, kuna mpango mzuri tu wa Serikali ambao baadaye itautangaza kuhusu masuala ya maji. Kwa hiyo, naamini kwamba suala la maji, basi tulipunguze kwa kule vijijini kutoka hiyo asilimia tunayosema 65 ifikie au izidi, bila hivyo, kila siku tutakuwa tunasema tu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali suala la maji pia liweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati nayo tunaomba sana na hasa ninapozungumzia masuala ya Wilaya hizi ambazo hazijapata kabisa umeme, lakini zipo Wilaya ambazo zimepata umeme, sisi tunamshukuru Mungu toka zamani kama Mafia, lakini hadi leo umeme ule umekuwa sasa kama adha, ni kwamba mashine zimechoka. Hivyo, kuna taabu gani na hasa baada ya kuangalia kwamba sisi tumetengwa, adhabu ya Kisiwa, leo mtu Dar es Salaam tu hapo Jijini umeme ukikatika adha yake inavyokuwa wewe mwenyewe unajiona hapo Mheshimiwa. Lakini hebu sisi tuliokuwa pembeni hali ikoje? Kwa hiyo, mtuangalie, mmetuambia kwamba Wizara ya Nishati na Madini ilisema kuna mashine zipo Njombe, tuleeteni Mafia ziweze kutusaidia na hizo mashine zikifika au Serikali wakati inaandaa bajeti yake, basi itenge fungu maalum kwa ajili ya mambo ya nishati na kuweza kusambaza umeme vijijini na sisi Mafia tupatiwe mitambo na hizo fedha zitarudi sio kwamba watu wanatumia bure. Kwa hiyo, hilo naomba nilisisitize.

Suala la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni katika ukurasa wa 15 katika kitabu chetu hiki cha Mwongozo huu wa Mpango wa Bajeti eneo (c) uvuvi. Maana yake bila kusema uvuvi hali yote itakuwa hakuna. Katika kitabu hiki wanasema: “Serikali itaendelea kuboresha uvuvi kwa kuhimiza matumizi ya dhana bora na za kisasa, kudhibiti uvuvi haramu na kuhamasisha uvuvi wa samaki.” Tunalikubali kabisa mia kwa mia. Lakini hebu angalia kwamba sisi kazi yetu itakuwa kuhamasisha na kuzuia, tunamsaidia vipi huyu mvuvi. Leo Serikali imetenga mabilioni ya fedha kwa ajili ya dhana za kilimo kwa maana ya pembejeo na mbolea, imetenga mabilioni ya fedha kwa ajili ya madawa ya mifugo na mambo mengine tunakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huyu mvuvi mnafikiria vipi? Ndiyo hata juzi Mheshimiwa Mbunge mmoja wakati anachangia alisema kwamba; hivi hao watu wa Mipango wana *allergy* gani na wavuvi? Wakati mwingine tunasema Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ana-*panic*, anafanya hivi, hatusemi hivyo, kwa nia

mbaya, lakini kumbe wataalam wetu wa mipango hawatilii maanani suala la uvuvi. Sasa nawaomba sana Mawaziri hao mliokaa mhakikishe kwamba uvuvi ni kitu ambacho pato lake ni papo kwa papo. Ukiwa na zana ukienda baharini ukivua ukipata samaki unapata hela. Hivyo mnaona taabu gani kumchukulia *guarantee* mvuvi wa kuweza kumkopesha au kutenga fedha za ruzuku kwa ajili ya zana na nyenzo za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hebu angalia zana za kilimo zilivyokuwa ghali, matrekta ni mamilioni mangapi, lakini uvuvi bei zake sio kubwa sana, labda nyavu ndiyo tutasema shilingi milioni tano hadi saba ni sawasawa na ile *power tiller* moja. Lakini mvuvi akienda baharini kwanza haichukui mwaka usubiri mvua, usubiri sijui jua kali, Mungu ajalie hiki, ukienda baharini Mwenyezi Mungu anakupa riziki yako ya uvuvi, unarudisha, unalipa hela. Sasa nini kinawapeni uzito kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya wavuvi au kuwawezesha wakope na kama tutafanya hivyo, basi Serikali itaweza kupata na kuchangiwa kwa kiasi kikubwa kabisa katika pato lake kupitia uvuvi. Kila siku Mheshimiwa John Magufuli hapa anasema kuna meli zinavua samaki na kama tutakuwa tunawapa nafasi wavuvi hawa, yaani pato la Taifa litakua, sasa mnategemea meli tu. Sasa mnasema nini kuhusu suala la wavuvi wadogo wadogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tupe imani kwa wavuvi hawa, tuwakopeshe na watalipa, hawana matatizo. Kwa hiyo, naomba sana mwaka unaokuja wa fedha wahakikishie kwamba kunakuwa na fedha maalum za kuhakikisha wavuvi wanapata zana bora. Hebu leo mtangaze kama Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi anasema zikusanye nyavu zote na zichomwe moto, tunakubali. Sasa nyavu zikishachomwa moto, yule mtu unamsaidia nini? Hivyo mifugo inavyoharibu mazingira, katika nchi hii mbona hamjakwenda pale Ihefu wakapigwa risasi ng’ombe, lakini walisangwa vizuri wakawaambieni wapelekeeni maeneo haya, nenda hivi, mabwawa wakajenga, wakafanyia hivyo, watu wanaendelea na maisha na ndiyo ubinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo mvuvi, ile bahari inaonekana kama ni sumu, anajuta kuzaliwa karibu na bahari, kwa nini? Mheshimiwa Rais amesema kabisa kwamba sasa mifugo iungane na uvuvi ili wananchi wake waweze kuboreka.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa kupitia ile kauli ya Rais wakati anaandaa mchakato huu wa kuchanganya Wizara kwamba sasa wavuvi waweze kufikiriwa, waweze kupata ruzuku, wapewe nyenzo kwa kukopesha na wao waweze kuchangia na kujiondoa na umaskini. Hebu angalieni umaskini, si ukanda wa Pwani, lakini hata kwenye Maziwa kando kando mle utakuta wananchi wake wote ni maskini, hawana uwezo. Sasa tuwasaidie tuwape kipaumbele wavuvi hao waweze kuhakikisha kwamba wanaboreka na wao wanakuwa mmoja ya watu wanaochangia pato katika Halmashauri zao na Taifa zima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kusema zaidi ya hayo, ila ni kusisitiza tu kwamba gati la Mafia, uwanja wa ndege asije akatokea mdudu mtu tena akasema sijui *millennium challenge account* sijui kuna hili, kuna hili, hapana. Fedha zetu zipo zimetamkwa, uwanja wa ndege ukamilishwe, gati la Mafia lijengwe na wavuvi wapate zana na nyenzo bora na wakopeshwe kama wanavyofanywa wakulima na wafugaji. Hata

mzee Marehemu Makongoro alisema,  Kuleni chakula bora, kuku, samaki na maziwa, unaona hata hiyo nyama imewekwa pembeni, lakini samaki katamkwa, liangalieni hili kwa maana afya zetu ni pato la nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naomba tu nisisitize hayo niliyosema na kuwatakia kila la kheri katika mpango mzima wa maendeleo ya nchi yetu.  Nashukuru sana, ahsante sana.  *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia mwongozo huo wa utayarishaji wa mpango wa bajeti.

Kwa kuwa katika Mkutano huu wa Kumi na Nne ni mara yangu ya kwanza kuchangia na mimi naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mbeya Vijijini ambao kwa kweli katika siku 20 tulipokuwepo na walivyotuunga mkono Wapinzani ni jambo la kufurahisha na yaliyotokea menginie wanayajua wenyewe na suala kwamba "kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi."  "Lililopita si ndwele tugange yajayo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo na mimi ninapenda niingie katika mchango huu wa utayarishaji wa mpango wa bajeti na nasukumwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika nyongeza ile ukurasa wa 128 (2) na kifungu (12) na hapa nataka kuzungumzia suala la umeme Pemba.

Kwa muda kama miaka 20 na bahati nzuri katika Manaibu, mmoja anayafahamu vizuri sana kwamba tumekuwa tukizungumzia umeme Pemba bila ya mafanikio. Lakini sasa hivi matumaini ni makubwa na inaonekana mambo yanatia sura. *(Makofi)*

Isipokuwa katika hali iliyoko na umeme unaotaka kupelekwa, kuna matatizo ambayo yametokana na ufinyu wa fedha ambapo Wizara haina budi kuchangia suala hilo na kutoa matatizo.  Mpango ulioko ukiacha uendelee kama ulivyo, basi utakuwa mkubwa. Ningependa nieleze na kwa vile watalaam wapo wanasikia wataona hali yenyewe. Mwaka 1978 na 1979 kulipokuwa na mpango wa kupeleka umeme Kisiwa cha Unguja ambapo masafa yale yalikuwa ni kilomita 38.5 kutoa Rasi Kilomoni kwenda Fumba umeme uliopelekwa ulikuwa na nguvu za MW 45 na line yenyewe ilikuwa na msongo wa KV 132.

Sasa baada ya muda kama miaka 28 *line cable* ile imezidiwa nguvu na katika mpango wa *Millennium Challenge* ndiyo maana zimetengwa dola 53.5 ili kuweka *cable* nyingine kwa ajili ya kusaidia Kisiwa cha Unguja na matatizo ya umeme yaliyopo sasa hivi. Sasa ikiwa kilomita 38.5 tuliweka umeme wenye msongo wa *KV 132,* leo iweje katika huu mpango wa Pemba ambapo kuna kilomita 72 za baharini halafu kuna kilomita sita za Tanga na kuna kilomita tisa kutoka Wesha mpaka Tibilizi, jumla ya kilomita 87 inataka kuwekwa *cable* yenye msongo wa *KV 33* ambazo baada ya kufika Tibilizi ziunge *line* nyingine ambayo inakwenda kama kilomita 25 Konde kufanya jumla ya kilomita 127 halafu kwenda Kusini mpaka Mkoani na Makombeni ziunge line nyingine ya 33 kufanya

kilomita 117. Kiufundi hii itakuwa ni tatizo. Angalau ingekuwa *cable* ile ina msongo wa *KV 66* hapo ingesaidia pakawa na kituo cha *transforma* cha kupoteza kutoka 66 kwenda 35 ikaungana na *line* nyingine.

Lakini mambo hayakupangwa hivyo na kwa sababu *fund* iliyotoka Norwad ya *Norwegian crone* 400 ni ndogo mno. Wizara yako ya Fedha katika mpango huu sijaona kitu hicho na ikifanywa na *cable* yenyewe yenye *MW 20* na kutokana na mahitaji makubwa hata miaka mitatu haifiki, miaka miwili. Ikiwa leo katika Kisiwa cha Unguja ukitoka Mjini Mtoni ukifika Nungwi kilomita 60 tayari umeme una matatizo makubwa kule sasa hivi. Je, iweje leo kilomita 87 au 127 upelekwe Msongo wa KV 33? Ama sijui hawa wenzetu wa Shirika la Umeme *ZECO* au Wizara inayohusika Zanzibar, wameomba kuongezewa hiyo *fund* au hawajaomba. Lakini kwa vyovyote Wizara ina wajibu angalau wananchi wa Kisiwa cha Pemba wasiwe *isolated* kwa muda mrefu kuhusu matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nilitoa angalizo na Mheshimiwa Waziri analifahamu na tumeshawahi kuzungumza.

**NAIBU SPIKA:** Kwa angalizo hilo, huyu Mheshimiwa ni *Engineer* wa umeme. Kwa hiyo, mambo anayosema ana uhakika nayo.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo na tumeshawahi kuzungumza na naomba katika mpango huu zitaongezwa hizo fedha whether wameomba, hawajaomba watatusikia wataomba. Lakini hiyo cable angalau iwe ni msongo wa *KV. 66* siyo 33 ikawa tuwafurahishe lakini kukawa kuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hapo hapo kuna bandari hii ambayo katika mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Bandari ya Mkumbuu na katika ukurasa wa 14 bandari zilizotajwa haijatajwa na mpango huu unakwenda mpaka 2012. Kwa hiyo, ni vyema tuone katika mpango huu katika bajeti hii Bandari ya Mkumbuu inatajwa na inapangiwa hela angalau kwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililokusudia kulizungumza ni hali ya uchumi na kuanguka kwa thamani ya shilingi. Hili kabla ya kuendelea ningeomba ninukuu. Hivi juzi tarehe 5 tulipokuwa na semina Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alikiri na kusema haya, kushuka kwa ukuaji wa uchumi na kiwango cha matumizi kutapunguza kasi ya ukuaji wa mapato yatokana na kodi na hivyo kuathiri bajeti ya Serikali katika muda wa kati. Halafu akaendelea kusema kwamba kushuka kwa thamani ya shilingi kunaweza kuchangia kuongezeka kiwango cha mfumko wa bei. Kwa maana hiyo, mimi ninachotaka kuliongelea hapa ni kwamba hivi tujiulize ni kwa nini shilingi yetu ishuke thamani siku hadi siku? Suala hili tumewahi kulizungumza hapa Bungeni na Waziri akaleta maelezo tamko la *dolarisation*.

Lakini mpaka sasa hivi hatujaona juhudi za makusudi za Benki Kuu za kuona shilingi yetu inaongezeka thamani. Cha kusikitisha zaidi kwamba hizi jirani zetu zilizotuzunguka fedha yao inaongezeka thamani na kiuchumi inaonekana wao wana

mahitaji zaidi kwetu kuliko sisi tulivyo na mahitaji kwao. Mfano mmoja hapo Songwe Mbeya pale juzi tumetembelea tulipokwenda Kiwira unakuta kwamba wale wanaozungusha fedha zile shilingi kwacha ya Malawi 500 ni Sh. 4,000/= za Tanzania. Lakini sisi tunategemea nini Malawi? Ni sukari tu Malawi vitu vyote wanachukua Tanzania. Iweje leo sisi fedha yetu iwe haina thamani kuliko fedha ya Malawi? *(Makofi)*

Vivyo hivyo *Mozambique*, hapo zamani tulikuwa tunanunua vitu vingi kutoka Kenya, lakini sasa Kenya Viwanda vyao wananunua mambo mengi sana kutoka Tanzania, lakini bado fedha yao wao ina thamani sisi yetu inashuka, kila siku inashuka. Suala hili tunataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupe maelezo, ni mikakati gani ya makusudi ya Benki Kuu itakayofanya fedha yetu kuwa na thamani? Hatuwezi kuendelea miaka yote kuona shilingi yetu inapoteza thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ziko nyingi, sababu ziko wazi sana na ifanywe *survey* ndogo tu. Leo mtu hapa aende kwenye mahoteli, ukifika unataka chumba cha kulala unaambiwa hoteli hii chumba dola fulani, huambiwi Tanzania Shilingi fulani. Kama huna ile Tanzania Shilingi ndiyo ukapewa *exchange rate* ya dola kwa kuongezewa thamani ya shilingi yetu.

Ukienda Kenya ukicheki Mahoteli yote huwezi ukaambiwa hapa Hoteli Dola fulani, hapana, wanakwambia ni Kenya shilingi fulani. Kwa hiyo, mifano iko mingi, tunataka tuone Wizara ya Fedha, Benki Kuu yetu inaweka misingi inayojulikana ya kuwa namna gani fedha yetu inaongezeka thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele inaanza kulia. Nakumbuka maoni ya Kamati ukurasa wa nane imezungumzia kwamba kuna tatizo, nchi yetu hapa uzalishaji wa umeme, katika takwimu zilizopo vyanzo vyetu vya umeme vyote viko MW 106. Lakini uwezo vinavyozalisha hivi sasa ni MW 542 na *average* ya wastani wa matumizi yanayohitajika ni MW 570 na ndiyo maana tarehe 14 Desemba, Waziri wa Nishati aliwahi hata kuishawishi Kamati ya Nishati na Madini kununua mitambo ya Dowans. Tukatamkiwa kwamba ilikuwa bilioni 70. Sasa tunafanya nini, kwa sababu kushuka kwa kiwango kutoka 1006 mpaka 542 ni *percentage* kubwa sana? Kwa nini tusifanye juhudi hizo? Fedha zilizokuwepo tukaweza kukarabati na kutengeneza vyanzo vyetu vya umeme vilivyopo ili kuweza kutoa umeme wa kujitosheleza badala ya mipango ya Zimamoto kila siku? Kwa hiyo, naungana na Kamati katika suala hili na ushauri wao waliotoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alizungumza katika msukosuko katika uchumi wa dunia. Suala hili akazungumzia kwamba na sisi tutaathirika na kweli likitokea huko na sisi tutaathirika. Lakini kuna kitu kinachoshangaza. Amezungumza namna mazao yetu kahawa, karafuu, zinavyopungua bei kwa sababu ya suala hili. Lakini tunajiuliza kitu kimoja, soko la dunia ni moja, leo Kahawa inashuka bei mpaka Sh. 350/= kule Kagera, lakini jirani zetu Uganda kahawa ile ile inauzwa kwa thamani ya fedha ya Tanzania mpaka Sh. 1,200/= inakuwaje haya mazao yashuke thamani, lakini wenzetu wawe na thamani kubwa nini kinaendelea. Kwa hiyo, suala hili lisichukuliwe msukosuko wa fedha za kidunia halafu mazao yetu yakashuka bei, lakini tukiona kwa jirani zetu zao lile lile bei yake ni kubwa tunajiuliza, kulikoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatia aibu na vivyo hivyo karafuu. Karafuu inashuka bei tunaambiwa soko la dunia, lakini karafuu hiyo hiyo, ukisema uiuze unakotaka hairuhusiwi, ni matatizo tu. Kwa hiyo, kisichukuliwe kisingizio cha kushuka kwa mazao haya au katika mtikisiko wa fedha duniani na kushuka thamani mazao haya au katika mtikisiko wa fedha duniani na kushuka thamani mazao haya halafu tena tukazidi kuwaweka mahali pabaya wananchi. Ni lazima juhudi zichukuliwe katika Wizara yako ili tuone kwamba wananchi hawa wanafaidika. Ni mipango madhubuti inahitajika na wananchi wetu hawa waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nitaunga mkono hoja vizuri ikiwa na suala la bandari na ikiwa kutapatikana nyongeza ya fedha kuongezwa katika ule mpango wa kupeleka umeme Pemba ili hili tatizo la sasa hivi ambalo kama litaachwa liendelee itakuja kuleta matatizo makubwa baadaye. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitumie hizi dakika chache kuzungumzia mambo makuu mawili. Niipongeze Serikali kwa mpango iliouleta. Lakini itabidi waangalie mambo ambayo amekuwa anaahidi muda mrefu ni lazima yatekelezwe. Mimi nizungumzie mambo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Kaskazini wakati wa kiangazi biashara nyingi na magari yote makubwa yanapitia Iramba Mashariki, yanakwenda Mbulu yanakwenda Arusha. Serikali kwa miaka minne imekuwa inatuahidi kutujengea Daraja la Mto Sibiti. Ni Daraja la Mto Sibiti tu na kilomita 28 pande zote halafu na kutengeneza milima ya Magala ambayo iko Mbulu. Hii barabara itakuwa inapitika wakati wote wa mwaka. Itapunguza, ukizunguka kutoka Mwanza kwenda Nzega, Singida, Arusha unachukua zaidi ya saa 11.00, lakini kwa kupitia Mto Sibiti unachukua chini ya saa sita kutoka Mwanza mpaka Arusha. Hebu tunaomba safari hii Serikali itekeleze hiyo ahadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, alitembelea majimbo yote ya Mbulu, Iramba Mashariki na hata Miaki. Aliahidi kujenga lile daraja. Sisi tumeshakubali kwa sasa hiyo barabara iende taratibu. Lakini tunamwomba Waziri na Watalaam wake kwa mwaka unaokuja wa fedha wasisahau hilo daraja na hizo kilomita 28 na zile kilomita karibu 35 za Mlima Magala. Hilo tunaomba sana msisahau. Wananchi wa Mikoa ya Ziwa na sisi wa Kati na wa Kaskazini tunaona umuhimu sana wa hilo daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nizungumzie juu ya elimu. Kwa kweli mimi nawapongeza Watanzania, wamejitolea sana kujenga shule zetu za msingi, shule za sekondari, lakini sasa hivi shule zetu hizi hazijakamilika kimajengo, walimu na kadhalika. Sasa mimi ningeishauri Serikali kwa sababu sasa hivi ndiyo wanatengeneza bajeti kuna hizo fedha za *Local Government Development Grand* ambazo zinatolewa kila Wilaya, hizi fedha kwa ajili ya maendeleo ya kila Kata na miradi inayoanzishwa kwenye Kata na ile miradi inayoanzishwa Wilayani. Sasa mimi ningewashauri kwa makusudi mazima kwa mwaka huu ambao karibu tutauanza hizo fedha ziende zikamilishe mambo

ya elimu kwenye Kata zetu. Kwa sababu hii ni miradi ya maendeleo iliyoko kwenye Kata kwa kweli, ni aibu tunajenga shule hatukamilishi, lakini hizi hela zikienda mimi nina uhakika kabisa zitatusaidia kukamilisha miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu walimu, kwa kweli inatia aibu. Jana nimetoka Jimboni, wananchi wangu wamejenga shule nzuri sana ya Sekondari Miganga, Tarafa ya Nduguti, Kata ya Nduguti, shule imekamilika madarasa na mwaka huu wanachukua wanafunzi, lakini hakuna mwalimu hata mmoja. Mimi ningeishauri Serikali kwamba ile shule ya Miganga ni mfano, kwanza waanzie pale tupate walimu kwa ajili ya kuanza masomo mwaka huu unaofuata, lakini hii iende kwa shule zote.

Kamati yetu tulitembelea Mikoa mbalimbali hapa nchini. Mwezi uliopita mimi na wenzangu tulitembelea Kigoma, Rukwa na Tabora kwa kweli inasikitisha, unakuta shule ya sekondari ina mwalimu mmoja, ina walimu wawili, mimi ningeomba kila juhudi zifanyike ili tupate walimu *at least* kuwe na uwiano wa walimu ili wanafunzi wetu wapate elimu bora kwa faida ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kutumia dakika saba. Kumbe inawezekana watu wakazungumza yote kwa dakika chache zaidi. Sasa Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi watakaoanza kuzungumza atakuwa Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenister Mhagama, atafatiwa na Mheshimiwa Michael Laizer halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda. Sina hakika kama tutafikia hapo, lakini labda Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae na Mheshimiwa Athumani Janguo. Lakini tunaweza tusiwafikie wengine, lakini hawa wawe tayari. Kwa hiyo, sina shughuli nyingine, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 06.05 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge mchana, nilikuwa nimeshawataja Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Michael Laizer. Sasa Mheshimiwa Ahmed Salum.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba ukae hapa.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Mpango wa Bajeti ya Serikali 2009/2010. Katika mpango huu ukitizama ukurasa wa sita, kodi ya mapato, ushuru wa bidhaa za ndani na za kutoka nje, imepungua kwa kiasi kikubwa. Ukitizama ukurasa wa 10 na ukurasa wa 12, yote kwa pamoja kwa maana ya kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya ndani. Ningependa sasa niongelee suala zima kuhusu bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari yetu ya Tanzania – Dar - es - Salaam ni zawadi kubwa mno ambayo Mwenyezi Mungu ametuzawadia. Bandari ni kitu muhimu sana katika nchi. Bandari ndio moyo ambao nchi nyingine zinautumia kama *specialization* yake. Nchi kama Dubai na Singapore inaiingizia Serikali au nchi husika fedha nyingi zenye kuweza kutosha kabisa kukidhi mahitaji ya nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari yetu imekuwa na matatizo makubwa. Naongelea bandari kwa sababu kwa namna moja au nyingine tunaweza tukaboresha na ikasaidia kuongeza pato la Tanzania. Suala zima la fedha, ufinyu wa bajeti, ukienda Wizarani unaambiwa hatuna fedha, ukienda Wizara hii unaambiwa ufinyu wa bajeti, sio kweli. Tanzania tuna hazina nyingi ambazo kama tunaweza kuzitumia vizuri, hata bajeti tegemezi kwa wafadhili hatutaweza hata kwenda kuwaomba. Sasa hivi dunia iko kwenye matatizo makubwa ya *financial crisis,* makontena katika Bandari ya Dar - es - Salaam, sasa hivi ninavyokwambia meli zinakaa siku 15 mpaka siku 20 zinangoja muda wa kushusha kontena ndani ya bandari. Uliona wapi nchi inafanya hivyo? Ni aibu kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kontena moja, niliwahi kuchangia wakati ule tulipokuwa kwenye Kamati, kwenye mpango kama huu, nikasema wafanyabiashara hawana tatizo la kulipa kodi, mfanyabiashara anachokijali ni uharaka wa kutoa mali yake ndani ya bandari. Leo kontena likishuka bandarini linakaa siku 14, siku 20, kontena moja. Mpaka watu wafanye maandamano, wafanye vurugu na sasa hivi imeshakuwa *worse,* kazi imewashinda. Nchi kama Singapore, kontena moja linachukua masaa sita kutoka nje *whether in or out.* Nchi kama Dubai ni 24 *hours,* ni sheria wamejiwekea, kama ikizidi hapo unakamatwa, kwa nini umelicheleweshа?

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hivi kwa sababu, kwa mfano, tunatoa kontena tatu kwa mwezi, kila kontena moja ni shilingi milioni 30, tungeweza kutoa kontena moja kwa siku nne kwa mfano, maana yake hapa tukisema 48 *hours* ni kitu ambacho hakiwezekani. Siku nne tunaweza tukatoa kontena nane na ukiweza kutoa kontena nane mara 10, maana yake ni kwamba umeongeza pato. Kwa hiyo, jinsi unavyotoa kontena haraka ndivyo jinsi unavyoongeza *revenue* ya nchi. Ni lazima wakiri bandari imewashinda. Kama viongozi ndani ya *TRA* wakuu wenye maamuzi moja kwa moja na Bandari, Wizara, Miundombinu, imewashinda, jamani semeni imetushinda! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni tutoe *consultants* wawili, tumtoe mmoja Singapore, kwenye nchi ambazo wamebobea na bandari tuwalete hapa, tuwatumbukize bandarini pale, tuwaambie jamani tunataka mtuletee ripoti ambayo itaweza kuisaidia nchi yetu. Sasa hivi kwa mwaka mmoja ni kontena laki tatu mpaka laki nne, lakini kama tungeweza kutoa kontena milioni moja kwa mwaka tungeweza kuongeza *revenue.* Kama ni kontena moja mara dola 10,000 tungeweza kuingiza trilioni 10 kontena peke yake, achana na mapato haya ya ndani. Sasa bandari tunaichezea, bandari ambayo Mungu ametupatia iwe *specialization* yetu! Burundi, Rwanda, Zambia, *DRC,* wanaitegemea bandari yetu na sisi tunaichezea tu.

Ukitaka kujua thamani ya bandari mwulize mtu wa Rwanda, bwana eeh, je, kama Mungu anakujalia wewe bandari mwaka mmoja; akasema, ingelikuwa inawezekana hivyo tungemwomba Mungu atupe Bandari ya Dar – es – Salaam angalau kwa muda wa mwaka mmoja tu, wangeweza kukusanya *revenue* ya miaka 10, leo sisi tunaichezea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mpaka nimemwona Mheshimiwa Rais ameingilia kati, amekwenda wamechukua *solution* kwamba tutafanya masaa 24, sijui tutatoa makontena huku sijui tutapeleka huku. Kinachotakiwa pale ni hizi *solutions* zote walizozifanya, mimi ni mdau mkubwa pale bandarini, *solutions* wanazozichukua ni tofauti kabisa na inavyotakiwa kuwa. Inavyotakiwa kuwa ni kupunguza urasimu tu, kwa sababu wewe unachotaka pale ni *revenue* una-*target* pesa. Mfanyabiashara hana shida, milioni 15 atalipa, mwambie tunakuongezea milioni mbili ya *express charge* atakuongezea tu, lakini umuahidi, bwana kontena lako linashuka leo na kesho kutwa unachukua kontena. Ataongeza hata *three million* kama *express charge* ili kontena litoke. Serikali ingeweza kuongeza *revenue* na tungeweza kufika mpaka trilioni nane mpaka trilioni 10. Leo tunakwenda kwenye trilioni tatu, trilioni nne, bajeti nzima ya Serikali tunakwenda nchi za nje tunaomba sijui bajeti tegemezi, hii sio kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPA* wameshindwa kufanya kazi, kuna makontena pale ukienda *TPA* wanakwambia bwana hii iko *ICD. ICD* maana yake ni *Island Contena Depot.* Unakwenda kulitafuta kule mpaka unachoka na ukirudi unalikuta liko ndani mwao. Hata *TPA* wenyewe wanakosa kuwa na rekodi ya makontena yao ndani ya bandari. Naiomba Serikali iichukulie maanani bandari kama ni kitu kikubwa na Mungu ametuzawadia kuingiza *revenue* ya Taifa letu. Tukitumia bandari peke yake na makontena peke yake tunaweza tukafika trilioni nane mpaka 10. Uwezo huo upo na tukaondokana na utegemezi wa nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea kwa uchungu sana. Leo Jimbo la Solwa tunahitaji maendeleo. Ukienda kuomba fedha za barabara wanakwambia bajeti ni finyu, ukitaka kufanya hivi unaambiwa bajeti ni finyu, wakati bandari ipo! Kama Makamishna, Bodi ya *TRA*, wameshindwa kazi mimi nadhani ni muhimu sana kuwajibika ukaachia ngazi ikaja damu mpya, watu wakafanya kazi kisasa na sio kizamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa pili wa namna ambavyo *TRA* sasa wanavyokuwa na maamuzi mawili baina ya *TRA* na *TIC. TIC* ni *Tanzania Investiment Cooperation,* ukisoma kwenye ukurasa wa 12 utaona kuendelea kuboresha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje. Ukienda *TIC* unapata *exemption; TRA* wanakupa baada ya miezi miwili; *TRA* wanatoa maamuzi tena kwa mara ya pili; *task force* wanakaa wanatoa maamuzi vizuri, lakini mapato yao yakianguka wanaanza kutafuta mchawi. Wanawaambia *TIC* tunapunguza kutoa *exemptions* kwenye magari.

Sasa hivi kuna *competition* Zambia, Msumbiji, Tanzania, Uganda, Kenya, wote wanakuwa na *incentives* za kuwavutia wawekezaji *whether* wa ndani au wa nje ya nchi, lakini hapa tunakuwa kama tunawa-*discourage. TIC* wanakupa *exemption,* ukileta gari ukifika pale *TRA* wanakwambia hapana, wakati wao wenyewe walikubali. Kwa hiyo,

kutakuwa na maamuzi mawili, *TRA* wana maamuzi yao na *TIC* wana maamuzi mengine, wanakanganyana wenyewe na Serikali ni moja. Naiomba Serikali iwe makini kwa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mwingine. Mtakumbuka wakati ule mimi nilileta *ambulance* hapa na nikamwomba Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, sijui na nini.

Walichonifanyia sasa hivi wamenisamehe *exice duty* tu, yaani ni kama *favour.* Mimi sikuomba *favour,* nimeomba kwa utaratibu wa sheria. Kuna hii barua aliyokuwa akijibiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ule yuko *TAMISEMI,* ikitoka kwa ndugu yangu Msangi wakati huo akiwa ni Katibu Mkuu wa Hazina, akisema tunapenda kukufahamisha kuwa katika sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *VAT,* jedwali Na. 3, kifungu cha tano, kinatoa msamaha wa kodi ya magari ya kubebea wagonjwa wa hospitali. Kinatoa msamaha wa kodi yote, lakini hapa leo wananiambia aah, tunakusamehe hii tu, mimi sikuomba *favour* na kama ni *favour,* basi sihitaji, nitalipa ushuru wote, siitaki hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaoumia ni wananchi wa Jimbo la Solwa Kata ya Tinde, leo unanipa *favour!* Mimi sihitaji *favour.*

**NAIBU SPIKA:** Unamaanisha mpaka leo haijatoka?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado. Walichoniruhusu ni *favour,* yaani ni kwamba milioni moja na laki mbili; sihitaji hiyo, mimi nawaambia, mimi nilitaka sheria hii ifanye kazi. Hii sheria haijafanya kazi kwangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, miaka miwili?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naongea kwa machungu sana, ninafanya kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Solwa na nitalipa ushuru kwa fedha zangu mwenyewe, sihitaji *favour.* Milioni tano na kitu, tunasamehe magari mangapi kwa ajili ya *incentives!* Tunasamehe kodi ngapi Serikalini? Hii *ambulance* moja kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Solwa unashindwa kunisamehe, tena kwa mujibu wa sheria! Sheria hii hapa, mimi siombi *favour,* sheria inasema hivyo na ndio maana nikaleta ile gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Ningependa kuishauri Serikali katika Jimbo la Solwa naomba sana tena sana Serikali iwekeze na itoe fedha nyingi katika kutekeleza au kupeleka umeme kwenye maeneo ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini au Tanzania nzima kwa maana ya zile Wilaya ambazo hazina umeme. Nasema hivi kwa sababu gani? Hata tukiboresha kilimo namna gani, hata tukifanya namna gani, lakini unapopeleka umeme unakuwa unachochea maendeleo ya maeneo husika; katika Jimbo la Solwa, tunaongoza sana…

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili hiyo? Nashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Jamani suala la *ambulance* mlifanyie maamuzi. Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli na mimi naomba nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini na mimi niunge mkono tu kilio cha Mheshimiwa pale kuhusu suala la *ambulance* kwa ajili ya wagonjwa hao kwa kweli lifanyiwe maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba Bunge, linakaa kupitia Mpango wa Bajeti wa Serikali yetu ili kuweza kusaidiana kuchambua na kuona ni namna gani Serikali yetu inaweza ikasaidia kukidhi mahitaji ya Watanzania kama inavyotakikana. Miaka 61 iliyopita nchi ya Marekani ilikumbwa na mtikisoko mkubwa sana wa kiuchumi, wa kisiasa, wa kimaendeleo, kwa ujumla. Hali katika nchi ile ya Marekani kwa kweli ilikuwa ni ya kuyumba kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na vita baridi, kulikuwa na masuala ya kupanda na kuanguka kwa tawala mbalimbali katika jamii za nchi za Ulaya na Amerika na hivyo mambo yalikuwa hayaeleweki, ni miaka 61 iliyopita. Mimi ni mwalimu, lakini nakumbuka historia ya miaka hiyo 61 iliyopita ya nchi ya Marekani inasema katika kipindi kile ambacho nchi hiyo ilikuwa inayumba kabisa kiuchumi, kiutawala na kadha wa kadha alitokea mtu mmoja *General Marshal* akatoa ushauri wa kuona ni namna gani nchi ile inaweza ikaondokana na matatizo yanayoikumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninapenda nikumbuke yale maneno yaliyosemwa na *General Marshal* katika mpango wake wa *Marshal Plan.* Alisema mambo matatu makubwa ya msingi sana; alisema, kwa kuwa nchi yeti iko katika mahangaiko makubwa ya kiuchumi, ya kimaendeleo, ya kijamii, ya kiutwala na kadha wa kadha haitatusaidia tukiendelea kukaa bila kujipanga vizuri kwa kufuata mambo makubwa matatu na leo mimi nataka nianzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, alisema ili tupambane na haya yanayotukabili, kwanza ni lazima tujiulize, *what is needed?* Kinachohitajika ni nini? Lakini pili yule bwana alishauri akasema pia ni lazima tuangalie *what can best be done?* Ni nini kinachoweza kufanyika kwa ufasaha mkubwa na kikatusaidia kwa wakati huu tulionao sasa? Tatu, akasema, ili tujipange vizuri, ni lazima tuangalie *what must be done?* Ni mambo gani ambayo sasa ni ya lazima? Yenye kipaumbele ili yafanyike yaweze kutusaidia? Ninamkumbuka sana na ninakumbuka sana haya maeneo yake matatu aliyoanza nayo wakati ule Marekani miaka 61 iliyopita alipokuwa anahangaikia uchumi na maendeleo ya nchi kama ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niunganishe tena kidogo. Jana kwenye mtandao pia nilikuwa nasoma, wenzetu wa *Konel University* wanaoshughulikia masuala ya kilimo na uchumi na muanguko wa uchumi wa kidunia, wametoa *statement* nzito sana. Wanasema, *"As police makers as people as human being we tempt not to deal with problems until they become very severe,"* ndio tunaanza kuzishughulikia. Hatushughulikii matatizo mpaka yawe yameshakuwa makubwa ambayo hayawezekaniniki, sasa leo mimi niseme baada ya kuwanukuu hawa watu wawili watatu, niseme kwamba ninaipongeza Serikali kwamba imekuja na mpango. Lakini sasa tujiulize, hivi yapi ni mambo ambayo ni lazima yafanyike kwa sasa? Ni mambo gani ambayo tunaweza kuyafanya kwa ufanisi wa kufa na kupona ndani ya nchi yetu ili kuokoa hali ya uchumi wa Watanzania? Lakini vilevile ni mambo yapi yanaweza kufanyika kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia eneo hilo, nikifuata mawazo ya hawa wana falsafa, wakubwa sana, ninagundua kwamba Watanzania sasa tunatakiwa kujiuliza, hivi kwa maliasili tulizonazo na vikorombwezo vyote tulivyonavyo, hivi ni kweli hatuwezi kujitosheleza katika uchumi wetu ndani ya nchi yetu ya Tanzania? Tumekosa nini kwa Mwenyezi Mungu? Tuna mali ya asili, tuna bandari ndugu yangu Salum hapa amesema, sisi tuna mvua zinazoweza kukidhi uzalishaji wa chakula cha kutosha na mazao mengine ya biashara, tuna wanyamapori wamejaa utafikiri siafu katika nchi yetu ya Tanzania, tuna kila kitu. Sasa ni nini kifanyike? Hapo ndio tatizo! Mimi ninaona kwamba nchi yetu imebarikiwa, ina wataalamu wa kutosha wana uwezo. Hawa wataalamu walioko nyuma yangu hapa leo, hizi ni *think tanks* ambazo hazijapata kutokea, hebu sasa zitupeleke huko. Leo tunasema kwamba uchumi wa dunia umeyumba, sasa kama uchumi wa dunia umeyumba turudi na tujiangalie sisi tunafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri mambo yafuatayo: la kwanza, ni kama tunazo maliasili za kutosha, tunavyo vitu ambavyo ni vitega uchumi vya kutosha ndani ya nchi yetu. Ni lazima tukubali kwamba umefika wakati tu-*review* mfumo wetu wa kodi katika nchi yetu ya Tanzania. Hivi ni kweli tukianza kupitia na kufanya mapitio ya mfumo wa kodi hatuwezi kweli kujenga uchumi wetu wa ndani na tukaacha kuwa tegemezi tukategemea uchumi wa watu wa nje ambao ukiyumba na sisi huku tunatetemeka, tufanye nini? Ni lazima vyanzo vyetu sasa hivi vya mapato vya ndani kwa kweli viimarishwe na vitafutwe vyanzo ambavyo ni endelevu na sio vya Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali kabisa ushauri ambao ni muhimu sana sasa hivi na mimi ninaomba niusisitize na nishauri tena; ni lazima sasahivi tuangalie suala zima la kuvutia wawekezaji waje ndani ya nchi yetu ya Tanzania wawekeze. Watakapowekeza kwa kuwapa *incentives* ambazo zinasemwa, kupunguza kodi ambazo hazina manufaa ili kujenga uchumi wa ndani, tunaweza. Lakini vilevile niseme ni lazima tuchukue hatua za kujenga upya mfumo wetu wa fedha, Benki Kuu watusaidie. Ninaomba Benki Kuu watusaidie katika mambo yafuatayo; wahakikishe wananchi wa Tanzania wanawezeshwa ili na wao waingie katika sekta ya mikopo kupitia mabenki tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hilo kwa sababu kupitia uwezeshwaji na Benki Kuu kwa wananchi na hasa wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaoshikilia sekta zisizohamishika. Hizi ni sekta zisizohamishika, bahari hawezi kuihamisha mtu yeyote, kilimo chetu hakiwezi kuhamishwa na mtu yeyote, maliasili yetu haiwezi kuhamishwa na mtu yeyote, ingawa sasa hivi *concept* inakuja kwamba uchumi unajengwa kwa picha nyingine ya sekta ya ujenzi na kadhalika. Lakini nasema sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, wanyamapori, hizo ziwawezeshe wawekezaji wa ndani na nje kushika uchumi huu wa nchi ili nchi yetu iweze kunufaika kupitia mfumo wa kodi tunaoweza kuufanyia mapitio mapya. Mazoea yanatuharibu, tusiendelee na tabia ya yaliyofanyika mwaka jana yahamishiwe mwaka huu, tutaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, tuangalie sana suala la *interest rates* kama nilivyoanza kulizungumzia ili tutengeneze *favourable balance of payment,* kwa maana ipi? Ili kweli uchumi huu uweze kwenda mbele ni lazima tuzingatie tuhakikishe tunajijenga ndani kwa ajili ya ku-*export* kuliko kufanya *importation,* wenzetu wamefanya haya na wamevuka. Kwa kweli inaniuma sana sisi tunashindwa nini jamani miaka 48 ya uhuru? Tunashindwa nini? Lakini niseme, ninadhani kama tumelogwa humu ndani tuna Wachungaji wawili, waombee na wakemee katika jina la Yesu kiroho hicho kiondoke. Ninaomba sana hebu tuangalie, nimesema *General Marshal* alitoa hayo maswali matatu, hebu na sisi tukae tujipange kwa kuzingatia hayo maswali matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema wakulima wathaminiwe. Sasa niseme kidogo niwawakilishe wananchi wa Jimbo la Peramiho, mpaka leo wanahangaika suala la mbolea ya ruzuku, ni shida. Tusipojipanga vizuri, nimemwomba Waziri wa Kilimo na ninampongeza, amekubali nimletee agizo la Mlale linaloongoza kilimo katika Mkoa wa Ruvuma. Kwa kweli bila kufuata agizo lile hata mbolea ikipelekwa tani elfu 100 na mia tano hamsini na ngapi, haiwasaidii wakulima wale. Ni lazima tuwe na mpango mkakati unaopimika na kutekelezeka. Kama mbolea itaendelea kuchelewa wale wakulima mbolea ikichelewa hawafai kitu, ikienda haitoshi haiwasaidii kitu. Tumekubaliana sekta hiyo ya kilimo inaweza ikasaidia kuinua viwanda, kusaidia kujenga uchumi wa ndani na pia kuwasaidia kabisa wakulima kuondokana na umasikini ule wa kipato.

Kwa hiyo, ninaomba kuishauri Serikali, haya ninayoyazungumza na niliyoyasema yanawezekana kama tutaamua kuwa *serious* na tutaweka nguvu zetu kwa pamoja, ninawapa changamoto. Sisi wenyewe na wananchi wa Tanzania kwa ujumla na Serikali yetu, mpango huu ni mzuri, unahitaji kwa kweli kuwekewa mkakati huu wa kuweza kumgusa mtu. Ni kweli sisi tunashindwa? Tubadili mfumo wetu wa utendaji wa kazi, tubadili mwelekeo wetu, tusimamie vizuri mipango yetu hii mizuri ili tuwakomboe Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante, naona umesahau kwamba sisi tunazungukwa na nchi nane. Bandari ipo, reli tunajenga, kiwanja cha ndege, hii ni mapato tosha. Sasa

ninamwita Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Dr. Mpanda ajiandae; Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae na Mheshimiwa Athumani Janguo pia ajiandae.

Mheshimiwa Laizer, hayupo. Mheshimiwa Dr. Mpanda.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii, ili na mimi nichangie japo kidogo yale niliyoyaona kwenye mpango mzima ambao umetolewa na Mheshimiwa Waziri. Awali ya yote, naunga mkono hoja hiyo, siwezi kuipinga ila nakumbuka sana siasa tuliyofundishwa na Baba wetu wa Taifa, Mwalimu Nyerere; ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Sasa kutokana na hiyo kitu, siku zote tunazungumzia Dar es Salaam sijui bandari imejaa shehena; lakini kuna Mtwara, bandari yake ni nzuri, ina kina kirefu na inaweza ikafanya vitu chungu nzima. Mimi nimeanza kuisikia Mtwara *Corridor*, tangu nimeingia Bunge hili. Wakachaguliwa na watu lakini mpaka leo Tandahimba wanalia, Peramiho wanalia, nchi nyingine za jirani huko Malawi, Zambia, Congo, wanalia; kitu gani tunafanya jamani? Tungetilia mkazo suala la kuifufua, yaani kuijenga vizuri ile Bandari ya Mtwara, bila kusahau bandari kongwe ambayo enzi ya Mwarabu mwenyewe aliitumia.

Nakuja kwangu sasa Bandari ya Kilwa Masoko, Waarabu walikuwa wanakuja pale na meli kubwa sana, hata juzi juzi hapa imekuja meli kutoka Marekani ilisimama pale ikapita; kwa nini Dar es Salaam makontena yanajaa mpaka wengine wanalalamika hapa? Jamani tunaukalia uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu kilimo; mimi nachangia kuhusu bodi ya mazao mchanganyiko. Jamani ni fedha nyingi mno tunazitupa; kuna ndizi, kuna minazi, yaani kila kitu tunacho ambacho hakijawekwa kwenye mazao yetu makuu yale tunayojua kwa *export.* Tungeweza kuyatekeleza hayo, tungefika mbali ndugu zangu. Sasa sisi tunabakia kulalamika tu, tunalalamika tutaishia wapi?

Kwa mfano, Kilwa sisi tuna mazao hayo mengi, tena mengi mno ukisema ndizi zipo, ukisema minazi ipo, ukija Kipatimu kule machungwa yapo, yaani chochote utakachokisema kipo. Nimeuliza maswali chungu nzima; jamani bodi ya mazao mchanganyiko? Hakuna jibu hata moja ninalolipata la maana; hivi tunangoja nini tunamngoja Mzungu tena aje kutuwekea bodi hapa? (Makofi)

Suala lingine nililotaka kuzungumzia ni matrekta. Nimeshukuru sana Rais amezungumzia kuhusu masuala ya matrekta na mimi sitataka kuzungumzia sana, lakini Kilwa tunaomba matreketa; mkitupa japo mawili tu tutaingia kwenye sita bora yenu. Kwa sababu kuna sehemu nyingi sana ambazo yanaweza yakalima matrekta yale, kwa mfano, Somanga, ukija pale Mitole, Njinjo, Kandawale na maeneo yote ya kanda ya chini ya Kilwa. Tupatiwe japo matrekta mawili tu, mimi nitashukuru hata nikifa leo watu watasema jamani alipiga kelele huyu bwana na matrekta yamekuja. *(Makofi*)

Suala lingine, maana nina uchungu, ningepata dakika nyingi ningezungumza zaidi, lakini naona bora niishie hapo kwa sababu yananiuma sana. Mheshimiwa Waziri, nadhani utanielewa maana mengi nimeyachangia kwenye maandishi na kwa sababu sasa hivi nimetoka kung'oa jino, sitaweza kusema sana, ahsante sana. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Mpanda, acha tu tatizo ni jino wala sio muda.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mpango huu wa Serikali, kama mwongozo wa bajeti. Natambua kwamba, mwongozo huu umeandaliwa na tunauchangia wakati ambapo tupo kwenye wakati mgumu sana; dunia ipo kwenye wakati mgumu kiuchumi.

Lakini pia Tanzania kama nchi ambayo haipo kisiwani, nasi tupo ama tumeingia wakati mgumu sana kiuchumi. Kwa hiyo, mpango na ni lazima tukubaliane sote kwamba, kuna maeneo lazima tutaumia. Bajeti itakapokuja, kuna maeneo ambayo ni lazima tuweke nguvu zaidi ili kuweza kujihami kama Taifa. Tupo kwenye mazingira ambayo mauzo yetu nje yanashuka chini, mapato yetu kutokana na utalii yanashuka chini, wawekezaji wamepungua kuja. Mapato kutokana na Serikali *(Central Government Revenue),* kama jinsi ambavyo Waziri ametueleza, *trade tax* zipo chini na *corporate tax,* kodi inayotokana na faida za makampuni inashuka chini. Hii ni ishara mbaya sana kwamba, makampuni hayapati faida, kwa hiyo, uzalishaji unapungua.

Baadhi ya sekta za kiuchumi tayari zimeshaumia sana; katani haina soko kabisa, pamba ipo kwenye magodauni. Tumeambiwa juzi na Gavana wa Benki Kuu, idadi ya makampuni ambayo yamekuja kuomba vibali kwa ajili ya kufanya *exploration* ya *minerals,* imeshuka sana. Kwa maana hiyo ni kwamba, eneo la sekta ambayo tulikuwa tunaitegemea ingeweza kuisaidia sana taifa nayo pia imeumia. Mazingira yanatufanya tuwe na mpango wa bajeti, ambao ni tofauti sana na miaka mingine. Hili tayari lilishaelezwa na Taarifa za Serikali.

Ninaomba niinukuu *Poverty and Human Development Report (PHDR)* ya Mwaka 2007, ambapo walipendekeza kwamba, tujiangalie upya. Naomba niinukuu kwa Kiingereza: "*Choosing few growth driver and concentrate on investments in few geographical areas, would produce higher and more sustainable growth turn to spread resource of many activities or sector and in large geographical areas*."

Kwa maana hiyo ni kwamba, bajeti itakayokuja mwezi Juni, iwapo tutazingatia mapendekezo haya ya kitaalamu ya *poverty and human development report,* kuna baadhi ya maeneo ni lazima kutakuwa na punguzo la matumizi, hatuna ujanja, ili kuweza kujihami. Katika kipindi cha kuanzia 2001 mpaka 2007, tumeweza kuongeza idadi ya watu maskini, kwa maana ya watu milioni moja na laki saba. Umaskini umepungua kwa asilimia mbili tu, umeshindwa kumeza idadi ya watu ambayo ukuaji wake ni asilimia 2.6 kwa mwaka, kama ambavyo ilielezwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika eneo hili. *(Makofi*)

*Inequality,* kwa maana ya tofauti ya kipato, miongoni mwa Watanzania imekuwa kubwa zaidi. Taarifa ya *House Hold Budget Survey,* inaonyesha kwamba, asilimia 35 ya Watanzania ndiyo wanachukua asilimia 75 ya pato lote la nchi. Kwa hiyo, hii inaonyesha kabisa kwamba, bado kuna kazi ya ziada ambayo inabidi tuifanye, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunapunguza *inequality*. Nini kifanyike; ndiyo hasa lengo la mjadala huu. Kwanza, kama *PHDR* ilivyo-*suggest,* lazima tuchague sekta chache za kufanyia kazi. Sekta ya kwanza ambayo imechaguliwa ni *transport services*. Sekta hii hivi sasa inachangia asilimia saba ya uchumi, lakini ni kitu ambacho wanasema kina *complement* kwa *other sectors,* lakini itaweza kuufungua uchumi na kuuwezesha kushindana na mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *transport services* ndiyo bandari, kama ambavyo Waheshimiwa mbalimbali wameelezea; ndiyo reli, ndiyo barabara na ndiyo viwanja vya ndege. Ili bandari iweze kufanya kazi sawa sawa ni lazima sekta nyingine za kimiundombinu, zifanye kazi sawa sawa. Hata bandari; *TPA* au *TICTS* ambayo tumewapa *lease* ya kuendesha *container terminal,* wafanye kazi saa 24 kwa siku waondoe makontena yote kutoka baharini kama reli haifanyi kazi ya kusafirisha hayo makontena, kwenda Ruanda Burundi, Kigoma na kadhalika, hakuna kitakachofanyika na ndiyo dailema tuliyonayo. *(Makofi*)

Kwa kuwa Watanzania tumezoea kurushiana lawama; ni rahisi sana kutafuta nani wa kumlaumu, badala ya kukaa chini na kuweza kuangalia ni jinsi gani ambavyo tuta-*solve* haya mambo kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwako na kikao cha *Parastal Accountability Conference* pale Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Fedha alikuwepo, moja ya pendekezo ambalo tulilitoa ni kwamba; inawezekana kabisa mrundikano wa makontena uliopo sasa hivi bandarini, unaweza kuwa unasababishwa na *uncertainty* iliyopo. Hii ni kwa sababu, kwa takribani miaka mitatu iliyopita, tumekuwa tukizungumzia Serikali kuchukua uamuzi kuhusu *TICTS;* uamuzi ama wa kufuata mkataba au kutofuta mkataba hauchukuliwi.

Mfanyabiashara yeyote hawezi ku-*invest* ambapo kuna *uncertainty*. Hata mchumi anayeanza mwaka wa kwanza Chuo Kikuu, *BA Economics,* atakwambia hili kama kuna *uncertainty,* hakuna mtu ambaye anaweza aka-*invest*. Kwa hiyo, hatuwezi kutarajia wale watu ambao tumewakodisha ile bandari wafanye *investment,* kama hakuna *decision* ambayo imechuliwa. Kwa hiyo, nilikuwa naitaka Serikali katika mpango huu, ihakikishe inachukua uamuzi kuhusiana na suala la bandari. Hata siku moja tusiingie tamaa ya kutaka mamlaka ya bandari, ifanye kazi ya *container terminal. Experience* tuliyonayo, wiki iliyopita tulikuwa tunashughulikia mgogoro wa *DAWASCO* na *DAWASA*, baada ya kuwa tumevunja mkataba wa *City Water* tukaipa kampuni yetu ya *DAWASCO,* hakuna kazi inayofanyika kwa sababu yote ni makampuni ya umma na hakuna mtu ambaye anachukua *business decision* na wala hakuna anayemwajibisha mwenzie. Tusiingie tamaa hata kidogo, Mamlaka ya Bandari, iendelee kuwa ni *run road*; cha msingi ni kuhakikisha kwamba, kunakuwa na ushindani wa kutosha katika upakuaji na upakiaji wa makontena

ili kuweza kuleta *efficiency*. *Competition* ni muhimu sana na suala hili katika maamuzi ya Serikali ni lazima iliangalie.

Maeneo ya *transport services* yameelezewa ukurasa wa 13 wa maelezo ya Waziri katika mpango huu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba waweze kuboresha eneo hilo, tuangalie uwezekano wa kuanzisha *rural roads agency* ili kuhakikisha mazao yaliyopo vijijini yanafika kwenye masoko. Sasa hivi ukiangalia barabara ambazo zimetengenezwa na *TANROAD*, zimetengenezwa vizuri sana, lakini barabara ambazo zimetengenezwa na Halmashauri za Wilaya zimetengenezwa ovyo ovyo. Hii ni kwa sababu, kule kwenye Halmashauri zetu, kila Diwani ni *contractor;* ana kampuni ya kutengeneza barabara na wanapeana. Suala hili tutaweza kuliondoa, iwapo tutaanzisha *Rural Road Authority*. Wenzetu Kenya tayari wana *Rural Road Authority*, ina fedha za kutosha, wanatengeneza barabara nzuri. Ili kuhakikisha kwamba, tunaunganisha uchumi wa vijijini na uchumi wa miji, hilo eneo la barabara ni lazima tuliangalie. Vilevile tusisahau eneo la *airports*, ambazo zitaweza kuchochea hali ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la madini lingeweza kutuokoa kidogo, kwa sababu katika hali ya sasa ya mfumo wa kiuchumi wa kidunia, madini hasa dhahabu, ndiyo *commodity* pekee ambayo haijashuka bei na inaonyesha kwamba bei zake zita-*stabilize* kwa muda fulani.

Rais aliunda Kamati ya Bomani, iliyopendekeza hatua za kuchukua kuhakikisha tunapata mapato ya kutosha kwenye madini, bila kuingia kwenye mgogoro na wawekezaji wa Sekta ya Madini. Naomba kununukuu aya ya 30 ya barua ambayo Waziri wa Fedha alimwandikia Mkurugenzi Mkuu wa IMF, tarehe 3 Desemba, 2008: "*Legislative changes to the physical regime of the Mining Sector basing on the recommendation of the Presidential Committee on the Mining Sector, have been prepared and will be presented to the Parliament in February, 2009*."

Bunge linaisha kesho, hizo *legislative changes* hatujaziona na eneo la madini katika maelezo haya ambayo Waziri ameyatoa, limezungumziwa *page 15* na ni eneo dogo tu; kwamba, tuongeze thamani ya madini. Kwa hali ya sasa ya nchi, kwa mpango wa muda mfupi au muda wa kati, hatuwezi kuongeza thamani ya dhahabu, kwa sababu gharama za kuleta mitambo ni kubwa mno. Hatuna umeme wa kutosha, hapa tunapozungumza tuna *diversity* ya umeme unaotakiwa leo *megawatt* 150, kuleta mitambo ya kuongeza thamani ya dhahabu, itahitaji *megawatt* nyingi sana za umeme. Mpango wa muda wa kati *should be* kuongeza mapato kwenye Sekta ya Madini ili yaje kufidia kwenye maeneo ambayo hatuwezi na kuna maeneo mengi.

Mwaka huu msamaha wa kodi ya mafuta peke yake, ambayo tutaisamehe Sekta ya Madini, migodi sita ni bilioni 91 na *road toll* ambayo makampuni ya madini tumeyesamehe ni bilioni 91; mwaka juzi tumesamehe bilioni 59, mwaka jana tumesamehe bilioni 32. Fedha hizi tukiziokoa, tunaweza kuziba maeneo ambayo yana mapengo na hasa eneo la Sekta ya Madini, ambapo ukiangalia jedwali lile ambalo Serikali imeleta, sekta hii itashuka *by negative 0.5.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye kilimo; naipongeza Serikali kuuchukua Mkoa wa Kigoma kama moja ya mikoa sita kwa ajili ya uzalishaji wa chakula. Sisi hatujawahi kupata njaa toka tumepata uhuru wa nchi hii; tunalisha Burundi na Eastern Congo. Naomba tuzingatie mazao ya biashara na nashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo yupo hapa. Hatuna uwezo wa ku-*deal* na bei za kimataifa, lakini tunao uwezo wa kuzalisha zaidi. Kwa hiyo, sisi tunapigania kuongeza *volume* ili tupate mapato zaidi, tusicheze na bei kwa sababu hatuna uwezo wa kui-*control*.

Kuna baadhi ya maeneo ambayo lazima tuyafanyie maamuzi; kwa mfano, mwaka huu viwanda vya sukari vimezalisha sukari ya kutosheleza matumizi ya ndani; kwa nini bado tunatoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje? Hili ni suala ambalo ni lazima Bodi ya Sukari na Waziri wa kilimo waliangalie. Katani imekosa bei hivi sasa, lakini tuna viwanda vya magunia ambavyo vimelala havifanyi kazi na wawekezaji hawawezi kuvifungua kwa sababu soko letu la magunia limejaa magunia ya *duty*.

Lazima tufanye maamuzi kwa baadhi ya mazao na hili liwe sehemu ya mpango; baadhi ya mazao ya ndani yawe na *compulsory usage* ya magunia ya katani ili wakati tunakosa soko la katani kwenye makampuni ya magari, kwa sababu katani yetu sasa hivi inanunuliwa na makampuni mawili tu ya kutengeneza magari kwa sababu hawawezi kununua *car industry* imeanguka, tuyanunulie katani itumike ndani ya nchi, tuweze kuhakikisha kwamba inatumika vizuri. Naomba Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha, waliangalie hili; tuchague baadhi ya mazao tuweke *compulsory* ya *uses* ya *sisal* ili *sisal* yetu ya ndani iweze kupata soko na iweze ku-*compete* na *duty* kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni la nishati; kama nilivyosema, tuna tatizo la umeme, suala hili ni lazima liangaliwe, fedha nyingi zaidi lazima iwekwe. Eneo la maji ni la muhimu zaidi. Bado tunaiangalia Sekta ya Maji kama maji ya kunywa, hatuangalii maji kama uhai wa Taifa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iangalie na mambo yote haya yapo kwenye *Poverty And Human Development Report*. Tuangalie ni jinsi gani ambavyo tuta-*invest* kwenye maji na tuanze na Dar es Salaam. Kwa nini hatuwezi kuwa na mpango kabambe kama tuliokuwa nao Ziwa Victoria, kwenda Kahama na Shinyanga uwepo pia kwa Jiji la Dar es Salaam? Tuondokane kabisa na kero ya maji kwenye Jiji la Dar es Salaam, tuwe na mfumo mzuri wa maji safi na maji taka. Vilevile tuhame Dar es Salaam tuanze kushughulikia maeneo mengine; suala hili ni lazima tuweze kuliangalia.

La mwisho, nilikuwa naomba Waziri Mkuu hayupo, lakini walioko hapa watampelekea salamu kwamba, mambo yote haya ili yaweze kuangaliwa kwa picha pana zaidi ni lazima tuwe na Tume ya Mipango inayoonekana, lazima tuwe na *political commissar*; *political commissar* ni Waziri wa Nchi, Mipango. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba na suala hili tumelizungumza toka wakati wa bajeti, nchi haiwezi kutetereka kwa sababu ya mtu mmoja ambaye tumemkosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(1); mzungumzaji aliyepita wakati anazungumzia masuala ya barabara alisema kwamba, kila Diwani ana kampuni ya ujenzi. Sisi Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zetu, ningeomba tu ama athibitishe au afute kauli hiyo. Naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mimi nilivyoelewa, alikuwa anasema liundwe shirika linalohusika na barabara vijijini na kwamba, *contractors* wa sasa hawana uwezo unaostahili. Nadhali hilo neno Diwani, mkienda neno kwa neno mtafika mahali mpaka mtamkosea Mungu; mimi nimeelewa hivyo. Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii muhimu ya bajeti ya 2009/2010 hadi 2011/2012. Mimi nilikwishakata tamaa, maana jana ilikuwa niwe mchangiaji wa kwanza, baadaye nikakosekana, lakini Mungu si Athumani zamu imefikia. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tumia muda wako kuongea.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitamke kwamba, naiunga mkono hoja hii. Ningependa pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na wasaidizi wake kwa kutayarisha hoja yenye matumaini kwa Watanzania na kuzingatia kwa sehemu kubwa sana, maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Mimi ni Mjumbe, kwa hiyo, nimeona kwamba maoni yamezingatiwa. Pili, hoja hii imewasilishwa kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango huu, sina nia ya kukosoa bali kutoa mchango wa kuweza kuiboresha bajeti yetu. Nianze na mwenendo wa uchumi jumla. Nakubaliana na malengo yaliyowekwa ya uchumi, ukusanyaji wa mapato, upandaji wa bei na akiba ya fedha za kigeni, kama yalivyowekwa katika ibara ya tatu. Ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri, lengo la kuweka akiba isiyopungua miezi mitano, naona ni legelege na ukiweka lengo legelege, utekelezaji wake utakuwa legegele. Nafikiri lingewekwa lengo la kusema tuwe na akiba ya kuweza, badala ya kusema kisichopungua, kusema kwamba zaidi ya miezi mitano.

Vilevile tukizingatia kwamba, unapoweka lengo la akiba la uagizaji la miezi mitano na shilingi ikiendelea kuporomoka, maana yake ni kwamba, utakuwa na akiba ya kuagiza kwa miezi mitatu au chini ya hapo. Kwa maana hiyo basi, tuweke lengo ambalo ni *motivated* kwa sisi kufanya jitahada zote kuhakikisha kwamba tuna akiba kubwa.

Katika ibara ya saba, tunaambiwa kuwa kiwango cha mikopo katika robo ya kwanza ya mwaka huu, kimeongezeka na baadhi ya sababu zilizotolewa ni kutoa mikopo kwa watu ambao ni waaminifu. Hapa nilikuwa nataka kutoa tahadhari tu, ambayo nilikwishatoa wakati wa Kamati, hili suala la uaminifu inabidi tuliangalie vizuri sana. Kwa sababu ni huo uaminifu wa mikopo mingi uliotolewa kule Marekani, ukaitumbukiza

dunia katika janga hili la msukosuko wa fedha. Hata hapa hapa nyumbani, katika miaka ya 70, mikopo ambayo ilitolewa zaidi na *NDC* kwa vyama vyetu vya ushirika, iliipelekea *NDC* karibu iwe mufilisi. Kwa hiyo, ni tahadhari tu kwamba, tuangalie nani hao tunawakopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi sita ya mwisho wa 2008, tunaambiwa kwamba riba za mikopo katika mabenki ya biashara zilipanda kutoka asilimia 15.5 hadi asilimia 16.5. Kwanza, niseme sisi tunaokopa katika mabenki haya, hivi viwango vinavyoonyeshwa inaelekea kuwa tofauti na kiasi halisi tunachotozwa. Riba sasa hivi ni kati ya asilimia 18 na 20.

Vilevile kupanda kwa riba kunapunguza kasi ya ukopaji, kwa maana hiyo hata uwekezaji na uzalishaji utakuwa unaporomoka. Sasa labda niulize swali tu; Benki Kuu ya Tanzania ina nyenzo *(tools)* za kuweza kudhibiti upandaji holela wa riba kwa kutumia *phyisical* na *monitary policies*; hivi kwa nini nyenzo hizi hazitumiki?

Katika mapitio ya mwenendo wa bajeti kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2008, kama inavyoelezwa katika ibara ya 14, ukusanyaji umepungua lengo letu kwa asilimia kwa asilimia saba, ambao umesababishwa na sababu mbalimbali; zikiwemo makusanyo hafifu katika ushuru wa forodha, kodi ya mapato, kwa makampuni na ushuru wa bidhaa za ndani na kutoka nje. Ni kweli naona katika bajeti hii, zililengwa hatua za kuweza kurekebisha hali hii ili mapato yaongezeke. Mimi nataka kutilia mkazo kwamba, pana haja ya kuhakikisha kwamba, Serikali inakuwa makini katika kutoa misamaha kwa makampuni, hasa yale makubwa ya biashara kama kwenye mawasiliano ya simu, kwenye migodi na mahali pengine. Hili litasaidia sana kuhakikisha kwamba, makusanyo yanapatikana kwa wingi zaidi.

Pili, kuimarisha utendaji katika bandari zetu. Wenzangu wamelizungumzia hili, lakini nitofautiane kidogo na baadhi ya wenzangu kwamba, pale bandarini tusiangalie tu bandari imefanya nini; ni *port operation* kwa maana ya kwamba, kuna *TRA* kuna *TPA* yenyewe au *TICTS*, kuna wasafirishaji wa nchi kavu, kuna *Clearing and Forwarding Agency* na kadhalika. Hawa wote wanahitajika wasimamie vizuri, waweze kutoa huduma zao kwa hali ya juu. Bahati nzuri, nafahamu kwamba, kuna *Port Operation Meetings.* Badala ya Serikali kungojea kutoa maagizo kwamba, ondoeni haraka katika wiki mbili, tatu; nafikiri wangehakikisha kwamba, hawa *operators* kila mmoja anatimiza wajibu wake.

Vilevile kuna haja ya kuwekeza vyombo vya kisasa. Bila ya kufanya hivyo, hatuwezi kuendelea ambapo kuna nyenzo hafifu. Ninajua mtaji siyo jambo rahisi, lakini tutumie fursa ya mifuko ambayo ipo, kwa mfano, *NEPAD* inasaidia miradi ambayo faida zake zinasaidia kwa nchi zaidi ya moja; na kwa kuwa sisi bandari zetu hasa ya Dar es Salaam zinahudumia nchi zaidi ya sita, kwa hiyo, itakuwa ni rahisi sana kwa Serikali kuvutia mpango wa *NEPAD* ukaweza kusaidia kuleta vitendea kazi na miundombinu ambayo inaweza kusaidia kuleta kuleta maendeleo.

Kubwa zaidi, umefika wakati sasa hivi badala ya *TPA* kuwa wao ndiyo *operators*, tuweze kukodisha kwa zaidi ya mtu mmoja. *TICS* wakipewa ushindani, naamini kabisa wao watafanya vizuri na wengine watafanya vizuri. Sasa huu ukiritimba tuuondoe, kwa sababu hivyo ndivyo inavyofanyika katika bandari zote ambazo zinafanya vizuri.

Mimi nimetembelea kule Singapore Port Authority, Port Kilang kule Malaysia, nimekwenda Kobe na Japan wakati nilipokuwa DG wa THA, nimekuta kwamba wenye bandari wanabaki kuwa *Landlords* na wapangaji wao ndiyo wanalipa kodi kule ya upangaji. Wakati huu si wa kutegemea kupeleka maagizo tu ni wakati wa kuacha nguvu za soko zifanye kezi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bandari zetu za Tanga, Mtwara na kwenye maziwa, tutangaze watu mbalimbali waje watoe huduma kwa mikataba. Hapa ninataka kutoa tahadhari; baada ya kutangaza na watu kujitokeza, tusije tukaburuza watu ovyo. Mfano ambao uko pale TRC, ambapo mimi niliwahi kuwa DG unasikitisha; hawa Rites walikuja wakati mimi niko pale, walikuja kama washauri lakini walipofika pale wakawa wanajifunza kutoka kwa vijana wangu. Leo hii tunapata matatizo ya kuiendesha Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitambua nia nzuri ya Serikali ya kuboresha miundombinu, kama ilivyoelezwa katika ibara ya 24 na hasa katika masuala ya barabara. Mimi nataka kushauri kwamba, tusiangalie zile barabara kuu peke yake, Barabara za Wilaya na Vijijini, zina mchango mkubwa katika kuchangia uchumi wa nchi hii. Nitoe mfano, pale Wilayani kwangu Kisarawe, nimepiga kelele juu ya barabara ya kutoka Pugu kwenda mpaka Vikumburu, kwa muda wa miaka 13 zimejengwa kilomita sita. Hadi leo, Serikali haijatambua kwamba, barabara hii ndiyo iliyokuwa karibu kufikia Mbuga za Selous kuliko nyingine yoyote ile; na kwa maana hiyo, ukiiboresha basi umeboresha utalii ambao sasa hivi tunasema kwamba unashuka. Barabara hiyo, ndiyo inayoweza kurahisisha usafirishaji wa watafiti wa mafuta. Hivi sasa wapo kule Kisangire lakini wanapitia Mkuranga, wanachukua saa moja na nusu kufika pale. Serikali hailitambui hili.

Barabara hii ndiyo ambayo ingeweza kurahisisha usafirishaji wa matunda, mboga, bidhaa za misitu na kadhalika na ingeweza kufika Dar es Salaam kwenye soko na kwenda nje ya nchi. Barabara hii ikiboreshwa, itasaidia sana kuinua maisha ya wananchi wa Kisarawe hasa waliokuwa kando ya barabara. Serikali ina kigugumizi gani; kilomita 95 tu wala siyo nyingi? Ninafikiri Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Fedha, wataangalia uwezekano wa kuhakikisha kwamba, wanaweza kusaidia kuongeza uchumi kwa kuangalia maeneo ya miundombinu katika maeneo ambayo yataleta fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini yameorodheshwa kama kipaumbele na sisi sote tunatambua, lakini kwenye hiyo ibara ya 24 unazungumziwa tu usafirishaji wa madini ili kuongeza thamani yake. Sisi tumeweza kuishauri Serikali mara nyingi sana, ukiondoa hii; kwa nini tusiongeze maeneo ya kodi? Kwa nini mrabaha ubakie katika 3%? Kwa nini katika maeneo ya machimbo na Serikali za Mitaa wasichangie mambo ya maendeleo? Kwa nini Serikali isitoze kodi zile za ziada? Leo dhahabu, kwa mfano, inaweza ikawa bei fulani wakati wanawekeza lakini baada ya miaka mitatu au mine, bei

imekwenda juu sana, wanapata faida za haramu. Serikali inasitasita kutoza *withholding tax!* Haya ni mambo ambayo yangeweza sana kusaidia kuinua uchumi katika Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu umetilia mkazo sana uzalishaji kwa matumizi ya ndani na nje. Mimi nashauri hebu tuangalie uwezekano wa kufanya *substitution* ya *import*. Kuna maeneo laba nikitumia kile Kiambatisho Namba E, hivi kweli tunataka kuagiza mbolea kutoka nje wakati maliasili zipo hapa ndani na nguvukazi ipo? Hivi kweli tunataka tuendelee kuleta chini ya *intermediate goods* tusitengeneze hiyo mbolea, tusitengeneze vifaa vya ujenzi, tusitengeneze *consumer goods.* Mgogolo SPM kilikuwepo pale, tuliwahi kuzalisha na viwanda vya nguo vilikuwa saba. Mimi niliwahi kuwa mmoja wa Viongozi wa *NDC,* wakati tukiendesha viwanda vile na Tanzania ilikuwa inaongoza katika Afrika Mashariki kwa viwanda hivi. Kwa nini tusivifufue ili tusiendelee kuagiza nguo kutoka nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nauliza Tegri Plastics iko wapo hivi sasa? Mwatex iko wapi? Urafiki iko wapi? Ubungo Textile Mills iko wapi? Ubungo Spinning iko wapi? Mutex iko wapi? Hivi viwanda tukivifufua, vitasaidia sana kukomboa fedha za kigeni tunazoagiza katika mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sitaki kugongewa kengele ya pili, naunga mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, ajiandae Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, nadhani na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ataweza kufikiwa pia.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyokuwepo jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Waziri, imezungumzia nakisi ya bajeti ya Julai – Desemba, 2008 ya milioni 172 na sababu amezieleza ambazo ni ushuru wa forodha, kodi ya mapato kwa makampuni na ushuru wa bidhaa kutoka nje. Yote hii imesababishwa na nini?

Moja, nina hakika ni suala zima la bandari yetu ya Dar es Salaam; kumekuwa na urasimu, meli inakaa kwa muda mrefu nje ya bandari mpaka kupata kibali cha kuingia ndani. Wafanyabiashara wengi, wameacha kuitumia bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huko nyuma, tulikuwa tunafanya vizuri bandarini. Sasa hebu Serikali irudi nyuma, ione wapi wamejikwaa kwa sababu zipo sababu na isije ikachelewa sana tukazidi kuumia katika suala hili. Kukosa pesa hizi nyingi na hatimaye tulikuwa tunapata nyingi zaidi; hebu turudi nyuma na tutazame tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa ni kushughulikia hii misukosuko ya uchumi duniani; hivi tunajiweka katika nafasi gani sisi kama Tanzania ambao tunategemea sana mambo kutoka nje, lakini sisi wenyewe Mungu ametujalia rasilimali za kutosha za kuweza kutunufaika sisi wenyewe na tukazitumia vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusisitiza hoja yangu ya kutumia rasilimali zetu, kama gesi tuliyokuwa nayo.

Tulikuwa na semina na watu wa BoT, walizungumzia suala zima la kuleta wawekezaji, lakini pia wameitaja Nchi ya China kwamba ni watu ambao tunaweza kuwatumia vizuri katika uwekezaji. China ni nchi pekee duaniani, ambayo haikutetereka na uchumi huu. China sasa hivi inachosikitika ni kwamba, haiuzi bidhaa zake kama ilivyokuwa inauza hapo mwanzo lakini ina *reserve* ya *trillion of dollars* katika benki. Sasa tujaribu kutumia nafasi hii; ni nchi rafiki wanatuelewa vizuri, tunazungumza nao lugha nzuri, hebu tujaribu kuwekeza katika Sekta muhimu ambazo zitatuondoa hapa tulipo. Kubwa zaidi linalotusababisha sisi kurudi nyuma, narudia tena katika suala zima la Nishati ya Umeme kwa kutumia gesi na kutumia maporomoko ya maji. Nasema tuwape miradi wawekezaji wakubwa, ambayo sisi Serikali hatuna uwezo wa kuweza kuishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mradi wa Umeme wa *Stigler's George*, ambao umelala katika *shelf* kwa zaidi ya miaka thelethini au arobaini. Hapo awali, gharama za kutengeneza umeme katika *Stigler's George*, ukilinganisha na sasa ni tofauti kubwa sana na jinsi tunavyochelewa, gharama zinakuwa kubwa na Serikali haiwezi. Kwa hiyo, ni lazima tutafute mwekezaji mkubwa aweze kuwekeza. Tukijenga *Stigler's George*, tutakuwa na uhakika wa umeme, *deficit* tuliyokuwa nayo sasa hivi itaondoka moja kwa moja; na tutakuwa na ziada, tutaweza kupumzisha mitambo mingine ambayo inatumia gesi na *diesel* ili tuweze kufanyia marekebisho mazuri. Tutaondokana na mikataba ya dharura iilyoitia hasara Serikali.

Sasa yote haya kwa kutengeneza tu Mradi wa *Stigler's George*, tutaokoa pesa nyingi; viwanda vyetu nchini vitakuwa vinafanya kazi vizuri bila *interruption* yoyote, tutazalisha kwa wingi, tutauza nje kwa wingi na hatimaye kuweza kupata pesa nyingi za kigeni na sarafu yetu iweze kupata nguvu. Nasema hiyo ni moja tu.

Vilevile tutaweza ku-*control* mafuriko ya maji katika maeneo ya Rufiji. Tukilitumia Bonde la Rufiji lile, tunaweza kuzalisha kwa utaratibu mzuri sana. Sasa yote haya, Serikali inayafahamu lakini tunapofika mahali kuamua tuanze na lipi; mbona Serikali tumeamua sasa tujenge barabara zetu kwa pesa zetu wenyewe na tumeweza. Naipongeza Serikali kwa hatua hii. Sasa hivi tunakwenda *systematic* kabisa kwamba, barabara zetu nchini tunaziweka kwa kiwango cha lami tunaweza. Sasa tuamue vilevile katika suala la nishati kwa kutumia sasa gesi tuzalishe umeme, tumtafute mwekezaji aweke mitambo ya gesi ambayo itazalisha megawatt 400, 600 au hata 500. Tujenge *line* za *grid* tuweze kusambaza na tuwe na *alternative;* kukiwa na ukame tuna gesi, kukiwa na tatizo lingine tutumie makaa yetu ya mawe.

Tuna matatizo ya reli yetu; reli inahitaji ukarabati, inabidi tuagize reli kutoka nje wakati tuna migodi ya Mchuchuma na Liganga. Chuma kipo kingi pale, tuagize reli kutoka nje wakati tuna migodi ya Mchuchuma na Liganga? Chuma kipo kingi pale, tutafute mwekezaji haraka ili angalau tutengeneze reli yetu kwa malighafi yetu wenyewe, tutauza reli na makaa nje.

Sasa haya yote ni kupanga na Serikali inaelewa, ina wataalamu wa kutosha, tatizo mimi ninaloliona ni kwamba, wataalamu wetu wamekaa pamoja na utaalamu waliokuwa nao, wanashindwa kufanya kazi yao kwa hali halisi inayotakiwa. Viongozi tunashindwa kutoa uamuzi wa haraka, kwa hiyo, tutakuwa hatuwatumii vizuri wale wataalamu, wanasubiri maamuzi ya Viongozi. Sasa hebu tujaribu kuwaambia hawa wataalamu wetu na kuwatumia vizuri, watufanyie kazi ambayo wao wanaijua na nina hakika wataifanya vizuri zaidi. Tatizo ni uamuzi wa Viongozi katika kutekeleza hayo mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kilimo kwa ardhi tuliyokuwa nayo, tukisema tunaipeleka sekta binafsi; sekta binafsi yenyewe ni sisi wenyewe Wananchi wa Tanzania, ambao wengi wetu ni wakulima na ardhi ipo. Tuhakikishe kwamba, tunawawekea miundombinu ya kuweza kufanya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Profesa Mwandosya, amezungumzia hapa hapa suala zima la maji, lakini ninasema bado maji tunayo na tunaweza tukayatumia vizuri tukaondokana na tatizo la kuogopa mambo ya ukame, njaa na kadhalika, lakini uwe ni utaratibu wa kuuza chakula nje. Tukifanya hivyo, nina hakika Serikali ikipanga vizuri tunaweza kutekeleza mambo yote sisi wenyewe, isipokuwa tusibebe mzigo ambao hatuuwezi; kuna utaratibu wa kuwekeza basi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi katika suala zima la maji, Mheshimiwa Profesa Mwandosya, alizungumzia hapa suala la maji. Kuna Miradi ya Maji Vijijini, ambapo vijiji vingi hata leo maswali ya matatizo ya maji vijijini yamezungumzwa. Kuna miradi mingi sana vijijini, lakini tunapata matatizo ya miradi kufanya kazi kwa sababu ya matatizo ya umeme. Pengine siyo umeme hasa, labda umeme upo lakini utakuta *transformer* hazipo. Hivi *transformer* 100 kwa ajili ya kukamilisha Miradi ya Maji kwa wananchi hii inatushinda nini? Ukiacha matatizo mengine makubwa, tumezungumzia hapa kwamba, maeneo yote ambayo ni vyanzo vya maji, wananchi waondoke ili yale maeneo tuweze kuhifadhi vyanzo vya maji.

Tunayo matatizo ya kwamba, wale kuwaondoa inabidi tuwalipe fidia ili waondoke tuwe na mfumo mzuri wa kuhifadhi maji. Haya ni moja ya matatizo ambayo tunayapata katika maji. Kwa hiyo, Serikali ikitekeleza haya yote, ndiyo mimi nataka kusema kwamba, mengi yamezungumzwa nitarudia tu yale yale, hakuna sababu. La msingi ninachotaka kusema ni kwamba, jamani Serikali tunapata vizuri, upangaji wetu ni mzuri na unatekelezeka, lakini naona tatizo la kuamua kuanza kutekeleza ndiyo linatupa tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Serikali ililizingatia kwamba, tunachoamua na tunachopanga basi tuamue kutekeleza mara moja, badala ya kupanga halafu hatimaye hatutekelezi kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIB SPIKA:** Ahsante sana kwa kuniokolea muda na sasa nitamwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya, naona hayupo; basi Mheshimiwa Wilson Masilingi na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ajiandae. Inaelekea Mheshimiwa Kimiti unaweza kufikiwa.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nishiriki katika mjadala huu wa mpango uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi katika kutuwekea mambo yetu sawasawa, tunapojiandaa kuandaa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia, napenda kuanza na nukuu iliyonivutia sana, kutoka kwenye mawasilisho ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Iko ukurasa wa 7, Ibara ya 19:-

"Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo hayo changamoto zilizopo ni pamoja na kuhakikisha kwamba matokeo ya ukuaji wa uchumi jumla yanawanufaisha wananchi katika ngazi ya kaya; kuendelea kuimarisha miundombinu muhimu katika sehemu za uzalishaji; kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji; kuendelea kuboresha huduma za jamii; na kuendelea kudumisha misingi ya Utawala Bora."

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Serikali kwa kuendelea kuzingatia mambo ya msingi na kwa ujumla wake, kwa miaka mitatu ambayo wamekuwa wanasimamia mambo yetu kwa niaba yetu, mmefanya kazi nzuri sana. Mfumko wa bei 13% kwa majirani ni mpaka 39% kwa nchi yetu umechangiwa na bei ya vyakula.

Zaidi akiba ya fedha za kigeni, hamjakula hiyo hela, bado mna akiba ya kuweza kuagiza bidhaa ya mpaka miezi mitano hivi. Huu ni uadilifu wa hali ya juu na umakini katika kusimamia uchumi. Waziri wa Fedha na Uchumi, ninakupongeza sana na kupitia kwako nawapongeza Wizara nzima na wanaokusaidia, Manaibu wote na Watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Serikali kwa ujumla. Miaka mitatu ilikuwa inatosha kula zile dola zote zikaisha, mfumko wa bei ukafika mpaka trilioni kama Zimbabwe na mambo yakaharibika kabisa. Mnastahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina ushauri mdogo kuongeza sauti kwa maneno mazuri ambayo yamezungumzwa na walionitangulia kuzungumza.

La kwanza, nawashauri Serikali mzingatie kwa makini sana, ushauri mzuri uliotolewa na Kamati Bunge ya Fedha na Uchumi. Nimevutiwa pia katika mawasilisho

ya maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwamba, Serikali ni sikivu katika mpango huu, mmezingatia ushauri wa Wajumbe wanaotuwakilisha kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi; hilo ni jambo jema mlizingatie na ushauri tutakaoutoa hapa mjaribu kuupa uzito wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa tisa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amezungumzia mpango wa dharura na hapo amenifurahisha sana kwa sababu wamegundua hatari ambayo inatunyemelea kwa uchumi wa dunia kuyumba. Jambo la msingi ambalo Serikali mmeliona na ninaliunga mkono mia kwa mia ni umuhimu wa chakula. Kama hatukuwa na chakula cha kutosha, tuko kwenye hali ya kutisha. Ninyi mmeona kuna umuhimu wa chakula na mmeweka mpango wa chakula na kuainisha Mikoa ambayo ina uwezo kutokana na ardhi yake nzuri, maji ya kutosha na mvua, kuweza kuwa ndiyo kikapu cha chakula cha Taifa.

Ninashauri kuongeza hawa wafuatao; tafadhali sana Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza, wapewe fedha ya kutosha, matrekta ya kutosha na katika mashamba yao ambayo ni makubwa, wawekewe miundombinu ya umwagiliaji. Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tuliitembelea Kambi ya Ruvu mwezi jana, wana uwezo mkubwa wa kuzalisha mpaka vifaranga vya kutosha nchi nzima, lakini hawapewi fedha. *Incubators* ziko tupu na zinafanya kazi, mayai yapo lakini tunaagiza vifaranga kutoka nje!

Hayo ni mambo ya kusahihisha, lakini hapa nasisitiza chakula; Jeshi la Kujenga Taifa wana uwezo, vijana wote walioko vijijini, ikiwezekana waingie kwenye Jeshi la Kujenga Taifa, tuwafundishe mbinu za kilimo na ulinzi wa nchi yetu, tutapunguza *pressure* ya vijana wasio na ajira vijijini. Katika mpango wa dharura na Serikali mtenge fedha kama Wamarekani wanasema, Serikali ina *stimulus plan*, sisi tuna bilioni ngapi zitafutwe.

Hii kutuambia mambo ya World Bank, IMF, wanasema Serikali haifanyi biashara tusiisikie safari hii kwa sababu dunia nzima ipo vitani. Tunaingia katika biashara na Serikali mfanye biashara, sekta binafsi hakuna hapa haijakua; mimi siwatukani, haiwezi kuhimili uchumi wetu na hawawezi kutusaidia kuzalisha chakula. Lakini kwa kutumia Watanzania wenzetu, kaya zitaondokana na umaskini na tutaweza kupata watu wenye kipato na umaskini wa kipato utapungua. Kwa hiyo, uchumi utakua maana yake kama tunakuza uchumi watu hawawezi kununua, huo ni uchumi tete. Uwezo wa kununua ni muhimu kwa jamii.

Hifadhi ya mafuta tuliashaamua hapa utekelezaji unachelewa nini? Masuala ya energy tusipoyasimamia vizuri; umeme; Stigler's George wanaililia hapa kila siku, tukaenda sehemu ambazo mmezibainisha vizuri, China, Japan, Mashariki ya Kati, wakawekeza kwenye maeneo hayo; tusipoyaangalia maeneo hayo siyo tu kwamba tutaathiri uchumi, bali pia tutatishia usalama wa nchi yetu. Masuala ya umeme ni muhimu sana.

Nimefurahi sana mmendelea kuweka kipaumbele kwenye barabara. Ninamshukuru Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, anipe taarifa nzuri sana kuhusu Barabara ya Kagoma, Muleba, Biharamunga, Rusahunga kilomita 182 pesa na mambo yamekamilika, mnasubiri tu idhini ya Benki ya Maendeleo ya Afrika ili Mkandarasi mliyemchagua aweze kuchemka. Serikali mnachapa kazi, lazima niwapongeze, mkivuruga nitawaambia mimi siwaogopi. *(Makofi*)

*Transit trade,* hii biashara ya kuhudumia bidhaa zinazopita nchini, Serikali na Gavana wa Benki wametuambia inaingiza fedha katika uchumi wetu. Hongera Serikali mmeliona, tafuteni fedha tulifanye hili litatusaidia.

Jambo lingine ni kusimamia fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, msiwaachie hawa; kwanza uwezo wa Halmashauri za Wilaya kusimamia mambo haya ni mdogo.

Pia uadilifu wao unatia mashaka baadhi yao, kwa sababu fedha inayopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo ni nyingi, hazifiki kwa walengwa.

Nitawapa mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali Kuu ilitupatia fedha ya ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo 3,965,473,534.87; hiyo ni ruzuku ya maendeleo mmetuletea Muleba kwa mwaka mmoja. Mkatuongezea dirisha lingine la *TASAF;* bilioni 1.6 milioni, jumla 5,565,473,534 bila senti. Kama tungezingatia vipaumbele vya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tukatenga milioni 80 kwa kila Kata, tuna Kata 30 Wilaya ya Muleba, milioni 80 tu tukaongezea michango yao ya fedha na nguvukazi, tungeweza kutumia bilioni mbili na milioni mia nne tu na zingebaki bilioni 3.1 kwa ajili ya shughuli nyingine.

Sasa aibu iliyopo Muleba, watoto hawana madarasa ya kuingia, wanaokwepa majukumu eti Mbunge anazuia maendeleo kwa kuwaambia zingatia vipaumbele, tumia fedha za watu sawasawa; hivi kweli kwa nini hizi pesa hazikusaidia kuandaa madarasa? Mnatoa kila mwaka, nitawaambia wakati wa bajeti na kama hamtazifuatilia, sitaunga mkono bajeti yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Serikali mnafanya kazi nzuri, hawa ambao walikula hela mtawashughulikia. Kuna vituko kule; Jumapili Mtumishi wa Serikali aliwatangazia watu Kanisani, Mzee wa Kanisa amenipigia simu analalamika Serikali imetoa maelekezo kila mwenye uwezo wa kufanya kazi 10,000 kwa kichwa; wazee, wajane na kadhalika. Namsubiri aje anipe waraka huo nije nao Bungeni. Kuhangaisha watu, tena wa Serikali Kuu siyo wa Halmashauri, anawatangazia watu Kanisani eti ana maagizo ya Serikali Kuu 10,000 kwa kichwa! Jumapili iliyopita Mzee wa Kanisa alinipigia simu; anisubiri tu nikimaliza Bunge nakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru Waziri wa Fedha na Serikali, wanachapa kazi vizuri sana, mengine tutasaidiana. Nitawapeni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, mtafanya kazi kuangalia utekelezaji wa miradi, thamani ya

fedha izingatiwe. Hii ku-*balance* vitabu hata ukijumlisha havi-*balance*; sijui ni kwa makusudi au hawajui? Nitawaletea taarifa baadaye.

Mungu awalinde, endeleeni vizuri sana na kazi yenu nzuri sana, wanaowavurugia tutawashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hoja hii muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hoja hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuileta kwa wakati muafaka, kwa sababu yapo mambo ambayo kimsingi ni lazima tuchangie mapema ili wakati wa bajeti tusianze kupigiana kelele. Nina mambo makubwa manne:-

La kwanza, ni lazima tukubali kwamba, dunia imebadilika, watu wamebadilika na mipango yetu ni lazima ibadilike ili ilingane na hali ya mazingira tuliyonayo. Ninachoomba cha kwanza kabisa, naogopa kuwa na mipango ya kijamaa, lakini utekelezaji wa kibepari. Nitaeleza sababu zake.

Unapokuwa na mpango wa kijamaa, tunategemea mpango huu ujibu matatizo ya watu uliokuwa nao. Marekani inaanza kuwaogopa sana Wachina, *speed* ya Wachina katika uchumi huwezi kuamini. Siri yao ni nini? Nilishapata nafasi ya kwenda China.

La kwanza, walikuwa na Mapinduzi ya Kilimo wanaita *agrarian reform*. Nimekwenda kujifunza, nikarudi nikaandika Ripoti sijui imeishia wapi. La pili, mapinduzi ya viwanda; msione *handsets* zote hizi zinaandikwa *Sonny Erricson, Samsung,* zinatengenezwa Uchina na hali yao inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niombe sasa ya kwamba, katika mipango yetu tuliyokuwa nayo kwanza tuanze na kilimo. Sisi tunaamini nguvu ya askari yeyote ipo tumboni na Walatin wanasema *"premum vivere dien de philosophal,"* maana yake kwanza, tumbo lishibe ndiyo siasa watu watakuelewa, wasiposhiba yote utakayozungumza unapoteza muda wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niombe yafuatayo; pamoja na nia nzuri sana ya Serikali yapo mambo ambayo tumekuwa tukizungumza hapa Bungeni yanaanza kuwa ni kero sasa:-

La kwanza, mishahara ya watumishi. Mimi nataka kuzungumzia, ninapokuwa kiongozi napenda kuangalia chini siyo juu. Naangalia hawa wa chini hali yako ipo namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya kima cha chini bado sijaridhika nayo, halingani na mazingira tuliyokuwa nayo. Upo mwaka Mwalimu Nyerere aliamua mishahara ya Mawaziri na Viongozi wote isimame ili kuhakikisha hao watu tunawavuta kidogo, wawe na afueni hata kidogo. Tutaendelea kutegemea wananchi watupe *support* kwa mishahara kidogo kiasi hicho? Kima cha chini cha mshahara kiangaliwe. Najua tuna matatizo, tunaweza kupunguza hata *OC* kidogo tukawaongezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia pensheni ni aibu. Kiwango kinachotolewa kwa pensheni ni utani, kama hatuwezi afadhali tuache kabisa. Unawezaje kumpa mtu shilingi 20,000, 30,000 kwa mwezi, kama haiwezekani tuseme pensheni hakuna. Tuwape viwango vitakavyoweza kukidhi wazee wetu waliolitumikia Taifa hili, kwa uaminifu wa hali ya juu sana, wapate angalau afueni ya kuweza kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la pensheni kwa Waheshimiwa Wabunge. lipewe umuhimu wake. Nalisema hilo, wapo marafiki zangu bahati mbaya Mheshimiwa Jackson Makwetta hayupo hapa. Wakati mwingine huwa ninajiuliza; hivi Mheshimiwa Jackson Makwetta akiacha Ubunge anakwenda kufanya nini, hana pensheni huyu, siku mbili atakatika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na utaratibu, Mbunge asionekane anang’ang’ania nafasi ile kwa kuwa anajua akitoka hapa hana pakwenda, tumuwezeshe. Ndiyo maana Viongozi Wakuu wa Serikali, wamepewa mihula miwili kwa makusudi mazima, lakini wamepewa angalau akitoka atatoka na asilimia 80 ya mshahara wa kiongozi mwenzake aliyekuwa madarakani, hata ukitoka huna wasiwasi una haraka gani? Baada ya vipindi vyako viwili, unaondoka huna wasiwasi. Katika mazingira haya ya watu kukaa hujui baada ya Ubunge unakwenda wapi, ndiyo haya tunagombana kwenye Majimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipozungumzia mipango ya kijamaa isiendane na utekelezaji wa kibepari, narudi sasa kwenye kilimo. Ili tuweze kufanikiwa katika kilimo, pembejeo ni ya awamu ya kwanza, lazima ipewe kipaumbele. Naisema hiyo kwa sababu ukitaka pembejeo iende kijamaa, lazima Serikali iweke mkono wake pale. Ukitaka kuagiza pembejeo, tumia chombo cha Serikali kikuletee pembejeo kutoka kiwandani moja kwa moja, kama tunavyoagiza wakati mwingine magari kutoka kwenye kiwanda moja kwa moja. Ukitaka mtu wa katikati awaletee, ndiyo ubepari unaingia pale; atakuletea ataweka bei zake na tutaumia sisi wenyewe. Naomba mliangalie litatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi; ningezungumza juu ya maji, juu ya tatizo la umeme, juu ya upungufu wa walimu, juu ya wastaafu na matibabu mengine. Naomba Mheshimiwa Waziri, anielewe; mwaka 1990 tukiwa Bungeni hapa na wakati huo bahati nzuri Mheshimiwa John Samuel Malecela, alikuwa Waziri Mkuu, tulikuwa na tatizo kubwa sana la barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga. Kwa mara yetu ya kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa, tulikubaliana kusaidiana na Mheshimiwa Marehemu Kinyondo, kuondoa shilingi na tulikaa karibuni siku mbili tumekataa shilingi isirudi mpaka barabara itengenezwe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati huo Mheshimiwa John Malecela, namshukuru sana, alikubali akasema sasa Sumbawanga - Tunduma wajengewe barabara angalau ya kudumu kwa kuanzia, halafu tutafute fedha kutoka Benki ya Dunia, wajenge kwa kiwango cha lami. Hiyo napenda kumshukuru sana Mheshimiwa John Malecela, aliisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ilitengenezwa na China SIETCO kwa kipindi cha miaka miwili, mitatu, tukiahidiwa ya kwamba barabara itajengwa kwa lami. Benki ya Dunia ikaahidi kwamba, kwanza, itatoa fedha ya kufanya upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu ulianza na kufika mwaka 1995 mpaka 1998 ukawa umekamilika, barabara hiyo ikafaa kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu mkubwa sana, ahadi hiyo mpaka leo haijatekelezwa. Tatizo lipo wapi? Tatizo lipo katika utaratibu wa kutumia fedha za wenzetu; katika kipindi chote hicho zipo barabara nyingi sana zimetengenezwa. Mimi nilishangaa wakati tunasubiri Benki ya Dunia, barabara zifuatazo kwa zimejengwa; Dodoma - Manyoni, Nangurukuru -Mbwemkulu - Minyongo, Somanga - Matandu, Geita - Kyamiorwa - Busingayombo, Marangu - Tarakea ambayo inajengwa, Dar es Salaam - Kibiti, Daraja la Umoja ambalo linaendelea kujengwa na barabara nyingine zinaendelea kukarabatiwa kama Mwanza -Shinyanga, Kagoma - Rusahunga, Arusha - Namanga, Chalinze - Segera, Songwe - Tunduma, Nelson Mandela inaendelea kujengwa, Sumbawanga – Tunduma; mpaka leo hata dalili ya kusema tutapata fedha hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yenu, MCC imeahidi kutoa fedha za kujenga barabara ya Tunduma mpaka Sumbawanga, lakini barabara hiyo imo katika *priority* ya mwisho mwisho. Kati ya barabara ambazo labda zitapewa kipaumbele ni Tanga – Horohoro, ambayo wanaona ni fupi, wanaogopa ile ya Tunduma - Sumbawanga labda ni ndefu sana. Halafu ipo barabara nyingine nadhani ni Songea - Namtumbo - Peramiho - Mbinga, Tunduma - Sumbawanga ni ya mwisho. Tumekosa nini watu wa Rukwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate maelezo; katika Ilani ya Uchaguzi tulikubaliana barabara namba moja ni Tunduma - Sumbawanga na sote ni mashahidi; wana-CCM someni Ilani ya Uchaguzi. Fedha zilizotolewa safari hii ni karibu dola milioni 373 au 378 kati ya zile dola milioni 700 ambazo zitatumika kwa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako, urefu wa barabara zote hizi za kuanzia Tanga kuja huku Songea mpaka Rukwa, ambapo nimeifanya hesabu; kilomita karibuni 433 kwa fedha hizi tulizopewa hazitatosha, itabidi barabara ya Tunduma - Sumbawanga iumie isipate fedha nyingine. Kwa msingi huo sasa, nataka kuiomba Serikali itusaidie yafuatayo:-

La kwanza, Mheshimiwa Waziri aone uwezekano katika Mpango unaokuja, zitengwe fedha kwa makusudi mazima kutoka kwenye Mfuko wetu wenyewe wa barabara ya Tunduma - Sumbawanga ili ziendane na hizo nyingine zitakazoongezwa, tusije kupata matatizo kipindi fulani zikakosekana kujengwa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, nimwombe Mheshimiwa Waziri, arudie kwenye Ilani ya Uchaguzi; kipaumbele kiwe cha Barabara ya Tunduma – Sumbawanga. Barabara hii imeumia kwa zaidi ya miaka 20, ipewe kipaumbele angalau ianze kutengenezwa. *(Makofi)*

La tatu, barabara hii wakati wa kujengwa ianze Sumbawanga ili tusije kudanganywa inaanzia Tunduma fedha zikaisha, watu wanaohusika Sumbawanga wakasema mlikuwa mnatudanganya, ianzie Sumbawanga tukutane katikati na wale ambao wanaanzia Tunduma. Barabara ikianzia mwisho, inalazimisha Serikali iimalize, lakini ikianzia huko inaweza kuishia katikati wakasema fedha zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, lakini aone uwezekano wa kuwasaidia watu wa Rukwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Aloyce Kimaro anaweza kufikiwa, najaribu kuona kama Mheshimiwa Siraju Kaboyonga atafikiwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali, kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 na 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia au kushauri yale niliyotaka kushauri, nataka niwaeleze Wananchi wa Mbozi, hususan wa Jimbo la Mbozi Mashariki kwamba, wasiwe na wasiwasi kuhusu *voucher* zao kukataliwa na mabenki. Leo nimezungumza kuhusu *voucher* za kilimo, bahati nzuri na Waziri wa Kilimo baada ya Wana-Mbozi wengi kunipigia simu kwamba, wafanya nini sasa kwa sababu Mawakala wameacha kupokea *voucher* zile za wakulima na kwa maana hiyo, zoezi la wao kuchukua mbolea limekwama. Mheshimiwa Waziri, amenitoa wasiwasi kwamba, Serikali imeshapeleka takriban bilioni 15 kwenye mabenki na kwa maana hiyo, Mawakala wanaweza wakazipokea zile *voucher* na wakulima watendelea kupata mbolea. Naipongeza sana Serikali, kwa hatua hiyo, wananchi waweza kufanya shughuli zao za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuzungumzia linalolingana na hilo, lakini sasa kwenye kilimo na kadiri ilivyozungumzwa kwenye mpango. Kwanza, niishukuru Serikali kwa sababu ninaona kilimo kimepewa kipaumbele kwenye maandalizi haya. Nina hakika kwa maana hiyo, hata kwenye Bajeti ya Serikali ambayo italetwa kwenye Bunge la Bajeti linaloanza mwezi wa sita, kitapewa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tunatoka kwenye maeneo ya kilimo na ambao tunategemea sana mbolea, tunaomba sana Serikali iweke mkazo na msisitizo mkubwa sana kuhusu upatikanaji wa mbolea nchini. Tusipofanya hivyo, tutaendelea kukabiliwa na tatizo la njaa mwaka huu, mwaka unaokuja na miaka mingine. Tunajua mipango mizuri ya Serikali ya kuhimiza wawekezaji binafsi kujenga viwanda vya mbolea katika nchi hii, lakini tusichelewe. Mimi nina hakika, kama mwaka huu hatutafanya

vizuri, tunaweza tukapata tabu kubwa sana kuwaeleza wananchi au kuwashawishi waelewe kwamba, kweli Serikali yao imedhamiria kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamelisema sana hili, lakini pia naomba nisisitize kwa uzito kwamba, Serikali kama ilivyoonyesha nia kwenye mpango huu, nia hiyo hiyo ndiyo ionekane kwenye Bajeti ya Serikali, ambayo tutaijadili hapa mwezi wa sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunatoa ruzuku kwenye mazao ya chakula; kule kwetu Mbozi tunapewa sana mbolea kwa ajili ya uzalishaji wa mahindi. Hii ni dhahiri kwamba, Mbozi tunazalisha kahawa na inachangia kiasi kikubwa kwenye Pato la Taifa. Bahati mbaya sana, mbolea ambayo wananchi wanaitumia kwa ajili ya uzalishaji wa kahawa, haina ruzuku. Kwa maana hiyo, wananchi wameendelea kubeba mzigo mkubwa sana na ukizingatia bei kubwa za mbolea ambazo tumenunua mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naimba Serikali; kama kweli Serikali inatambua umuhimu wa zao la kahawa kwa uchumi wa nchi hii na kwa wananchi wenyewe, ione umuhimu wa kuzifanya mbolea za uzalishaji wa kahawa na hususan *CAN* ziwe na ruzuku ya Serikali. Tutakuwa tunawasaidia sana wakulima, ambao wanatumia mbolea ya *CAN* na mbolea nyingine ambazo zinatumika kwa ajili ya uzalishaji wa kahawa. Ninaomba Serikali ilitilie maanani hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wananchi wanatumia zana duni sana kwa ajili ya kilimo, kwa maana ya majembe ya mkono. Hata hayo majembe yenyewe ya mkono, leo hayapatikani kwa urahisi; jembe moja la mkono wale wanaoyajua; kuna chapa cha jogoo, chapa ya mamba, leo linauzwa jembe moja karibu shilingi 20,000. Wakulima wangapi wanaziweza bei hizi na mtu huyu hahitaji jembe moja, anahitaji pengine majembe matano au kumi kwa ajili ya familia yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji pia majembe ya kukokotwa na ng'ombe, majembe haya hayapatikani kwa urahisi. Pale Mbeya tulikuwa na kiwanda ambacho kilikuwa kinazalisha zana za kilimo, tulikuwa tunakiita ZZK; kiwanda kile kilikufa. Tunashukuru kwamba, Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Mkoani Mbeya, mwishoni mwa mwaka jana, alipokuwa kwenye majumuisho ya ziara yake, aliahidi kwamba, anaagiza kile kiwanda kifufuliwe. Wananchi tuliokuwa pale, tulimshangilia sana na tulipiga makofi sana. Tunaomba Serikali sasa ihakikishe kwamba, Tamko la Mheshimiwa Rais la kufufua kiwanda cha kuzalisha zana za kilimo, ikiwemo majembe ya mkono na majembe ya kukokotwa na ng'ombe, sasa linafanyiwa kazi kikamifu ili zana hizo ziweze kuzalishwa na wananchi waweze kuzipata kwa urahisi, kwa maana ya kurahisisha uzalishaji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua Waziri wa Viwanda na Biashara, atakapokuja na taarifa yake Bungeni kwenye Bunge la Bajeti na hili pia atakuwa nalo; kwa sababu sisi wa Mkoa wa Mbeya na Watanzania wanaolima, tumechukulia Ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa uzito unaostahili, baada ya Mheshimiwa Rais kuona hali ilivyo kule Mbeya.

Napenda niseme kwamba, Mheshimiwa Rais alipotembelea Mbeya alisema hajapata kuona mahali ambapo wananchi wanadai mbolea, lakini Mbeya wananchi wanadai mbolea; mzee tupe mbolea sisi tunataka kulima. Maeneo mengine wananchi wanakimbia kilimo, lakini Mbeya watu wanadai mbolea ili wapate kilimo. Sasa kama hivyo ndivyo, tunaomba basi tuwape zana za kilimo na pembejeo ili waweze kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nishauri sana kwenye hili, tungeweka yale maeneo ya uzalishaji sana, tuyape kipaumbele kiwe cha kwanza kinachostahili kwa maana ya maeneo yote yanayohusu pembejeo na zana za kilimo. Nina hakika, suala la njaa katika nchi hii litakuwa ni hadithi. Kwa kweli ukichukulia hali ya hewa tuliyonayo, sisi Tanzania kuagiza chakula nje ya nchi ni aibu kubwa sana. Sasa naomba Serikali iweke mipango mizuri ili tuweze kuondokana na aibu ya kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kwa kifupi masuala ya mawasiliano. Wenzangu wamezungumzia sana suala la bandari na mimi naomba niseme bandari yetu ni kiungo muhimu sana; tutoe kipaumbele kikubwa kwa ajili ya kuifanya inatuletee fedha nyingi katika nchi hii. Mimi ninavyojua, zaidi ya asilimia 50 ya *GD* inatoka pale bandarini. Umuhimu pengine ambao nina hakika Serikali inauona, lakini tunaona kigugumizi cha kuifanya bandari ikawa eneo zuri kwa ajili ya kutupatia mapato katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba niseme kwamba, tusikubali *TICTS* iendelee na *monopoly* ya kufanya biashara kwenye Bandari ya Dar es Salaam; tusiruhusu hilo. Maeneo mengine wanaruhusu ushindani, leo tunasema *TICTS* iruhusu ushindani iweze ku-*handle* makontena zaidi ya 650,000, hilo linaweza lisiwepo wakati wowote ilimradi wanataka kuwe na *monopoly*. Kwa hiyo, ninaomba turuhusu ushindani hata kama hao *TICTS* watakuwa na sifa, lakini kuwe na ushindani. Suala la mtu mmoja kuhodhi biashara leo halipo. Kwa hiyo, hilo naomba Serikali pia itilie maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la umeme. Ninaishukuru Serikali imesisitiza sana suala la kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuimarisha miundombinu ya umeme katika nchi hii. Ninataka nizungumze na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ananisikiliza; mwaka jana nilisema kama bajeti ya Nishati na Madini itakuja mwaka huu bila kuzungumzia viporo vya miradi ya umeme katika Wilaya ya Mbozi na maeneo mengine nchini, sitaiunga mkono Bajeti ya Serikali. Kuna miradi ya umeme ya miaka kumi, miaka sita haijatekelezwa, sijaona kama kuna mkazo wa kumaliza viporo vya umeme katika mpango huu. Kwa hiyo, naliomba sana na hilo; miradi ya umeme iliyoko Mbozi, miradi ya umeme iliyoko Mbeya na maeneo mengine nchini, ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tulipokuwa kwenye kampeni kule Mbeya Vijijini wakati wa uchaguzi mdogo, moja ya eneo ambalo tulipata shida sana kulieleza ni suala la viporo vya umeme kutotekelezwa kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Tukienda kwenye uchaguzi mwaka kesho, hali ikiwa hivyo hivyo, nina hakika tutapata tabu mara

mbili zaidi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba, miradi yote ya viporo vya umeme inatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naona nikazie elimu kwa walipa kodi; kwenye mpango huu tumeelezwa kwamba, kuna baadhi ya maeneo ambayo kodi ilipungua sana. Nilichogundua kwa sababu na mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Ushauri wa Kodi katika Wilaya; wananchi hawana elimu ya ulipaji wa kodi. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iziwezeshe mamlaka zake katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ili ziweze kutoa elimu kwa Watanzania walio wengi, waone umuhimu wa kuilipa kodi Serikali. Hili ni eneo ambalo ningependa nisisitize, kwa sababu tumezungumza kwenye kikao chetu cha ushauri wa kodi Wilayani, tukaona huo ni upungufu. Kwa hiyo, Bodi hizi katika ngazi za Wilaya, ziweze kupewa umuhimu na kwa maana hiyo ziwezeshwe kufanya makusanyo ya kodi yawe mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga sekondari nyingi sana, kipaumbele sasa kiwe kujenga maabara katika shule hizi. Tutakuwa tunazalisha walimu ambao wanajua *theory* tu, lakini vitendo hawajui. Kwa hiyo, mimi naomba tukazanie sasa kujenga maabara katika shule za sekondari. Niliona mpango wa Serikali, nichukulie mfano wa Mbozi; tuna Sekondari za Serikali karibu 43, lakini tunajenga maabara mbili tu. Kama kweli tunataka hawa vijana wasome masomo ya sayansi na kwa maana hiyo wapate vitendo ambavyo vinaendana na masomo ya sayansi, naomba Serikali pia katika hilo itilie maanani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine wenzangu wamezungumza lakini niseme kwa kifupi, riba za mabenki hasa kwenye mikopo zinakatisha tamaa. Wakati amana unayoweka wewe inapewa *interest rate* kidogo sana, lakini wewe unapokwenda kukopa mkopo una riba kubwa. Tunaambiwa kwenye bajeti, zaidi ya asilimia 16 wamezungumza wenzangu nisiendelee sana, pengine tuulize hivi Benki Kuu haiwezi kudhibiti hizi *interest rates* katika mabenki; vinginevyo Benki Kuu kazi yake itakuwa nini kama inaweza ikaacha vyombo vinavyokopesha vikajiamulia vyenyewe kwa ajili ya kukopesha?

Mabenki haya yana hela nyingi sana, wanazifanyia nini wanapokaa nazo; kwa nini wasipunguze viwango vya ukopeshaji ili wananchi wengi zaidi waweze kukopa; na kwa maana hiyo kuwapunguzia Watanzania hawa umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulipitisha Sheria ya *Lease Financing and Mortgage and Financing*, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba, wanatungia *regulations* zake na iweze kufanya kazi. Mwaka huu wananchi waweze kuitumia kwa ajili ya kupata mikopo kwa madhumuni ambayo yalidhamiriwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wanasema ni *Mortgage*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** *Mortgage Finance Act*. Naomba pia niseme kwamba, vitambulisho vya taifa vimekuwa hadithi. Serikali kama ilivyosema kwenye

mpango wake, ihakikishe hili linakamilika. Pengine Watanzania wamechoka kusikiliza vitambulisho vya utaifa haviji. Ninaomba Serikali itilie mkazo vikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nilizungumze ni utekelezaji wa Ahadi za Rais. Mheshimiwa Rais aliyepita, kwenye kampeni mwaka 2005, aliahidi mambo mengi sana kwenye sekta ya maji, sekta ya barabara na kadhalika; tunaomba zitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika mpango huu wa Serikali, kama mwongozo wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka nitoe angalizo kwa Watanzania wote kwamba, hali ya hivi sasa ya uchumi siyo nzuri duniani kote. Duniani kote kuna mtikisiko wa uchumi na sisi kama nchi, hakuna jinsi ambavyo tunaweza kukwepa. Kwa hiyo, tutarajie kwamba, kuna hali ngumu na tujipange katika kuikabili. Hatuwezi kuiachia Serikali pekee iweze kutatua matatizo hayo, lazima sote tushirikiane. Serikali lazima ije na mipango ya uhakika ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo linaweza kuwa ni zuri kwa kukabiliana na tatizo hili la kilimo. Watanzania wengi wanategemea kilimo, zaidi ya asilimia 81 ya walio vijijini, wanategemea ajira kutoka kwenye kilimo. Nchi yoyote ambayo haiwezi kujitegemea kwa chakula, kukitokea mtikisiko lazima iyumbe. Nchi inayoomba chakula, lazima itayumba tu hali ya uchumi duniani ikiwa mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Serikali iweke kipaumbele katika kilimo cha umwagiliaji; haiwezekani karne hii tukaendelea kutegemea kilimo cha kutegemea mvua. Unasema wananchi hawakuvuna kwa sababu mvua haikunyesha, lakini Tanzania imejaliwa ina mito mingi, ina maziwa mengi na pia ina wataalam wa kilimo. Chuo Kikuu cha Sokoine kinatoa watalaam wa kilimo kila mwaka; je, wanakwenda wapi; wanakwenda kukaa kwenye madeski kule Wizara ya Kilimo na Chakula?

Waziri wa Kilimo yupo hapa, pamoja na Waziri wa Fedha, iwekwe mipango maalum ya kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kinapangwa kama vile mipango ya barabara inavyopangwa. Umwagiliaji unahitaji miundombinu iliyopangwa kwa uhakika. Tuangalie ni Mikoa gani ambayo tunaweza tukapeleka fedha, tukaweka miundombinu ya umwagiliaji, wananchi wa eneo lile wakazalisha chakula kwa wingi ili wauze kwa Watanzania wengine ambao hawazalishi. Lazima tupange mikakati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru Rais, amesema atasitisha ununuzi wa mashangingi na matumizi ambayo siyo ya lazima ili anunue matrekta. Ukinunua matrekta na hakuna mpango maalum wa kilimo cha umwagiliaji, ukapeleka matrekta maeneo ambayo mvua haikunyesha, vilevile tutatakuwa hatujafanya kazi ambayo tungetegemea matrekta yale yafanye. Kwa hiyo, naomba mkakati uwepo maeneo yote,

ambayo yangeweza yakawa na kilimo cha umwagiliaji; Serikali isiendelee kusema mwaka hadi mwaka, itoe fedha katika mipango yake ya maendeleo. Fedha za maendeleo zitoke kwenye Bajeti ya Serikali, badala ya kutegemea wafadhili. Unategemea wafadhili hawatoi fedha, baadaye kile tunachopanga hapa kinakuwa ni bajeti hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naiomba Wizara ya Fedha; la kwanza, kilimo cha umwagiliaji, kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Vunjo, kuna maeneo ya tambarare, ambayo wakulima wapo tayari kulima kama miundombinu ambayo imeshaanza kutengenezwa itakamilika. Watalima na wataweza kulisha hata mikoa mitano. Kwa hiyo, naomba mojawapo ya *priority*, Serikali ndani ya mpango huu ipeleke fedha maeneo ya tambarare. *Lower Moshi Irrigation Scheme*, ilishaanzishwa na Wajapan, kwa hiyo, wamalizie vizuri maeneo yale yaweze kuzalisha chakula ambacho tunaweza kulisha mikoa mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka Serikali itoe kipaumbele baada ya kilimo kama unataka maendeleo, ukitoka kwenye kilimo lazima uingie kwenye viwanda. Unaanzisha viwanda vidogo vidogo viwanda ambavyo vinaweza vikasindika yale mazao ambayo yanatokana na kilimo ili uuze kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishauri Serikali iangalie *priority;* ni kitu gani kinapaswa kuagizwa kutoka nje kwa kutumia fedha ambayo inatokana na jasho la wakulima. Fedha za kigeni tunazozipata sasa hivi nyingi zinatokana na mauzo ya pamba, kahawa, katani na mazao mengine ya kilimo. Sasa inakuwaje ile fedha kidogo tuliyonayo, tunautumia kuagiza bidhaa ambazo wala hatuwezi kuzitumia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano leo hii ndani ya soko la Tanzania, kumejaa bidhaa hafifu, ambazo hazina ubora na Serikali ipo. Bidhaa hizo zinanunuliwa kwa fedha za kigeni ambazo zinazalishwa hapa nchini. Kwa hiyo, tunatoa fedha yetu ambayo ingeweza kununua vitu muhimu kwenda kununua takataka kutoka nchi za nje na zile takataka zikifika hapa, baada ya miezi miwili, mitatu, zinaharibika tunakuwa na tatizo la *disposal*. Uharibifu wa mazingira unatokea kwa sababu tunanunua bidhaa hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uliona wapi redio inauzwa shilingi 5,000! Kama redio inauzwa shilingi 5,000, maana yake hata yule mwekezaji wa hapa nchini, hata mimi kama nataka kutengeneza kiwanda cha redio, siwezi kutengeneza kwa kuwa wale wanaoleta redio hafifu, watauza kwa bei ya chini na wale wanaotaka kutengeneza viwanda hawawezi kutengeneza. Kwa hiyo, tutaendelea kulishwa bidhaa ambazo hazina ubora. Naomba Serikali iweke vipaumbele katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuanzisha viwanda ambavyo vitaleta ajira. Kwa mfano, tuna misitu, tuna mbao za kila aina leo hii viwanda vya Malaysia, China, Singapore vinanunua mbao hapa wanakwenda kutengeneza fenicha hafifu. Wanaajiri watu wao kule, leo tunanunua fenicha kwa mamilioni. Fedha za kigeni ambazo zinazalishwa na wakulima, zinatolewa hapa nchini kwenda kulipa wawekezaji wenye viwanda nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano; inakuwaje viwanda vya mbao, Keko yote Watanzania ambao wanaweza kuzalisha fenicha wapo. Serikali yenyewe bila ya kuangalia *priority,* inanunua fenicha ambazo ni hafifu kutoka nchi za nje. Mimi naomba katika bajeti hii, hilo likome kabisa; tutengeneze fenicha hapa, maana yake tunaongeza ajira. Tunaposema maisha bora kwa kila Mtanzania, maana yake tumtengenezee Mtanzania, ajira aweze kulipwa fedha naye awe na uwezo wa kununua na kuondokana na hali duni kwa kutengeneza vitu ambavyo tutanunua sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka hapo, unakwenda kwenye eneo la utalii, ambalo tungeweza tukapata fedha za kutosha kutoka nchi nje, lakini usimamizi wake bado ni hafifu. Sasa hivi Wazungu wanasema, dunia imekuwa ni kijiji; wanazungumzia mambo ya utandawazi, kumbe kule kwao sasa hivi hakuna ajira, hakuna jinsi ya kupata fedha sasa wanarudi tena Afrika kinyemela. Wanasema tunakwenda Afrika kufuatilia, kwa Kiingereza wanasema *the Emerging Markets,* masoko mapya ya Afrika; kumbe sasa kwao kule Serikali zao zinawasaidia zinasema nendeni mkavune mlete huku kwetu. Sisi tunasema hatukatai wawekezaji, waje lakini tuweke sheria nzuri na taratibu ambazo wao watafaidi na sisi tutafaidi.

Angalia nchi kama Dubai, ilikuwa jangwa; leo miaka kumi kila nchi inaona kwamba eneo la Dubai linashangaza kwa nini wameweza kuendelea kiasi hicho. Sisi Watanzania ambao hali ya hewa ni nzuri, kuna kila kitu, tuna maliasili za kutosha, tuna maziwa ya kutosha, tuna bandari ambayo inazungukwa na nchi nyingi, tungetumia tu hii bandari kwa ajili ya kupitisha bidhaa za Congo, Rwanda, Uganda, Zambia tungekula mpaka tukachoka. Angalia Wadachi wanavyotumia bandari yao, kila Mdachi ni tajiri kwa ajili ya Bandari ya Rotterdam. Leo hii majirani zetu wanajaribu kuangalia ni jinsi gani watatokana na kupitisha bidhaa zao Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam haiwezi kuwa na ufanisi kama hatutaboresha njia ya reli, kama hatutaboresha wafanyakazi wanaozunguka maeneo yale ambayo yanahudumia bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye vitengo vile vya kontena, wanao-*clear* mizigo bandarini, leo hii mpaka Rais anakwenda anasema jamani kwa nini msifanye kazi saa 24! Bandari *TRA* wanafunga kazi saa 9.00 au saa 11.00 na siku za Sikukuu na *weekends* wanakwenda kulala wakati meli zaidi ya 20 zipo bandarini zinangoja kupakuliwa na huku Serikali inaendelea kulipa *demurrage* kwa meli kukaa pale bandarini. Maeneo mengine saa 4.00 au 5.00 usiku ndio watu wanatoka kazini, leo hapa Tanzania saa 9.00 mchana watu wamesharudi wanatafuta wafanye nini, saa 12.00 jioni tayari kwao ni kulala. Hatuwezi katika karne ya 21 kama watu wanalala saa 2.00 au saa 12.00, lazima tuendelee kufanya kazi mpaka kwenye saa 4.00 ama saa 5.00 usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni eneo la madini. Natoa mfano wa Mererani Arusha; wakati wawekezaji hawajaja, wale wachimbaji wadogo wadogo walikuwa wanaweza kupata kipato, Mji wa Arusha umejengwa kwa madini ya *Tanzanite.* Mji wa Mererani umejengwa kwa madini ya *Tanzanite*, baada ya wawekezaji kuja wamechukua yale maeneo na jinsi tunavyotoa

leseni zetu ni kwamba, yale maeneo yanakuwa ni yao hata kama yuko Uingereza au yuko sehemu nyingine ana eneo lake Tanzania. Akizalisha yale ni ya kwake sio ya Tanzania na hakuna udhibiti kamili. Angalia Mji wa Arusha sasa hivi, hauna maendeleo na maendeleo yao yamerudi nyuma baada ya kuanza kuleta wawekezaji wa madini kwenye machimbo ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono mpango huu, lakini natoa angalizo kwa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya mwisho, adhimu ya kuchangia. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hiyo, mawazo yangu mengi yamo ndani ya maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wetu wa Kamati, nitatumia fursa hii kusisitiza mambo mawili, matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, habari ya kutumia *transit trade,* kwa maana ya biashara ya usafirishaji unaotumia miundombinu yetu kuanzia bandari, reli na barabara imezungumzwa sana. Kwa hiyo, jambo hili kusema kweli kama ningekuwa upande wa Serikali si jambo la mjadala tena ni jambo la Serikali kukaa na kutafakari tunafanya nini ili mawazo haya ya Wabunge yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie kwenye eneo la reli. Kama walivyosema Wabunge waliotangulia, mathalani Mheshimiwa Kimaro, aliyemaliza sasa hivi amesema, Bandari ya Dar es Salaam kama walivyosema wengine ni sawa sawa na mgodi wa dhahabu ambao hatuhutumi. Kwa hiyo, hata kama leo tutakwenda pale tutafanya kazi usiku na mchana, kama hatujaiimarisha reli yetu, barabara ya kati iendayo mpaka Kigoma ni sawa na hatujafanya kitu. Sasa reli ina matatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, reli yetu hii kulikuwa na Kampuni yetu wenyewe ya *Tanzania Railways Corporation,* ambayo kabla ya ujio wa Kampuni mpya ya sasa *(TRL),* ambayo inamilikiwa kwa ubia baina ya Serikali na Kampuni ya India ya *RITES*, kwa wastani wa *shares* 49 za Serikali ya Tanzania na 51 India. Hii ni Kampuni yetu, ilirithi vitendea kazi vibovu, imerithi reli mbovu tena ya kizamani ya mita moja.

Kwa hiyo, kuna matengenezo makubwa sana ya kufanyiwa kwenye reli hii, pamoja na vitendea kazi vyake. Wakati Serikali inaanzisha Kampuni hii kwa ubia, ilikuwa imefahamika kwamba, kwanza mtaji uliokubalika ni shilingi bilioni 20. Sasa shilingi bilioni 20, kuanzisha Kampuni ya Usafirishaji ambayo vitendea kazi vyake ni vibovu na reli ni mbovu, ulikuwa ni sawa sawa na utani. Kwa hiyo, tulikwishanzisha Kampuni na mtaji mdogo, wakati mahitaji ni makubwa. Sasa tatizo lililo mbele yetu ni kurekebisha mtaji huo na wanaopaswa kuurekebisha ni wabia wenyewe, kwa hisa zao hizo hizo 49 na 51 au waende wakakope mikopo nafuu katika Benki ya Dunia au katika nchi rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, nchi moja rafiki ipo tayari kuikopesha Tanzania, kwa jina inaitwa India. India ipo tayari kuikopesha Tanzania takriban dola 83,000, kwa masharti yale yale ya *International Bank Foreign*

*Reconstruction* ya *World Bank.* Tatizo letu ni maamuzi. Sasa kwa sababu hatuamui, ndiyo maana Kampuni yetu ambayo mtaji wake umekwishaliwa na kazi za mwanzo za kuandaa namna ya kuirekebisha Kampuni leo hii inasuasua vibaya sana. Tutapiga kelele usiku na mchana, ufumbuzi upo katika kuongeza mtaji wa Kampuni ya Reli ama kwa wabia waliopo kuongeza hisa zao au wakaribishe mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, Kampuni ya *IFC* ambayo ni dirisha la *Private Sector* la *World Bank,* ambayo ndiyo imeikopesha *TRC* mpaka sasa na kwa bahati mbaya katika mkopo wa dola milioni 44 ni dola milioni 7 tu ndio zimekwishatolewa. Tatizo kubwa la *TRL* ni kukosa mtaji uliotegemewa wa dola milioni 44 kutoka *IFC*. Leo hii tunavyoongea ni dola milioni saba tu ndiyo zimepatikana. Mahitaji ya Kampuni hii ni makubwa sana na fedha hakuna. Kwa hiyo, wabia kwa maana ya Serikali na *RITES*, wakae wazungumze watafute namna watakavyoongeza mtaji wa Kampuni hii. Tunaihitaji sana Kampuni hii, matatizo yake yatafumbuliwa kwa kuongeza mtaji. Baada ya kusema hayo, ukishamaliza tatizo la mtaji wa *Tanzania Railways Corporation,* umeifungua Reli ya Kati kwa sababu zitapatikana *spares*, mabehewa yatatengenezwa, *engines* zitatengenezwa na kila kitu kitajipa. Bila ya hivyo, itakuwa ni hadithi isiyokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, sasa huu ni ushauri maana yake huko mwanzo wote tunasema tutengeneze barabara, tutengeneze reli tunatengenezaje? Ushauri wa kuitengeneza reli ndio huu. Wabia walete fedha ndani ya Kampuni, hawana waende IFC, waiingize IFC kama mbia; hilo linawezekana kwa sababu *as a private window* ya *World Bank.* Vilevile inachukua hisa kwenye Makampuni inayokopesha na hii haitakuwa ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nazungumzia juu ya *Finance and Credit Plan* ya nchi hii. Tunaelekea huwa tunaacha *long term financing* zinazofanywa na *Pension Funds,* nje ya utaratibu wa bajeti. Kwa mfano, sasa hivi tunajenga Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa kutumia fedha za *Pension Funds*. Tunajenga nyumba za Polisi, kwa kutumia fedha za *Pension Funds.* Nashauri *Pension Funds* hizi, mikopo yake iingizwe kwenye *sources* za Serikali kama sehemu ya mapato yake. Isiwe ni sehemu tu kwamba, watu wana-*negotiate* wakisha-*negotiate,* basi tayari nje ya utaratibu mzima wa mfumo wa bajeti; utaratibu huu uingizwe kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumezungumzwa tatizo la *exchange rate. Exchange rate* yetu inakuwa mbaya, kwa sababu ya *poor performance* ya *exports* zetu. Tuongeze *exports,* kwa bahati nzuri *imports* zetu ambazo kiasi kikubwa zilikuwa ni mafuta ya petroli, sasa imepungua bei. Kwa *quantity* ile ile, tutatumia fedha kidogo za kigeni kununua mafuta yale yale tuliyokuwa tukiyanunua mwaka jana; ni dhahiri tutafanya *savings na* tukifanya *savings* tuielekeze vizuri kwenye maeneo ya maendeleo. Moja ya maeneo hayo ni kuhakikisha viwanda vyetu vya ndani vinakarabatiwa, hususan Kiwanda cha Matairi cha Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kiwanda cha Matairi cha Arusha kingetengenezwa na kuzalisha matairi, kwanza kingeongeza wigo wa kodi za ndani, pili

soko la matairi lipo, hatuna ubishi juu ya hilo. Hivi kwa nini tunaingiza matairi ya *Continental*, matairi ya *Dunlop* na kadhalika kutoka nje wakati tuna kiwanda hapa hapa nchini? Soko lipo, matairi hayatengezwi! Kodi hamna, hilo ndio eneo la kulibana tukishaanzisha tutapata fedha.

Tanzania Bajeti yetu kwa kiasi kikubwa, inategemea pombe na sigara. Likitokea tatizo katika maeneo haya mawili, Mapadri na Masheikh wakifanya kazi zao vizuri, watu wakaacha kunywa pombe, bajeti yetu itaanguka. Huo ndio ukweli. Tuanze kuangalia maeneo mengine, ambayo hayana utata kama pombe na sigara. Tutapata matatizo makubwa sana, watu wakiacha kunywa pombe na kuvuta sigara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia barabara. Tunafanya vizuri lakini sasa kwa makusudi mazima, Serikali iamue barabara ya kutoka Manyoni, Itigi, Tabora, Kigoma ijengwe. Kwa sababu barabara hii ndiyo itakayofungua nchi yetu kwenda kule Zaire, Burundi na Rwanda. Ijengwe hii ni barabara ya uchumi, sio barabara ya anasa. Hali kadhalika, barabara ya kutoka Nzega – Tabora - Sikonge hadi Mbeya, itaunganisha nchi yetu kibiashara kwa maana ya *surplus production* inayofanyika huko chini, itapata soko huku juu tena mpaka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuachia dakika zilizobakia, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Ulipokuwa unachangia habari ya TRA, ungesema pia wewe ni *Board Member*, habari ingeeleweka vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona dakika zetu ni chache mno, kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5), tutaongeza dakika 30 ili mtoa hoja aweze kukamilisha. Dakika 30 baada ya saa 1.45 usiku, aweze kukamilisha hoja zake kwa kujibu.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niungane na baadhi ya Wabunge wenzangu katika kuchangia mpango wa bajeti ambayo ndiyo tumaini la Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajikita katika uchangiaji huu napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba kwa kunipa uhai na afya njema inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kila siku katika kuwatumikia wapiga kura wangu na Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Manaibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wengine katika Wizara hiyo ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie machache tu katika mpango huu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, utulivu wa familia au nchi yeyote duniani ni kuwepo kwa chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu kilimo chetu kimekuwa cha kubahatisha kwa vile tunategemea huruma ya Mwenyezi Mungu ili mvua inyeshe ndiyo tuoteshe na hii ni hatari sana kwa vile majira yanabadilika na ratiba ya Mwenyezi Mungu sisi kama wanadamu hatuifahamu, hivyo basi, ni vigumu kufanya jambo lolote kwa kukisia.

Hivyo basi, kilimo cha uhakika ni kile cha umwagiliaji maji kwa vile unaweza kulima wakati wowote ule kwa sababu kunakuwa na uhakika wa maji ya kuoteshea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya katika kujikita kilimo cha umwagiliaji gharama yake ni kubwa sana na vile uwezo wetu ni mdogo wa kifedha, hivyo basi tutoe kipaumbele kwa baadhi ya maeneo machache na kutumia nguvu zetu zote ili maeneo hayo yazalishe chakula cha kutosha kwa ajili ya Watanzania na hata kuuza nje ya nchi yetu ili kupata fedha za kigeni kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tunalo Bonde la Mto Rufiji, ni bonde zuri sana, kubwa na lenye mbolea ya asili na maji ya kutosha kando kando ya bonde hilo, ni bora kutoa kipaumbele katika uzalishaji hasa zao la mpunga na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkoa wa Morogoro, Mkoa huu umebarikiwa sana kwamba ardhi yenye rutuba, mvua ya wastani kwa mwaka mzima, unao mito 148 ambayo haikauki kwa mwaka mzima, ni mkoa njia panda karibu robo tatu ya mikoa yote ya Tanzania na hivyo kurahisisha kuufikia (*accessibilities*) lakini pia Mkoa huu sambamba na Bonde la Mto Rufiji upo karibu sana na mji wa biashara yaani Dar es Salaam ambako ipo bandari kuu ya uwanja mkuu wa ndege, hivyo basi kupeleka pembejeo katika maeneo hayo sambamba na kusafirisha mazao kutoka maeneo hayo na kuyasambaza mikoani au kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa maarufu ya ulimaji hasa mahindi kama Mbinga, Mbeya, Rukwa, Ruvuma na hata Kigoma ipelekwe tu pembejeo ya kutosha hasa mbolea ili kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo, mifugo yetu si bora kwa vile wanyama wetu wanachungwa kiholela katika makundi, hivyo basi, kuwa na wanyama wenye uzito mdogo na hivyo hutoa nyama chache na ngozi ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, katika sekta ya mifugo, Serikali ijikite katika kutoa elimu kwa wafugaji ili kuanza na kuendeleza mpango wa kunenepesha mifugo yetu ili iwe bora yenye kutoa nyama nyingi na ngozi kubwa na bora, hivyo kuongeza pato la Taifa. Kwa vile suala kunenepesha mifugo ni la kibiashara hivyo basi itasaidia kupunguza wingi wa mifugo na hivyo kupunguza mgogoro kati ya wafugaji na wakulima na hivyo kuleta utulivu miongoni mwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine muhimu ni sera ya wachimbaji wadogo wadogo kuwapa uwezo wa kuchimba na kuuza kwa uhakika.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi ni ya kina na yanatoa picha kamilifu ya mpango mzima wa bajeti ya Serikali. Nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo ya kipaumbele katika mpango wa bajeti 2009/2010 – 2011/2012 ni kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo na kuanzisha Benki ya Kilimo. Wananchi Wilayani Kyela wameniagiza niiombe Serikali yafuatayo kuhusu mbolea:-

Kwanza, pamoja na ruzuku ya mbolea inayotolewa na Serikali, bei ya mbolea bado iko juu mno kwa wakulima walio wengi. Hivyo, Serikali iendelee na jitihada zake za kuishusha bei ya mbolea zaidi. Wanajiuliza ni muujiza gani Serikali ya Malawi inafanya kwa mbolea yake kuuzwa kwa bei ya chini (karibu robo ya bei ya zamani)? Inawalazimu wakulima wa Kyela watumie njia za panya kuipata mbolea ya Malawi, kitendo ambacho kinaipa nchi sifa mbaya kwa majirani.

Pili, Serikali itoe mbolea kwa wakulima kwa mkopo ambao utalipa baada ya mkulima kuvuna mazao yake. Mkulima anayeshindwa kurejesha mkopo huo, atakuwa amejitoa mwenyewe kwenye mpango huo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi hayo ya wakulima wa Kyela yazingatiwe katika mpango na bajeti ya Serikali ijayo. Kwa ujumla wake naiunga mkono Serikali.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii lakini Mkoa wa Ruvuma ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kama vile mahindi, kahawa, korosho, mpunga na kadhalika. Mkoa wa Ruvuma hasa kando kando ya Ziwa Nyasa kwa uzalishaji wa samaki wa chakula, mapambo pamoja na fukwe nzuri za kuvutia watalii. Pamoja na hayo yote, mkoa uko umbali wa kilometa karibu 1200 toka Dar es Salaam wanapofikia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ilenge kuusaidia mkoa kujikwamua kiuchumi katika kutelekeza yafuatayo:-

Kuwe na barabara za lami na za uhakika kutoka Dar es Salaam – Songea – Mbinga – Mbamba Bay; Barabara ya kutoka Mtwara – Tunduma – Songea na kutengeneza na kuanza kuruka kwa ndege kufika Kiwanja cha Ndege cha Songea. Mtalii hawezi kuwa na hamu ya kuwekeza kwa kusafiri kwa basi mwendo mrefu na pengine barabara za vumbi; na

Kuimarisha kilimo tena kwa mbinu za kisasa kwa kutumia matrekta au plau, pamoja na kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno mengine bajeti ilete maisha bora kwa Watanzania na hasa wana Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. *KAYOMBO*:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na wafanyakazi wa Wizara hiyo kwa kutuletea mpango huu ambao kwa kiwango kikubwa umezingatia mambo muhimu. Mchango wangu ni kama ifutavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka huo tutakuwa bado tunakabiliana na athari ya kuanguka kwa uchumi duniani, hivyo nilitarajia kwanza kupunguza vipaumbele vyetu na pia kuvibadilisha. Jambo la muhimu kwa sasa ni chakula. Tuwe na mipango ya dhati ya kuhakikisha tunapata na kujitosheleza na kuuza chakula, ndio uwezo tulionao. Lazima tubainishe mikoa (imefanyika)? Lakini ni nani katika mikoa hiyo analima? Je, tunaweza (Serikali) kuingia na wakulima (kwa majina) mkataba ili wawezeshwe kwa pembejeo na baadaye waiuzie Serikali chakula hicho (Serikali inaweza kupata fedha yake kama ni lazima baada ya mauzo) chakula hiki kitapelekwa kwa mikoa yenye upungufu wa chakula, hii itatuwezesha kuzalisha chakula kingi. Kuhusu miundombinu tuhakikishe nchi inafunguka na kufikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wizara hii iweze kwa kweli kuratibu mipango yote. Hivyo Wizara zote lazima zitekeleze mpango huu na zionekane zinafanya hivyo. Wizara hizo zitoe taarifa kwa Wizara ya Fedha na Uchumi. Hivi sasa inaonekana kama Wizara zipo huru mno (*independent*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu, ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa yale tunayokubaliana. Lazima tuwe na taratibu nchini zitakazoonyesha kiwango cha utekelezaji wa shughuli kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. FERDINAND S. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa, napenda kuongeza yafuatayo ili kuboresha zaidi mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, uboreshaji wa kilimo unategemea sana namna bora ya kufanikisha kilimo hususan kwa upande wa ununuzi wa pembejeo na zana bora kama matrekta. Katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini tunahitaji sana matrekta kwa ajili ya kuboresha kilimo chetu ili taratibu tuachane na kilimo cha kizamani cha kutumia jembe la mkono endapo kama Serikali itatupatia matrekta japo mawili tu tungeweza kubadilisha hali ya upatikanaji wa mazao na kuondokana mara kwa mara na

balaa la njaa. Wakulima wangu wanao utashi mkubwa wa kupanua mashamba yao lakini kwa kuwa wanatumia jembe la mkono wanashindwa kupata kile ambacho wanategemea kukipata sehemu kama Kata za Mitole, Njinjo, Kandaware ambazo zipo kwenye uwanda wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ungesaidia sana kukuza kilimo cha minazi, mikunde, michungwa na miembe, sasa imekuwa kama wimbo wa Taifa kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko itaundwa ambapo Kilwa ina utajiri mkubwa na ungeweza kuinua balaa la njaa kwa kuwa Jimbo la Kilwa Kaskazini limepakana na Hifadhi za Mbuga za Wanyama Selous, wanyama kama ndovu wanashambulia sana mazao machache walimayo wakulima wetu. Hivyo, napendekeza fidia iwe ya kutosha kwani makosa yanakuwa si ya wakulima bali wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu, barabara itokayo Kata ya Kipatimu Wilaya ya Kilwa kuelekea Mkoa wa Pwani sehemu ya Nambunju barabara ile kama ingetengenezwa ingeweza kukomboa usafirishaji wa mazao kama nazi, machungwa, kunde, ndimu, ndizi na kadhalika hasa ukizingatia kuwa barabara hiyo ni fupi sana kuliko kupitia (40 km) njia ndefu ya Njia Nne-Somanga hadi Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nishati, gesi asilia itokayo Songosongo ina uwezo wa kufufua umeme na gesi hiyo inapatikana Kilwa. Sasa nashangaa umeme unapita pale ambapo bomba la gesi linapita kuelekea Dar es Salaam, vijiji vilivyopo mbali na bomba hilo wapo gizani na endapo kama umeme ungefika tungeweza kuweka viwanda vya matunda kama juisi na kadhalika.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi kwa busara zake za kuona umuhimu wa kuleta mwongozo wa bajeti kabla haijashughulikiwa ili Bunge letu Tukufu liipitie, kuijadili na kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya nchi ni jambo la muhimu sana na ndio moyo wa utekelezaji wa shughuli za nchi kwani fedha ndio kila kitu, kwa hiyo lazima sisi wote tushirikiane kuandaa matumizi na umuhimu wa lipi litangulie, kwa fedha ambazo tutategemea kuw anazo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hali ya umaskini wa wananchi wetu hususan waliopo vijijini/wakulima, sikubaliani na kauli ya Waziri kwamba MKUKUTA umefanikiwa, hiyo siyo kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na elimu, elimu yetu inazidi kupoteza mafanikio, kwani kuwa na majengo mengi na watoto wetu wengi kuingia darasa la tisa sio mafanikio kwani watatoka huko wakiwa mbumbumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu sio kuwa na kauli za kukatiza, tunahitaji sana kuhakikisha kuna walimu wajuzi sio bora mwalimu hapana ni walimu bora, tunahitaji maabara na pia vitabu vya kufundishia, lazima Wizara ya Fedha inapopanga bajeti

ihakikishe kwamba inatoa kipaumbele kwa Wizara ya Elimu, kwani bila ya elimu hata hiyo miundombinu itakuwa hakuna kwa sababu tutakuwa na nchi ya wajinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea siku zote kuhusu kilimo lakini mpaka leo bado tuko kwenye kupanga tu, je, ni lini utekelezaji utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na benki za wakulima, mikopo rahisi isiyokuwa na riba kubwa kwa wakulima wetu, urahisi wa kupata pembejeo na mbolea iliyo na uhakika kwa ardhi husika, mabwana shamba wa kuwapa elimu ya kutosha wakulima wetu, mikopo ya matrekta, tutakuwa tunatwanga maji, lazima tukubali kutumia fedha ili tupate fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA utafanikiwa kwa kuwa karibu sana na wanakijiji na kuhakikisha kila senti inayotoka inatumika kwa uhalali na inawafikia wahusika, sio tu kukaa huku na kusema mafanikio yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misukosuko ya uchumi wa dunia na madhara ya uchumi hapa kwetu, tusibweteke hali huko nje ni mbaya sana, nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha tunaimarisha vivutio vyetu vya utalii kwa kuvipitia vyote na kuviona viko kwenye hali gani kwani tuna vivutio vingi sana na vingine wala hatuna habari navyo. Watalii wanapotoa fedha zao kuja waitane kwa jinsi watavyoona kuna mambo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha tunatoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu kutunza mazingira yetu, kuweka miji yetu kwa hali ya usafi ili kujinusuru na magonjwa ya milipuko ambayo inapotokea huwa inabidi Serikali kutumia fedha nyingi za matibabu, kuchukua tahadhari ni bora kuliko kutibu magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha miti haikatwi ovyo kwani wanapoharibu misitu kwa kukata miti ovyo husababisha ukame na ukame unapotokea hata hicho kilimo tunachojitahidi itakuwa kazi bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuzilazimisha benki zetu kutoa mikopo rahisi isiyo na riba kubwa na kuwataka wawe na fungu la kusaidia jamii sio shilingi milioni tano ambazo wanatudanganya nazo na wao wanapata faida kubwa kwetu, kwani tunahimiza kuweka fedha benki lakini hatuna faida tunayopata. Mfano, unaweka fedha zako lakini kila unapokwenda kuchukua huwa wanakukata fedha za kutoa lakini faida ya kuweka ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa dharura, hivi sasa tunatabiri ukosefu wa chakula kwenye maeneo mengi na Wizara inasema kuna chakula cha kutosha kwa kipindi cha miezi 12 ijayo je, kuna mpango maalum ambao Serikali watahakikisha chakula hicho kinawafikia walengwa? Tumeshasikia na kuona chakula hicho cha dharura kuangukia mikononi kwa walanguzi na wananchi huambulia robo kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke utaratibu wa kutosha wa kuhakikisha chakula hicho kinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kupongeza mpango wote uliomo kwenye hotuba ya Waziri, lakini nikiendelea pia kuomba yasibaki kwenye makabrasha, kesho tukiuliza kulikuwa hakuna fedha, mikakati ni mizuri basi tujitahidi kuitekeleza kwa mpangilio wa lipi litangulie kwa umuhimu, sio tu kuingia na kuanza kutelekeza yote kwa pamoja na fedha yetu ni ndogo sana, vipaumbele ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwakilisha, naitakia nchi yetu mafanikio mema, ili wananchi wetu wafaidike na waondokane na umaskini uliokithiri.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niishukuru Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kutoa mwongozo wenye kuzingatia maeneo matatu: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005. Mchango wangu utajikita zaidi katika sekta ya kilimo, maji, mifugo na uvuvi nikiwa kama mjumbe wa Kamati ya Bunge katika sekta tajwa. Pamoja na kwamba kupanga ni kuchagua kama Kamati tulipendekeza yafuatayo ili yapewe kipaumbele, kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, mapendekezo ni kama yafuatayo;

Kwanza, bajeti ya Wizara iongezwe ili ifikie kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC* sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya 2005 cha asilimia mia moja.

Pili, Mfuko wa Pembejeo upatiwe fungu maalum kutoka Hazina na upatiwe fedha zinazolingana na mahitaji ya wadau.

Tatu, Vituo vya Utafiti viboreshwe kwa kuwapatia vitendea kazi muhimu pamoja na maslahi mazuri ya watafiti. Aidha, matokeo ya utafiti yafikishwe kwa wakulima kwa wakati muafaka.

Nne, huduma za ugani ziboreshwe kwa kuhakikisha wataalam wa ugani wanaongezwa ili kuweza kufika kila sehemu ya nchi na kupatiwa vitendea kazi kama vile pikipiki, makoti ya mvua (*rain coats*) na viatu (*gum boots*).

Tano, Benki ya Wakulima ianzishwe ili kuweza kuwapatia wakulima mikopo yenye masharti nafuu.

Sita, Mchakato wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko uharakishwe ili kuweza kusimamia mazao hayo.

Saba, hifadhi ya chakula iimarishwe kwa kuongezewa fungu ili kuhakikisha kunakuwa na chakula cha kutosha hasa katika kipindi hiki cha uhaba wa chakula duniani

kote. Aidha, uwepo mpango endelevu wa kununua nafaka toka kwa wakulima na kwa bei nzuri.

Nane, mchakato wa ujenzi wa Viwanda vya Mbolea kwa kutumia malighafi za *phosphate* na gesi uharakishwe ili wakulima walio wengi wapate mbolea ya kutosha na kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Aidha, Kiwanda cha Minjingu kiboreshwe ili kitoe mbolea kama aina ya *DAP* na usambazaji wake uzingatie misimu ya kilimo.

Tisa, fursa za hali ya hewa, ardhi nzuri na uhakika wa maji, zilizopo Mikoa ya Kusini zitumike kikamilifu ili kuifanya nchi ijitosheleze kwa chakula na hata kuzalisha ziada.

Kumi, utaratibu wa vocha kwa wakulima ufanyiwe tathmini ya kutosha ili uboreshwe kwa msimu unaofuata.

Kumi na moja, Serikali itimize ahadi zake za kutoa ruzuku kwa Bodi za Mazao ili ziweze kufanya kazi zake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi:-

Moja, bajeti ya Wizara iongezwe, itolewe kwa wakati na vile vile fedha za miradi ya maendeleo zipangwe bila ya kutegemea sana fedha za wafadhili.

Pili, kutokana na uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu, Serikali itenge maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji na yawe na hatimiliki. Aidha, miundombinu muhimu kama malambo, majosho na kadhalika yajengwe na pia ranchi za Taifa zitumike kuwapatia wafugaji mbinu za ufugaji bora.

Tatu, Serikali iangalie ranchi za Taifa zilizopo na kuwa au kuwakodishia wafugaji maeneo ya kuweza kufugia. Hii itasaidia wafugaji kujinasua kiuchumi na pia kuongeza Pato la Taifa.

Nne, bei ya pembejeo za mifugo na zana za uvuvi, zipunguzwe au kuwepo na ruzuku kwa pembejeo na zana hizo ili wafugaji na wavuvi waweze kuzalisha kwa tija. Aidha, fungu maalum litengwe kwa shughuli za ufugaji na uvuvi.

Tano, Serikali ihakikishe zinakuwepo taasisi au sekta binafsi zenye kutoa masharti nafuu ya mikopo kwa ajili ya wafugaji na wavuvi.

Sita, Serikali ijenge mazingira ya kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi.

Saba, dawa za mifugo zipatikane kwa wingi na kwa bei nafuu ili wafugaji wadogo wadogo waweze kuzimudu. Aidha, kuwepo na mawakala kuuza dawa hizo katika kila mkoa.

Nane, Serikali ihakikishe inatoa taarifa za masoko kwa wafugaji ili waweze kuwa mifugo yao kwa bei nzuri.

Tisa, kutokana na kusuasua kwa viwanda vya maziwa nchini Serikali iandae utaratibu wa kuona matatizo yaliyopo ya viwanda, hivyo yanatafutiwa ufumbuzi wa haraka.

Kumi, Serikali ifanye utafiti wa zao la mwani na ufugaji wa samaki na iweke mtandao wa kusaidia wakulima wa mwani na wafugaji wa samaki nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Maji na Umwagiliaji:-

Moja, kutokana na mahitaji makubwa ya maji mijini na vijijini, Serikali itenge fedha za ndani za kutosha ili kupunguza utegemezi wa nje. Aidha, Bajeti ya Wizara iongezwe kuweza kutatua matatizo ya maji nchini kuanzia kipindi cha mwaka 2009/2010.

Pili, kwa jinsi hali ya hewa ilivyo, masuala ya umwagiliaji yanahitaji kipaumbele zaidi. Bajeti ya miundombinu ya umwagiliaji ipewe uzito unaostahili.

Tatu, Mradi wa Maji wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo jirani pamoja na jitihada zinazofanyika bado Serikali inahitaji kulipa uzito unaostahili kwa kuendelea kupunguza tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuacha hujuma dhidi ya miundombinu ya maji ambayo imekuwa ikichochewa zaidi na biashara ya vyuma chakavu. Aidha, Serikali ihakikishe huduma ya maji ya Jiji la Dar es Salaam inatolewa kikanda ili kuongeza ufanisi.

Nne, kwa kuwa tatizo la maji ni la nchi nzima, Serikali ihakikishe fedha za miradi ya maendeleo zinakwenda katika miradi ya maji katika wakati muafaka.

Tano, wataalam wa maji na umwagiliaji wawepo kuanzia ngazi ya Halmashauri ili kuhakikisha wanaisimamia sekta hii. Aidha, Wizara iweke mipango maalum ya kuzisaidia Halmashauri za Wilaya kutoa wataalam wa uainishaji wa miradi mbalimbali ya maji na umwagiliaji ili kusimamia sekta hii muhimu.

Sita, Ofisi za mabonde hazina uwezo wa kujiendesha, Serikali izisaidie zisimame na kufanya majukumu yake.

Saba, suala la umwagiliaji maji lisitegemee vyanzo vya asili tu, Serikali ihakikishe uvunaji wa maji ya mvua, ujengaji wa malambo na mabwawa unatiliwa mkazo unaostahili.

Nane, Serikali itilie mkazo uchimbaji wa visima virefu na vifupi ili kupunguza matatizo ya maji yaliyopo, pia uchimbaji wa visima hivyo uzingatie kina cha maji (*water table*) na wakati wa uchimbaji inapendekezwa visima vyote vichimbwe kipindi cha kiangazi.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa mapendekezo ya mpango ambao kama utatekelezwa kama ulivyo, utatuletea mafanikio makubwa katika mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo ningependa Mheshimiwa Waziri ayawekee kipaumbele pia katika mpango wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, Serikali ijihusishe kuagiza pembejeo na zana za kisasa zake (matrekta madogo) moja kwa moja kutoka viwanda husika ili kukwepa gharama kubwa ya mtu wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara, mkazo sasa upewe kwenye kima cha chini zaidi. Mishahara ya juu isipande badala yake mishahara ya KCC ipewe umuhimu ili azma ya Sera ya Taifa ya kupunguza tofauti kubwa sana za mishahara ambayo haiendani na ukweli wa maisha. Pia, suala la *pension* kwa wastaafu lipewe umuhimu wa pekee ili viwango hivyo vifikie angalau kima cha chini (tutumie fedha za *OC's* ambazo ni budi zipunguzwe).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, tuimarishe upatikanaji wa walimu na ujenzi wa hosteli pamoja na maabara ili ubora wa elimu upewe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu, suala la barabara kati ya Tunduma hadi Sumbawanga ni kitendawili ambacho sasa wananchi wanakiona ni kitendawili sababu mwaka 1990 Wabunge wa Mkoa kupitia marehemu Mbunge wa wakati huo ndugu Kinyonto, hoja ya kuondoa shilingi ililazimisha Serikali kuitengeneza barabara hiyo kwa fedha za benki ya Dunia na ikaahidi kuwa itafanya upembuzi wa kina ili ijengwe kwa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wakati huo mpaka leo pamoja na kukamilika usanifu, upembuzi wote wa kina, bado barabara hii haijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitegemea sana fedha za wahisani, naona bado barabara hii itaendelea na vikwazo vya urasimu wa fedha za MCC. Pamoja na kwamba fedha za MCC zilizotengwa kwa barabara kuwa *USD 378* ambazo zitatumika kwa Barabara za Tanga – Horohoro, Songea – Namtumbo, Peramiho – Mbinga na Tunduma – Sumbawanga zote zikiwa na urefu wa km.433. Kama ujenzi utatekelezwa kwa mtiririko huo, basi sehemu ya barabara kati ya Tunduma – Sumbawanga haitapata fedha za kuikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, barabara ya Tunduma – Sumbawanga ipewe kipaumbele kati ya hizo zote na ianze mapema kuliko kuwa ya mwisho hili lisiwe la kusita, maana hata ilani inaielezea vizuri barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa fedha za *MCC* hazitatosha, nashauri mwaka huu wa fedha, utenge angalau shilingi 10 – 20 bilioni kwa ajili ya malipo ya fidia na *balance* itumike kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ujenzi uanzie Sumbawanga ili wananchi waamini ukweli wa nia hiyo ya Serikali ipo na wanaishuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuwa kwa kutegemea fedha za wahisani, barabara hii imepuuzwa hata kwa kuanzia kwa fedha zetu wenyewe. Mbona barabara nyingi zimejengwa hata kabla ya hii ya Tunduma – Sumbawanga (fedha za kukarabati) mfano Mwanza – Shinyanga, Kigoma – Rusaunga, Arusha – Namanga, Chalinze – Segera, Nelson Mandela, Singida – Babati. Fedha zilizojenga barabara zifuatazo ni zetu: Manyoni – Dodoma, Nangurukuru – Mbwemkuru – Mingoyo, Somanga – Matandu, Geita, Kyamiorwa – Buzirayambo, Marangu – Tarakea, Dar es Salaam – Kibiti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na mipango yote inayoandaliwa, mradi wa maji vijijini upewe umuhimu wa kwanza katika mwaka huu na waganga wa zahanati zetu ambazo hazina hata madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga hoja hii nzuri ya Waziri kwa masharti kuwa Barabara ya Tunduma – Sumbawanga itaheshimiwa na kupewa umuhimu wa kwanza safari hii.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Mifugo, nashukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia mwongozo wa Bajeti yetu. Naomba niseme na kuiomba Serikali yetu kwa vile sikivu, isikie kuhusu suala la wafugaji kwa vile Serikali imesema itatenga fungu la kupima maeneo ya wafugaji, basi iendeshe zoezi hili mapema na kasi zilizopo zitiliwe mkazo na utekelezaji mwema ili kuwaweka wananchi wetu katika hali nzuri na ya amani zaidi kwani sasa hivi hali iliyopo si nzuri kwa vile makundi mawili nchini hayana amani ya kutosha kwa maeneo ya wakulima na wafugaji. Watu hawa kwa muda mrefu wamekosa amani kwa kugombania ardhi lakini kwa nini watu hawa tuwaache wakosane tu bila sababu za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za msingi ni kwamba imezoeleka tu kuwa maeneo mengi nchini ni kwa ajili ya kilimo, maliasili, miji na maji. Maeneo mahsusi kwa ajili ya wafugaji hayapo na pamoja na kutokuwepo maeneo hayo tumekuwa tukizungumzia wakulima bila kuangalia takwimu zetu kwa maana ya ongezeko la watu, kwa mfano idadi wa watu iliyokuwepo Kanda ya Ziwa na mifugo kwa miaka ya nyuma ilikuwa ni ndogo kwa sasa takwimu zetu ziko juu, je, niiulize Serikali ardhi hii iliyokuwepo zamani ndiyo iliyopo sasa? Jibu, kama ni hapana Serikali inatoaji kauli ya kutimua wafugaji wetu kila mahali walikoelekea kutafuta riziki bila kujali kuisha kwa maeneo au ongezeko la idadi ya watu? Mbali na ongezeko miundombinu husika haipo, hilo Serikali inasemaje, je, tunatupilia mbali wananchi hao (wafugaji) bila sababu za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni zito naomba na kushauri Serikali chonde chonde Wizara zifuatazo Kilimo, Ardhi, Maliasili, Mifugo, Maji na TAMISEMI zikae pamoja waweze kutatua tatizo hili na kuwaokoa wananchi wetu kuepukana na ugomvi uliopo ikiwa ni pamoja na elimu ya kupunguza mifugo kwa wahusika, wapunguze,

wauze, wajenge nyumba bora, wasomeshe watoto wao na kadhalika. Ikiwezekana wapatiwe maeneo yenye tija kwa Serikali na wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni maji, nitatoa mfano halisi, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Maji na Umwagiliaji nimejionea baadhi ya hujuma zilizopo kwenye miundombinu ya maji kama kwenye mitambo yetu ya maji ya Ruvu juu na Ruvu chini. Kila wanapotengeneza mitambo watu wasio na huruma na jamii hufungua vyuma na kuiba kwa kuuza kwenye soko la biashara ya vyuma chakavu.

Naomba kuiuliza Serikali je, haiwezi kupiga marufuku biashara hii inayolisababishia Taifa hasara kubwa na kupotea fedha za walipa kodi na wahisani wetu bure bila mafanikio yeyote kwenye miradi yetu? Ndiyo maana tatizo la maji halitakwisha au kupungua hasa katika Jiji la Dar es Salaam lenye tatizo kubwa la maji na lenye wakazi wengi nchini. Nitashukuru iwapo Serikali itakuwa makini kwa masuala yangu mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DR. LUKA J.B. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake yenye kuelezea kwa kina na ufasaha na kwa kuzingatia dira ya maendeleo ya Taifa 2025, MKUKUTA na Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wote walioshirikishwa katika kuainisha vipaumbele katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa uchumi, kwa jumla naunga mkono kwa dhati maelezo na viambatisho mbalimbali vikionyesha hali halisi katika viashiria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na hali ya uchumi duniani kuporomoka tena kwa kasi kubwa ni vema Serikali ikaweka mikakati kabambe ya kuhakikisha njia mbalimbali zinatumiwa ili kujinusuru na athari za hali hiyo ambazo Mheshimiwa Waziri ameziorodhesha katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuelezea bayana mpango wake wa dharura na wa kati wa kukabiliana na hali hii. Kuhusiana na mpango wa kuhakikisha kuwa kuna chakula cha kutosha kutoka kipindi cha miezi 12 ijayo kwa kushirikisha mikoa sita ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma ni vema Serikali ikawa *serious* katika utekelezaji wa mkakati huo. Hivi sasa tunashuhudia maeneo mengi ya nchi hii yakikumbwa na ukame mkubwa na hivyo kuashiria hali mbaya sana ya chakula nchini katika kipindi cha miezi michache ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu huu pia maeneo karibu yote ya mikoa yote iliyotajwa hapo yanapata mvua nzuri na ya uhakika lakini kwa sehemu kubwa hakuna pembejeo za ikilimo hususan mbolea na mbegu bora. Iko haja ya kuangalia uwezekano

wa ku-*reroute* pembejeo hizo kutoka kwenye maeneo ambayo ni dhahiri hayataweza kuzitumia kwa msimu huu wa kilimo na kuzipeleka kwenye mikoa inayozihitaji sana katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilio hiki cha mahitaji ya pembejeo za kilimo, hususan mbolea na mbegu bora, Wilaya yangu ya Mbozi Mkoani Mbeya ni namba moja na hivyo ipewe kipaumbele. Tuna uwezo mkubwa wa kulima mazao ya chakula kuanzia mahindi, mpunga na mtama ya kutosha kulisha idadi kubwa ya wananchi wa Jamhuri hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali mbaya ya uchumi kwa mpango wa muda wa kati, naipongeza kwa dhati Serikali kwa kuelezea bayana nia yake ya kujenga na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, reli, bandari, umeme na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya ya barabara, kukosekana kwa umeme na maji katika maeneo mengi ya vijijini inachangia kwa kiwango kikubwa katika udidimiaji wa uchumi wetu. Kwa mfano, ukosefu wa barabara hususan vijijini ambako wananchi wengi wanategemea kipato chao kutokana na mazao yao ambayo soko lake liko mijini ama nchi za nje, unaochangia kwa kiasi kikubwa umaskini uliokithiri.

Naiomba Serikali ichukue uamuzi wa makusudi kuelekeza nguvu zake katika kuhakikisha wakulima hawa wanapewa soko la mazao yao kwa kufungua milango ya miundombinu barabara ili waweze kusafirisha mazao yao. Katika suala hili, Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilayani Mbozi limeathirika sana kutokana na sehemu kubwa ya Jimbo hili kutofikika kirahisi au kabisa kuanzia mwezi Novemba hadi Juni kila mwaka. Hivi niandikapo ni kwamba barabara zifuatazo hazipitiki kutokana na mvua zinazoendela: Kakozi – Kapele – Kisinde – Ilonga, Chapwa – Namole – Chiwezi – Chindi – Msangano, Igamba – Msangano – Chitele – Utambalila, kwenye Barabara ya Mkowo – Kamsamba, Kilometa 25 za Itumbula – Kamsamba. Pia Barabara ya Tunduma – Sumbawanga pia iko katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mikopo kwa wananchi wa vijijini na wajasiriamali mbalimbali pamoja na nia njema kabisa ya uanzishwaji wa mpango huu mpaka sasa wananchi wa vijijini hawajatendewa haki kwani mikopo hiyo imeishia mikononi mwa wajanja wachache waishio mijini na miji midogo. Maombi mengi ya wananchi wetu yanaishia mezani kwa wakopeshaji na waamuzi wa nani apate mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya kuliangalia kwa makini suala hili kwani limeleta kusononeka sana miongoni mwa wananchi wengi, kiasi cha hata kusababisha wawakilishi wao hususan Wabunge kunyooshewa vidole. Mfano dhahiri ni Jimbo la Mbozi Magharibi ambapo mikopo hiyo imetolewa kwa kiasi kikubwa kwa wakazi wa mji mdogo wa Tunduma tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo machache naomba tena Serikali katika kipindi cha mpango huu ilipe kipaumbele Jimbo la Mbozi Magharibi,

ambalo kwa hakika liko pembezoni katika mambo yafuatayo: Barabara, maji, umeme, pembejeo za kilimo, elimu, mawasiliano ya simu na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia yetu ni kuendeleza uchumi katika nchi yetu, wakati umefika sasa wa kuongeza pesa katika Halmashauri zetu ili ziwe na nguvu ya kutengeneza barabara za kudumu za vijijini ambako ndiko yanakotoka mazao mengi yanayotakiwa kupelekwa sokoni tayari kwa kuuzwa na kuchangia Pato la Taifa. Kwa mfano, katika Jimbo la Lulindi ambako kuna korosho nyingi barabara zake zimejaa mchanga na kusababisha magari yanayochukua korosho kukwama mara kwa mara na kuchelewesha uchukuaji wa korosho au kuongeza gharama ya uchukuzi kwa sababu barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Barabara ya Mtwara, nchi yetu ya Tanzania ina bahati ya kuwa na bandari nyingi pamoja na Bandari ya Mtwara. Kutoitumia Bandari ya Mtwara ni sawa na kufunga milango ya kuingiza mapato ya Serikali na kwa maana hiyo ni kuchelewesha maendeleo ya nchi yetu. Suala hili limezungumzwa kwa muda mrefu lakini mpaka sasa hakuna maendeleo yoyote ya matumizi ya Bandari ya Mtwara, hivi sasa ni hatari sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote zenye bandari kama sisi zimepiga hatua katika maendeleo kwa sababu bandari zote zinafanya kazi na kuchangia kwa asilimia kubwa maendeleo ya nchi, dunia inatucheka kuona kuwa bandari nyingi tunazo lakini hatutaki kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa tena haraka sana hasa katika kipindi hiki cha matatizo ya uchumi wa dunia, kuhakikisha kuwa Bandari ya Mtwara inatumika. Kama kuna sababu za kutokutumika basi sababu hizo tuna uwezo wa kuziondoa mara moja ili Bandari ya Mtwara itumike sasa.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa maandalizi mazuri ya mpango wa bajeti kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 hadi 2011/2012 kama alivyouwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mawazo yangu kuhusu taarifa ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:

Ili kipaumbele kwa uwekezaji katika sekta ya kilimo na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara uongezeke kwa kiasi kikubwa, Serikali ihakikishe Halmashauri katika mikoa sita, maarufu kwa kilimo inawatambua wakulima wakubwa na wadogo wanaosifika kwa uzalishaji wenye tija ili wapewe kipaumbele kushawishiwa kukopa *power tillers* ili waongeze ufanisi na tija katika kilimo cha mazao wanayolima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Serikali ipange na kutenga fedha maalum, kwa kila wilaya zitakazopelekwa kulingana na mahitaji halisi kufuatana na utambuzi wa wakulima wenye ufanisi unaokubalika.

Serikali itenge fedha maalum za kutosha ili kuibua ujenzi wa maghala ya ziada ili kuhifadhi cha ziada kitakachovunwa ili kuepusha upotevu wa mazao baada ya mavuno. Sambamba na hili, Serikali ihakikishe fedha zinatengwa maalum kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinazounganisha mashamba na maghala vijijini na pia zinazounganisha maeneo yalikojengwa maghala na barabara kuu ambazo zinakwenda kwenye masoko makuu mijini.

Naishauri Serikali katika fedha za uwezeshaji zinazojulikana kama 'mabilioni ya JK', utolewe mwongozo kuwa asilimia fulani, kwa mfano asilimia 40 ya fedha zote zikopeshwe kwa wajasiriamali wenye miradi ya kulima na sio kuchuuza mazao yaliyolimwa. Pia, asilimia fulani itengwe kwa ajili ya miradi inayoendeshwa na wanawake ili kuwapa fursa ya upendeleo kwa sababu mara nyingi hupuuzwa wanapowasilisha miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya ujenzi wa barabara hasa za vijijini na hata za Kitaifa. Nimebaini kuwa tenda nyingi hutolewa kwa namna kwamba wakandarasi huanza ujenzi kipindi cha mvua na kusababisha hali ngumu katika kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Hali hii hucheleweesha sana kazi na pia kiwango cha ubora wa barabara huwa kibaya ambacho huigharimu Serikali fedha nyingi mno.

Kwa hiyo, naishauri Serikali, ipange kutoa fedha kwa miradi ya barabara katika kipindi kitakachowezesha wakandarasi wa ujenzi wa barabara kujenga barabara wakati wa kipindi cha kiangazi ili kazi itendeke kwa ufanisi mzuri na kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uamuzi wao wa kuona umuhimu wa kuwasilisha mwongozo wa utayarishaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2009/2010 – 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kipindi hicho haina budi kurudisha hadhi ya *TAFICO* ikiwa ni sambamba katika kuisukuma Sekta ya Uvuvi, miundombinu ya *TAFICO* imetupwa mbali ya kuelewa thamani kubwa ya miundombinu hiyo. Aidha, uhimizaji wa kuanzishwa viwanda vya kusindika samaki na ufanyike kwa umuhimu hasa katika ukanda wa Dar es Salaam – Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kutoa kipaumbele ujenzi wa Barabara ya Feri – Pembamnazi kwa kiwango cha lami ili sekta ya utalii iweze kutoa mchango wa ziada katika Pato la Taifa. Kuwepo kwa barabara ya uhakika katika eneo hilo la fukwe kutahamasisha ujenzi wa haraka wa hoteli za kitalii ambao unasita kwa sasa kutokana na kutokuwepo miundombinu hasa barabara safi na ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wamo katika mpango wa kuendeleza Mji wa Kigamboni ambao mipango yake ni kuweka pia miundombinu muhimu ya kiuchumi. Hivyo naishauri Wizara ya Fedha na Uchumi kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda kwa pamoja katika mipango hiyo hasa ya utalii, hoteli na biashara kwa jumla pamoja na uwekezaji.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara walioshiriki kuandaa mwelekeo huu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo au maoni, *TRA* ibuni vyanzo vipya vya mapato kwa kuwatumia wadau mbalimbali wa maendeleo hata kwa kuiga nchi mbalimbali ulimwenguni na hasa nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya utendaji kazi kwa watumishi wa *TRA* uende kwa kasi zaidi ili kukidhi hali halisi ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti katika kuwezesha vijana kwa kuwapatia mafunzo na mitaji kupitia taasisi kama *TIRDO, SIDO* na *SACCOS* ni muhimu sana ikizingatiwa vijana wengi hawajanufaika na mfuko wa uwezeshaji (*JK Fund*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam utengewe bajeti kubwa kulingana na idadi ya watu ambao wanakadiriwa kufikia watu 4.5 milioni. Idadi hiyo inahitaji huduma mbalimbali kama barabara, afya, maji, ajira, elimu, ulinzi na usalama, nishati ya umeme katika maeneo ya pembezoni mwa Dar es Salaam. Mfano, Mfuko wa JK Mkoa wa Dar es Salaam unapata sawasawa na mikoa mingine haizingatii idadi ya vijana (watu). Hali hii inaleta malalamiko kwa jamii kukosa ajira na huduma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunahitaji kuendelea lazima tupange mambo yetu na kufuata *priority*. Kabla ya yote lazima Taifa lolote duniani liweze kujitegemea kwa chakula ili kufikia lengo hilo lazima Wizara ya Fedha ama Serikali iwe na mikakati maalum ya kilimo cha umwagiliaji.

Maeneo maalum yatengwe, pesa itolewe kujenga miundombinu ya Taifa ya umwagiliaji, maeneo yatengwe kikanda matrekta, mbolea na wataalam wapelekwe huko, haisaidii kununua matrekta ya kutegemea kilimo cha mvua mvua. Mkulima mzuri ni yule anayelima kwa wakati, kupanda kwa wakati, kuweka mbolea kwa wakati na kuvuna kwa wakati. Kila mkoa umewekewa lengo, uongozi upo kuanzia *RC, DC,* Halmashauri hadi watendaji wa Vijiji na Kata, kwa hiyo inawezakana.

Tukitaka kilimo lazima tuende kwenye uzalishaji wa viwanda, tuboreshe mazao yetu kabla ya kuuza nje, tuwe na viwanda kwa ajili ya matumizi ya kila siku, kwa sasa tunanunua nje kwa wingi sana kuliko tunavyouza nje. Ndio maana dola inapanda kila leo,

hakuna sababu ya kutumia akiba yetu ya fedha za kigeni kununulia bidhaa hafifu na zisizo za lazima.

Kwa mfano, *furniture*, tungeweza kabisa kutengeneza hapa na kutumia zingine tukauza nje. Radio, *TV*, majembe na kadhalika ubora wake ni duni, kwa hiyo, wanaotaka kuanzisha viwanda vyenye ubora hawataweza kuingia kwenye ushindani, uliona wapi *radio* ya Sh. 5,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuweke sheria, kanuni na taratibu za kuwabana wawekezaji ili wao wapate na sisi tupate. Kwao wameshaharibu sasa wanakuja kuchuma huku kwetu kama wanapata faida lazima na nchi nayo ifaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, tusimamie kwa makini maeneo yafuatayo: Kilimo cha umwagiliaji na maeneo yatengwe, uzalishaji wa viwandani, utalii, tusimamie bandari zetu vizuri sana na madini ni eneo pia la kuangalia.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi kwa Serikali kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri yafuatayo katika vipaumbele vya mpango na bajeti ya 2009/2010.

Moja, kuhusu Miundombinu (barabara na viwanja vya ndege):-

(i) Ni vema barabara ya kati ikakamilishwa kujegwa kwa kiwango cha lami. Haikubaliki kuona kuwa hadi leo barabara hiyo bado inaachwa tu, hususan kipande cha kufika Manyoni kutoka Dodoma na Manyoni – Siuna (Singida).

(ii) Barabara za Minjingu – Babati – Singida, Babati – Dodoma ni vema zikazingatiwa ili zikamilike kujengwa kwa kiwango cha lami na kukamilika katika kipindi hiki.

(iii) Barabara ya Nzega – Tabora ni muhimu sana izingatiwe kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

(iv) Barabara za Mwingumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi na Kilandoto – Lalago – Meatu zitengewe fedha za kujengwa kwa kiwango cha lami.

(v) Kiwanja cha Ndege Shinyanga (Ibadakali) ni muhimu sana kwa usafiri wa anga kwa viongozi, wafanyabiashara, watalii na wananchi wote kwa ujumla. Tayari usanifu wa kina wa uboreshaji ulishafanywa mwaka jana. Bajeti hii itenge fedha za upanuzi na ujenzi wa kiwanja hicho ili ndege kubwa ziweze kutua. Hii itachangia kupanua wigo wa utalii kwa maeneo ya Serengeti, Maswa na Ngorongoro kuliko kutegemea mlango mmoja tu wa kutokea Arusha.

Pili, ni kuhusu elimu, bajeti izingatie kazi kubwa ya kukamilisha ujenzi wa shule nyingi za sekondari zilizoanzishwa na wananchi.

Tatu, kuhusu afya, Mkoa wa Shinyanga utengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Mkoa. Mkoa huu hakuna Hospitali ya Mkoa bali ipo Zahanati kubwa pale mjini Shinyanga ambayo inatumika kama Hospitali ya Mkoa, licha ya kuwa hata Wilaya ya Shinyanga haina hospitali. Hospitali ya Mkoa stahili itachangia kuboresha huduma za afya na hivyo kupunguza tabia ya wananchi wa mkoa huu kukimbilia kwa waganga wa jadi.

Nne, kuhusu maji, kwa kuwa huduma ya maji katika Mji wa Shinyanga itaboreka wakati wowote kuanzia sasa kwa maji ya kutoka Ziwa Victoria, Serikali ione umuhimu wa kutenga bajeti ya kuwezesha kupanua mtandao wa huduma ya maji hayo ili kila Kata ya Manispaa ya Shinyanga iweze kufikiwa. Wananchi watashangaa kutofikiwa na huduma ya maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kupendekeza kuwa matumizi ya fedha za Serikali zianzie mwezi Januari, badala ya mwezi Juni, Mwezi wa Juni uwe wa kujadili na kupanga tu Bungeni ili Januari iwe matumizi, kwa sababu nimeona hata pesa hizo za mwezi Juni zikiidhinishwa haziwezi kutumika mara nyingi zinasuasua kupatikana hasa zile za wafadhili. Kwa hiyo: Je, unaonaje Bajeti ya matumizi ianze Januari na mjadala Juni?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la utalii. Tungeweza kujipatia pesa nyingi sana kupitia utalii hasa kwa kuongeza wigo wa utalii kwa sehemu za Mkoa wa Lindi na Mtwara. Kuna vivutio vingi sana vya utalii ambavyo havijafanyiwa kazi, kwa hiyo tunaiomba Serikali ielekeze pesa kwa utalii ili kuvuna pesa za watalii (bahari, mapango, mambo ya kale, utamaduni na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni maji, Lindi na Nachingwea kuna tatizo kubwa sana la maji nchini. Mfano Lindi Mjini wananunua ndoo moja ya maji Sh.1,000/= tena kwa mtu binafsi aliyeamua kuyaleta maji hayo kutoka Ndanda kilometa 150 Mkoani Mtwara. Je, hii ni haki? Mji wa Lindi mzima umezungukwa na bahari kwa hiyo hauna vyanzo vya maji. Kuna haja ya kuangaliwa kwa jicho la huruma. Bajeti ya maji Lindi ni muhimu kuangaliwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la shule ya ufundi *VETA* Mkoani Lindi, tumeahidiwa miaka mingi kwamba tutajengewa cha kushangaza ni kwamba kabla mikoa haijakwisha kujengewa *VETA*, wengine tayari wanajengewa Shule za *VETA* Wilayani kabla humo mkoani hawajamaliza kujengewa. Tunaomba kuuliza kwa nini hadi leo Mkoa wa Lindi hawajengewa Shule ya Ufundi *VETA*, tunaomba bajeti hii ielekezwe huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la wachimbaji wadogo wadogo, wapewe msaada na nyenzo za kufanyia kazi, Ruangwa Mkoani Lindi kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi, endapo watasaidiwa, Serikali ingeingiza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tungeiomba Serikali iangalie sana suala la Mtwara *Corridor* na shughuli zake. Milango ikafunguliwa, miradi yake ikafanya kazi basi Tanzania ingeingiza fedha kwa sababu nia ya Mtwara *Corridor* ni kufungua biashara na nchi jirani za *SADC* vile vile utalii, mawasiliano, kilimo na uchumi ungekuwa vile vile Chama cha Liganga na Mchuchuma ingefanya kazi na uchumi ungekuwa zaidi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa nchi pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha kuna haja ya kupunguza wingi wa vipaumbele ili kuongeza *impact* ya kuwekeza katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda wa kati uzingatie utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga ili kuchochea maendeleo ya Mikoa ya Kusini. Pamoja na hayo upunguzaji urasimu uzingatiwe katika kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza kiwango cha uvuvi katika Ziwa Victoria katika mpango wa kati na muda mrefu tuboreshe uvuvi katika maziwa mengine hususan Ziwa Nyasa na Tanganyika kwa kuzingatia uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilimo viambatane na uboreshaji wa miundombinu ili kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima upesi na kwa wakati na mazao yanafika kwenye masoko kiurahisi na kwa gharama nafuu. Hapa kuna haja ya kuboresha barabara za Njombe – Manda na Njombe – Mkiwa – Mundindi.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu pamoja na watendaji wengine kwa kutuletea mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono yote yanayopendekezwa lakini tatizo langu ni utekelezaji wa mipango yote hii mizuri. Mfano katika bajeti zilizopita unakuta kuna mambo/fedha tunaidhinisha mapema kabisa lakini fedha kutoka Hazina kwenda kwenye miradi husika huchukua muda mrefu sana na wakati mwingine unakuta nyakati/majira yameshabadilika na hivyo kuathiri sana ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala nyeti sana kwa nchi kama vile kuliwezesha Shirika letu la *TPDC* kushiriki katika biashara ya mafuta kinachosababisha kutoliwezesha hili Shirika, halieleweki na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *D by D* ni mpango mzuri sana lakini shida kubwa ni ufuatiliaji hadi huko kwenye Halmashauri zetu ambako maeneo mengi ile *value for money* haiko au haionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kikubwa hapa Tanzania kwa sasa tunachokihitaji pamoja na mipango yote mizuri ni usimamizi pamoja na uzalendo kwa kila mmoja wetu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuandaa rasimu hii ya mpango wa bajeti na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi ambazo zimeanza kuchukuliwa na Serikali kukipa kilimo kipaumbele ni muhimu sana zikawekewa msisitizo na mikakati ya kweli ili kusaidia wananchi wa Tanzania kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu iliyopita Serikali haikuwahi kuonyesha nia ya kweli ya kuwekeza kwenye kilimo ambacho kinategemewa na kila Mtanzania awe mjini awe vijijini, kwa kuzingatia asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima halafu mbolea hizo zikapewa mawakala ambao sio waaminifu, mbolea zinafika wakati msimu umekwisha, kwa hiyo, haiwasaidii walengwa zaidi ni kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa kuna mikoa minne iliyoainishwa kupatiwa pembejeo za kilimo ambayo ni Morogoro, Rukwa, Mbeya na Kigoma kwa ajili ya kupata akiba ya chakula, ni muhimu pia Serikali ikatambua mikoa mingine ambayo ina rutuba na mabonde mazuri ya kilimo kama Tabora ikafikiriwa kupata ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kutoa ruzuku ya mbolea kwenye wilaya moja tu haijatenda haki kwa wananchi wa Tabora. Wananchi wa Tabora wanalima zao la tumbaku ambalo inaliingizia Taifa hili fedha nyingi za kigeni. Kwa mwaka 2007, thamani ya mazao ya tumbaku ilikuwa dola 72.8 milioni, kwa kigezo hicho ni muhimu sana Serikali itoe mbolea kwa wilaya zote za Mkoa wa Tabora kwani wana mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora umeendelea kubaki nyuma kimaendeleo kutokana na kukosa miundombinu bora. Hali hii pia imesababisha wawekezaji kutokuwekeza kwenye mkoa huu pamoja na mikoa mingine ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti/mpango wa bajeti hii ni muhimu na tunaomba sana barabara ya inayotoka Nzega kwenda Tabora ikakamilishwa ili kufungua njia hiyo kwa wawekezaji na usafirishaji wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kutoka Tabora – Urambo ni mbaya sana, wakati wa mvua haipitiki, itengewe fedha Serikali itimize ahadi za Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji kwa Mkoa wa Tabora ni sugu na hasa Wilaya ya Urambo maji ni ya udongo, ni hatari kwa afya ya wananchi hao. Tunaomba sana Serikali isikie kilio cha wananchi wa Tabora cha maji na sasa ielekeze miradi mikubwa Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, Shule za Msingi zimejengwa kila wilaya lakini hazina vifaa, maktaba, madawati na pia wakulima ni wachache kwa kuwa tunataka watoto wetu wapate elimu iliyo bora na siyo bora elimu, ni muhimu kwenye mpango huu wa bajeti suala la vifaa vya shule hizo likawekwa kwenye mpango ili tuboreshe shule zetu na watoto wetu wapate elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya, Serikali imekuwa inatoa tangazo hapa Bungeni na hata kwenye vyombo mbalimbali kwamba watoto chini ya miaka mitano, kina mama wajawazito na wazee wasiojiweza kupata huduma za afya bure. Hilo halitekelezwi mahali popote kwenye hospitali zetu, kina mama wanapoteza maisha, watoto wanapoteza maisha na wazee wanapoteza maisha kwa kukosa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti hii sasa, au katika mpango huu Serikali iweke fungu la kutosha kuhakikisha hospitali zote zinapatiwa maagizo na fedha za kununua dawa za kutosha kwa makundi ya wananchi niliowataja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la aibu na kusikitisha nchi yetu imekuwa dampo la bidhaa feki na zilizo chini ya viwango, hali inatisha sana, vifaa vinaingia mipakani, bandarini hadi madukani, sokoni, Serikali iko wapi, tutawezaje kusimamia uchumi wetu usiyumbe wakati tunaruhusu nchi za nje kututumia kuuza bidhaa feki kwa wananchi wetu? Sababu zinazotolewa kwamba wananchi wa Tanzania hawana uwezo wa kununua bidhaa *standard* (*low purchasing power*) siyo kweli, huu ni udhaifu mkubwa na ni kuharibu sifa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya China inatengeneza vifaa au vitu (*very poor*) kwa ajili ya Tanzania tu, kitu hicho hicho ukikinunua nchi nyingine hapa jirani kutoka huko huko China ni *high quality*. Mamlaka zetu kama *TBS*, EWURA na kadhalika zitahakikishaje ubora wa bidhaa hizo kabla hazijaingia sokoni? Leo kuna saa Sh.1000/=, Simu Sh.5,000/=, Khanga Sh.1,000/=, kitenge Sh.2,000/=, viatu Sh.1,000/= vifaa vya umeme bomu vinaunguza nyumba, majiko yanaungua, ni tatizo. Wakati tunaua viwanda vyetu vya ndani tunaingiza bidhaa feki za kutumaliza. Naomba Serikali iliangalie hili kwa makini sana, Kariakoo kuna soko la usiku saa 12.30 – 6.00 usiku, wataalam watembee waone nini kinauzwa.

**MHE. ZAYNAB M. VULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nami nashiriki katika kutoa maoni yangu juu ya mapendekezo ambayo nina hakika yatasaidia kuboresha, kuinua uchumi wa nchi yetu. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimebahatika kuwa na rasilimali za kuweza kuinua pato la nchi na hatimaye kuwezesha wananchi wake kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nigusie maeneo mawili tu, moja, bandari zetu na barabara na pili ni kilimo. Kwa kuwa kutumia Bandari za Mtwara na Lindi tunaweza kuongeza pato letu kwani nchi jirani ambazo ziko zaidi ya sita (6) zinaweza kutumia bandari hizo na hatimaye kwa kutumia barabara zitakazojengwa na kuimarishwa na kutoka Mtwara au Lindi hadi Ruvuma na hatimaye nchi jirani kutaweza kuvutia sana wafanyabiashara na nchi hizo jirani na kuimarisha uchumi wa nchi hii. Kwa kuwezesha hili wananchi nao watapata ajira na kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ujenzi wa Gati la Mafia uharakishwe nini kinachocheleweshа? Je, hii haionekani ni kuzidi kudumaza uchumi wa Mafia? Naomba kupatiwa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Gati la Mafia litajengwa nina hakika hali ya uchumi/utalii wa kisiwa hicho utaongezeka na pia hata nchi jirani kama Comoro nayo inaweza kutumia bandari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kilimo, ifike wakati kilimo chetu kilenge kuwa cha kibiashara zaidi kwani tuna ardhi kubwa sana yenye mabonde mengi yenye rutuba. Tuna wanafunzi wengi ambao wamemaliza fani ya kilimo na hawana ajira, ni lini Serikali itawaweka pamoja na kuwawezesha kwa pembejeo ili waweze kutumia utaalam wao na hatimaye kulima kibiashara na kuuza nchi za nje. Kama kutakuwa na utaratibu huu tunaweza kufanikiwa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ni jambo la msingi katika ufanisi wa jambo lolote lile, hivyo kama nchi ili tuweze kufikia ufanisi na ustawi wa nchi yetu ni lazima tuwe na mipango kwa kutoa vipaumbele na mipango ambayo inatekelezeka na kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati dunia ipo katika msukosuko mkubwa wa kiuchumi tunapaswa kuwa waangalifu sana kama nchi katika kupanga ukuaji wa uchumi katika nchi yetu na kwa sababu Tanzania si kisiwa ni sehemu ya dunia yenye misukosuko, tutaathirika kwa namna moja au nyingine bila ya kutaka au kupenda iwe ilivyo.

Kwa hiyo, jambo la kwanza ni kuangalia uwezo wetu kama nchi bila kuweka tumaini kubwa la misaada katika mipango yetu, hivyo, itakuwa busara kuchagua vipaumbele vichache ambavyo vitasukuma ukuaji wa uchumi kutokana na rasilimali zetu chache tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni lazima tuwe waangalifu sana katika matumizi yetu na wapi tunawekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tunayo mipango ambayo kama nchi tuliamua kuwa ni vipaumbele katika bajeti zilizopita hususan elimu na afya pia sekta nyingine za huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za jamii ni za msingi sana lakini ni lazima sekta nyingine ziongeze tija ili kuwekeza katika elimu, afya na kadhalika. Hivyo basi, naona itapendeza sasa kuangalia Sekta ya Kilimo pamoja na tatizo la kukosa masoko na bei ya uhakika katika mazao tunayouza nje kama pamba, katani, kahawa, chai, korosho na kadhalika. Hivyo, tuwekeze katika mazao ya chakula kwa kujitosheleza kama nchi na kuuza ziada kutokana na mahitaji ya chakula duniani na hasa kwa nchi jirani katika mipango yetu sasa tuweke umuhimu katika Sekta ya Kilimo na kile ambacho tunaelekeza katika sekta hii kitumike ipasavyo na siyo kubakia katika vitabu vya mipango tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, upo mpango wa mapinduzi ya kilimo ambao umeanza miaka miwili iliyopita na tuliambiwa zimetengwa kiasi cha zaidi ya *trillion* mbili tu. Kwa kipindi hiki tumetumia kiasi gani na nini tija iliyopatikana? Ni lazima tujitathmini kila mara ili tupate ufanisi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mpango huu wa Serikali kwa mikoa hii sita ya uzalishaji chakula iwaguse moja kwa moja wakulima wetu wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo, nyenzo za kisasa za kilimo rahisi na ambazo wanaweza kuzitunza, mbegu na mbolea. Kwa kuwa hatuna wakulima wakubwa katika mikoa ya mpango lazima sasa tuwasaidie sana hawa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, baada ya kuongeza uzalishaji wa chakula kinachofuata ni namna chakula hicho kitakavyofika katika masoko na maeneo yenye shida ya chakula kwa kuimarisha miundombinu kwa maana ya barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya makusudi sasa ya kuangalia barabara chache ambazo zitasaidia kufikisha mazao haya katika masoko, kwa kuangalia barabara zifuatazo Tunduma – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma; Mpanda – Tabora – Nzega; barabara ya Iringa – Dodoma - Arusha na Itigi – Tabora - Kigoma na Barabara ya Songea – Tunduru – Masasi. Pia sasa ni lazima kuwekeza katika reli kwa maana ya njia (reli) na mabehewa ya mizigo (*rolling stocks*) reli ya kati na reli ya Mpanda ni vipaumbele kwa sasa, kadhalika reli ya Tazara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa reli kutasukuma sana kuondosha mizigo ambayo imekuwa kero katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza ufanisi wa Bandari na kuongeza mapato ya nchi na kutimiza wajibu wetu kwa majirani zetu wasio na bandari na kujenga imani kwao ya kutumia bandari yetu na kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa *Hub Port*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusiwepo miradi mipya katika elimu na afya, tutumie rasilimali kidogo tulizonazo kukamilisha miradi iliyopo na kuboresha huduma katika sekta hizo na kuwekeza katika Sekta ya Maji ambayo ni kero kwa wananchi. Pia katika kukuza uchumi maji ya uhakika yanahitajika katika viwanda na matumizi ya binadamu.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa na kuwasilisha mpango na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutushirikisha sisi Wabunge mapema katika mchakato wa kuandaa bajeti ya mwaka ujao wa fedha. Kama wawakilishi wa wananchi, Wabunge wanafahamu shida wanazozipata, hivyo ushiriki huu utayawezesha matatizo hayo kupatiwa ufumbuzi kwa kupitia bajeti hii inayoandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kuwa elimu bora ndio ufunguo wa maisha, kwa kupitia bajeti zilizopita na michango ya wananchi mambo mengi mazuri yamefanyika, mashule ya msingi yamekarabatiwa, madarasa mapya, Shule za Sekondari kila Kata, wanafunzi darasa la kwanza, kidato cha kwanza, kidato cha tano na wanaoingia elimu ya juu wameongezeka, lakini bado kuna viporo vingi kwenye elimu ya Msingi, sekondari na juu. Kuna umuhimu wa kuendelea kuifanya elimu kuwa kipaumbele cha kwanza, ili iweze kutolewa elimu bora, itakayovusha Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Taifa letu liweze kuendelea kuna maeneo ambayo bajeti hii inabidi iyape kipaumbele, miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, vyombo vya majini vitawezesha kuifungua nchi yetu na mikoa yetu kibiashara. Ili kuuwezesha Mkoa wa Kagera kufanya biashara vizuri na Uganda, Rwanda, Burundi na Mikoa ya Shinyanga naiomba Serikali itenge fedha ili barabara za Kyaka – Kayanga – Mulongo, Kayanga – Murushaka – Benako, Kagomba – Biharamulo – Lusahunga, Biharamulo – Bwanga zijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu, hadi leo ni Watanzania chini ya asilimia 10 ndio wana umeme, ili tuweze kuwa na viwanda, ili tusindike mazao yetu tunahitaji umeme vijijini. Mfano Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini Missenyi, Karagwe, Muleba na Wilaya zote za mkoa wana mvua, kuna mazao mengi kama mananasi, nyanya, ndizi yanayoweza kusindikwa na kuwaongezea wananchi kipato, kuwaondolea umaskini, lakini umeme hakuna. Ili kuinua nchi yetu ili kukuza uchumi naiomba Serikali itenge kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini kwani maendeleo katika kila sekta yanategemea kuwepo kwa nishati, waongezewe bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi dunia imekumbwa na misukosuko ya uchumi, mazao yetu ya biashara kama kahawa na pamba tunazouza nje, yamepungua bei sana na hivyo kuleta hasara kwa wakulima kwa kuwa nchi nyingine huwapa wakulima ruzuku au *compensation* ili wafidie hasara wanayopata kutokana na majanga ya mafuriko, ukame, magonjwa na kadhalika sasa hivi Amerika, Ulaya wanatoa fedha wanazipa taasisi zao za kifedha na mabenki ili kuzinusuru zisifilisike. Je, Serikali inaweza kutoa *compensation*/fedha kwenye Vyama vya Ushirika kama *KDCU, KCU* na vya pamba ili kupunguza hasara waliyopata kutokana na misukosuko ya uchumi ili wasifilisike?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua kuwa wakati umefika wa kutoa vipaumbele na kuamua kuweka nguvu kwenye mikoa michache inayozalisha mazao ya kilimo sana, kama Tanzania tunataka kuendelea lazima tuwekeze kwenye kilimo, tunaweza kujipatia chakula cha kutosha na tuuze nje, inawezekana.

Kinachotakiwa ni Serikali kuamua kufanya yafuatayo; kulima eneo kubwa kwa trekta, kuweka miundombinu ya kumwagilia, kuvuna, kuanika, ku-*grade* na kufunga kitaalam kwa kutumia mitambo ya kisasa, kutoa mikopo ya muda mrefu ya kilimo, kuongeza maafisa ugani. Tukilima tu kwa trekta bila kuwa na miundombinu ya umwagiliaji, tutakuwa hatujafanya vya kutosha, jua/ukame unaweza kuharibu mazao. Hivyo, napendekeza hayo ili kusaidia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali iliyoahidi, naishauri walipe madeni na wasilimbikize madeni, je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha kwa Wizara ya Elimu ili walipe madeni makubwa waliyonayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali ina mipango mizuri sana, ili iweze kutekelezeka inabidi kuibua vianzio vipya vya mapato, tukusanye mapato kwa wingi na vile vile tuhakikishe tunasimamia Wizara, Mikoa, Halmashauri kuhakikisha kuwa fedha inafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza Wizara ya Fedha ikiongozwa na Waziri na viongozi mbalimbali kwa kazi nzuri ya kuwasilisha *framework* ya mpango na bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hata hivyo nina mchango ufuatao:

Moja, kuhusu chakula (ukurasa wa 9 kifungu cha 21(i) kwa maoni yangu utaratibu wa mwaka huu wa kutoa mbolea na mbegu za ruzuku ni mbaya sana na utachochea uzalishaji duni na kusababisha njaa. Utaratibu huo ni ubaguzi, umecheleweshа ruzuku na kulazimisha wakulima kugharamia mbolea wasizozitaka. *NMB* imeshindwa kurejesha fedha kwa mawakala kiasi kwamba mawakala wengi wameachilia mbali biashara hiyo. Nashauri utaratibu huo utazamwe upya na uandaliwe mapema msimu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu umwagiliaji, ukurasa wa 24 (iii) hauwezi kupiga hatua inayostahili kama tutaendela kukosa wataalam wa kutosha. Pia mfumo wa Wizara/Idara ya Umwagiliaji ngazi ya Wilaya unakosa *focus* kwa sababu mfumo wa kanda unafuga urasimu na kusumbua mikoa isiyo na ofisi za kanda, wilayani umwagiliaji uliokuwa chini ya kilimo umetengwa baada ya kuanzisha Wizara ya Maji na Umwagiliaji kitendo ambacho kimesababisha kukosekana *focus* ya usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo mawili, Serikali iendeshe *training programme* ya wataalam wa kutosha kwa Mikoa yote (na siyo kanda tu) na Wilaya, Serikali iweke wazi katika ngazi ya wilaya umwagiliaji uko chini ya Wizara gani kisekta kati ya *DALDO* na *District Water Engineer* ambaye si mtalaam wa umwagiliaji (bali ni mtaalam wa maji tu).

Tatu, Kifungu cha 25 sentensi mbili za mwisho zinatatanisha wakati maelezo yanasema Serikali itaendelea kutafuta mikopo ya nje na ndani, inasema wazi sentensi ya mwisho kwamba itaendelea kutokopa kwa ajili ya bajeti, sasa tushike lipi? Nahitaji ufafanuzi,

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yeyote ile. Pamoja na hali ya mtikiso mkubwa wa kiuchumi hapa duniani bado kilimo ndio kimbilio la kuleta usalama na amani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu mibovu imefanya hata ile mikoa inayozalisha kwa wingi kama Mbeya, Rukwa, Ruvuma na Iringa kushindwa kusafirisha mazao yao na bado hali ya chakula imekuwa mbaya nchini kutokana na ubovu wa miundombinu. Hii imesababisha nchi yetu kuendelea kuagiza vyakula nje ya nchi huku mazao na hata matunda vikiharibika kutokana na kukosa miundombinu ya barabara na reli. Naamini tukiboresha miundombinu basi nchi itakuwa na chakula cha kutosha na hata kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo ni muhimu mno kwani bila chakula amani hutoweka. Pamoja na mtikiso mkubwa wa uchumi duniani, Tanzania tumebahatika kuwa na eneo kubwa la kilometa 888,200 za mraba lakini ni kilometa 480,622 tu za mraba zinazofaa kwa kilimo. Lakini kinachosikitisha ni kwamba ni asilimia 10 tu inayotumika kwa kilimo, ina maana asilimia 90 ya ardhi inayofaa kwa kilimo haitumiki. Lakini lazima tujiulize ni kwa nini eneo kubwa hivi kilometa 362,360 za mraba hazitumiki? Sababu kubwa ni ukame lakini ukosefu wa utaalam wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Mtanzania na kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, basi ni bora Serikali isaidie wakulima ili kilimo kiwe na tija. Kwa kuwa tuna Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambacho kwa muda mrefu kimekuwa kikitoa wahitimu wa kilimo lakini wahitimu hao hawaajiriwi katika kilimo, kibaya zaidi idadi ya wahitimu hao inapungua. Ushauri wangu ni kuwa na mikakati ya kuhakikisha vijana wanaochukua kilimo wapewe asilimia mia moja ya mkopo ili tuweze kupata wataalam wengi wa kilimo na hivyo kilimo kiwe na tija zaidi. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa ni asilimia moja tu ya kilimo cha umwagiliaji kinafanyika hapa Tanzania. Hii ni aibu kubwa kwa nchi yetu iliyo na mito, maziwa na mabwawa lakini tunashindwa kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Sudan na Misri walio na ukame zaidi yetu lakini wanategemea Mto Nile unaotoka Ziwa Victoria lililo Tanzania. Hivi Serikali haioni umuhimu wa kutumia maji haya ya Ziwa Victoria katika kilimo cha umwagiliaji? Kama Misri iliyo umbali wa zaidi ya kilometa 5000 kutoka Ziwa Victoria inatumia maji haya sisi tulio ndani ya kilometa mia moja tunashindwa kuyatumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchumi, pamoja na hali mbaya ya uchumi duniani bado Tanzania tuna bahati kubwa mno kuwa na bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kijiografia Tanzania tumezungukwa na nchi nyingi zilizofungwa (zisizo na bandari – *landlocked*). Uwepo wa nchi hizi ni ishara tosha ya kupata fedha nyingi kwa bidhaa zinazopita katika bandari zetu kwenda Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Congo na Zambia.

Ni jambo la kusikitisha kuona bandari zetu zimeweza kupokea makontena (*twenty foot equivalent units – TEUs*) 260,000 tu kwa mwaka wakati nchi ya Singapore, nchi ndogo iliyokuwa na uchumi unaoungana na Kenya miaka ya 80, leo hii ina-*handle* 35 milioni *TEUs* kwa mwaka. Hivyo naamini Serikali ikiboresha bandari zetu Tanzania itapaa kiuchumi na kamwe hatutalia kwa ukosefu wa chakula au kuomba misaada yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la chakula hapa nchini kama zilivyo nchi nyingi zinazoendelea limezidi kuchochewa na ukuaji wa kilimo cha mazao ya mafuta yaani *biofuels* au *ethanols*. Wakulima wengi sasa wameamua kuacha kilimo cha mazao ya chakula na kwenda kwenye *biofuels*. Hii ni hatari sana hasa ikizingatiwa kuwa mazao haya ya mafuta huchukua muda mrefu kutoa mazao lakini pili yamechukua mashamba makubwa. Lakini kubwa zaidi wakulima hawa wamevutika na kilimo hicho na kuacha kilimo cha chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme tu usalama wa chakula ni usalama wa Taifa. Hivyo kunapokuwa na tishio la chakula, amani nayo hupotea, hivyo ni jukumu la Serikali kuboresha kilimo na kuleta mapinduzi ya kijani pamoja na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vipaumbele vilivyowekwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010 ni vyema Serikali kwa makusudi kabisa ifanye jitihada kuhakikisha bandari zetu zilizopo Bahari ya Hindi zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa ili kuongeza pato la kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa Serikali baada ya kujenga barabara ya lami toka Mtwara hadi Dar es Salaam ni vyema barabara hiyo ikatumika kuinua uchumi wa nchi kwa kuiboresha Bandari ya Mtwara ili iwe inapokea mizigo yote (*contena*) inayokuja hapa nchini na magari (malori) yatasafirisha mizigo hiyo kwenda mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam itumike kwa ajili ya mizigo ya nchi jirani (*transit*) pamoja na meli za mafuta. Hii itasaidia kuondoa msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam na kufanya nchi nyingi zaidi kuitumia Bandari ya Dar es Salaam, hivyo kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Tanga ni vyema ikatumika kwa ajili ya meli zinazoleta magari. Hii itasaidia pia kuondoa msongamano wa meli zinazoleta

magari Dar es Salaam, lakini pia itasaidia hata Watanzania wenzetu ambao hutumia Bandari ya Mombasa kupitishia magari na baadhi ya mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua, ni vyema sasa Serikali yetu ikaamua kuzitumia bandari hizi ili kuliongezea Taifa pato, lakini pia kuongeza ajira katika mikoa hiyo ambayo ina bandari. Nia aibu kwa nchi yetu yenye bandari tatu kushindwa kuzitumia bandari hizo na kuacha nchi jirani zikitumia bandari za mbali kuingiza mizigo yao. Barabara nzuri tulizojenga zitakuwa hazina maana (faida) yoyote kama hazikutumika kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta mpango huu mbele ya Bunge lako kwa ajili ya kupata maoni na ushauri wa Wabunge, kwa mantiki hiyo hiyo, naomba nishauri katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, nchi yetu kwa nyakati tofauti tofauti imekuwa inakabiliwa na tatizo la chakula, wakati mwingi tunalazimika kuagiza chakula kutoka nje ya nchi. Kwa ujumla na kwa kuzingatia hali ya hewa ya nchi yetu hatukustahili kuagiza chakula nje ya nchi, tufanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ijayo 2009/2010, Serikali iweke mkazo katika kuhakikisha kwamba mbolea na pembejeo nyingine zinapatikana kwa wingi, aidha, uzalishaji wa mbolea nchini utiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenge maeneo maalum ya uzalishaji yaani *agricultural zones*, maeneo hayo kama vile Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Morogoro yapewe kipaumbele katika masuala yetu nchini kama vile mbolea, mbegu na zana za kilimo. Kwa kufanya hivyo nina hakika nchi yetu itaondokana kabisa na upungufu wa chakula nchini na uagizaji wa chakula nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji kipewe umuhimu mkubwa na ikiwezekana pia yatengwe maeneo maalum ya kilimo cha umwagiliaji, kusambaza nguvu na rasilimali (*resources*) katika maeneo madogo madogo hakutakuwa na tija kubwa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziwekwe jitihada za dhati katika kuhakikisha kwamba vyuo vyetu vya utafiti wa mbegu za mazao mbalimbali vinapata pesa za kutosha katika kufanya utafiti wa mbegu za mazao na kuzitumia. Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba tumeagiza asilimia 75 ya mbegu kutoka nje ya nchi. Hivyo, ni asilimia 25 ya mbegu zinazotumika nchini zinazalishwa na vyuo vyetu vya utafiti, hali hii haiwezi kuachwa kuendelea hivyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu riba za mabenki, katika kipindi cha mwaka ulioishia Desemba 2008, inaonesha kwamba riba za mabenki (hasa riba za amana) zimekuwa zinaongezeka kwa kiasi kidogo sana wakati riba za mikopo katika mabenki

zimeendelea kuwa za juu sana, hali hii inakatisha tamaa wananchi wengi kukopa kutoka kwenye mabenki. Nashauri, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Serikali iyabane mabenki ili kupunguza riba kwenye mikopo ili wananchi wengi wapate fursa ya kukopa na hivyo kujiondolea umaskini na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya umeme ya zamani, najua nia thabiti ya Serikali ya kuimarisha miundombinu ya umeme. Hata hivyo, sijaona kama kuna mpango wa dhati wa kukamilisha vipolo vya umeme vya muda mrefu kama kule Mbozi kuna miradi ya umeme ya Ruanda – Iyula – Idiwili kilometa 26; mradi wa Mahenge – Iyula kilometa 5 na mradi wa Uwawa – Hasamba kilometa 13. Miradi hii ni ya tangu mwaka 2002/2003. Nashauri miradi ya namna hii ipewe kipaumbele katika bajeti ijayo ili kumaliza malalamiko ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli, sijaona mkakati wa kuinusuru TAZARA. Shirika hili muhimu sana katika uchumi wa nchi liko kwenye hali mbaya sana. Nashauri bajeti ijayo ionyeshe mpango bayana wa kunusuru TAZARA ili tupate manufaa yaliyokusudiwa wakati wa ujenzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za Rais za 2005, bajeti ya mwaka 2009/2010, itilie mkazo sana katika kuhakikisha kwamba ahadi zote za Rais zinatekelezwa. Ahsante sana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana mapendekezo ya mpango huu. Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa mambo machache muhimu yafuatayo. Mheshimiwa Waziri naomba nikukumbushe ahadi ya Serikali ya kujenga darala la Mto Sibiti lilikuwa lianze kujengwa 2008/2009, ikaahirishwa na ahadi ikatolewa kabisa kwamba litaanza kujengwa 2009/2010.

Pia naomba ikumbukwe kwamba Mheshimiwa Rais alipotembelea Iramba Mashariki aliahidi Serikali kutekeleza ahadi ya kujenga daraja la mto Sibiti na Iramba Mashariki kupewa hadhi ya kuwa wilaya. Gharama ya kujenga daraja na mpaka sasa pamoja na kutengeneza tuta na barabara kilometa 28 ni 5.0 bilioni, naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu nawapongeza sana Watanzania wote nchi nzima kujenga Shule Msingi na Sekondari kila Kata na kwangu tumefikia kujenga mpaka kwenye vijiji. Hata hivyo, shule hizi hazijakamilika na wananchi sasa wanaendelea kwa kusua sua kwa sababu sasa hivi kuna mpango wa ujenzi wa zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila Kata. Kazi ambayo inaanza kabla ya kukamilisha ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, majengo ya utawala vyoo vya kudumu na kadhalika kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza ili kumaliza tatizo la elimu tuanze ujenzi wa zahanati fedha za *Local Government Development Grant* zinazotolewa na Serikali kwenda kila wilaya kuanzisha miradi ya maendeleo kwenye Kata na nusu miradi ya

Wilaya, kwa mwaka huu wa fedha 2009/2010 kwa makusudi kabisa fedha hizo zote zielekezwe kwenye kukamilisha miradi ya elimu, madarasa, nyumba za walimu, vyoo, majengo ya utawala na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona utata mkubwa kwenye Wizara hii kwenye bajeti hii hii ya Ilani ya MKUKUTA, sioni kama inalenga sehemu yenyewe au tunasoma kwenye vitabu tu!

Kwa mfano, huduma ya afya, pembejeo, barabara siamini! Je, Serikali ina mikakati gani? Kwenye mikakati yote hii wakulima wana shida sana. Mfano ni Mbeya, wananchi wananyanyaswa, wanaombwa vitambulisho vya kupigia kura na hata hivyo hawapati mbolea. Tatizo lipo kwenye mawakala, unakuta wananchi hawana pesa ya kupeleka kwa wakala: Kwanini Serikali isiwakopeshe? Mbolea yenyewe inafika wakati umeshapita! Mbolea ya kupandia wakati mazao yameshaota! Je, sasa hiyo mbolea ni ya nini? Naomba ufuatiliaji uwepo.

Je, katika utaratibu huu barabara ya Muleba Lusaunga ipo kupunguza utekwaji; majengo ya hospitali ya Mkoa Bukoba wodi za wagonjwa zinabomoka: Je, katika bajeti hii tutaweza kupatiwa madaktari?

Suala la madai ya madaktari na wastaafu wa Afrika Mashariki watakamilishiwa lini madai yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilete zana halali wavuvi wetu wasiwe wanateseka pamoja na hata mkiwakopesha, hasaidii bila kuletewa zana halali. Tutashukuru sana tukipatiwa zana hizo katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa zana hizo ziko madukani, kwa nini wavuvi wasiletewe zana halali na viwanda vya zana haramu vifungwe? Nitashukuru nikijibiwa vizuri.

Pia mikopo haiwafikii walengwa. Nashauri pesa zote ziwe a ufuatiliaji.

Pia nakumbusha uwanja wa ndege Mheshimiwa Waziri usisahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa maelezo yake ya kina kwa Bunge kuhusu mwongozo wa utayarishaji wa mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2009/2010 – 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hayo yamezingatia kikamilifu dira ya maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 pamoja na MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukuza uchumi hususan kwa njia ya kilimo ni lazima kuongelea mawasiliano hasa ya barabara za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuboresha sekta ya barabara za vijijini suala la kukuza uchumi maeneo ya vijiji litakuwa la nadharia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa wazi ni kwa kiasi gani Serikali yetu inaliona hilo, kwa mfano kwa kuanzisha Mifuko mbalimbali ya barabara kwa mfano; *Road Fund, LGTP Fund, VTTP Fund* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko yote niliotaja hapo juu inahusu Serikali za Mitaa (Halmashauri).

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko yangu ni kwamba, fedha zinatengwa katika Mifuko yote niliyotaja lakini cha kusikitisha mara nyingi fedha hizi huchelewa au kutofika kabisa kwenye Halmashauri husika. Fedha za *LGTP* na *VTTP* za 2008/2009 hadi leo hazijapelekwa kwenye Halmashauri husika ukiacha Iringa na Dodoma. Miradi ya barabara vijijini itatekelezwaje kama hali yenyewe ndio hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nia ya Serikali ni njema basi ucheleweshwaji wa *Funds* hizi kwa Halmashauri husika ukomemeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango na muda wa utekelezaji, Mheshimiwa Waziri ameleta mwongozo huu mbele yetu uliojaa mwongozo mzuri sana. Tatizo lililo mbele yetu ni tatizo la taratibu za utekelezaji wa bajeti zetu hapa nchini. Kwa mfano uletaji au uuzaji wa mbegu kwa majira sahihi ya mvua, usambazaji wa pembejeo kwa wakati muafaka, elimu sahihi ya utaalam kwa wananchi kwa wakati stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, maandalizi kwa wataalam wa fani husika yawe chini ya usimamizi thabiti kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishirikiane kwa karibu sana na Wizara zingine, mfano, Wizara ya Maji na Mazingira ili waweze kubaini mabonde yote nchini. Lengo ni kuongeza uzalishaji wa chakula nchini, hii inaweza kuinua hali ya uchumi nchini, pia wananchi kupata chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuunga mkono nguvu za *SIDO*, chombo cha *SIDO* ni muhimu chenye msaada mkubwa sana kwa wananchi wanaojishughulisha na

shughuli ndogo ndogo na hasa wenye kipato cha chini.  Katika kuinua ajira hapa nchini *SIDO* ndio mkombozi, wananchi wanataka kuanzisha viwanda vidogo vidogo lakini uwezo wa chombo hiki *SIDO* ni mdogo sana.  Hivyo, niiombe Serikali inapotenga fedha katika bajeti yake iwafikirie kuwainua *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha mawasiliano, naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa iliyoonyesha kuhusu miundombinu, barabara. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara ilenge katika kufungua barabara zilizo nyingi ikiwezekana nyingi ziwe za kuungana (Ring Roads), kwa mfano, barabara zitokazo maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi zifikiriwe kupewa fedha za kutosha ili ziimarike tayari kwa kusafirisha chakula nyakati zote za majira (masika na kiangazi).

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuimarisha Bandari ya Tanga ili bidhaa ziweze kusafirishwa kwa kutumia njia ya maji, bidhaa ziweze kusafirishwa kwa njia ya barabara na bidhaa ziweze kusafirishwa kwa kutumia njia ya anga.

**MHE.  GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu, suala hili ni muhimu sana kama kweli tunataka kuleta mabadiliko ya uchumi katika nchi yetu, barabara zetu nyingi za vijijini sio nzuri na hii inachangia umaskini mkubwa huko vijijini. Wananchi na wakulima wanashindwa kusafirisha mazao yao au wao wenyewe kusafiri kwenda mijini kwenda kuuza au kununua mahitaji yao muhimu kutokana na gharama kubwa za usafiri na usafirishaji kuwa kubwa.  Hivyo, tunaomba Wizara iweke msisitizo mkubwa katika suala hili la barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme, tunajua umuhimu wa umeme katika nchi, lakini kumekuwa na matatizo mengi ya umeme katika nchi yetu na imesababisha upungufu wa uzalishaji katika viwanda vyetu na hata kwa watu binafsi.  Hivyo, tunataka Serikali ilitazame tatizo na kuweza kulisaidia shirika hili la *TANESCO* ili liweze kupata pesa za kuweza kuanzisha vyanzo vingine vya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji, maji ni uhai, bajeti iliyopita Wizara hii ilipata pesa kidogo kama kweli tunataka kuleta mabadiliko katika kilimo lazima Wizara hii ipewe pesa za kutosha.  Tunazungumzia suala la umwagiliaji mashamba lakini kama hakuna pesa haya yote tunayosema hayatawezekana.  Hivyo, tunaomba Wizara hii ipewe pesa za kutosha ili yale maisha bora kwa kila Mtanzania yaweze kutimia, mengine wenzangu wameyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kutuletea rasimu ya Mpango na bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye haraka kuanzisha *mortgage banking* ili wananchi wakope kwa riba ya chini na mkopo wa muda mrefu. Hatua hii itaondoa vishawishi vya ufisadi Serikalini kwani mtumishi aliyekwishalipia nyumba yake ya mkopo kutakuwa hakuna haja ya kula fedha kifisadi fisadi kwa watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, Serikali imekubali umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa chakula nchini. Serikali isisahau kuwa Bonde la Mto Rufiji na maji ya Mto Rufiji na likalimwa vizuri, basi linaweza kulisha Tanzania nzima. Lakini viongozi wanang'ang'ania Morogoro, Mbeya, Ruvuma, Iringa na Rukwa tu. Hii ni kujitia upofu tu, itajeni Rufiji katika sehemu ya nchi yenye *biggest potential*' katika kulisha Watanzania.

Hivyo sasa, tunaomba kuletwe matrekta mengi ya kukopa au ya kukodisha, hii itapanua kilimo mara moja, bonde hili la Rufiji tulichangamkia kwa kufanya mipango ya umwagiliaji (*irrigation*), Wizara ya kilimo ipewe *target* ya kutoa chakula kwa mwaka ili tusipeleke fedha nyingi huko Wizarani lakini hatupati mavuno ya kutosha. Fedha nyingi za *DADPS* zipelekwe Wilayani, kwa ajili ya semina, kupeana uzoefu, mikutano, usafiri na kadhalika, fedha hizi hazikuleta tija yoyote kwa nchi yetu. Waziri wa Kilimo lazima ajibu kwa nini fedha nyingi zimetumika kiholela bila ya kuzalisha hata gunia moja, fedha zimeliwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji, Rufiji imeletewa ng'ombe wengi kuliko uwezo wake, tunaomba Serikali iweze *quota* kwa kila mfugaji asifuge zaidi ya ng'ombe kadhaa tu ziada yote ya mifugo iuzwe ili tusaidie kuokoa ardhi yetu. Kuwe na dhamira ya dhati ya kupunguza mifugo hii, tujaribu kuwaelimisha wafugaji waachane na kufuga kienyeji wingi wa ng'ombe wasio bora ni hasara tu kwa Taifa. Kilimo chetu Rufiji kinaathirika sana na ng'ombe kuingia na mashamba ya nafaka yanaliwa na kuwatia umaskini wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme, kwa vile tuna matatizo makubwa ya nishati hii. Hivi sasa bidhaa za Tanzania haziuziki kwa sababu ya umeme unazidisha *cost of production*. Serikali sasa ikubali kuwa jibu la tatizo hili ni kujenga *Stigglers Gorge Hydropower Station*. Tuvisaidie viwanda vyetu, pia tungeuza umeme wa ziada kwa nchi za jirani na *small scale and medium scale industries* zingeweza kujengwa kwa wingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Serikali kwa kuandaa mwongozo unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika (ukurasa wa 13) kipengele cha (ix) imetuambia kuwa lengo la kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika kipengele hiki nakubaliana na jitihada zinazofanywa na Serikali kuhusu uwezeshaji, lakini nieleze wazi kuwa mifumo inayotumika katika kuwezesha wananchi kwa sasa wala haiwasaidii wenye ulemavu hasa

wengi walioko vijijini.  Hivyo, nasisitiza katika bajeti tunayoitarajia kupata maelekezo mahsusi ni jinsi gani jamii hii itawezeshwa ili nayo iweze kuchangia maendeleo ya nchi yao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la huduma za jamii, katika eneo hilo kuna suala la kuendeleza miradi ya elimu na afya, maeneo ambayo bado watu na watoto wenye ulemavu wananyanyasika kupata huduma hizo.

Upande wa elimu mingi ya hiyo miradi ya elimu na afya haizingatii mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu tofauti na Ilani ya Uchaguzi inavyoelekeza.  Majengo ya shule za zahanati, hospitali si muafaka kwao kwani hayafikiki kwa urahisi na wala si rafiki kwao.  Huduma za afya kutolewa bure kwa wasiojiweza na wazee hata wenye ulemavu si bure hata kidogo, kwa madai kwamba fedha hazitoshelezi.  Hivyo, ni lini Serikali itatenga fedha katika maeneo haya ili walengwa wapate huduma stahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pawe na mkakati unaoweza kutekelezeka kwa manufaa ya wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu mfupi, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa yafuatayo:-

Kutayarisha hoja yenye kuleta matumaini kwa Tanzania, kwa kuzingatia kwa sehemu kubwa ya maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kwako wewe mwenyewe kuiwakilisha hoja hii kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango wangu, nia yangu siyo kuikosoa hoja hii bila kuchangia maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa uchumi, hapa nakubaliana na malengo ya ukuaji wa uchumi, ukusanyaji wa mapato na upandaji wa bei kama yanavyoonekana katika Ibara ya 3. Kuhusu akiba ya fedha za kigeni, nashauri tusiwe na lengo lege lege.  Tulenge kuwa na akiba ya kutosha kuagiza zaidi ya miezi mitano, zipo sababu mbili nazo ni; lengo la juu litatusukuma tufanye kazi zaidi ili tuongeze uingizaji wa fedha za kigeni, kwa kuwa thamani ya shilingi inashuka na kama itaendelea kushuka tutajikuta akiba yetu ikitosha matumizi ya miezi mitatu au chini ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo, mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka.  Hili ni jambo zuri litaongeza uzalishaji.  Lakini tuwe waangalifu juu ya nani wanakopeshwa siyo wote ni waaminifu, vinginevyo tutaingia kwenye matatizo. Mifano miwili itasaidia kueleza hili, msukosuko wa sasa duniani ulioanzia Marekani, umetoka na mikopo mingi katika sekta ya nyumba za majengo, hapa Tanzania mikopo ya *NBC* kwa Vyama vya Ushirika katika miaka ya 70 karibu iifilisi *NBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu riba, hoja inaeleza kuwa katika kipindi cha miezi sita ya mwisho wa 2008, riba katika mabenki ya biashara imepanda kutoka asilimia 15.5 hadi 16.5. Kwanza, kwa wakopaji riba halisi kwenye mwisho wa mwaka 2008 ili kati ya asilimia 18 na 20. Pili, kupanda kwa riba kunapunguza kazi ya uwekezaji, hivyo kupunguza uzalishaji kwani wakopaji wanahofia riba za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, kwa nini Benki Kuu isitumie nyenzo zake za *monetary* na *fiscal policies* kuzuia upandaji holela wa riba?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupungua kwa makusanyo, dawa ni kuimarisha nyenzo na utendaji katika bandari zetu, kuruhusu ushindani katika uendeshaji wa bandari badala ya kutegemea maagizo kwa *TPA* na kuacha *TPA* iwe mpangishaji pamoja na kuimarisha usafirishaji nchi kavu, zikiwemo reli, barabara na katika maziwa makuu. Mira kama ya bandari, barabara na reli zinazovuka mipaka yetu, tunaweza kuvutia fedha na mitaji/mikopo kwa kutumia mpango wa *NEPAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijijini, kuhusu barabara tusizingatie barabara kuu pekee, barabara za vijijini zina mchango mkubwa sana kwa Taifa. Naikumbusha Serikali kero ya Wilaya ya Kisarawe (Pugu – Vikumbulu) kujengwa katika ngazi ya lami. Nimeipigia kelele tangu 1995 hadi leo, Serikali imejenga kilometa sita tu. Matengenezo ya barabara hii yana faida zifuatazo: Itarahisisha kufika Mbunga za Selous, hivyo, kuinua utalii, itarahisisha usafiri/usafirishaji wa vifaa vya utafiti wa mafuta na gesi kwenda Kijiji cha Kisangire ndani ya Kisarawe; Itarahisisha kufikisha Dar es Salaam mazao ya misitu, matunda, korosho na mbogamboga na itainua na kuboresha mapato ya wananchi wa Kisarawe inakopita barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini, nashauri Serikali iongeze viwango vya kodi ikiwemo mrahaba, kodi ya mapato, michango ya makampuni kwenye miradi iliyoko kwenye machimbo na *windfall taxes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *import substitution*, ukiangalia kiambatisho ’E’ utashangaa kwani tusianze kutengeneza hapa nchini vifaa vya ujenzi, mbolea, karatasi, nguo na *plastics* ambavyo vyote tumewahi kuvizalisha katika miaka ya 70. Leo viko wapi viwanda vya Mgololo, *TFC*, *TEGRY*, Urafiki, *MWATEX*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya ugonjwa wa UKIMWI. UKIMWI ni janga la Taifa lakini asilimia kubwa ya fedha za UKIMWI tunazipata kutoka kwa wafadhili. Je, siku wafadhili wakijitoa ina maana waathirika wote ndo mwisho wao? Inabidi katika mpango wetu tuweke bajeti ya kutosha kwa ajili ya janga hili. Afya za watu kwanza ndio mengine baadaye, bila watu hata hii bajeti itakuwa na maana?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii Tanzania, biashara ya utalii ni mojawapo inayoliingizia Taifa fedha nyingi sana za kigeni. Lakini watalii wanapungua sana kwa

sasa hivi ukizingatia huu mtikisiko wa uchumi umeanzia huko huko watalii wanapotoka USA na UK. Wenzetu nchi ya jirani Kenya wakati yalipotokea matatizo wakati wa uchaguzi watalii waliacha kabisa kwenda Kenya lakini wenzetu kuokoa jahazi ilibidi wapunguze *park fees*, bei za mahoteli zilipunguziwa *levy* na watalii wakaanza tena kwenda Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, Tanzania kwa mwaka huu ambao kuna mtikisiko wa uchumi ili kupata watalii wengi tufanye *promotion* (kwa mwaka huu tu) kwa kupunguza kodi za *park fees* ambazo ni ghali sana. Kwa mfano *fees* ya kupanda Mlima Kilimanjaro ni 8630 kwa kichwa. Turudishe zifike 8430 kama zamani na watalii watakuwa wengi, hii ni pamoja na *fees* za *park* nyingine. Tunaona nchi kama Marekani Rais Obama ameamua kutoa marupurupu yote ya Wakurugenzi, ameagiza viwanda vifufuliwe kwa kuongeza fedha kwenye mabenki yao. Hata nchi ya Uingereza wameweka fedha za walipa kodi kwenye benki zao kama *Llyods Bank* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, inabidi na sisi tuwe na mpango wenye kutekelezeka ndani ya uwezo wetu. Tukumbuke nchi wahisani wakijitoa itakuwa hatari. Tukitumia madini yetu, kilimo, utalii na kadhalika, vyote hivi vinatosha kabisa kwa bajeti ya nchi yetu bila kutegemea wahisani. Kipaumbele viwanda vifufuliwe tuzalishe hapa nchini na tu-*export* nje, tuchukue mfano wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji, ningeshauri *tax-holiday* ya miaka mitano ipunguzwe la sivyo tunapoteza kodi nyingi sana unakuta wanabadilisha majini ya kampuni ili kukwepa kodi.

**MHE. MARTHA MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Tume ya Mipango haijaleta matokeo maalum mazuri kwa kuwa tumeona mkazo wa maendeleo umewekwa katika mikoa au kanda fulani tangu uhuru hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado haijateua Makamishna hadi sasa hivyo mambo hayaendi kwa kasi, je, itateuwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwe na ofisi za kanda ili Makamishna wawe karibu na maeneo husika badala ya kusubiri taarifa na takwimu maofisini. Mipango gani iliyopo kukabiliana na ongezeko la watu sawia na mahitaji ya elimu na afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ubinafsi limerudisha nyuma maendeleo ya maeneo mengine. Mfano, mtendaji anaweka mipango ya ujenzi wa kiwanda, au umeme, barabara na kadhalika kwenye eneo alilotoka au mkoa, ni mbaya sana iachwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa ulinzi wake, niwashukuru Mawaziri na watendaji kwa kuandaa mwongozo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo katika kuboresha bajeti ya Serikali ambayo inakabiliwa na mtikisiko wa uchumi wa dunia. Kwanza ni kuwezesha wananchi kiuchumi, ili kukabiliana na changa moto hii ni vizuri kuwe na uwezeshaji wananchi kiuchumi na ni vizuri fedha za mikopo ziwafikie wananchi. Mikopo mingi ya fedha inaishia mijini ambapo inasababisha mzunguko mdogo wa fedha katika uchumi wa nchi, ni vizuri maeneo ambayo hayana benki, taasisi zingine za fedha zitumike kutoa mikopo kama vile *SACCOS* ambazo zilishajenga uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la kilimo, mpango wa kuanzisha Benki ya Kilimo ni mzuri na kuiwezesha Benki ya Rasilimali (*TIB*), ni sawa lakini wakulima wadogo hawatafaidika. Tusipoweka mikakati mizuri mikopo hii itaishia kwa wakulima wakubwa na kuwaacha wadogo wanaendelea kama kawada. Ushauri wangu ni kuwa, Halmashauri za Wilaya/Jiji/Manispaa zipewe mamlaka ya kukopa fedha za kilimo au pembejeo za kilimo ili wao wawakopesheje wananchi katika maeneo yao. Tukifanya hivyo tutafanya mzunguko wa fedha ufike vijijini. Sasa hivi wakulima wengi wanahangaika sana hata kupata mikopo ya matrekta kwa sababu hawakopesheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo ni vema wananchi wamilikishwe ardhi haraka tena kwa vitendo. Kwa mfano unapopanga kupatia hatimiliki vijiji 30 katika Wilaya kati ya vijiji 121 ni lini umaskini utakwisha? Haya nimeyaona Wilaya ya Bukombe, hili halifai lazima Serikali iamue kwa dhati, mambo magumu yanahitaji maamuzi mazito/magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha juhudi za ukusanyaji mapato. Kkatika eneo hili Serikali iangalie maeneo mbalimbali ambayo yanapoteza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari, mfumo wa utoaji mizigo bandarini lazima ubadilike, wafanyabiashara wanatumia muda mwingi kwa ajili ya urasimu hii inapoteza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara na reli ziimarishwe na kuboreshwa ili wanaozitumia wasikate tamaa. Mfano Barabara ya Isaka – Kahama - Bukombe – Rwanda/Burundi ni mbaya sana haiwavutii wafanyabiashara. Kwa hali hiyo watumiaji wanakuwa wachache hapa tunapoteza uchumi/pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo wawekwe mfumo mzuri wa kuuza madini yao. Kwa kuwa hawana mfumo mzuri wanunuzi na wachimbaji hawalipi chochote kwenye Pato la Taifa na kwa kuwa ni wengi sana wanaweza kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri watafiti wa madini wakawekewa kiwango kikubwa cha kulipia mapato Serikali, kwani wanatafiti kwa muda mrefu ambapo hatuna imani kama huwa hawatuibii rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kubana matumizi, katika eneo hili waangalie matumizi ya Halmashauri za Wilaya, hata hivyo, Serikali inaweza kubana matumizi eneo la usimamizi wa miradi, hapa ndipo hela nyingi inatumika bila kuwa na *value for money,* miradi inakuwa si ya kudumu, hela zinazotumika ni nyingi hakuna ubora wa miradi. Hata hivyo yapo matumizi mengine siyo ya lazima ambayo hela yake wanaweza kuhamishia kwenye huduma za jamii pamoja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharakishaji wa kujenga miundombinu, umeme ni vema uharakishwe katika makao Makuu ya Wilaya na vituo vyote vya kibiashara ili kuharakisha maendeleo, barabara mfano Isaka – Kahama – Ushirombo – Lusumo, haifai kusafirisha mizigo ya jirani zetu, bila kuboresha tunapoteza mapato ya nchi. Ujenzi wa Reli ya Tanzania/Rwanda Serikali iharikishe ili kukomboa fedha za mizigo ya kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima isimamie mashirika ya umma kutoa gawio Serikalini isipokuwa yanayohusika na hifadhi za wanyamapori. Matumizi katika Mashirika ya Umma yako ovyo mno, Serikali ikisimamia vizuri mapato ya Taifa yataongezeka.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale kwa kuibuka mshindi kwa uchaguzi mdogo wa Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuweka kipaumbele katika suala la maji nchini. Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 ilitamka kuhakikisha maji yanapatikana vijijini kwa asilimia 65 na Mijini asilimia 90, lakini hali iliyoko nchini ni ya matatizo. Jimboni kwangu Tandahimba, Newala, Mtwara Vijijini na Jiji la Dar es Salaam, maji ni tatizo, ni vyema uamuzi wa makusudi wa kutumia fedha *ZA* ndani kupunguza tatizo hili ufanyike. Miradi ya wafadhili na wadau wa maendeleo inatucheleweshа.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mtwara uchumi wa Mkoa wetu utegemea sana barabara ya uchumi namba moja yaani Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi. Vikao vya *RCC* - Mtwara vilipitisha na kuomba Serikali (Wizara ya Miundombinu) kuanza kujenga kwa lami barabara hii. Ombi ni kwamba, barabara hiyo ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iamue kuwekeza katika kilimo kweli kweli kwa kuwekeza kwenye pembejeo na usindikaji wa mazao yetu ya kilimo (chakula na biashara) hapa nchini. Kwa kufanya hivyo tutaongeza thamani ya mazao yetu na hivyo kuongeza pato (*export levy*) tunapoyauza nje. Mfano, korosho zikisindikwa hapa nchini, kwanza tunawapa ajira wananchi wetu lakini pia thamani ya korosho hizo inapanda. Hivyo basi, Serikali ione uwezekano wa kusaidia wakulima kupata kwa urahisi zana za kubangulia mazao hayo kama vile mashine ya kubangulia korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ihakikishe pembejeo za kilimo zinawafikia kwa wakati wakulima wetu, hali ya sasa ya maeneo ya korosho ambapo

pembejeo za mwaka jana ndio kwanza zinafika leo.  Hiyo ni dalili tosha kuna mazao ya kilimo yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tuna vyanzo na ardhi nzuri ya kilimo, hatuna sababu ya kupata njaa kwani kama uwekezaji ukiwepo kwenye maeneo kama vile Rufiji *Basin* ukanda wa Mto Ruvuma toka Songea – Mtwara hadi Bahari ya Hindi na maeneo mengine hatuna sababu ya kutosonga mbele kwa kilimo au uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa kuwekeza na kutoa kipaumbele kwa bandari ya Mtwara ili usaidie kuongeza uchumi wetu kupitia nchi za Malawi, Zambia, Zimbabwe, Botswana na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati uwekwe kupunguza urasimu na masharti magumu kwenye mabenki yetu. Wilaya kama Tandahimba ina mabenki manne *NMB, CRDB* na *TACOBA (Tandahimba Community Bank)* Lakini wananchi hawapati mikopo ili kupunguza umaskini kwa sababu tu masharti ni magumu.  Ipo haja ya kuangalia upya mfumo mzima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi  kwa kazi nzuri sana ya kusimamia fedha, sera ya fedha na sera ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, natoa pongezi kwa mpango mzuri ulioainisha vipaumbele sahihi. Pamoja na pongezi hizi, nina ushauri wa kuboresha mpango wetu na bajeti ijayo 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa kwanza ni Serikali kuwekeza fedha nyingi katika maeneo ya uzalishaji wa uhakika kama vile bandari zetu, barabara zetu ikiwemo ya kati (kipande cha Kagoma – Muleba – Biharamulo – Lusahunga), reli na umeme (*energy*) ili kuchochea uzalishaji katika Sekta ya Kilimo na Ufugaji.  Aidha, nashauri fedha ya kutosha itengwe kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi mkubwa na mdogo. Nchi kama Namibia inategemea pia uvuvi.  Wavuvi wadogo wadogo kama wale walioko Ziwa Victoria wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili ni katika mpango wa dharura pamoja na Mikoa iliyoainishwa kwa lengo la kuzalisha chakula haraka. Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza wapewe fedha, mitambo, matrekta na pembejeo ili vijana wengi waliomaliza darasa la saba waende kufundishwa ulinzi, kilimo bora na stadi za kazi. Kwa upande wa Magereza, wafungwa wataweza kujilisha na kupata ziada ya kuuza katika ghala la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu ni kuandaa mapema hifadhi ya mafuta hasa wakati huu ambapo mafuta yameshuka bei.  Mapungufu katika hifadhi ya mafuta na uzalishaji umeme sio tu unaathiri uchumi, bali pia ni kuhatarisha usalama wa Taifa. *TPDC* wapewe fedha ya kutosha, Serikali irudi katika biashara kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa nne ni kuongeza mbinu kuvutia majirani zetu *DR Congo*, Rwanda, Burundi, Zambia, Uganda na Malawi kupitisha bidhaa zao kwenye bandari zetu *(transit trade).* Hii ni biashara yenye fedha nyingi na haihitaji fedha kama kilimo cha sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tano ni kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji ili tuachane na kutegemea mvua katika kilimo chetu. Naunga mkono mkakati wa Serikali kutafuta fedha nafuu kwa ajili ya maendeleo toka kwa marafiki zetu China, Japan, Mashariki ya Kati na India tukilenga kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa sita, ni kusimamia fedha inayopelekwa kwenye Serikali za Mitaa. Nitatoa mfano wa fedha ya ruzuku ya maendeleo iliyopelekwa Wilaya ya Muleba mwaka wa fedha 2007/2008. Serikali Kuu ilituletea fedha Sh. 3,965,473,534.87 kama ruzuku ya miradi ya maendeleo.

Pamoja na hizo kupitia mpango wa maendeleo ya jamii *(TASAF)* tulitengewa Sh.1,600,000,000/= maeneo mawili tu, haya yalikuwa na jumla ya Sh. 5,565,473,534/=. Kama Halmashauri ya Wilaya ya Muleba wangezingatia vipaumbele vya wananchi Elimu ya watoto wetu ikiwa ni kipaumbele namba moja, Afya, Maji na Barabara Vijijini. Pia, tusingekuwa na matatizo ya vyumba vya madarasa ya Shule za Sekondari zetu. Zingetengwa Sh.80,000,000/= kwa kila Kata, zingebaki Sh.3,165,473,534/= kwa ajili ya Maji, Barabara Vijijini, Afya na shughuli nyingine muhimu kama kuwezesha wananchi kuzalisha ili wapate kipato na kuondokana na umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia maeneo kama Muleba Kusini yataendelea kudidimia katika dimbwi la umaskini kwa sababu hatuna mifugo, hatuna viwanda, watu wanaongezeka, lakini ardhi kwa ajili ya kilimo hakuna! Tunahitaji viongozi wanaotambua umaskini wetu wa kipato na hivyo kutuwezesha kushiriki katika uzalishaji katika maeneo yetu kwa umwagiliaji. Tunaweza kuzalisha ndizi nyingi, maharage, mbogamboga, matunda, maziwa na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwapatia wananchi uwezo wa kununua *(purchasing power),* uchumi hauwezi kukua. Naishukuru Serikali kwa kutambua hili kama changamoto. Mpango mahsusi unahitaji kama vile Serikali kutenga fedha ya kununua mazao ya wakulima na kujenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata kuchangia kuhusu vipaumbele ambavyo nadhani vitasaidia sana katika hali na wakati tulionao. Lakini nafikiri pia kama tunaweza kupunguza gharama za utalii nchini tunaweza kushawishi wageni wengi ambao kipato chao kimepungua kuja kutalii Tanzania. Naamini idadi ya watalii ikiongezeka na ada zikalingana angalau na ada za Kenya tutafaidika kwani tuna vivutio vingi zaidi kiasi cha kuwavutia watalii kuja kwetu na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya maisha kwa Watanzania wengi leo ni ngumu sana na hasa kupanda kwa gharama za maisha, hivyo sioni sababu ya kuongeza kodi za ndani kwa kupandisha viwango vya kodi ambazo tayari ni kubwa na Watanzania wengi wa kawaida wanalalamika sana. Ni vyema sasa tukaangalia misamaha holela kwa bidhaa na kodi kwa makampuni na hususan Sekta ya Madini. Tunapoteza fedha nyingi kutokana na misamaha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi, tumeshuhudia katika nchi hii namna uvuvi holela uliofanywa katika Ziwa Victoria. Uvuvi ambao haukuwa endelevu hata kidogo ambapo leo unatugharimu sana kwa doria na kadhalika. Lakini uvuvi huu umesaidia Taifa kwa kiasi gani? Ulikuwepo udanganyifu mkubwa na kupoteza fedha nyingi kama kodi.

Tumesikia gari na trela tani 40 walikuwa wanaandika tani nne na ukwepaji huu wa kodi haukudhibitiwa. Mpaka leo hatuna samaki wa kusafirisha tena. Basi ni vyema sasa tukawekeza katika Uvuvi katika bahari kuu na mkakati wa makusudi kwa Ziwa Tanganyika ambapo raslimali iliyomo katika ziwa hilo haijavumbuliwa. Pengine ni kwa sababu ya kina cha ziwa lenyewe ilivyo, utafiti wa kina wa zana bora zinazofaa kwa uvuvi katika Ziwa Tanganyika na kuwasaidia wavuvi wadogo na kuboresha mfumo wa masoko. Leo samaki wengi wanaovuliwa wanauzwa Zambia (samaki wabichi) na samaki wakavu Congo na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nadhani ipo haja pia ya kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo vya kuimarisha *SIDO*. Nadhani badala ya kuendelea kupanua wigo wa wachuuzi wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo kupitia mifuko ya Mheshimiwa Rais (*JK Fund*) na *SACCOS* sasa tuelekeze katika viwanda vidogo vidogo ambavyo mwisho wa soko Serikali itapata kodi toka viwanda hivyo na kwa sasa hawakusanyi kodi kutoka kwa maelfu ya wachuuzi ambao wamezagaa nchi mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa kuwekeza katika viwanda hivyo, watu watapata ajira angalau watu wawili kuliko ilivyo sasa ambapo ni kumwezesha mtu mmoja mmoja lakini pia nitahadharishe kwamba tuwe makini sana kwa aina ya viwanda hivyo na maeneo ya viwanda hivyo kwa kuzingatia malighafi zinazopatikana katika kila eneo. Naamini tutapiga hatua katika vita hii ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa maelezo yake mazuri aliyoyatoa kwa ufasaha. Nina mchango kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu tumekubaliana kuwa yapo maeneo tukiyasimamia na kuyaendeleza tutaweza kuondokana na umaskini uliokithiri. Maeneo hayo kwa ufahamu wangu ni Elimu na Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, kwa miaka mingi sasa tangu uhuru nchi yetu imekuwa ikiwekeza sana katika Sekta. Uwekezaji huu hata hivyo haujawa endelevu, umekuwa ukikatikakatika. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni tumezinduka na kwa ushirikiano wa hali ya juu wananchi, Serikali na wafadhali tumeshikamana sana katika uwekezaji huo. Kwa maoni yangu kumesogeza kidogo lakini tumeanza kulegeza kamba tena hata kabla ya kulifikia tena lengo letu. Wafadhali, Serikali na hata wananchi wote wanaelekea kukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri katika mipango yetu ya mwaka huu tushirikiane tena kwa kufumba macho hapa tunapoelekea kuchoka tupavuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusambaza umeme na maji vijijini kwa nini tumejenga shule nyingi sana vijijini? Shule hizi hazina umeme wala maji. Vyote hivyo ni vivutio vikuu vya walimu kubaki na kufanya kazi vijijini. Ni vyema katika mpango huu kama wendawazimu tuelekeze nguvu zetu tena kwa wingi katika kufikisha shule zetu nyingi kama sio zote umeme na maji. Tukiamua, inawezekana kabisa. Hii ni muhimu kwa kuwa miundombinu ya elimu, madarasa na nyumba za walimu za kuanzia tayari tunavyo, wanafunzi tunao wa kutosha na walimu tunao. Tatizo tulilonalo ni jinsi ya kuwaweka walimu mashuleni hasa vijijini. Shule bila walimu haiwezi kutoa matunda yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, elimu vijijini inaathiriwa sana na upungufu wa walimu wanaopangwa na kushindwa kubaki huko kutokana na kukosekana kwa umeme na maji. Ni vyema katika mpango wetu tukaweka usambazaji wa umeme na maji. Ni vyema katika mpango wetu tukaweka usambazaji wa umeme na maji vijijini kama moja ya vipaumbele kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara vijijini, kazi hii imefanyika kwa kiwango cha juu. Serikali iweke katika mpango wa mwaka ujao 2009/2010 ukamilishaji wa ujenzi wa barabara katika maeneo ambayo hayana barabara hizo hususan maeneo ambako shule hazifikiki kwa urahisi. Jambo hili litachangia sana watumishi kukaa vijijini wakiwemo walimu. Barabara vijijini pamoja na kuwa motisha kwa watumishi mbalimbali kukaa vijijini yatachangia sana katika kusafirisha mazao mashambani na bidhaa za viwandani kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na kurahisisha bei ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja umeme, maji na barabara vijijini vikipewa kipaumbele katika mpango huu vinaweza kuchangia uanzishwaji wa viwanda vidogo vijijini, ajira vijijini na kupungua kwa kiwango sehemu vijana kutoka vijijini kwenda mijini jambo linalopunguza nguvukazi vijijini ambako kimsingi ndiko kuliko na maeneo ya uzalishaji wa mazao mashambani na utumiaji wa bidhaa za viwandaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naupongeza mpango huu ambao kimsingi kwa kuzingatia mazingira ya nchi yetu na ya dunia nzima, hatuna jinsi, ni lazima tukubali kwenda nao na hasa vipaumbele vikipangwa kama nilivyoshauri japo kwa miaka miwili ijayo kuanzia na mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukihangaika mara kwa mara kama Taifa kupambana na mfumuko wa bei, kupanga kwa gharama za usafirishaji na kadhalika kutokana na bei ya mafuta duniani. *Fluctuations* za bei ya mafuta imetuathiri mara kwa mara na itaendelea kutuathiri kwa sababu hatuna *control* ya mafuta na bei zake.

Kwenye mpango wa bajeti hakuna mkakati wowote unaonyesha nishati mbadala ili hatimaye tupunguze matatizo ya nishati ya mafuta ya *diesel* na hata umeme. Zao la Jatropha halizungumzwi kabisa. Nishati hii mbadala inatumika Philippines, Brazil, Malaysia, India na Barani Afrika nchi ya Mali imeanzisha zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wanasema (a) *Jatropha is resistant to drought and pests, and produces seeds containing up to 40% oil. When the seeds are crushed and processed, the resulting oil can be used in a standard diesel engine, while the residue can also be processed into biomass to power electricity plants.*" (b) *Jatropha can also be intercropped with other cash crops such as coffee, sugarcane, fruits and vegetables.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini tuko kimya juu ya zao hili? Kuna taarifa kuwa viwanda viwili vinajengwa Rukwa na Arusha vitakavyosindika zao la Jatropha. Sasa kwa nini kimya kimya wananchi hawatayarishwi kulima zao hili muhimu?

Mhesimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha miundombinu ya barabara na reli ni muhimu sana, lakini inasuasua kwa kukosa fedha za kumalizia miradi ya barabara na kurekebisha reli zetu. Mfuko hai ni barabara ya Dodoma – Manyoni na Manyoni – Isuna. Barabara hizi zimekwama kumalizika kipande cha kilometa 14 tu kuingia Manyoni. *Contractor* (Konoike) amesusia kumaliza kwa kukosa malipo katika muda unaostahili. Tumeshuhudia kuunganisha nchi yetu kwa barabara ya kati kwa umbali wa kilometa 54 + 14 = 68 tu. Reli zetu ziko hoi! Hivi karibuni Kenya na Uganda wameamua kujenga kwa pamoja reli ya Mombasa – Kampala upya. Je, sisi tuna mipango gani katika hili? Maana wenzetu wakikamilisha reli yao, basi Bandari ya Dar es Salaam itakuwa hoi zaidi. Nashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha katika miundombinu ya barabara na reli. Barabara ya Mayoni – Itigi – Tabora – Kigoma (ipewe kipaumbele) na barabara ya Mkiwa – Itigi – Chunya – Mbeya (ipewe kipaumbele).

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha maji ni muhimu pia. Pamoja na Serikali kutoa fedha nyingi kuwapatia maji wananchi, fedha hizi zimeishia katikati hazikuzaa matunda. Wataalam wa maji wameangusha wananchi. Nashauri fedha itakayotengwa ni vyema ikabidhiwe vijiji vyenyewe, vitafute wataalam wao wa kutafiti maji na kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza Serikali inunue majembe ya plau na kuwakopesha wananchi plau na jozi za mifugo ya kulima kuliko kukimbilia zaidi *power*

*tillers* na matrekta, hawana uwezo wa kuyatunza matrekta na gharama zake za mafuta na spea.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri azingatie mependekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi isipokuwa lile la kurejesha Tume ya Mipango, badala yake tuige mfano wa Rais Barack Obama wa *America*. Yeye ameunda makundi ya wataalam waliobobea *(top experts, best brains)* kushauri hatua gani zichukuliwe kufufua uchumi wao. Mfano, nini kifanyike kuhusu fedha/mabenki nishati na nishati mbadala, mazingira, maeneo yenye migogoro kama vile Israel, Gaza, Afghanistan, Iran na kadhalika. Hayo makundi *(task forces)* yanatoa *practical, doable, recommendations* sio nadharia.

Hapa kwetu yapo makundi yenye mawazo ambayo baadhi tayari yamejadiliwa, mfano na Tanzania *Private Sector Foundation*, *CTI*, *TCCIA* na kadhalika, *BoT* wangeweza kuratibu makundi hayo na kusimamiwa na Hazina moja kwa moja. Mawazo ya makundi/Hazina yangepelekwa *BLM* (ikibidi) na kuingizwa kwenye Bajeti ya 2009/2010 au kuelekezwa kwa *specific private sector.* Nilipokuwa Hazina nilifaidika sana na *task force* maalum kuhusu hatua za kodi ambayo ilichanganya wasomi na wataalam waliopo kwenye kazi mbalimbali wanaofahamika kwa uwezo wao.

Tusiyumbe kuhusu barabara za aina zote hasa Magharibi mwa nchi na zile zinazoibua uchumi na kuwezesha usafirishaji wa mazao na watalii.

Tusilegeze uwekezaji kwenye Elimu. Hivi sasa hatuwekezi vya kutosha hasa kwenye kufundisha walimu, kuwa na vitendea kazi kufundishia mfano vitabu, maabara na mishahara. Nchi haitaendelea na uchumi hautakua bila *skilled manpower* kwa ngazi zote..

Nawasilisha ushauri kuunga mkono.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa kuzingatia msukosuko wa uchumi wa dunia na madhara yake.

Katika kukuza mapato ya nchi, kuna haja ya kuangalia sana suala la nchi kuendelea kuvutia wawekezaji kutoka nchi rafiki ambazo hazina rekodi ya kuwekeza hapa nchini. Nashauri Mikoa ipewe msukumo wa kufanya kazi hiyo ya kuwavutia wawekezaji. Makongamano ya uwekezaji yamefanyika lakini la muhimu Serikali iziwezesha Ofisi za *TIC* Mikoani ili zifanye kazi. Hata hivyo, ni muhimu kuondoa *Bureaucracy* ya katika zoezi la kuwaandikisha wawekezaji kabla hawajatekeleza miradi yao. Ucheleweshaji huu unawakwaza wawekezaji na hivyo kupunguza mapato.

Kuhusu chakula, Serikali imetoa mpango mzuri wa kuichagua Mikoa muhimu kwa uzalishaji wa chakula. Naomba kusisitiza usafirishaji wa chakula kutoka vijijini kuelekea Mijini kwa kuweka utaratibu mzuri. La sivyo, suala la *inflation* hatutakuwa tumelitatua. Chakula kisambazwe kwa wakati.

Mwisho, nashauri Serikali ianze utaratibu wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa maeneo yote yanayozalisha chai kwani wakulima hao wanalitegemea sana zao hilo badala ya nafaka. Wilaya hizo ni pamoja na Rungwe, Njombe, Mufindi na Lushoto. Uchangiaji wao katika pato la Taifa ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Serikali kwa kuiweka Sekta ya Maji kuwa Wizara ya Kipaumbele kwani itapunguza malalamiko ya wananchi kuhusu upatikanaji wa maji safi. Ni mategemeo yangu kuwa ifikapo mwaka 2010 tatizo la maji ya kunywa na ya umwagiliaji litapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta mapendekezo haya. Naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kuhusu Kilimo, mageuzi ya kilimo ni muhimu sana na upatikanaji wa pembeljeo za kilimo ni muhimu sana. Hivyo, wananchi wapatiwe pembejeo za kilimo na zana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji wa wanyama wadogo wadogo kwa familia duni utiliwe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaalam wa ugani, wataalam wa kilimo/ugani waendelee kupata mafunzo na kuajiriwa ili waendelee kutoa elimu ya kilimo bora vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanawake kuwezeshwa, uwezeshaji wa jamii utiliwe umuhimu. Naipongeza Serikali kuanzisha Mfuko wa uwezeshaji (fedha za JK). Umuhimu utolewe kwa *SACCOS* za wanawake wa vijana ili waweze kufanya shughuli za kiuchumi na uzalishaji. Mtaji imekuwa ni tatizo kubwa ili tuweze kuwakomboa katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme vijijini, ili kuwezesha wananchi/vijana kubaki vijijini wa kuweza kujiajiri ni lazima suala la umeme vijijini litiliwe umuhimu kwani viwanda vidogo vidogo vinaweza kuanzishwa na kuweza kusaidia vijana na wananchi kujiajiri. Shirika la *SIDO* liongezewe raslimali ili liweze kutoa mafunzo mbalimbali kwa wananci ikiwa ni pamoja na mafunzo ya ujasiliamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananachi wawezeshwe kwa kupatiwa mikopo. Benki kuu watusaidie (wananchi) ikiwa ni wavuvi, wakulima, wafugaji. Wakiwezeshwa ndipo ufugaji utaboreshwa, uvuvi utaboreshwa na kilimo kitaimarishwa na miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kitapanuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ni kiungo muhimu kwa ajili ya kutuletea mapato nchini. Hivyo, bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Kigoma ziendelezwe na ziboreshwe pamoja na reli ya Kati, barabara na viwanja vya ndege

Mheshimiwa Naibu Spika, vianzishwe viwanda ambavyo vitaleta ajira na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Madini tunayo mengi, dhabaru ni nyingi, nguvu ielekezwe kwenye kuongeza thamani ya madini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwapongeza Waziri na Manaibu Waziri wote wawili kwa utendaji mzuri na wataalam wote katika Wizara

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mustafa H. Mkulo - Naibu Waziri Mheshimiwa Omary Mzee - Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa mpango mzuri wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho Na. 29 naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wa mawazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi zaidi, ni vyema Serikali kuu iangalie jinsi ya kuharakisha ruzuku kwenye Halmashauri, Manispaa ili kuondoa kero kama wananchi na kuleta maendeleo mara tu baada ya bajeti kupitishwa na Bunge kwa kuangalia maeneo ya lazima kama afya, elimu, miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa kodi kwenye Halmashauri na Manispaa Serikali iangalie sheria ndogo ndogo ambazo zitaruhusu ukusanyaji wa kodi kwa biashara zinazotakiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti/mipango hii iangalie jinsi ya kuelekeza wawekezaji kwenye maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo. Kwa mfano Mkoa wa Tabora uko nyuma ingawaje ni Mkoa wa zamani na ni mkongwe. Mkoa huu uko nyuma kimaendeleo kwa kukosa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni miundombinu, kufungua Mkoa wa Tabora kwa kukamilisha barabara ya kutoka Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma kwa kuweka lami, kufungua barabara ya Tabora – Sikonge – Rungwa – Mbeya, kufungua barabara za ndani Sikonge – Urambo – Kaliua – Kigoma, kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege ambacho mpaka sasa kiko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhudu reli, Serikali iongeze bidii kwa kusaidia kuboresha huduma ambayo imezorota kiasi kwamba ni kheri hata ilipokuwa chini ya *TRC*, Serikali iangalie upya mishahara yao ili kusiwe na migomo baridi. Mpaka sasa Tabora iko kisiwani kwa kukosa usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji, Tabora ina bwawa ambalo limejengwa tangu ukoloni ambalo hivi sasa halikidhi mahitaji ya wananchi kutokana na ongezeko la watu, (Igombe). Huduma hii kukosekana ni kero kwa wananchi kwa kukosa maji safi na salama. Katika mpango huu, ni ombi langu kwamba ifikiriwe kukamilisha upanuzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, Serikali katika mpango wake wa bajeti iangalie jinsi ya kusaidia madeni ya wakulima na tumbaku na madeni ya pamba kwani deni hili ni la muda mrefu kiasi kwamba wamebebeshwa wakulima badala ya vyama vya msingi. Ni vyema kuwa na mpango endelevu wa hali ya kutayarisha chakula kwenye maghala kutokana na hali ya hewa kubadilika ili wananchi wasife njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo ya Shule za Sekondari/Msingi ambazo zimefikia hatua ya lenta kwani karibu Tanzania nzima kuna hali hiyo. Tathmini ifanyike ili kuona hali halisi kabla ya kupitisha makadirio ya bajeti ya mwaka huu ili gharama zake ziingwe, kuhakikisha madai ya walimu yaliyobaki yanatekelezwa kabla ya 2010 kwa kada zote, kuhakikisha ukamilishaji wa maabara mashuleni.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali ya uchumi hivi sasa duniani naomba kuishauri Wizara ya Fedha ipange mpango wa bajeti kwa mkakati ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa mapato ya Serikali yatapungua ni lazima tuwekeze kwenye *economic drivers* na tupunguze matumizi kwenye sekta za huduma. Tuwekeze kwenye sekta ya usafiri bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege, kilimo katika kupunguza matumizi kwenye sekta ya huduma, tukubali kuwa na shule chache na zahanati/vituo vya afya vichache katika taasisi za elimu chache tutakazokuwanao zitoe huduma bora. Ni vyema kuwa na *Engineer* wachache kuliko kuwa na *University Graduates* wengi wasio *competent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tuweke mkakati mzuri wa kuhakikisha kila mtu anafanya kazi, kwa hakika kufanya kazi iwe lazima. Mtu asiruhusiwe kumnyonya mwenzake, vijana wasiruhusiwe kuwa kijiweni kwa kisingizio kuwa ni wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tusaidie wawekezaji wa ndani ili uchumi umilikiwe na Watanzania,

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tufute misamaha ya kodi isiyo ya lazima hasa kwenye madini na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, tulinde wazalishaji wa ndani kwa kuweka kodi, mfano mafuta ya kula toka nje sasa yatozwe kodi kubwa ili wakulima wetu wa alizeti na

pamba wanufaike. Tusiendekeze hofu kuwa mafuta ya kula yametoka nje hivyo kuweka kodi ni kuwaumiza walaji wengi. Hii sio kweli, mbona mafuta ya petroli yanatozwa kodi na maisha yanaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, tupunguze matumizi yasiyo ya lazima ndani ya Serikali, magari ya kifahari na uagizaji wa samani toka nje upigwe marufuku. Wakuu wa Idara katika Wizara watumie gari ndogo na ikiwezekana gari za 4 x 4 ziwe chache kwenye *pool* na si kila mtu yake. Pia matumizi ya semina na warsha na safari yapunguzwe.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Manaibu wake na watendaji wote katika Wizara ya Fedha na Uchumi kwa matayarisho mazuri ya mwongozo wa mpango wa bajeti 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, nilipata fursa ya kuchangia rasimu ya mpango huu na mawazo yangu mengi yamo katika taarifa ya Kamati yetu iliyowakilishwa Bungeni na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kusisitiza jambo moja muhimu kuhusu hali mbaya za huduma za reli ya kati ambayo ikirekebishwa itakuwa ni ufumbuzi mkubwa wa matatizo yetu ya upungufu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Reli ya Tanzania ambayo inamilikiwa kwa ubia baina ya Serikali asilimia 49 na Kampuni ya *Rites* (India) asilimia 51. Kampuni hii ina tatizo kubwa la upungufu wa fedha za kujiendeshea *(working capital).* Hali hii inatokana na ukweli kwamba kampuni hii ilianzishwa ikiwa na mtaji mdogo sana (shilingi bilioni 20.0) ikilinganishwa na majukumu iliyotarajiwa kuyakidhi kwa kutumia vitendea kazi vikukuu (vibovu) ilivyorithi toka Shirika la Reli la Tanzania *(TRC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya Serikali na Kampuni ya Reli *(TRL)* ilikuwa kupata mkopo hata *IFC* (Benki ya Dunia dirisha la sekta binafsi) wa $ 44.0 milioni. Kutokana na kuchelewa kwa kukamilisha masharti ya kupata mkopo huo mpaka leo ni Dola milioni 14.0 tu ndizo zilizokwishatolewa lakini ni Dola milioni 7.0 tu kati ya hizo ndizo ambazo zimeanza kutumiwa na *TRL*. Kwa hiyo, mpaka leo vitendea kazi (injini, mabehewa, reli na kadhalika) havijatengenezwa kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba *TRL* haina vitendea kazi vizuri vinavyokidhi uendeshaji mzuri wa shughuli za usafirishaji wa bidhaa na abiria. Hivyo kufanya mapato ya kampuni kuendela kudidimia na kwa hiyo, kushindwa kumudu kukabiliana na kazi kubwa ya kubeba bidhaa na abiria kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba Serikali ihakikishe tatizo la upungufu wa mtaji/*working capital* ya *TRL* linapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Aidha, wabia waliopo wawe tayari kuongeza mchango wao wa mtaji au watafute mikopo rahisi na ya muda mrefu toka ama Benki ya Dunia au nchi marafiki kama India ambayo

tayari imekwishaonyesha dhamira ya kuikopesha nchi yetu kiasi cha kama Dola milioni 83.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wabia wa sasa wanaweza kuikaribisha *IFC* kama mwekezaji na mkopeshaji. Hali hii inaweza kutokea tu kama wabia wa sasa Serikali na *RITES* watakuwa tayari kupunguza hisa zao na kuzimia kwa *IFC* hususan kama *reference and redeemable shares*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Serikali pamoja na ushauri niliyoutoa hapo juu na katika Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAM A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini kuna maangalizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sikuona mahali katika mpango panapozungumzia masuala ya ulinzi na usalama, sio tu katika matumizi ya kawaida, lakini pia katika mipango ya maendeleo. Ulinzi na usalama wa Taifa hauwezi ukawa unategemea mataifa ya nje. Hili ni lazima Taifa lenyewe lijitegemee!

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kiwango cha akiba ya Taifa katika maeneo yafuatayo:- chakula, kiwango cha hifadhi *(SGR)* ya tani 100 haitoshi, hicho ni chakula cha dharura na sio akiba. Tanzania inahitaji kiasi cha tani milioni 10 kwa mwaka. Angalau tuanze na tani milioni moja kwa mwaka na kiasi hicho kiwe kinaongezwa ili hatma yake tuwe na akiba ya chakula cha miaka mitano mpaka hata kumi na kuendelea. Vivyo hivyo mafuta ya magari na mitambo. Akiba ya Taifa ya mafuta iko wapi? Hatuwezi kutegemea fadhila za akiba ya wafanyabiashara binafsi! Suala la kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta limepotelea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kigeni akiba yetu inayotosheleza mwezi wa tano haitoshi, tuendelee kuweka akiba angalau itosheleze mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mwongozo wa utayarishaji wa mwongozo mpango na bajeti una nia nzuri, lakini nia tu haitoshi, ni lazima utekelezeke na ilivyo hivi sasa upo uwezekano wa kushindwa kufikia baadhi ya malengo ya Ilani ya CCM 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE.LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi, hakuna *cordination* kati ya taasisi za Serikali katika kumsaidia Mtanzania wa kawaida kiuchumi. Hili tunaendele kuleta urasimu usiomsaidia mwananchi kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kujenga miundombinu ya barabara na reli ili kufungua Mikoa iliyoko Magharibi Rukwa, Kigoma, Tabora, Shinyanga na pia kuunganisha na nchi jirani za Malawi, Zambia, Congo, Burundi, Rwanda na Uganda ili tufanye biashara ya uhakika na nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kipewe msukumo unaotakiwa ili tuondokane na jembe la mkono ili tulime zaidi tupate mbolea kwa wakati mitaji ya kutosha katika kilimo toka taasisi za fedha ili mkulima apate uwezo wa kununua matrekta ili tuwe na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila umwagiliaji uliopangiliwa vizuri, uliojengewa miundombinu bora bila kutumia wataalam walioelimishwa na Taifa ili kuwasaidia Watanzania, wakulima wadogo na maskini hatutajinasua na njaa. Tujifunze toka China, Malasia, Indonesia na Vietnam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa karne ya mwanzo wa kuumbwa dunia unaoendeshwa na wafugaji wanaohamahama na kusambaa nchi yote ya Tanzania na kuonekana kama wafugaji wana haki ya kuharibu mazingira ya nchi hii bila kukemewa na wakulima hawana haki yoyote mbele ya wafugaji, basi balaa katika nchi hii, njaa na migogoro itatufuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme upatikane kwa uhakika katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma ili mazao ya Mikoa hiyo yasindikwe ili kuongeza thamani ya mazao hayo na kupata pato zaidi kwa wakulima maskini wa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu iboreshwe kwa kiwango cha juu ili iwanufaishe Watanzania wote na siyo kuwakosesha watu wa Magharibi kwa kutopata fedha za kutosha ili kuboresha elimu katika Mikoa iliyo nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ENG. STELLA MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu Waziri wake bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa kuleta mpango huu ambao nauona ni makini na upo katika sura ya *macro level*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona sasa wakati umefika wa kumnenepesha ng'ombe ili tumkamue maziwa. Nimejifunza kuwa mipango yetu mingi ni ya matumizi katika kuongeza pato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kufunga mikanda na kuchagua mipango michache ya kutekeleza kwa mwaka na inayoweza kupimika.

Sisi Wabunge ni wajibu wetu kusema mengi lakini hebu tuseme tutatoa kipaumbele kwenye barabara, bandari, umeme, *information/data base* (*IT*) ili kuongeza uwigo wa kulipa kodi, pamoja na ku-*finalize small business date base* ya watu ili kuainisha watu wenye uwezo wa kulipa kodi na nchi zinazostahili kulipwa kodi; kupunguza msamaha wa kodi; kuongeza maeneo ya kuchangia elimu kutoka kwa wadau

wa ndani ili pesa kidogo toka nje zisaidie mengine na kuhakikisha uanzishwaji wa mipango ya maendeleo vijijini utakaowawezesha wananchi kuiona fursa zilizopo kwenye maeneo husika. Hii ni mbali na mipango mizuri uliyoainisha Mheshimiwa Waziri.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi juu ya mwongozo wa mpango wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2009 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali halisi ya sasa duniani, naomba tuzingatie mambo yafuatayo:-

Kwanza, tuongeze uzalishaji wa chakula cha kutosheleza mahitaji yetu na ziada ili ili Taifa lisitumie *resources* zake kuagiza chakula nje wakati uwezo wa kuzalisha tunao sana. Hivyo nashauri bajeti ya Wizara ya Kilimo iongezwe mpaka ifikie asilimia 10 kama ilivyo katika makubaliano ya nchi za *SADC*.

Pili, mpango wa sasa wa *voucher system* uendelee, lakini ifanyike tathmini ya utekelezaji wa mpango huu na kupanua wigo ili wakulima wadogo wengi wafikiwe katika Wilaya zinazohusika. Tathmini itamsaidia kupunguza yafuatayo:-

Uuzaji wa vocha kwa baadhi ya wakulima; ucheleweshaji wa makusudi wa vocha; malipo ya mawakala; Kamati za ugawaji ngazi ya Kijiji/Mtaa kuwa na upendeleo na baadhi; viongozi kuficha pembejeo/vocha na kuongeza nguvu ya *Minjingu phospates* ili ifikie nguvu inayokaribiana na *DAP*.

Tatu, vituo vya utafiti viboreshwe kwa kupatiwa vitendea kazi muhimu pamoja na maslahi mazuri ya watafiti yaboreshwe bila utafiti, hatuwezi kufuka popote.

Nne, mfuko wa pembejeo (*agricultural inputs fund*) upatiwe fungu maalum kutoka Hazina na upatiwe fedha zinazolingana na mahitaji ya wadau. Kuwepo kwa mfuko imara, utafanya zana za kilimo mfano matrekta yapatikane kwa urahisi, hili litatusaidia katika mapinduzi ya kijani.

Tano, Serikali ionyeshe dhamira ya wazi juu ya ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea kwa kutumia malighafi *phosphates* kule Mbeya na Mpanda. Pia gesi kwa ajili ya mbolea za chumvi chumvi (mfano *urea* na kadhalika) Kiwanda cha Mbolea kitatusaidia kutotumia fedha za kigeni kuagiza mbolea toka nje.

Sita, mbinu madhubuti zibuniwe kukabiliana na mtikisiko/msukosuko wa kiuchumi na kifedha duniani. Hali iwe *monitored* kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri,

Waheshimiwa, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam kwa utayarishaji na utoaji mwema wa mwongozo wa mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri katika hali ngumu ya uchumi duniani hapana budi kuwa makini zaidi katika kuandaa na kupanga mipango na bajeti ambayo itatunusuru kutetereka kwa uchumi wetu; kurejesha na hatimaye kuendelea kwa kasi kubwa zaidi malengo tuliyojiwekea chini ya dira ya maendeleo ya Taifa 2025; Mkakati wa Taifa wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo umeainisha vipaumbele stahiki na sahihi katika jitihada za kuuhamisha kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia maeneo machache ambayo hayakuchangiwa vya kutosha na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kabla yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, urari wa bidhaa na huduma, nakisi ya urari wa biashara umeongezeka kwa asilimia 34.2. Changamoto hii sugu itaendelea kuongezeka makali yake endapo hatua thabiti hazitachuliwa kutekeleza kwa umakini na kiwango cha juu mipango na vipaumbele tunavyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya dhamira na ya muda wa kati iliyoainsihwa katika kurasa tisa hadi kumi na moja za mwongozo ni sahihi na zitasaidia sana kuongeza tija, uwingi na ubora wa bidhaa na masoko na hivyo kuchangia kupunguza urari wa biashara endapo zitatekelezwa ipasavyo. Lakini shida kubwa tuliyonayo hapa Tanzania ni kuandaa mipango mizuri bila kuitekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele katika mpango wa bajeti 2009/2010 – 2011/2012 ni sahihi kulingana na malengo yetu ya Dira ya Taifa 2025 malengo ya Milenia na *MKUKUTA* lakini tutatekeleza ipasavyo. Ningependa hapa kufanya mapitio ya vipaumbele na kuona jinsi ambavyo tumefanikiwa au kusuasua katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu, miaka nenda rudi tumezungumzia kuhusu ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro kwa kiwango cha lami, lakini hadi leo utekelezaji wake unasuasua, uimarishaji wa reli ya Tanga – Arusha na Ruvu – Mnyuzi pamoja na ujenzi wa reli mpya ya Arusha – Musoma ni kitendawili kisicho kifani na ujenzi wa bandari mpya ya Tanga kule Mwambani haujatajwa kabisa miongoni mwa vipaumbele.

Pamoja na kuainishwa katika bajeti na kutengewa fedha katika bajeti ya 2008/2009, uwekaji umeme vijiji vya Daluni, Gombero, Kwale na Vuga bado unasemekana unatafutiwa fedha na haifahamiki bado ni lini utekelezaji utaanza, ingawaje jitihada za kusisimua na kuwa na masoko ya uhakika ni pamoja na kujenga masoko ya Kimataifa ya Segera na Makambako. Ahadi hii ya Serikali ya muda mrefu haina dalili ya kutekelezwa kwa siku hizi za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji, mwongozo kuhusu uzalishaji kwa Sekta ya Kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, kuendeleza ujuzi wa utaalam, madini na huduma ya jamii kama ulivyo katika ukurasa wa 14 – 16 ni barabara kabisa, lakini ni muhimu kuhakikisha kwamba hayo yote kwa kiasi fulani yanafikia Mikoa na Wilaya mbalimbali licha ya mkazo maalum kwa Mikoa minane yenye kipaumbele maalum kwa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwezesha viwanda vidogo na vya kati (*SMEs*) hapana budi kuzipa taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda kama vile *SIDO*, *TIRDO*, *CARMATECH*, *TEMDO*, *TBS* na Taasisi za Udhibiti kama vile Tume ya Ushindani, Baraza la Ushindani, Barala la Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, *EWURA*, *SUMATRA* na kadhalika, uwezo kisheria kifedha na kiutaalamu kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuwezesha kwa hali ya juu Taasisi za Kimkakati kama vile *TPDC*, *TANTRADC*, *TANESCO*, *NDC*, *ATCL*, *TTB*, *TIC*, bandari, *TRCL* kutekeleza wajibu wao wa kukuza, kuendeleza na kutuongoza ipasavyo katika shughuli zilizo chini ya mamlaka zao.

Sera ya kutotoa ruzuku kwa taasisi kama hizi sio sahihi. Inapobidi, sera na sheria zinazohusu taasisi hizi zitazamwe upya ili ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo wa *monitoring* and *evaluation* wa mpango wa bajeti ni muhimu sana. Kwa mantiki, nashauri pawepo na mfumo mahsusi wa kupanga mipango na malengo kwa kila sekta na ngazi. Malango na mipango hiyo ifuatiliwe na kutathminiwa na hatimaye pawepo motisha za kuwazawadia wanaofanya vizuri. Kwa hili, ni vyema pia pakawepo na msisitizo mkubwa kuhusu mikataba ya kazi na tathmini *(OPRAS na Client Performance Charter)* ili kuongeza ufanisi, ushindani, changamoto na uwajibikaji. Aidha, kuupunguza kwa kiasi kikubwa umangimeza (urasimu hasi).

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini yaliyomo katika mwongozo na mengi yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge yakizingatiwa ipasavyo, Taifa letu litavuka salama katika msukosuko wa kiuchumi unaoikumba dunia hivi sasa na kusonga mbele kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niombe radhi kwa yaliyotokea jana kwamba, ilibidi Kikao cha Bunge kiahirishwe saa 11.05 kwa sababu mimi mwenyewe na Naibu Mawaziri wangu, wote hatukuwepo. Tulikuwa tumejipanga vizuri, lakini nadhani ni bahati mbaya tu ilitokea. Kwa hiyo, kwa ujumla wake, Waziri Mkuu ameomba radhi asubuhi na mimi naomba niongezee kuomba radhi, kwa haya yaliyotokea na sidhani kama yatatokea tena.

Kwa mara nyingine katika kikao hiki cha Bunge, Waheshimiwa Wabunge, wamepata nafasi ya kujadili kwa kina Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2011/2012. Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kuongoza kwa hekima kubwa mjadala wa Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha muda wa kati. Kwa kiwango kikubwa, busara zako na za Spika zimetuwezesha kupata maoni ambayo yataboresha mwongozo huo.

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao ambayo itasaidia sana katika kukamilisha mwongozo huo. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, pamoja na Kamati nzima ya Fedha na Uchumi na Kaimu Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Fatma Fereji, kwa michango yao muhimu sana na ambayo inasaidia sana katika kuboresha mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujadili Mwongozo wa Utayarishaji Mpango wa Bajeti ya Serikali, Waheshimiwa Wabunge wamepata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:-

Kwanza Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi walikuwa wengi sana nao NI wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Dr. Harrisson Mwakyembe, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda, Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Janet Massaburi, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni  Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyiy, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, amewasilisha maoni ya Kamati ambayo nakubaliana nayo yote.  Baadhi ya mambo hayo ni haya yafuatayo:  Kwanza, kuundwa kwa Tume ya Mipango, ambako pia kumechangiwa na Wabunge wengine akiwepo Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, mchakato wa uundaji wa Tume uko katika hatua za mwisho.  Ni matarajio ya Serikali kuwa, Tume itaanza kazi mwanzoni mwa mwaka wa fedha ujao.  Tume itakayoundwa ni tofauti na Tume zilizoanza kuundwa huko awali; Tume hii inatakiwa kuwa Tume ya Wasomi, Tume ya kikundi cha watu ambayo miaka mitano au miaka kumi ijayo, Taifa hili lipige hatua. Kwa hiyo si Tume ambayo itakusanya *bureaucracy* pale Makao Makuu hapana; ni tofauti kidogo.  Nataka kuwahakikishia kwamba, mchakato upo tayari, Baraza la Mawaziri limeshauzungumzia, tunangojea wakati wowote kabla ya mwaka ujao kuanza, Tume hii itakuwa imeshaanza kazi.

Pili, Kamati imeishauri Serikali kubuni mikakati madhubuti ya kushughulikia msukusuko wa kiuchumi.  Kama nilivyoeleza kwenye muhtasari wa mwongozo, tayari Serikali inaunda Kamati ya kushughulikia suala hilo.  Kwa hiyo, pendekezo hili tumelikubali moja kwa moja. Tatu, Kamati imeishauri Serikali ihakikishe inaandaa mpango wa kunusuru uchumi wetu na madhara yanayotunyemelea kutokana na msukosuko huo.  Ili kufanikisha hili, Serikali ina mpango wa dharura na wa muda wa kati, kama nilivyowasilisha katika maelezo yangu wakati nawasilisha muhtasari wa Mwongozo wa Mpango wa Bajeti.

Nne, Kamati imeshauri Serikali kuchagua vipaumbele vichache.  Serikali inakubaliana na ushauri huo.  Tano, mambo mengine yaliyoshauriwa na Kamati ni pamoja na kupunguzwa kwa misamaha ya kodi; Serikali itashirikiana na wadau kama vile *CTI* na *TSSA* ili kupata ushauri juu ya uwajibikaji wao katika kuchangia kuendeleza uzalishaji, pamoja na kutoa mawazo ya mfumo sahihi wa kodi, kuboresha utendaji wa bandari zetu, kuendelea kuboresha sekta ya kilimo kwa mapana yake, kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo na kuhamasisha utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi.  Kama nilivyoeleza kwenye mada yangu au kwenye Waraka wangu, Serikali inakubaliana na ushauri huu na itatekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani yamejumuisha yafuatayo:  Umuhimu wa Serikali kudhibiti mfumko wa bei, kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kuhimiza uzalishaji kwa mazao yanayotumia muda mfupi, kukuza uchumi vijijini ili kuwanufaisha Watanzania wote, kupanua vyanzo vya mapato, kupunguza utegemezi wa wafadhili, kuimarisha sekta ya uvuvi na kuimarisha bandari na sekta

nyingine za usafirishaji. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itazingatia kikamilifu ushauri wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, takriban michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, imeelekezwa katika sekta za kilimo, miundombinu, huduma za jamii; yaani afya, maji na elimu, mifugo, uvuvi, uwezeshaji wa wananchi na kuongeza mapato ya Serikali. Maeneo yaliyotajwa na Waheshimiwa Wabunge, mengi ndiyo vipaumbele vya mwongozo wa mipango na Bajeti. Maelezo ya kina yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo haya, yatazingatiwa katika maandalizi na mipango wa Bajeti za Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, kwa masuala yanayohusu kuongeza mapato, Kamati ya kupitia Mfumo wa Kodi ambayo inaratibiwa na Wizara yangu, itashughulikiwa kikamilifu na mtayaona katika mpango kamili wa Bajeti mwezi wa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza wakati nawasilisha maelezo yangu kuhusu mwongozo wa utayarishaji wa Mpango wa Bajeti, baada ya kupokea michango ya Waheshimiwa Wabunge, mwongozo utakamilishwa na kusambazwa kwenye Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa ili waweze kuandaa mipango na Bajeti zao kwa mwaka wa fedha ujao, kwa kipindi cha muda wa kati.

Mpango wenyewe na Bajeti, utawasilishwa Bungeni kama ilivyo kawaida mwezi Juni, 2009, baada ya kupitiwa na Kamati mbalimbali za Bunge. Kwa hiyo, tunataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, michango yenu yote ambayo ni mizuri kweli kweli itaingizwa kwenye mpango utakaotengenezwa upya na mpango huo ndiyo utakaowasilishwa Serikalini ili uweze kutekelezwa. Napanda kusema kuwa, tayari Serikali imepokea michango ya Waheshimiwa Wabunge na itazingatiwa katika kukamilisha mipango yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kidogo kuhusu swali lililoulizwa na Mbunge wa Solwa, kuhusiana na kupata msamaha katika gari ambalo anataka kulitumia kama *Ambulance*. Tatizo tulilonalo ni kwamba, zipo Sheria ambazo zimetungwa na Bunge hili.

Sasa gari lililoagizwa na Mheshimiwa Mbunge si *Ambulance* ni la kawaida ila anataka kulibadilisha libebe wagonjwa. Kwa bahati mbaya, Sheria haina kifungu cha aina hiyo; unaagiza *Ambulance* au huagizi. Mheshimiwa hakuagiza *Ambulance,* kaagiza gari ya aina tofauti. Sasa kwenye vitabu vya watu wa TRA, ile si *Ambulance* na kwa sababu si *Ambulance,* haingii kwenye kifungu cha kupata msamaha. Kwa hiyo, ushauri nilioupata kutoka kwa TRA ni kwamba, kwa sababu siyo *Ambulance,* Waziri wa Fedha hana madaraka ya kusamehe kodi

Waziri anayo madaraka ya kusamehe VAT na hilo ndilo ninalifanya mimi; kwamba, lile ambalo nina madaraka nayo, tumemsamehe Mheshimiwa, yale ambayo sina madaraka nayo tumewambia alipe. Lazima muelewe kwamba, mnaposema unamsamehe mtu, ukimsamehe VAT umesamehewa, ukisamehe *import duty* au *exercise duty,* maana yake ni kwamba, Halmashauri ya Solwa haitalipa kodi.

Mimi Waziri wa Fedha, natakiwa nimwamrishe Katibu Mkuu wa Hazina, alipe kupitia *treasury voucher;* kwa maana nyingine walipa kodi wa Dar es Salaam walipie kodi ya Solwa. Hiyo ndiyo maana yake na mimi kwa busara za TRA, nilikataa kutumia kodi za watu wa Dar es Salaam, kutoa msamaha kwa kodi za Manispaa ya Solwa. Maana yake ni kwamba, mtu akiagiza pikipiki halafu nyuma yake afunge *trailer,* aseme hili sasa ni gari la wagonjwa lipate tafsiri ya *Ambulance* na Waziri wa Fedha asamehe kodi, sitasamehe kwa sababu Sheria inasema kitu kingine.

Sasa ningetaka kuelewa wazi kwamba, Waziri hajakataa kusamehe kodi, Waziri kashauriwa kwamba, hili gari si *Ambulance.* Sasa kung'ang'ania kwamba ni *Ambulance* wakati siyo, itatuletea matatizo. Waheshimiwa Wabunge, humu mlimokaa leo, tunazo kesi Mahakamani au tuhuma za kwamba, umekataa ushauri wa TRA, kwa hiyo, umefanya makosa. Mimi nimeshauriwa nikatae, kwa hiyo, nikikataa ushauri ule Waziri nitakuwa mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kama ni kweli kuna kitu ambacho kinastahili kusamehewa kodi, sisi Wabunge tulete na tutasamehe kodi. Hapa tunasema tupunguze misamaha ya kodi, halafu tunasema Waziri avunje Sheria, asamehe kodi mahali ambapo hapatakiwi kusamehewa kodi! Nafikiri ndugu yangu atakuwa ameelewa, hatukukataa kwa sababu tumetaka kukataa hapana; ni sheria ndivyo inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kujibu yote, lakini kuna hili la Mheshimiwa Kaboyonga, kuhusu Kampuni ya Reli. Kwanza, nashukuru umesema yeye ni mdau katika Bodi, ambapo ni Mjumbe wa Bodi. Hili ni la kibajeti zaidi kuliko la kisera, kwa sababu Mheshimiwa anajua kuhusu mchakato ambao Serikali inauchukua sasa hivi, kuhusiana na milioni 44.0

Dola za *IFC* na kuhusiana na milioni 83.0 za Wahindi. Sasa nadhani kwa sababu ni za Wahindi, kwa sababu ni la kisera na ni la kiutendaji, niishie kusema tu kwamba, suala hilo linashughulikiwa na litakapokamilika, nadhani Bodi itajulishwa na kama ikibidi Bunge lijulishwe litakuja kujulishwa mbele ya safari. Hili si suala ambalo linashughulikiwa na sisi ambao tupo upande wa Serikali, tunalifahamu vizuri na nisingependa Bunge hili tuondoke humu kama vile dunia itaporomoka kesho, kwa sababu ya milioni 44 za IFC, hapana linashughulikiwa kikamilifu kabisa.

Kuhusu barua ambayo Mheshimiwa Kabwe ameionyesha ni kweli iliandikwa, lakini pia kuna mchakato wa mambo ya kiserikali, sasa mchakato ule haujakamilika. IMF wamejulishwa kwamba, mchakato haujakamilika, ndiyo maana hakuna *paper* ya kubadilisha Sheria ya Madini, ambayo imeletwa humu ndani ya Bunge. Utakapokamilika, kwa hushirikiana na wenzetu wa madini, nadhani wakati wowote Sheria italetwa na Bunge litajulishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni ya kibajeti. Mwongozo huu haukusudii kujenga barabara ya Sumbawanga kwenda Tunduma, hayo yatakuja mwezi Juni na atakayeshughulikia ni Waziri wa Sekta.

Kwa hiyo, Waziri wa Miundombinu baada ya kumpatia mwongozo huu, atakaa chini na kuandaa mkakati, kuandaa Bajeti ya Mwaka 2009/2010, ambayo itajumuisha pamoja na mengine, hizo barabara zilizozungumzwa au madaraja ya kupunguza saa kumi mpaka saa sita, kutoka Mwaza kwenda Arusha. Tusingeweza kuyaweka hayo hapa, kwa sababu ni sera, tunaweka mwongozo. Nashukuru kwamba, Waheshimiwa Wabunge wengi wameelewa vizuri sana na michango yenu ni mizuri, itatusaidia kuuboresha mwongozo huu. Nataka nikuhakikishie kwamba, Bajeti ya Mwaka huu itaandaliwa kwa umakini zaidi, kuliko nyingine ambazo tumeziandaa huko nyuma, kwa sababu ya michango ambayo tumeipata kwa Wabunge wote; Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na wa Upinzani.

Tunawashukuru sana na naahidi kwamba, tutashughulikia vizuri. Sasa wale ambao walitegemea nijibu yale maswali ya kibajeti, tulizungumza kwamba Kiserikali hatujafika; ninayo hapa majibu lakini wakati wa kujibu masuala ya kibajeti haujafika. Kwa hiyo, huo utamu mliotupa na michango hii, nataka niwaahidi kwamba, tutakuja na Bajeti ambayo kila mmoja wenu ataifurahia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani, kuanza kujitokeza hapa nchini na kama Wabunge wengi walivyochangia, Serikali inachukua hatua za kukabiliana na msukosuko huo kama nilivyoeleza katika waraka niliouwasilisha. Matumaini ya Serikali ni kuwa, hatua zilizoandaliwa katika mwongozo huo zitaweza kutuvusha katika tatizo hili. Pamoja na kwamba, Serikali imejizatiti kuchukua hatua hizo, ushiriki wa wananchi na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu katika kufanikisha azma hiyo.

Baada ya maelezo haya na baada ya angalizo, ninachojibu mimi ni sera na mwongozo na si Bajeti. Naomba kuwashukuru tena kwa michango kuhusu mwongozo wa utayarishaji wa mpango na Bajeti kwa mwaka 2009/2010 hadi 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 yalikubaliwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelezane yafuatayo: Suala hili la kuwa sisi kama Kamati ya kujadili Mpango wa Bajeti wa Serikali sio tu ni kitu ambacho sisi Wabunge tunapenda kukifanya; ni kitu ambacho tunapata mamlaka yake kutokana na Kanuni yetu ya 94, ambayo inasema hivi: "Ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa Mwezi wa Februari ili kujadili na kushauri kuhusu

mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa Fedha unaofuata.”

Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba inasema hivi; “Kwa madhumuni ya utekelezaji wa Madaraka yake, Bunge laweza kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango huo.”

Kwa hiyo, mimi lazima nikubali huu ni mwaka wa tatu. Mwaka wa kwanza hatukufanya vizuri, mwaka wa pili hatukufanya vizuri kabisa, mwaka wa tatu tumejitahidi, lakini bado hatukufanya vizuri. Kwa hiyo, namna tutakavyokwenda baadae, hili takwa la Kikatiba na takwa la Kanuni zetu ni muhimu sana katika mfumo mzima unaoitwa mzunguko wa bajeti.

Sasa hivi katika Jumuiya za Kimataifa hasa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, tuna utaratibu ambao unatakiwa kulingana wa namna ya kuendesha Bunge na tuna vipimo pia kupima Bunge gani linakuwa *more democratic* kuliko Mabunge mengine katika Jumuiya yetu. Moja ya vipimo hivyo ni uhuru wa Bunge katika *financial independence,* ambayo kwa bahati sisi tumeshatunga Sheria ya *Parliamentary Administration Act.*

Sheria ya pili ni *Administrative independence,* sasa hivi Ofisi ya Bunge, inaweza kuajiri watumishi wake. Tatu ni *Oversight Independence* na katika hii mojawapo ni kuweza kuingia katika *Budget Cycle* ya nchi.

Kwa hiyo, naomba sana tusilichukulie kama ni kitu cha kawaida. Nilikuwa namkosoa hata Waziri wa Fedha, namwambia taarifa yake hakutoa madaraka aliyopewa, maana yake hajanukuu Mamlaka iliyoko ndani ya Kanuni hii, wala ndani ya Katiba kwamba, nawasilisha hii *document* kwa Mamlaka hii hakusema. Ni kikaratasi ambacho amekuja kukisoma hapa aondoke. Sasa baadaye mwaka unaofuata na bahati nzuri tumeahidiwa kwamba na Tume yenyewe ya Mipango itakuwa imeundwa, pengine twende kwa undani zaidi na kwa umakini kuliko tulivyofanya mpaka sasa. Kwa hiyo na sisi katika Ofisi ya Bunge, tunaendelea kuimarisha namna ya kushughulikia masuala haya.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kuamua haya tuliyofanya, lakini nadhani tuna nafasi ya kuendelea kufanya vizuri zaidi na likawa Bunge la mfano kwa nchi nyingine.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru kwa kazi nzuri na niwatakie jioni njema. Wale wa Chama cha Mapinduzi, nadhani kuna mkutano saa mbili katika Ukumbi wa Msekwa. Naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 11 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*